

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

KIKAO CHA ISHIRINI – TAREHE 9 JULAI, 2008

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Nasibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Na. 177

Kampeni Dhidi ya Wahujumu Uchumi Mwaka 1983

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka 1983 Serikali iliendesha kampeni ya kuwanasa wahujumu uchumi:-

- (a) Je, ni watu wangapi waliofungwa kwa kuhujumu uchumi?
- (b) Je, ni watu wangapi walioachiwa na mahakama kwa kutokuwa na kesi na kurejeshewa mali zao?
- (c) Je, ujisadi uliozuka kwenye miaka hii ya 2000 hauwezi kushughulikiwa kama ilivyofanyika mwaka 1983?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kampeni ya kuwanasa wahujumu uchumi ya mwaka 1983 ilikuwa ni operesheni ya Serikali katika kukabiliana na wafanyabiashara wa magendo wenye kuhodhi bidhaa na kusababisha upungufu mkubwa wa mahitaji muhimu hususan vyakula, dawa na vifaa vya hospitali kwa ajili ya matibabu na pia kuadhibiti watoroshaji wa bidhaa nyingi kwenda nchi za nje.

Zoezi hilo lilibidi litekelezwe ili kuwashtukia na kuwabaini wahusika wote na wadau wao. Wengi wao walikuwa ni wafanyabiashara wa bidhaa za aina mbalimbali zisizo halali.

Kutokana na zoezi la waliotuhumiwa kuhujumu uchumi ni watu wengi walikamatwa. Kati yao walishitakiwa na kupatikana na hatia. Kwa mujibu wa maamuzi ya mahakama waliohusika walifungwa na kutumikia vifungo vyao magerezani.

(b) Idadi ya waliokamatwa mwaka 1983 walikuwa zaidi ya watu 4,000 hii ni kwa mujibu wa Tume ya Jaji Mwita iliyotembelea mikoa yote Tanzania Bara mwaka 1990. Walioachiliwa na mahakama yakiwepo maamuzi ya mahakama ya kurejeshewa mali zao au kulipwa fidia Serikali ilitekeleza maamuzi hayo. Katika uhakiki wa mwisho wa zoezi hilo watu 148 walilipwa kifuta machozi kilichofikia jumla ya shilingi 849 milioni. Hii ni kutokana na mapungufu mengi yaliyojitekeza hususan kukosekana kwa vielelezo na kumbukumbu sahihi.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, matukio ya kupotea kwa fedha za umma katika miaka ya 2000 na kuhusishwa na ufisadi yamekuwa yakishughulikiwa kwa utaratibu tofauti na ule wa operesheni ya mwaka 1983. Mazingira ya upotevu wa fedha katika taasisi za umma na sekta binafsi umesababishwa na ubadhirifu, kutokuwajibika na ukiukwaji wa maadili. Tayari Serikali imeunda tume mbalimbali kuchunguza tuhuma hizo na ukweli utakapobainika hatua za kisheria zitachukuliwa.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, ninapenda kuipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu kwa sababu nimeingia hapa nimekuta majibu ya swali hili yapo kwenye eneo langu hapa. Kwa hiyo, nashukuru sana na nadhani Mawaziri wengine wafuate mfano huo wa kutekeleza Kanuni zetu.

(a) Kwa kuwa zoezi la sasa hivi la kupambana na ufisadi linashughulikiwa katika ngazi ya juu zaidi na kwa kuwa kuna ufisadi mdogo mdogo huko vijiji wa kula michango ya wananchi, kutotoa hesabu za michango ambayo inatakiwa itolewe kisheria. Je, si vizuri zoezi hilo likiendelea mpaka sehemu ya chini na hivyo ikawa ni kampeni ya aina peke yake? (*Makofi*)

(b) Kwa kuwa Serikali imesema kabisa kwamba wale walionekana hawana makosa wameachiliwa na mahakama wamelipwa fidia. Je, ni lini Mzee Omar Mpalahole wa Kijiji cha Manga, Kata ya Funta, tarafa Bumbuli, Jimbo la Bumbuli atalipwa fidia yake kwa sababu ilidhihirika waziwazi kabisa kwamba alikuwa hana kesi na namshukuru sana Msajili wa Mahakama Kuu kwa kumsaidia kutafuta faili la kesi hiyo ya mwaka

1983 na ilipatikana mwaka 200. Kuanzia mwaka 2001 mpaka sasa hivi anafuatilia kulipwa fidia yake, ameshakuja Dodoma mara 8 kwa tarehe ambazo ameziandika. Je, ni lini atalipwa fidia yake? Nashukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Hilo la pili tatizo. Lakini la kwanza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, jaribu kujibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, maswali yake mawili kama ifuatavyo:-

Kwanza, lile analoliita ujisadi mdogo mdogo ngazi ya chini kwa sasa linashughulikiwa na sheria zilizopo na sheria hizo zinajitosheleza. Pili, kuhusu suala la mpiga kura wake, kutoka Bumbuli ambaye alikumbwa wakati huo na operesheni hii naomba nimkumbushe Mheshimiwa Shellukindo kwamba ule ulikuwa ni wakati muhimu na zoezi hili lilikuwa gumu sana kutekeleza. Kwa hiyo, hata fidia nayo ilikuwa ngumu kwa sababu mbalimbali hasa nyaraka na ushahidi. Hata hivyo na hili analifahamu kwa sababu aliwahi kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu na wengi katika Bunge hili baadhi yetu tumeshughulikia masuala haya. Kwa hiyo, suala lake kama lina ushahidi na kuna jalada tunaomba alete vielelezo hivyo tuone namna ya kumsaidia huyo mpiga kura wake.

MHE. ALOYCE B. KIMARO: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina swali moja kama ifuatavyo:-

Waziri anaweza kuahidi hapa Bungeni kwamba wale waliokamatwa na wana vielelezo kamili na hawajalipwa fidia wakileta vielelezo yuko tayari kuvishughulikia na kuwapa fidia?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Aloyce Kimaro Mbunge wa Vunjo, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Nimemwelezea Mheshimiwa William Shellukindo kwamba tutaangalia nyaraka alizonazo mpiga kura wake kwa vile inaonekana nyaraka hizo zilikuwepo kabla mlanga wa kutoa kifuta machozi ulikuwa haujafungwa.

Kwa kweli masuala yote yanahu su wahujumu uchumi ya mwaka 1983 yalishughulikiwa na hatimaye kufikia mwaka 2000 basi yote yalikuwa yamefungwa na hatushughuliki tena na malalamiko kuhusu wahujumu uchumi kwa makosa yaliyotokea mwaka 1983.

NAIBU SPIKA: Dakika za swali hilo zimekwisha.

Uboreshaji wa Barabara Vijijini

MHE. ANNA RICHARD LUPEMBE aliuliza:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuziboresha barabara za vijijini ambazo ndiyo vyanzo vya mapato kama ilivyo kwa barabara ya Mtimbwa kwenda Chipu na ile ya Sintali kwenda Kala ambako kunapatikana samaki wabichi na dagaa biashara ambazo zinafanywa na wananchi wa maeneo hayo?
- (b) Je. Serikali haioni kuwa ikitengeneza barabara hizo kutawawezesha wananchi wa maeneo hayo waweze kusafirisha bidhaa zao wakati unaofaa kwenda sokoni na kuongeza ajira kwa vijana?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kwamba barabara za vijijini ni muhimu kwa wakulima kusafirisha mazao yao na pia kupeleka huduma mbalimbali kwa wananchi kwa maeneo hayo. Mnamo tarehe 23 Juni, 2008 katika Kikao cha Tisa cha Mkutano huu wa kumi na mbili unaeondelea hapa nilijibu swali Na. 75 linalofanana na swali hili kutoka kwa Mheshimiwa Suleiman Omar Kumchaya, Mbunge Lulindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilieleza Bunge lako tukufu kwamba Serikali imekuwa ikiongeza Bajeti ya matengenezo ya barabara zinazohudumiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hata hivyo ukweli ni kwamba fedha za mfuko wa barabara zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa mwaka 2008/2009 ni shilingi bilioni 65, kama ilivyokuwa mwaka wa fedha uliopita. Pamoja na hali hiyo, mwaka wa fedha wa 2007/2008 Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi imetengewa jumla ya shilingi milioni 323.4na kwa mwaka 2008/2009 imetengewa shilingi milioni 353.94.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kuboresha barabara analogzungumzia Mheshimiwa Mbunge, ni jukumu la Halmashauri (Baraza la Madiwani) kuainisha barabara zitakazotengewa Bajeti kwa mwaka husika. Barabara ya Mtimbwa- Chipu aliyoizungumzia Mheshimiwa Mbunge, ni sehemu tu ya barabara ya Mtimbwa – Ntalamila yenyе urefu wa km. 42. Barabara hii awali ilikuwa ikihudumiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga. Kwa hivi sasa barabara hii inafanyiwa matengenezo na wakala wa barabara *TANROADS* Mkoo wa Rukwa. Kwa mwaka huu wa fedha 2008/2009 barabara hii imetengewa shilingi milioni 32 kwa matengenezo ya kawaida (*routine maintenance*).

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Sintali kwenda Kala ina urefu wa km 67. Barabara hi inahudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi. Katika Bajeti ya mwaka 2007/2008 barabara hii ilitengewa shilingi milioni 48 kwa ajili ya matengenezo ya muda maalum (*periodic maintenance*) na shilingi milioni 40 kwa ajili ya matengenezo ya sehemu korofi (*spot improvement*).

Kwa mwaka wa fedha 2008/2009 Serikali imetenga shilingi milioni 44 kwa ajili ya matengenezo ya muda maalum km. 4 na shilingi milioni 30 kwa ajili ya matengenezo ya sehemu korofi kwenye barabara ya Nkana – Kala yenye urefu wa km. 20 ambayo ni sehemu ya barabara ya Sintali – Kala.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali ikitengeneza barabara hizo itawawezesha wananchi wa maeneo hayo waweze kusafirisha bidhaa zao kwa wakati muafaka kwenda maeneo mbalimbali yakiwemo masoko. Hii itasaidia kuongeza ajira kwa wananchi wa maeneo husika ikiwa ni pamoja na vijana.

Pamoja na fedha zilizotengwa kutoka mfuko wa barabara, kwa mwaka 2008/2009 Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi pia imetengewa shilingi milioni 80 kutoka programu ya usafiri katika Halmashauri. Juhudi zote hizo ni kielelezo dhihiri kwamba Serikali imedhamiria kufungua barabara za vijiji kwa kuwa ni kiungo muhimu kwa barabara za Wilaya na Mkoa.

MHE. ANNA RICHARD LUPEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo aliyonijibu na vile vile naomba nimpongeze Naibu Waziri kila asubuhi kwa swali anakupigia simu mteja wake kama je, uko salama ili uweze kuja kuuliza swali. (*Makofî/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali inapanga fedha kwa ajili ya miradi ya barabara za vijijini na ile miradi haikamiliki zile fedha zinakuwa hazitoshi kutokana hali ya bei za vifaa zinaongezeka siku hadi siku, mafuta yanaongezeka bei, nondo na vitu ambavyo vinahusiana na miradi ya barabara.

(a) Je, Serikali sasa hivi ina mikakati gani ya kuweza kupanga fedha hasa mahususi ili hiyo miradi iweze kwisha kwa wakati wake?

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali mbaya ya barabara zile, barabara inayokwenda Kala na watu wanapata tabu. Je, Waziri yuko tayari Bunge hili likiisha mimi na yeze tuongozane aende akaangalie hali halisi ya barabara hizo? (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Anna Lupembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa naomba nikuchukue nafasi hii kwa niaba ya Serikali kumshukuru sana Mheshimiwa Anna Lupembe, kwa *appreciation* yake kwa namna tunavyo-*handle* maswali hapa Bungeni.

Baada ya kusema hayo naomba sasa nijibu kama ifuatavyo: Ni kweli kabisa sisi wote Watanzania tunajua kwamba bei za vitu zimekuwa zikipanda kila wakati pamoja na kwamba tumeweka Bajeti. Katika hali hiyo, ni kwamba mkandarasi anaweza akakuletea kitu kinachoitwa *variation* kwa maana ya kwamba *cement* zinapanda bei, nondo zinapanda bei na vitu vingine.

Sasa anasema kwamba tunafanya nini kama Serikali. Tunachofanya hapa ni kwamba inapotokea hali ya namna hiyo ni kwamba mnakuja tena hapa Bungeni kwa sababu hela zote zinaidhinishwa na Bunge la Jamhuri la Muungano wa Tanzania kwa maana ya kuomba kibali cha kutumia. Lakini tunachofanya sisi ni kwamba kunakuwa kuna masuala ya ya *emergency* kwa maana ya dharura. Kwa hiyo, Halmashauri mbalimbali zimekuwa zinaomba na tunajaribu ku-*consider* kesi yao kufuatana na hali halisi inavyojitokeza.

La pili, ametaka kujua kama nitakuwa tayari kuondoka na yeze twende katika Halmashauri hii na Manispaa hii. Itakuwa ni faraja kubwa sana kwangu kwenda kule hasa nikitambua kwamba ndiyo Mkoa anaotoka Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofi/Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Lakini siyo wakati wa Bunge. Mheshimiwa Nyami, yeze anafahamu tena hizo barabara uliza swali la nyongeza.

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii niulize swali moja. Kwa kuwa barabara hizo zilizotajwa hii ya Chipu kwenda Sintali ina tatizo kubwa la kutokuwa na tuta na vile vile kuanzia Sintali kwenda Nkana na kuanzia Nkana kwenda Kala hasa eneo la kati ya Nkana na Kasapa tuta ni baya sana sana. Mara nyingi tulishaomba barabara hiyo iwe ni ya *TANROAD* bila ya mafanikio.

NAIBU SPIKA: Sasa uliza swali.

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Swali sasa, je, Serikali iko tayari kutupatia fedha za kutengeneza matuta hayo ili kuondoa usumbufu uliopo ingawa nashukuru sana kupewa hizo fedha nyingine ambazo zipo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la ndugu yangu rafiki yangu Ndugu Ponsiano Nyami, Mbunge wa Nkasi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ametaja hii barabara inayotoka Chipu kwenda Sintali na ametaja pia Sintali kwenda Nkala na kwa vile sasa tumekubaliana kwamba nitakwenda kule nitakwenda kuziona vizuri zaidi kujua kwamba zikoje na kwamba waliwahi kuomba *TANROADS* wawakubalie kwamba hii ingie katika kiwango hicho. Utaratibu wa kuipandisha barabara kwenda kwenye ngazi nyingine unaanzia kule kule kwenye Halmashauri tunakwenda kwenye *TANROADS* kwa maana ya Bodi ya Barabara

ya Mkoa na tunapeleka pia katika ile Kamati yetu ya ushauri ya Mkoa na baadaye tunamalizia na sisi wenyewe kukubali kwamba hii ipandishwe daraja. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Nyami ahakikishe kwamba wanafuata hizo taratibu ili kuona uwezekano wa kuipandisha hii barabara *grade* kwa maana hiyo anayozungumzia.

Lakini ametaka pia kujua kama tutakuwa tayari sisi hapa kutoa hela kwa ajili ya matuta. Kuwa na matuta maana yake ni kwamba watu wanapata ajali na vitu vingine vya namna ile. Ninachoweza kusema hapa ni kwamba tumetamka hela nyingi tu hapa. wanachohitaji wao katika Halmashauri ni kukaa na kujaribu kuangalia kipaumbele katika eneo hili. Kama wanafikiri kwamba eneo hili ni muhimu zaidi basi wao ndiyo wenye mamlaka ya kuona kwamba wafanye mabadiliko ili matuta haya yaweze kujengwa. Hata hivyo kama nilivyosema tutashirikiana na Halmashauri ili kuona kwamba kazi hiyo inafanyika. (*Makofi*)

Na. 179

Utoaji wa Vibali vya Uvunaji Shamba la Longuza

MHE. HERBERT J. MNTANGI aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwa na malalamiko juu ya utoaji vibali vya uvunaji wa miti shamba la Longuza – Muheza kwamba waombaji wa nje ya eneo la msitu hupewa idadi kubwa ya vibali:-

- (a) Je, Serikali inachukua hatua gani kurekebisha dosari hiyo?
- (b) Je, kwa nini Serikali za vijiji zenye kusimamia miradi ya Maendeleo ya eneo la msitu hazikupewa vibali licha ya maombi yaliyofanywa kwa niaba yao wakati wa kuwasilisha Bajeti ya Wizara husika ya mwaka 2007/2008?
- (c) Je, kwa nini muundo wa Kamati ya uvunaji usiangaliwe upya ili viongozi wa Serikali za vijiji wahanishwe?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, wavunaji wadogo wote wanaogawiwa mitiki ya kuvuna katika shamba la miti la Longuza huchaguliwa kwa kufuata vigezo vifuatavyo:-

1. Kipaumbele hutolewa kwa wenyehi kutoka vijiji vinavyozunguka shamba la miti Longuza katika Wilaya ya Muheza.

2.Wananchi wanaotoka Wilaya nyingine za Mkoa wa Tanga.

3.Wananchi wanaotoka Mikoa mingine ya Tanzania

Wizara inatoa kipaumbele kwa wananchi wanozunguka shamba la mitiki la Lounguza. Kwa mfano kwa mwaka wa Fedha 2007/2008 takriban asilimia 20 ya waombaji waliopewa vibali walitoka maeneo hayo. Ikumbukwe pia kuwa shamba la mitiki ya mitiki la Longuza ni rasilimali ya Taifa. Hivyo, kila wananchi kutoka kila Mkoa hapa Tanzania anayo haki ya kuomba miti hiyo na kuuziwa. Tunachokifanya sisi Wizara ni kutoa kipaumbele kwa wananchi wanaoishi vijiji jirani na shamba hilo.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kikao cha Kamati ya kugawa miti kwa mwaka 2007/2008 katika shamba ya miti la Longuza kilifanyika mwezi wa Julai, 2007 ambapo maombi yaliyowasilishwa kabla ya tarehe hiyo yalijadiliwa na kutolewa maamuzi. Maombi yote yaliyoletwa baada ya kikao hicho hayakujadiliwa, hivyo Wizara inashauri kuwa waombaji wote, wakiwemo wavunaji wadogo wa vijiji jirani na shamba hilo kutuma maombi kwa kufuata utaratibu uliowekwa yaani kuanzia mwezi Januari hadi tarehe 30 Aprili kwa mwaka husika.

(d) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeandaa mwongozo wa uvunaji endelevu na biashara ya mazao ya misitu ambazo nakala zake zililetwa hapa Bungeni na kugawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge, wote tarehe 24/6/2008. Katika mwongozo huo miundo ya Kamati za uvunaji katika misitu ya asili na mashamba ya miti ya Serikali Kuu inatofautiana. Hata hivyo, Wizara yangu kwa sasa inaangalia uwezekano wa kupitia miundo iliyopo ya Kamati za uvunaji kwa upande wa mazao ya asili na mashamba ya Serikali ili kuboresha usimamizi mzima na kuondoa malalamiko ambayo yameanza kujitokeza.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyotoa. Hata hivyo, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

La kwanza, kimsingi kumekuwa na matatizo ya watu wanaotoka nje ya maeneo ya vijiji kugushi majina pamoja na vikundi, na kwa sababu hiyo basi wao wakapata nafasi ya kupata vibali, lakini si wenyeji wanaotoka katika maeneo hayo. Kwa sababu hiyo, je, Serikali haioni ipo haja sasa ya kufanya haraka kutengeneza utaratibu upya katika ugawaji ili kuwashirikisha wenyeji waliopo pale hasa viongozi wa Serikali za vijiji ili waweze kutambua vikundi na watu ambao wanatoka katika maeneo hayo?

La pili, ni kwamba mara nyingi Serikali za vijiji nazo zimekuwa zikiomba vibali ziweze kufanya shughuli za Maendeleo. Lakini hakuna hata mara moja ambapo Serikali ya Kijiji imepewa kibali. Serikali haioni kwamba ipo haja ya kufikiria Serikali za Vijiji ambao ndiyo wasimamizi wakubwa wa shughuli za Maendeleo katika maeneo hayo ya vijiji?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ni kweli tatizo la wafanyabiashara wasioishi maeneo jirani na shamba na kuomba kana kwamba ni wakazi jirani limejitokeza. Lakini niseme kwa bahati nzuri

ugawaji kwa mwaka huu wa Fedha bado hatujafanya. Kwa mashamba yote tulikwishakamilisha lakini bahati nzuri kwa shamba hilo la Longuza bado hatujagawa kutokana na uhakiki wa rasilimali iliyopo kuchelewa kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme kwa niaba ya Wizara kwamba ushauri huu tutauzingatia sana. Kwa sababu nia yetu kwa kweli ni kuhakikisha kwamba tunawashirikisha wenyeji wetu na jirani zetu kwenye eneo hilo. Kwa maana hiyo tutawashirikisha katika kuhakiki kwamba wote wanaomba na tunaokusudia kuwapa kwa msingi wa ujirani mwema basi wanapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swalii la pili, kwa bahati mbaya mwongozo ulivyokuwa umeandaliwa mwanzoni ulikuwa unalenga kuruhusu wafanyabiashara ambao wanafanya biashara ya miti. Kwa hiyo, katika masharti ukiangalia Ibara ya 3(2) ya Mwongozo ambao tuliugawa kwa Waheshimiwa Wabunge, hivi karibuni unasema mwombaji awe na leseni ya biashara, awe na *TIN*. Halafu vilevile awe amejiandikisha kufanya biashara ya mazao ya misitu. Kutokana na masharti hayo imekuwa ni vigumu kuwa tunatoa nafasi kwa waombaji wa kawaida ambao si wafanyabiashara. Lakini mazingira ambayo yamejengeka au tuliyyona kutokana na uzoefu ni kwamba kuna maeneo ambayo kwa kweli ni muhimu kuangalia masharti hayo upya. Kwa hiyo, kama nilivyo sema katika jibu la msingi kwamba tunaangalia upya huo muundo na tutajitahidi kuhakikisha kwamba tunaboresha ili kuwapa kipaumbele jirani zetu.

Na. 180

Uendeshaji wa Shirika la Reli Kutawaliwa na Wawekezaji

MHE. TATU M. NTIMIZI aliuliza:-

Kwa kuwa, Shirika la Reli limekodishwa kwa wawekezaji ambao wanamiliki hisa ya asilimia 49 na Serikali inamiliki hisa asilimia 51, na kwa maana hiyo pande zote mbili zinawajibika kwa huduma zitolewazo na Shirika hilo:-

(a)Je, kwa nini mwekezaji anakuwa na maamuzi zaidi katika utendaji wa kazi kuliko Serikali kwa kukataza kupakua mizigo midogo midogo katika vituo vidogo vilivyopo kando kando ya reli?

(b)Je, kwa nini mwekezaji ameamua kuwa mtu ye yeyote anayetaka kupakia mizigo apakie katika Vituo vya Dar es Salaam, Tabora, Kigoma au Mwanza?

(c)Je, Serikali haioni kuwa wananchi waishio kando kando ya reli hiyo wanadhalilishwa na kunyimwa haki yao ya kufanya biashara ndogo ndogo ili wajikwamue kiuchumi?

WAZIRI WA MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Tatu Musa Ntimizi, Mbunge wa Igalula, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, Shirika la Reli Tanzania (*TRC*) limekodishwa kwa Kampuni ya Reli Tanzania (*TRL*) tangu tarehe 1 Oktoba, 2007. Kampuni ya Tanzania *Railways Limited (TRL)* ni ya ubia kati ya Serikali ya Tanzania kwa asilimia 49 na M/S *RITES* ya India kwa asilimia 51. Kampuni hiyo ndiyo iliyopewa jukumu la uendeshaji wa shughuli za reli baada ya *TRC* kukodishwa, Kampuni hii ndiyo wenyewe maamuzi ya shughuli za kiutendaji za kila siku katika utoaji wa huduma za usafiri wa reli.

Ni kweli kwamba mwanzoni, hali ambayo inayolalamikiwa na Mheshimiwa Mbunge ilikuwepo katika Kampuni ya *TRL*. Serikali kwa kupitia Kampuni ya Reli *Assets Holding Company (RAHCO)* iliwasiliana na Kampuni ya *TRL* na kwa sasa tatizo hilo limeshughulikiwa. Abiria wanaruhusiwa kuteremsha na kupakia mizigo yao midogo midogo katika vituo vidogo vidogo viliwyopo kando kando ya reli. Serikali itaendelea kufuutilia kuhakikisha kuwa wananchi wanakuza uchumi wao kwa kutumia huduma za reli, kuwaruhusu kupata huduma za upakiaji na upakuaji wa mizigo yao midogo midogo kwenye stesheni zote za reli ili mradi tu upo urahisi wa kupakia na kuondosha behewa kwenye stesheni husika.

MHE. TATU M. NTIMIZI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ambayo niseme siyo sahihi sana. La kwanza, kwa sababu naomba anifafanue kwamba pamoja na kukubali stesheni kubwa zile wameanza kupakia na kwenye vituo vidogo vidogo. Lakini bado Morogoro, Dodoma, Shinyanga hawaruhusiwi kupakia vifurushi. Sasa na hao pia ni walinzi katika reli hii.

La pili, hata hivyo, katika vituo vidogo wanaruhusiwa kupakia, lakini bado kutokana na vichaka viliwyopo, usafi umekuwa haupo kutokana na kupunguza wahudumu katika maeneo hayo. Je, wananchi wanasaidiwaje kwa usalama wa kupakia mizigo yao katika maeneo ambayo majani yameota, vichaka vimeduwa vingi katika vituo vidogo vidogo hivyo?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika majibu ya awali ya jibu kuu kwa swal la msingi kwamba Kampuni ya *RACO* tayari imefanya mawasiliano na *TRL* kuhakikisha kwamba usumbu huu wa wananchi kutokuruhusiwa kupakia na kupakua mizigo yao katika Vituo mbalimbali uishe na makubaliano yamefikiwa kwamba sasa wananchi wanaruhusiwa.

Kama bado kuna tatizo, tutaendelea kulifuatilia ili kuhakikisha ahadi hii ambayo *TRL* wameitoa wanaendelea kuitekeleza.

Suala la usafi katika vituo hivi vidogo vidogo, nimelipokea na tutalishughulikia, tutaliwasilisha *RACO* na kwa niaba ya Serikali *RACO* watalifikisha *TRL* ili *TRL* waweze kutoa huduma nzuri zaidi kwa wananchi wa Tanzania.

NAIBU SPIKA: Lakini Mheshimiwa Waziri mnadaiwa maelezo ya taarifa ya Hoja aliyotoa Mheshimiwa Arfi na ndiyo maana siulizi maswali ya nyongeza, kwa sababu mnadaiwa hiyo taarifa ya utekelezaji.

Na. 181

Kuweka lami Mlima Kinolombedo

MHE. JUMA A. NJWAYO aliuliza:-

Kwa kuwa mlima Kinolombedo uliopo katika barabara ya Mtama-Newala umekuwa unasababisha vifo na hasara ya mali kama vile magari, bidhaa na kadhalika kufuatia mlima huo kuangusha magari mara kwa mara:-

Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kuweka lami katika eneo hilo la mlima kama ilivyo kwa Nanyamba, Mtwara na Namaleche Newala ili kupunguza hasara zinazopatikana sehemu hiyo?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mbunge wa Tandahimba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimpe pole Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Tandahimba kwa usumbufu ambaa wamekuwa wakiupata. Wizara yangu kuitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) Mkao wa Mtwara inalielewa tatizo la sehemu ya mlima Kinolombedo katika barabara ya Newala-Mtama yenyeye urefu wa kilometra 5 ambaa una mteremko mkali, kona tatu na ni eneo lenye udongo wa mfinyanzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi milioni 188.5 katika mwaka wa fedha 2007/2008 kwa ajili ya matengenezo ya kipande hicho cha barabara, kati ya shilingi 264.14 milioni ambazo zilizotengwa kwa ajili ya barabara nzima, ili kuifanya ukarabati sehemu ya mlima huu kwa kiwango cha changarawe na kwa kuipanua barabara na kujenga mifereji ya maji ya mvua. Kazi hizi zimefanyika na kukamilika kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada hizi za muda, Serikali inatafuta njia muafaka yenyeye utatuzi wa kudumu kwa sehemu hiyo, ikiwa ni pamoja na kuijenga kwa kiwango cha lami kutegemeana na uwezo wa kifedha.

MHE. JUMA A. NJWAYO: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, na naomba kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu. Lakini kwa matengenezo yanayotajwa siyo ufumbuzi wa kudumu. Ufumbuzi wa kudumu ni lami. Je, Waziri anaweza kuliahidi Bunge hili na wananchi wa Kata ya Mkwiti, sehemu ambayo mlima

uko pamoja na wananchi wa Tandahimba na Newala kwamba kwenye Bajeti ijayo ya 2009/2010 zitatengwa pesa kwa ajili ya barabara hii au kipande kile cha mlima kiwe cha lami?

Pili, kwa kuwa matatizo makubwa ya mlima Kinolombo ya yamechangiwa sana na mafuriko yaliyokumba Mikoa ya Mtwara na Lindi mwaka 1990 na kwa kuwa mafuriko ni dharura na hivyo kwenye dharura kipaumbele lazima kingewekwa.

Je, Serikali haioni ni aibu kwa muda wa miaka 18 sasa kutotatua na kuweka ufumbuzi wa kudumu kwenye eneo lile la mlima wa Kinolombo huku watu wakiendelea kufa na kuumia pamoja na mali kupotea? Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Inaeleweka ahsante. Mheshimiwa Waziri, sasa mkihutubia sana maswali, majibu yatakuwa madogo. (*Kicheko*)

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu katika swali la msingi kwamba Serikali inafahamu kero na tatizo la wananchi wa eneo hilo na kwamba inaweka nia kwa juhudini kwamba tatizo hili linakwisha. Tumetoa pesa za kufanya ukarabati kwa mwaka huu wa fedha mwaka uliokwisha 2007/2008 na tutaendelea kufanya hivyo mpaka tumalize hili tatizo kabisa. Kwa hivyo nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge na wananchi kwamba kazi hiyo tutaifanya kwa kadri tutakavyoweza kupata fedha katika Serikali. Ahsante sana.

MHE. MOHAMED S. SINANI: Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Katika barabara hiyo kuna daraja la Nangoo ambalo lilichukuliwa na *El-Nino* miaka 18 iliyopita. Vile vile na kwa kuwa daraja la Umoja linakamilika na barabara ya Dar es Salaam mpaka Masasi nayo inakamilika na kufanya kukamilika huko kutokuwa na faida yoyote iwapo daraja hilo halitajengwa. Je,

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sinani, swali.

MHE. MOHAMED S. SINANI: Je, ni lini Serikali itajenga hili daraja? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri mjibu kwa kifupi.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu daraja hili Nangoo, niseme tu kwamba taarifa kamili za mipango yake kwa sasa hivi sina. Nitazitafuta taarifa hizi za mipango ya Serikali katika kulijenga daraja hili mapema iwezekanavyo na nitampatia Mheshimiwa Mbunge.

Taaluma ya Uuguzi na Ukunga

MHE. SAID A. ARFI aliuliza:-

Kwa kuwa uuguzi na ukunga ni taaluma yenyе maadili ya kimataifa na kwa kuwa inaelekeea kuwa katika nchi yetu taaluma hiyo imekufa kutohana na watu kutojali maadili ya kazi na rushwa imekuwa mbele katika hospitali za Serikali:-

- (a) Je, Serikali inasema nini juu ya hali hiyo?
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua taaluma hiyo muhimu ili kuokoa maisha ya wagonjwa?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Said Arfi, Mbunge wa Mpanda Kati, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa wapo baadhi ya watumishi wa sekta ya afya, wakiwemo wauguzi wasiozingatia maadili ya kazi na taaluma zao wanapotoa huduma kwa wananchi.

Hata hivyo, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa wapo wataalam mbalimbali wa afya wakiwemo wauguzi wanaotambulika kwa kutoa huduma za kitaaluma na zenye ubora wa hali ya juu tena kwa upendo na uadilifu mkubwa. Hivyo, haitakuwa sahihi kusema taaluma ya uuguzi imekufa kwa sababu ya watumishi wachache wasiozingatia maadili ya kazi zao.

Wizara itaendelea kusisitiza wauguzi na watumishi wote wa afya kwa ujumla kufanya kazi kwa kuzingatia maadili ya kazi na taaluma zao na kupiga vita vitendo vya rushwa katika hospitali zote nchini.

- (b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kushughulikia tatizo la mmomonyoko wa maadili hatua zifuatazo zimechukuliwa:-

1. Somo la maadili limepewa uzito wa ziada katika mitaala ya wauguzi na wakunga na limewekwa kama somo la kufanyiwa mtihani wa kuhitim.

2. Mkakati umefanyika wa kuwajengea uwezo wakufunzi wa vyuo vya uuguzi wa kufundisha somo la maadili.

3. Vjarida na vipeperushi vinavyoutaarifu umma kuhusu wajibu wa muuguzi na mkunga na hatua za kuchukua pale mteja atakapotendewa kinyume na inavyotakiwa vinaendelea kugawiwa.

4. Mafunzo yametolewa kwa wauguzi wafawidhi wa hospitali za Wilaya, Mikoa na Rufaa kuwajengea uwezo wa usimamiaji, uzingatiaji wa maadili na utawala bora pamoja na ufuatiliaji wa kina juu ya uboreshaji wa huduma za uuguzi kote nchini; na vile vile

5. Baraza la Wauguzi na Wakunga limeshughulikia mapema malalamiko yaliyopokelewa kutoka kwa umma dhidi ya wauguzi na wakunga na adhabu zimetolewa kwa wauguzi waliopatikana na hatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusisitiza kuwa, mshikamano wa umma katika kupiga vita vitendo vya rushwa ni muhimu. Hivyo basi, napenda kutoa rai kwa umma kuwa wanapoona dalili yoyote inayoashiria mtaalamu wa afya kudai rushwa wawasilishe taarifa kwenye mamlaka husika. Aidha, napenda kukumbusha kuwa huduma yoyote inayopaswa kulipiwa, mgonjwa anatakiwa kupatiwa risiti halali ya malipo ya fedha kwa huduma aliyopewa. Vile vile, sehemu zote za huduma ziwekwe maandishi makubwa yanayowakumbusha wananchi kutokutoa na wala kutokupokea rushwa.

MHE. SAID A. ARFI: Nakushukuru Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Napenda nikushukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yako mazuri na kupitia kwako naomba unifikasihe pongezi za dhati kwa Madaktari na Wauguzi wote wanaofanya kazi katika mazingira magumu. Nina maswali mawili ya nyongeza:-

Moja, kwa sababu wagonjwa wanatumia muda mrefu hospitalini kuchelewa kupata huduma na hii huwapelekea kudhania kwamba madaktari na wauguzi wanahitaji rushwa kwa sababu ya uchache wa wataalam. Je, Serikali iko tayari sasa kutuungezea madaktari na wauguzi katika hospitali ya Mpanda?

Pili, kwa kuwa katika jibu lake la msingi Naibu Waziri amesema pia kwamba Serikali inafanya jitihada ya kuhakikisha kwamba malimbikizo ya madeni ya madaktari na wauguzi yanalipwa na hii inawafanya madaktari na wauguzi kutokutimiza wajibu wao na kuvunjika moyo.

Je, sasa Serikali iko tayari kuhakikisha kwamba inalipa madeni hayo kwa madaktari na wauguzi wote nchini na hususan hospitali ya Wilaya ya Mpanda?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru sana kwa pongezi ambazo umewapa wafanyakazi wa Wizara ya Afya na wanakusikia. Kwa hiyo, tutajitahidi i kuweza kuboresha huduma za afya. Ni kweli kabisa kwamba kwa sababu ya mlundikano unakuta kwamba wananchi huwa wanachukua muda mrefu labda kwa sababu hakuna kuna uhaba wa watumishi katika maeneo wanapokwenda kupata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema ni kwamba naushauri Mpanda ilete orodha ya mahitaji yao ya watumishi na sisi kama Wizara tutaweza kuwapatia kwa kadri tutakavyokuwa tunawapata. Lakini vile vile napenda nikumbushe kama

nilivyokuwa nikikumbusha siku zote kwamba inapokuwa katika foleni na kuna mgonjwa aliyezidiwa bila kujali kwamba kuna wataalam wachache au vipi, yule ambaye amezidiwa anapaswa kupata huduma za haraka bila kusubiri katika foleni. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili kama nilivyo sema katika jibu langu la msingi ni kweli kabisa Serikali inajitahidi. Lakini vile vile ningependa kukumbusha Halmashauri upande wa TAMISEMI na wenyewe waangalie watumishi ambao wanadai malimbikizo yao ili waweze kuwatambua na kuwaweka katika Bajeti ili basi pesa itakapopatikana basi waweze kulipwa, badala ya kuwaacha wanahangaika na kila siku kuendelea kuomba au kuhangaika na kuulizia kuhusu yale malimbikizo yao. Ni jukumu la Halmashauri husika na vile vile Tawala za Mikoa wahakikishe watumishi hawa wanaangaliwa na waweze kulipwa mafao yao.

Na. 183

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya

MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA aliuliza:-

Kwa kuwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya huchangiwa na wanachama wake kila mwezi na kwa kuwa upatikanaji wa dawa katika zahanati, hospitali za Serikali na vituo vya afya ni mgumu sana:-

- (a) Je, kwa nini Serikali isifungue maduka ya dawa muhimu Wilayani Bukombe?
- (b) Je, kwa nini mfuko huo unabagua magonjwa ya kugharamia?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Jumanne Luhahula, Mbunge wa Bukombe lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa maduka ya dawa muhimu ulianzishwa mwaka 2003 kwa madhumuni ya kurahisisha upatikanaji wa huduma za dawa kwa wananchi. Utekelezaji wa mpango huu uliana katika Mkoa wa Ruvuma. Hadi sasa tayari mpango huu upo katika Mikoa ya Mtwara, Rukwa na Morogoro. Azma yetu ni kuhakikisha kuwa mpango huu unaenezwa nchi nzima ifikapo mwaka 2010.

Kutokana na upungufu wa rasilimali watu pamoja na ufinyu wa fedha imekuwa vigumu kwa Wizara peke yake kuueneza mpango huu nchi nzima kwa haraka. Kwa sababu hiyo, jukumu la kuanzisha mpango wa maduka ya dawa muhimu katika Mikoa iliyosalia imekasimishwa kwa Mamlaka za Halmashauri. Tayari mafunzo na uhamasishaji umefanywa kwa Halmashauri za mikoa 16 ambako mpango huu bado haujaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Mbunge awasiliane na Halmashauri ya Wilaya yake ili kuona uwezekano wa kujumuisha mpango huu wakati wa kuandaa mpango kamambe wa huduma za afya wa Wilaya (*Council Comprehensive Health Plan*).

(b) Si kweli kwamba mfuko wa Bima ya Afya unabagua magonjwa ya kugharamia. Naomba kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge pamoja Bunge lako Tukufu kwamba Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya unagharamia magonjwa yote nchini isipokuwa magonjwa yanayoangukia katika makundi yafuatayo:-

1. Magonjwa ambayo yanashughulikiwa na mipango maalum ya Serikali kama vile kifua kikuu na UKIMWI. Hata hivyo, mfuko unalipia matibabu yote ya magonjwa nyemelezi.

2. Magonjwa yanayotokana na uvunjaji wa sheria kama utoaji haramu wa mimba, utumiaji wa pombe haramu na madawa ya kulevya.

3. Madhara yanayotokana na upasuaji wa urembo (*Cosmetic surgery*).

4. Aidha, mfuko haugharamii huduma ambazo kimsingi bado ni wajibu wa mwajiri kama:-

Gharama za usafiri wa kwenda na kurudi kwenye matibabu. Gharama za mazishi.

Fedha za kujikimu mtumishi anaposafiri kwenda kwenye matibabu ngazi ya rufaa na gharama za chakula.

MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA: Nashukuru kwa majibu. Swali la kwanza kwa kuwa katika majibu yake amesema ni mpango ambao 2010 watakuwa wamekamilisha nchi nzima na kwa kuwa anasema kwamba niwasiliane na Halmashauri yangu. Je, haoni kwamba ni jukumu la Serikali kuagiza Halmashauri hizo kwamba sasa uwekwe *Comprehensive Plan* katika *health*, jukumu la Serikali? (*Makofî*)

Pili na kwa kuwa ni mpango wao kamambe ifikapo 2010 nchi nzima maduka yawe yamekamilika. Anaweza akalihakikisha Bunge hili Tukufu kwamba kwenye Bajeti yake wametenga hela kiasi fulani kwa ajili ya mpango huu angalau ukaanzie huko Bukombe? (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi sana.

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza. Halmashauri zote zinafahamu kwamba zinapokuwa zinapanga mpango mkakati wao huwa wanatakiwa wajumuisha katika mambo haya. Hapa nimemwambia hivi Mheshimiwa Mbunge ili wakati anapokwenda kule aweze kuhakikisha kwamba hili analiona katika vikao vyake vya Halmashauri ndiyo maana

nimesema hivi. Lakini Serikali imeshatoa maagizo. Kwa hiyo, Halmashauri zote zinafahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Ni kwamba kama nilivyo sema kwamba Serikali ni kazi yetu na sasa hivi kuitia kwenye fedha ya *global fund round seven* fedha imetengwa ili kuweza kuhakikisha kwamba tunawafundisha hawa wataalam ambao watawafundisha wale watoa huduma. Lakini kitu ambacho nilitaka kusema tu ni kwamba suala la kufungua maduka ya dawa ni suala ambalo wananchi wenyewe kule katika maeneo wanatakiwa wafungue maduka ya dawa ili sisi Serikali tutawafundisha wale wanaotoa zile dawa na hii ndiyo ambayo sitagharamia. Lakini kama kule Bukombe hakuna duka la dawa, itakuwa ni vigumu. Kwa hiyo, namshauri pia Mheshimiwa Mbunge ahakikishe kwamba Bukombe wanafungua maduka ya dawa ili tuweze kuliteua duka hili ili wale watu wa Bima ya Afya waweze kupata dawa katika duka hilo.

Na. 184

Ujenzi wa Maeneo ya Fukwe za Bahari

MHE. JOB Y. NDUGAI (K.n.y. MHE. MGANA I. MSINDAI) aliuliza:-

Kwa kuwa ni wazi kwamba baadhi ya wananchi na wageni wanajenga nyumba binafsi na mahoteli ufukweni wanakiuka Sheria za Ujenzi fukweni ambapo badala ya kujenga umbali wa mita mia mbili zilizowekwa kisheria wengi wanajenga mpaka kugusa bahari hivyo kuwanyima haki wananchi wengi wanaotumia fukwe na kuharibu mazingira ya fukwe, mikoko, mazalia ya samaki na kadhalika:-

- (a) Je, Serikali inasemaje juu ya vitendo hivyo vya ukiukwaji wa sheria?
- (b) Je, Serikali inaweza kuheshimu sheria ambayo ni msumeno kwa kuwaondoa watu wenye makosa hayo ili kulinda fukwe zetu kwa faida ya vizazi vijavyo?
- (c) Je, Serikali itawachukulia hatua gani Maofisa Ardhi ambao wamekiuka Sheria kwa kuwapatia wahusika viwanja hivyo?

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Msindai, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inazo Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia mazingira ya maeneo ya fukwe. Sheria zinazosimamia uendelezaji wa maeneo ya fukwe ni pamoja na Sheria ya Ardhi Sura Na. 113, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004, Sheria ya Mipangomiji Na. 8 ya mwaka 2007 na Sheria ya

Usimamizi wa Maeneo ya Wazi Sura Na. 320. Aidha, ili kurahisisha utekelezaji wa sheria hizo, lilitolewa Tangazo la Serikali Na. 76 la mwaka 1992, ambalo pamoja na mambo mengine linaelekeza kuwa kila mara inapoandaliwa mipango ya kuendeleza ardhi inayopatikana na ufukwe wa Bahari hupana budi kuacha wazi ukanda wa mita 60, na kwa fukwe za maziwa mita 30. Maelekezo haya hayahusu uendelezaji uliokuwepo kabla ya tangazo hili.

Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za Miji na Wilaya tunaendelea kusimamia na kubaini uendelezaji unaofanywa kinyume na Sheria na ikibainika kuwa kuna ukiukwaji wa Sheria hizo, wanaohusika sharti wachukuliwe hatua za kisheria na za kinidhamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali mara zote imekuwa ikiheshimu sheria za nchi. Hata hivyo, mapungufu yanayojiteza katika usimamizi wa sheria za ardhi na mipangomiji yanababishwa na watumishi wachache wanaofanya kazi bila ya kuzingatia sheria na maadili ya taaluma zao. Udhaifu wa eneo hili umetungiwa sheria ya kudhibiti maadili taaluma ya Maafisa Mipangomiji Na. 7 ya mwaka 2007. Sheria hii itasaidia kudhibiti mianya ya ukiukaji wa sheria zikiwemo zinazosimamia viwanja katika fukwe za Bahari na Maziwa.

MHE. JOB Y. NDUGAI: Nakushukuru Mheshimiwa Naibu Spika, kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza ikiwa ni pamoja na kushukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Kwa kuwa ni kweli kuwa kuna upungufu mkubwa katika utekelezaji wa Sheria za Mipangomiji na Sheria za Ardhi kwa wananchi wengi kujenga hovyo, holela pemberi mwa bahari, pemberi mwa maziwa, pemberi mwa mito na hata katika miji yetu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kule Kongwa, Kibaigwa, Kongwa mjini na miji mingine. Je, Serikali inaijiendaaje ili kutoingia katika gharama kubwa sana ya kulipa fidia kwa hawa ambao wanavamia kila mahali kinyume na mipangomiji na Sheria ya Ardhi? (*Makofi*)

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hapa la ujengaji holela ni kwa sababu ya kasi ndogo ya upimaji wa viwanja mijini. Hilo Ndilo linalosababisha wananchi wanajenga katika maeneo ambayo hayajapimwa wanajenga holela. Wale wanaovamia ni kwamba eneo limepimwa, amevamia. Huyo halipwi fidia. Sheria inasema aondolewe. Lakini wale ambao wanajenga maeneo ambayo hayajapimwa ndilo tatizo ambalo sasa hivi Wizara yangu tukishirikiana na Halmashauri za Miji kwa sababu upimaji wa viwanja ni suala la Halmashauri za Miji. Tunajitahidi wao na sisi Wizara kutafuta fedha ili kuongeza kasi ya kupima viwanja. Kwa hiyo, changamoto iliyoko ni kuongeza kasi ya kupima viwanja. Halmashauri na Wizara yangu tunatafuta fedha kwa ajili ya kuongeza kasi na maelezo zaidi nitayatoa wakati wa hotuba ya Bajeti yangu.

Na. 185

Uchakavu wa Magari ya Mizigo na Abiria

MHE. JUMA SAID OMAR aliuliza:-

Kwa kuwa, uchakavu wa magari ya abiria na mizigo ni mionganoni mwa sababu zinazochangia kusababisha ajali na vifo kwa wananchi wengi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa makusudi wa kupambana na tatizo hili?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Said Omar, Mbunge wa Mtambwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kuwa uchakavu wa magari ya abiria na mizigo ni mionganoni mwa sababu zinazochangia kusababisha ajali na vifo kwa wananchi wengi. Ili kupambana na tatizo hili, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na *SUMATRA, TBS*, wamiliki wa vyombo vyaya usafirishaji, vyama vyaya madereva na wadau wa usalama barabarani, limekuwa linatekeleza yafuatayo:-

- (i) Kusimamia na kuhakikisha kwamba sheria za usalama barabarani zinafuatwa na watumiaji wote wa barabara.
- (ii) Kukagua ubovu wa magari ya abiria na mizigo na kuhakikisha kuwa magari mabovu hayaruhusiwi kutembea barabarani.
- (iii) Kuhakikisha kuwa viwango vyaya ubora wa magari vilivyowekwa na *TBS* vinafuatwa na wamiliki wote wa magari hasa uundaji wa *body*, viti na matairi imara.
- (iv) Kuboresha mazingira ya utendaji wa askari wa kikosi cha usalama barabarani kwa kuwapatia vifaa vyaya kisasa kama vile *speed radar*, magari na pikipiki kwa ajili ya doria.
- (v) Kufanya doria kwenye barabara kuu, *highway*, ili kuwabaini madereva wanaoendesha magari mabovu na kuwachukulia hatua za kisheria; na mwisho.
- (vi) Kuendeleza elimu ya usalama barabarani kwa madereva na wamiliki wa magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la ukaguzi wa magari ya abiria na yale ya mizigo yakiwemo, ambayo yanaendelea kutoa huduma ni indelevu na la kudumu. Hivyo kila taasisi inaendelea kutimiza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria za Usafirishaji, Usalama Barabarani, Sheria ya Viwango na Kanuni nyingine za usalama wa barabarani kwa lengo la kulinda usalama wa raia na mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kuchukua fursa hii kuwakumbusha na kuwaasa watumiaji wote wa barabara wakiwemo madereva, abiria, watembea kwa miguu, wafanya biashara na wamiliki wa magari kufuata taratibu na Kanuni za usalama barabarani na matumizi bora ya barabara ili kupunguza wimbi la ajali za barabarani. Naomba tuthamini maisha yetu.

MHE. JUMA SAID OMAR: Ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa mionganoni mwa magari machakavu ni mabasi ya Bunge ambayo yamefikia hatua sasa yanatoa moshi mwangi. Je, Serikali haioni kwamba kuendelea kuyatumia mabasi hayo ni kuhatarisha maisha ya Wabunge pamoja na wafanyakazi wa Bunge? (*Makofî*)

Swali la pili. Je, Serikali inangojea nini au mpaka maafa yatokee ndiyo hatua zichukuliwe? Ahsante. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Haya Mheshimiwa Naibu Waziri, unajua habari hizo? (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba yapo magari barabarani ambayo mengine ni machakavu na mengine ni mabovu sana.

NAIBU SPIKA: Naomba ujibu kwa kifupi maana yake ni swali fupi sana hili.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI: Sikusikii Mheshimiwa Naibu Spika.

NAIBU SPIKA: Nasema ujibu kwa kifupi sana.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI: Ndiyo nilikuwa naanza kujibu hivyo. *SUMATRA* ndiyo chombo ambacho kipo kutazama viwango vya magari na tunawasiliana nao na sasa hivi *regulations* za *SUMATRA* zitaletwa ambazo zitawezza kuhakikisha kwamba hayo unayoyasema Mheshimiwa Mbunge yatatizamwa.

Aidha kuhusu maafa hayo ni kweli na ndiyo maana nimejibu katika jibu langu la msingi kwa swali lako la msingi kwamba tunawaomba madereva wote na tunawaomba wamiliki wa magari kwamba wazingatie hivyo.

Lakini pia sisi upande wa Sheria tutatimiza wajibu wetu kuhakikisha kwamba haya magari machakavu hayako barabarani. Kwa hiyo, kwa hatua hizo ni kupunguza athari ambazo zinazotokea katika barabara zetu.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mmiliki wa mabasi ya Bunge ni Katibu wa Bunge. Tunaendelea na swali lililobakia.

Ukuaji wa Kilimo kwa Asilimia 20

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA aliuliza:-

Kwa kuwa, ili uchumi wetu ukue kwa kiwango cha asilimia 10 ifikapo mwaka 2010 lazima kilimo kikue kufikia angalau asilimia 20 ifikapo mwaka huo; na kwa kuwa, moja kati ya hatua zinazopaswa kuchukuliwa na Serikali ni pamoja na kumpunguzia mkulima, hasa mwanamke, suluba ya kazi za kubeba mizigo, kutwanga, kukoboa na kusaga nafaka kwa kuwapatia nyenzo muhimu za kisasa za kufanya kazi hizo:-

- (a) Je, Serikali imeshaanza kutekeleza zoezi la kusimamia, kuwawezesha na kushawishi kuenezwa kwa utengenezaji/upatikanaji wa mikokoteni ya kuvutwa na wanyama, vinu vya kisasa vya kukobolea na kusagia nafaka?
- (b) Je, kwa nini wakulima wa Mpunga wa Kata ya Mahurunga, Mtwara Vijijini, hawajawezeshwa kupata kinu cha kukobolea mpunga?
- (c) Je, kwa nini mradi wa ASDP unafadhili kilimo cha umwagiliaji kwa lengo la kuongeza uzalishaji pasipo kujali ni jinsi gani mpunga huo utakobolewa?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri za Wilaya 54, zimenufaika na mpango wa Wizara wa kuhimiza matumizi ya wanyamakazi katika kilimo kwa kukarabati vituo vya maksai 55 na kuvipatia zana timilifu kwa ajili ya kufanya maonesho na kutoa mafunzo ya matumizi bora ya wanyamakazi na zana zake.

Kituo cha wanyamakazi cha Mtawanya Wilaya ya Mtwara Vijijini kilikarabatiwa kwa shilingi 9,650,000/= na kupatiwa zana zenye thamani ya shilingi 3,930,000/= kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo kwa wakulima.

Aidha, kuna jumla ya wanayamakazi 4,657,477 kwenye kaya 1,105,832 na mikokoteni 86,217 ya wanyamakazi nchini. Kuna karakana binafsi katika kila Mkoa zinazoweza kutengeneza vinu vidogo vya kusaga na kukoboa nafaka. Yapo makampuni binafsi na taasisi kama vile *SEAZ, INTERMEC, NANDRA, SIDO, CARMATEC* na

TEMDO yenyewe uwezo wa kutengeneza zana za kukokotwa na wanyamakazi na vinu vidogo na vya kati vya kukoboa na kusaga nafaka. Aidha, vipo vinu vikubwa na vya kisasa vya kukoboa mpunga katika maeneo ya Kapunga, Dakawa, Ruvu, *Lower Moshi*, Ulanga, Mpanda, Igunga na Dar-es-Salaam.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo, *Agricultural Sector development Program – ASDP*, imeweka mfumo wa kuendeleza kilimo katika ngazi ya Wilaya kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya, *District Agricultural Development Plans – DADPs*. Kupitia *DADPs* miradi mbali mbali huibuliwa na walengwa.

Timu za wawezeshaji za Wilaya na Kata, zinafanya kazi ya kuwawezesha walengwa kuibua miradi ya maendeleo kulingana na fursa za uzalishaji na uchumi zilizopo vijijini. Fursa za uchumi ni pamoja na miradi ya kuongeza thamani kwa mazao yenyewe fursa kubwa ya uzalishaji. Hivyo, wakulima wa Kata ya Mahurunga wanashauriwa kuitumia fursa hiyo kuibua miradi ya vinu vya kukoboa mpunga kupitia *DADPs* ya wilaya yao.

(c)Mheshimiwa Naibu Spika, Programu ya *ASDP* hufadhili shughuli zote za maendeleo zinazoibuliwa chini ya *DADPs*. Kwa msingi huo, Serikali imeweka fursa mbalimbali za kuwasaidia wakulima ikiwa ni pamoja kutoa mafunzo na maelekezo ya kuibua miradi kupitia *DADPs*.

Hivyo, si kweli kwamba mradi wa *ASDP* unafadhili kilimo cha umwagiliaji kwa lengo la kuongeza uzalishaji pasipo kujali ni jinsi gani mpunga huo utakobolewa bali inategemea kama *DADPs* za maeneo hayo zimejumuisha pia vinu vya kukoboa na kusaga nafaka kwa lengo la kuongeza thamani.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa, pamoja na jitihada zote zinazofanywa na Serikali kupitia *DADPs* bado tunaona kwamba ukuaji kilimo ni 4% kwa mwaka 2007 na hili ni ongezeko la 0.2% kutoka mwaka 2006. Je, Serikali inaweza kutuambia kwamba tatizo hasa ni nini ambalo linasababisha kasi ya ukuwaji wa kilimo kuwa ndogo kiasi hiki?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili ni kwamba, Serikali inatarajia hasa ni lini ambapo tunaweza tukafikia ukuwaji wa kilimo wa 20% kama ambavyo imepangwa? Ahsante.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Anastazia Wambura, kwa kifupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ukuaji wa sekta ya kilimo unategemea mambo mengi ambayo hayawezi kuelezwaa kwa kifupi. Kwahiyoo ninamwomba Mheshimiwa Abastazia

atuvumilie ili tutakapotoa hotuba yetu tuweze kueleza kwa kirefu kwanini kilimo kinakuwa kwa asilimia ndogo kuliko kilivyotazamiwa. (*Makofi*).

NAIBU SPIKA: Nashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, mana mimi nawajua Mawaziri wanaojibu kwa kirefu na Wabunge wanaouliza maswali kwa kutoa hotuba. Kwahiylo tunafahamiana sisi wote. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, maswali yameisha na....

KUHUSU UTARATIBU

MHE. DR. JOHN S. MALECELA: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu. Ningombwa kuomba Mwongozo wako, chini ya Ibara Namba 68(7). Naona kwamba jana tuligawiwa ripoti ya Bomani, mtu ambaye alijulishwa hapa kwamba ni Mtu Mashuhuri, na wote waliokuwa katika Tume ile ni watu Mashuhuri, na ripoti hii ina mambo mengi sana ya muhimu na mimi ninafikiri labda ndio pengine wakati muafaka wa nchi yetu kupata sera mpya ya madini.

Kwahiylo, kutokana na kuomba huo Mwongozo, ningekwenda kwenye ibara namba 37(6), kuomba kwamba ripoti hiyo ili tuifanyie haki ipewe muda wake iwe *debated*. Ili tuweze kutoa maoni yetu na kutoa mapendelekezo yetu. Kwahiylo naomba kutoa hoja chini ya kifungu 37(6) baada ya kupata muongozo wako. (*Makofi*).

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, jana wakati Mheshimiwa Spika, yuko mezani bahati nzuri yeye alikuwa na nakala ya taarifa inayozungumzwa lakini kwenye *Order Paper* yetu hatukuwa nayo hiyo. Kwasababu ya mvuto wa suala zima la swali la madini kwamba ni suala linaonekana la kitaifa, Spika akaomba iwasilishwe mezani jana, lakini haikuwa kwenye *Order Paper* na hivyo ingekuwa kwenye *Order Paper*, ingekuwa rahisi watu kusema taarifa ijadiliwe janajana ileile. Sasa haikufanyika hivyo lakini halikuharibika neno.

Kwa hiyo, ametumia kifungu cha 37(4) ndio kinasema kuwasilisha hotuba mezani na mtu yejote anaweza kusimama na kusema tunaomba hotuba ijadiliwe, na Spika, atasema ipangiwa muda wake. Na kwasababu imeungwa mkono na watu wengi sana humu ndani, kwahiylo tunafikiri tutapata muda wakati mzuri wa kuweza kujadili. Kwasababu kama hivi sasa tuna mambo mengi katika Wizara hii. Kwahiylo naweza kuzamia kwenye hii, haiwezekani kwa mujibu wa utaratibu wetu. Kwahiylo Mheshimiwa Mbunge, tutaangalia muda muafaka wa kuweza kujadili hoja hiyo. (*Makofi*).

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni mezani kwetu. Tuna wageni wa Mheshimiwa Ngeleja, Waziri wa Nishati na Madini. Hawa ni *Tanzania Chamber of Minerals and Energy*, kwa kifupi *TCME*. Naomba wasimame waliko wote, manaake wako wengi. Kama kuna *members* hao wasimame. Kuna Kabanga Mikel, kuna *Geita Gold Mine*, kuna *Resolute Tanzania*, kuna *Barric*, kuna *Tanzania 2000*, kuna *Engineering Association Ltd*. Asanteni sana, tunategemea mutaingalia *industry* hii vizuri na iweze kutoa manufaa kwa Watanzania. Karibu sana.

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Kahika Teleke, ni bwana Majid Mwaga, Mjumbe wa Kamati ya Siasa Mkoa wa Arusha, sijui yuko wapi. Karibu sana. Tuna wageni kutoka Chuo Kikuu cha Tumaini Iringa, naomba wasimame waliko, Chuo Kikuu cha Tumaini, ahsante sana. Kuna wageni wa *Professor Raphael Mwalyosi*, Mheshimiwa Gaudencia na Mwakipokile, Madiwani kutoka Ludewa. Waheshimiwa Madiwani, wako wapi? Ahsante sana, karibuni.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Fatuma Fereji, hawa ni watoto wake wasimame walipo. Watoto wa Mheshimiwa Fereji, naona wamechelewa. Kuna wageni wa Mheshimiwa *Dr. Ibrahim Msabaha*, hawa ni Mwenyekiti wa *CCM* Wilaya ya Kibaha Vijijiini, yuko wapi? Tuna Mheshimiwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, naona wamechelewa. Kuna wageni wa Mheshimiwa Ester Nyawazwa, naomba wasimame walipo, kuna dada yake na mdogo wake. Karibuni sana kwa kuja kumtembelea Mheshimiwa Nyawazwa. Tuna wageni wa Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, ni Mtoto wake na binamu yake, wako wapi wageni wa Mheshimiwa Zarafi? Karibuni sana. Tuna wageni wa Mheshimiwa Janeth Kahama, yupo dada yake na wajukuu zake, wako wapi? Ahsante karibuni sana. Tuna wageni wa Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, ni mama na watoto wake, wako wapi? Karibuni sana.

Tuna Ujumbe wa watu 24 kutoka *SRL International Uganda, Tanzania Branch*. *Can we, wako wapi hawa ndugu zetu? Karibuni sana, we are pleased to have you in this Public Gallery, you are all welcome.* Tuna wanafunzi 50 kutoka Dodoma Sekondari na walimu wao, wako wapi Dodoma Sekondari? Karibuni sana, Bunge liko kwenu kwahiyo mnakaribishwa kila wakati. Tuna wanafunzi 50, kutoka *City Secondary School*, hii iko wapi sijui? Karibuni sana, hata jana wengine tuliwaona. Ni lazima itakuwa Dodoma tu.

Kuna wanafunzi 15 kutoka Chuo cha Ardhi, wako wapi? Wanafunzi kutoka Chuo cha Ardhi? Hawakufika. Tuna Mheshimiwa Mama Kam, ye ye alikuwa Mbunge Mwenzetu hapa kwa miaka mingi. Alikuwa Mwenyekiti wa Chama cha Wabunge Wanawake, wa Bunge wote *TWPG*, sasahivi nadhani ndio Mkuu wa *Mama Clementina Foundation*. Nadhani ameongozana na wafanyakazi 20, wapo? Wasimame walipo, ahsante. (*Makofi*).

Karibu sana mama, tunakukumbuka. Na tunakumbuka matokeo ya kuweza kujenga Chama hiki cha Wabunge Wanawake na sasa kiko *very strong*. Uliacha wanawake 20, sasa wako 98 na wanatafuta 50/50, wengine wanasesma, karibu sana, ahsante sana.

Shughuli za kazi. Waheshimiwa Wabunge, jana tulipaswa kukutana na Mheshimiwa *Dr. Shija*, ambaye ni Katibu Mkuu wa *CPA International*. Sasa bahati mbaya wakati tulioutangaza ulikuwa kidogo haukuwa mzuri, wengi walikuwa hawapo. Kwa hiyo, sasa tunaomba Wajumbe wa Kamati zifuatazo saa 4.30 wakutane kwenye Ukumbi wa Pius Msekwa. Ni Kamati ya Mambo ya Nje na Ulinzi na Usalama, wajumbe wote.

Kamati ya Huduma za Jamii, wajumbe wote na Kamati ya Mazingira Maliasili, wajumbe wote na Kamati ya Masuala ya *UKIMWI*, wote wajumbe hao wanaombwa wakutane saa 4.30 Ukumbi wa Pius Msekwa. Tafadhali naomba msikose, kutakuwa na mazungumzo kidogo, kwasababu sisi ni *Branch* na mwaka kesho tutakuwa wageni wa Mkutano Mkuu, ambaye yeche na *Secretary General*, ni vizuri tukajua habari hizi. Kwahiyio, naomba Wenyeviti, na wajumbe wote wahudhurie kikao hicho saa 4.30.

Halafu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali, Mheshimiwa John Cheyo, yeche anaomba wajumbe wa Kamati yake ya *PAC*, kuwa watakuwa na kikao tarehe 9 Julai, 2008 saa 5.0 katika chumba namba 231.

Kwahiyio, ni Kamati ya *PAC* saa 5.00 chumba namba 231, lakini pia ule mkutano wa *CPA*, na Wabunge wengine wanaopenda kushiriki pale wanaweza kushiriki itakuwa ni kikao cha muda mfupi sana. Kwahiyio munakaribishwa pale.

Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyosema orodha yetu ya wachangiaji ni kubwa sana na hawatakuwa wengi wa kutosha na ni nia yetu kwamba asubuhi hii tumalize wachangiaji ili jioni Waziri na Naibu wake waanze kutoa majibu. Kwa hiyo, kwasababu pia na mimi napaswa kushiriki kwenye ugeni huu, Mheshimiwa Spika, atakuja kuchukua Kiti chake. Mheshimiwa Spika (*Makofî*).

Hapa Spika (Mhe. Samueli J. Sitta) Alikalia Kiti

SPIKA: Ahsante sana Waheshimiwa, kama ambavyo alikuwa anatangaza Mheshimiwa Naibu Spika, orodha ya wachangiaji ni 34 na haitawezekana kwa kweli kuwafikia wote lakini tutajitahidi.

Ukiwa na mchango amba si wakurudiarudia na watu wakachukua muda mfupi badala ya kumaliza dakika zote 15, tutapata upana mzuri zaidi wa mawazo.

Kwahiyio, wachangiaji wa kwanza katika orodha yangu, niwataje wanne. Kwanza ni Mheshimiwa Emmanuel Jumanne Luhahula, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama na Mheshimiwa Chrostopher Ole-Sendeka. Tunaanza na Mheshimiwa Emmanuel Luhahula.

Aah, kuna Kauli ya Mawaziri, samahani sana. Katibu endelea na *Order Paper*, kwa shughuli hiyo.

KAULI YA WAZIRI

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, toleo la mwaka 2007, kanuni namba 49, naomba kutoa kauli ya Serikali kuhusu utekelezaji wa miradi ya maji Vijijini kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, tangu nchi yetu ipate uhuru, serikali imekuwa ikitekeleza sera na mikakati mbalimbali kwa lengo la kuwapatia wananchi huduma ya maji. Programu ya Maji Vijijini ya miaka 20 ya 1971 mpaka 1991 ilihusu utekelezaji wa miradi mingi ya maji iliyojengwa kwa gharama ya Serikali na wafadhili. Serikali ilikuwa ikibuni miradi na kuisanifu, kuitekeleza na kuiendesha, miradi mingi iliyojengwa wakati ule haikuwa endelevu. Kwasababu hiyo lengo la kitaifa la kuwapatia wananchi wote huduma ya maji katika umbali usiozidi mita 400 ifikapo mwaka 2002 hakika lisingeweza kufikiwa.

Baada ya kubaini hilo mwaka 1991, Serikali iliandaa sera ya maji ambayo ilitamka kwamba kila mwananchi achangie sehemu ya gharama za uendeshaji wa miradi ya maji. Tathmini ya sera ya maji ya mwaka 1991 ambayo ilifanyika mwaka 1997 ilibaini kuwa miradi ya maji ingekuwa endelevu, iwapo tu wananchi wangeshiriki katika kuibua na katika ujenzi na uendeshaji wa miradi hiyo.

Msingi mmoja muhimu wa Sera ya Maji ya mwaka 2002 ni ushirikishaji wa wananchi vijijini mmoja mmoja katika miradi ya maji na vilevile katika vikundi. Msingi mwingine muhimu wa sera ya maji ya mwaka 2002 ni utekelezaji wa azma ya serikali ya kupeleka madaraka kwa wananchi, yaani *Decentralization by Devolution au D by D*.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha utekelezaji wa Sera ya Maji na kuiwezesha sekta ya maji kuchangia ipasavyo katika malengo ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umasikini Tanzania, Malengo ya Milenia na Dira ya Taifa ya Maendeleo, Serikali imeandaa mkakati wa kitaifa wa uendelezaji wa sekta ya maji na programu ya maendeleo ya sekta ya maji.

Maeleo yafuatayo ya utekelezaji wa mpango wa Serikali, wa kuwapatia wananchi wa vijijini maji safi, maji salama, yanajikita katika misingi hiyo.

Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 2002 miradi ya maji na usafi wa mazingira vijijini imekuwa ikitekelezwa na wananchi na wadau wengine wa sekta ambao wanawenza kujumuishwa katika makundi yafuatayo:-

1. Mheshimiwa Spika, wananchi wenyewe. Ili kukabiliana na changamoto ya kukosekana kwa maji, mwananchi mmoja mmoja na kwenye vikundi katika maeneo mbalimbali wanatekeleza miradi ambayo wanaigharimia wao wenyewe.
2. Mheshimiwa Spika, Taasisi zisizo za kiserikali. Taasisi zisizo za kiserikali pamoja na madehebu mbalimbali yanaendeleza miradi mbalimbali ya kuwapataia wananchi maji, inayofadhiliwa na wao na wahisani.
3. Mheshimiwa Spika, Halmashauri. Kwa kutumia ruzuku ya Serikali za Mitaa, *Local Government Capital Development Grants*, na vyanzo vingine vya mapato, Halmashauri zimekuwa zikitekeleza miradi ya maji kama zinavyotekeliza mipango mingine ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji na usafi wa mazingira vijijini, ulianza kutekelezwa mwaka 2002 kwa mkopo nafuu wa Benki ya Dunia, wa dola za Marekani 26,000,000/= na mchango wa serikali na walengwa wa dola milioni 1.7.

Utekelezaji ulianza katika Wilaya tatu za Mpwapwa, Kilosa na Rufiji, kama majoribio ya utekelezaji wa Sera ya Maji ya mwaka 2002. Mwaka 2004, mradi uliendelezwa katika Wilaya nyingine 9 za Handeni, Igunga, Iramba, Kiteto, Kondoa, Kongwa, Manyoni, Morogoro na Singida.

Wilaya ziliongezeka kuwa 14, baada ya Wilaya ya Handeni na Morogoro, kugawanywa na kuanzisha Wilaya mpya za Kilindi na Mvomero, sawia. Utekelezaji wa mradi huo umehusu maeneo muhimu 4 yafuatayo:-

- (i) Utendaji katika ngazi ya wilaya.
- (ii) Ujenzi wa miradi ya maji safi na mazingira vijijini.
- (iii) Kuimarisha ofisi zinazohusika katika ngazi za mikoa na wilaya.
- (iv) Kuandaa programu ya maji safi na usafi wa mazingira vijijini kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji na usafi wa mazingira muda wake umekwisha mwezi Juni mwaka 2008. Kuanzia mwaka 2008/2009 miradi ilioanzishwa chini ya mradi huo itakamilishwa au kuendelezwa chini ya programu ndogo ya maji na usafi wa mazingira ambayo ni sehemu ya programu ya maendeleo ya sekta ya maji. Uzoefu uliopatikana katika utekelezaji wa mradi wa maji na usafi wa mazingira vijijini katika wilaya hizo 14, hususan katika manunuvi na usimamizi wa wataalam, washauri na wakandarasi, utasaidia sana katika kufanikisha utekelezaji wa program hiyo.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, iliandaliwa kwa miaka 3 na kuanza kutekelezwa rasmi mwaka 2006/2007. Programu hiyo ina programu ndogo nne ambazo ni:-

- (i) Uendelezaji wa rasilimali za maji.
- (ii) Huduma ya maji na uondoaji wa maji taka mijini.
- (iii) Huduma ya maji na usafi wa mazingira vijijini.
- (iv) Uimarishaji wa taasisi zenye majukumu muhimu katika sekta ya maji.

Mheshimiwa Spika, makubaliano na washirika wa maendeleo. Wakati wa kuandaa programu hiyo Serikali ilikuabaliana mambo yafuatayo na washirika wa maendeleo katika sekta ya maji, kuhusu miradi yote ya maji itakayotekelzwa kwa fedha wanazozitoa:-

(i) Taratibu za manunuzi za Benki ya Dunia, zitatumika katika manunuzi yenye gharama kubwa na ya kimataifa.

(ii) Taratibu za manunuzi za sheria ya manunuzi ya umma ya 2004, zitatumika kwa manunuzi ya kitaifa.

(iii) Fedha za utekelezaji wa miradi ya maji na usafi wa mazingira vijijini zitatumwa na Wizara ya Fedha na Uchumi, moja kwa moja kwenye mafungu ya mikoa na halmashauri bila kupitia Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

(iv) Halmashauri zitawasilisha *TAMISEMI* na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, taarifa za utekelezaji na matumizi ya fedha kila robo mwaka.

Mheshimiwa Spika, programu ndogo ya maji na usafi wa mazingira vijijini. Tangu mwaka 2007/2008 programu ndogo ya maji na usafi wa mazingira imekuwa ikitekelezwa kupitia aina 3 za miradi. Kwanza mradi wa maji na usafi wa mazingira vijijini ambao nimeshauelezea. Pili miradi mikubwa ya maji vijijini, yaani vijiji 10 katika kila Halmashauri na tatu, miradi inayoleta matokeo ya haraka ya *quickwins*.

Mheshimiwa Spika, miradi mikubwa vijijini na miradi inayoleta matokeo ya haraka. Katika kutekeleza programu hiyo ndogo, majukumu ya taasisi zinazohusika ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika ngazi ya Serikali za Mitaa, Halmashauri zinapanga na kutekeleza miradi katika Wilaya, kwa kuwatumia wataalamu, washauri na wakandarasi, chini ya mikataba ambayo Halmashauri zenyewe zimeingia na washauri na wakandarasi hao.

Mheshimiwa Spika, katika ngazi ya Mkoa, Sekretarieti za mkoa zinafuutilia na kusimamia utekelezaji katika ngazi ya wilaya.

Mheshimiwa Spika, katika ngazi ya Taifa, Wizara ya Maji na Umwagiliaji, inaandaa miongozo na kuratibu programu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Fedha na Uchumi, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, na washirika wa maendeleo.

Vilevile Wizara hufuutilia upatikanaji wa fedha kutoka Hazina na Washirika wa maendeleo. Ni jukumu la Wizara, kuhakikisha kwamba fedha zinazopatikana zinatolewa kwa Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa kulingana na utekelezaji wa mipango ya utekelezaji wa taasisi hizo.

Mheshimiwa Spika, wahandisi wa maji. Wakati wa maandalizi ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya maji, ilibainika kuwa baadhi ya Halmashauri na Sekretariet za Mkoa, zilikuwa hazina wahandisi wa maji. Mwezi Novemba, mwaka 2006, Wizara ya Maji iliajiri wahandisi 96 na kuwakabidhi kwa Halmashauri na Sekretariet za mikoa husika ili kuziongezea uwezo wa kutekeleza na kusimamia programu.

Wahandisi 75 walipangiwa kazi kwenye Halmashauri, 17 kwenye Sekretarieti za mikoa minne kwenye miradi ya maji ya kitaifa. Hadi mwezi Juni mwaka 2008, wahandisi 37 walikwisha ajiriwa na Halmashauri na 14 walikuwa wameacha kazi.

Taratibu za Halmashauri kuwaajiri wahandisi waliobaki zinaendelea na inatarajiwa kuwa wataweza kuajiriwa katika mwaka wa fedha wa 2008/2009. wahandisi hao wataendelea kulipwa na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, chini ya mikataba ya muda hadi mwezi Oktoba, mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, kupatikana kwa wataalamu washauri. Sasa naomba nitoe maelezo ya ziada kuhusu makubaliano niliyoyataja yanayohusu taratibu za manunuzi ambayo utekelezaji wake umechelewesha utekelezaji wa miradi ya vijiji 10 katika kila Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, juhudzi za kuwaajiri wataalamu washauri wa kusanifu miradi ya maji chini ya mikataba na Halmashauri zote nchini zilianza mwaka 2005 kwa kutumia taratibu za Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004. Mwezi Februari mwaka 2007, baadhi ya kampuni za wataalamu washauri zilionyesha nia ya kusanifu miradi hiyo kufanyiwa tathmini.

Wizara ya Maji na Umwagiliaji, iliiomba Benki ya Dunia, kutoa ridhaa ili Kampuni zilizobainika kuwa na uwezo zitakiwe kuingia mikataba na Halmashauri.

Mwezi Aprili, mwaka 2007, Benki ya Dunia, ilishauri zoezi zima la kuwatafuta wataalamu washauri lianze upya kwa kufuata taratibu za manunuzi za Benki hiyo, kutohana na kwamba wataalamu hao wangefanya kazi chini ya programu mpya, yaani programu ya maendeleo ya sekta ya maji ambayo inafadhiliwa na Benki ya Dunia na wahisani wengine.

Wahisani wote wa sekta ya maji waliunga mkono ushauri huo wa Benki ya Dunia. Baada ya hapo mwezi Septemba mwaka 2007, Serikali ilitoa tangazo kwa niaba ya Halmashauri zote, kuzitaka kampuni za wataalamu washauri ziwasilishe upya maombi yao kwa Halmashauri. Mwezi Novemba, mwaka 2007, Serikali ilitoa mafunzo kwa Maafisa wa Halmashauri zote nchini kuhusu taratibu za manunuzi za Benki ya Dunia.

Baada ya mafunzo hayo Halmashauri zote zilianza zoezi la kufanya tathmini ya kampuni za wataalamu washauri zilizoonesha nia ya kusanifu miradi ya maji na kuwasilisha tathmini zao Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, kulingana na taratibu za Benki ya Dunia, za kutafuta wataalamu washauri, kampuni sita zinatakiwa kushindanishwa kwa kila Halmashauri na kati ya hizo kampuni zinazotoka nchi moja hazitakiwi kuwa zaidi ya mbili. Hadi sasa zoezi la kuwapata wataalamu washauri limefikia hatua zifuatazi kwa halamashauri mbalimbali:-

(i)Mheshimiwa Spika, Halmashauri sita tu ndizo zilizotimiza kikamilifu masharti yote ya Benki ya Dunia. Halamashauri hizo ni Arusha, Kasulu, Manispaa ya Kinondoni, Manispaa ya Moshi, Rombo na Manispaa ya Temeke.

(ii)Halmashauri tisa zimependekeza kampuni sita lakini hazikutimiza sharti la kutokuwa na zaidi ya kampuni mbili kutoka nchi moja.

(iii)Halmashauri 49, zimependekeza kampuni kati ya tatu na tano.

(iv)Halmashauri 33 hazikupata idadi ya kutosha ya kampuni za kupendekeza. Zilipata kati ya kampuni moja na kampuni mbili.

(v)Halmashauri 35 hazikuzingatia taratibu za kutathmini kampuni za wataalamu washauri hivyo zimelazimika kurudia tathmini zao, na kati ya hizo 18 zimeshawasilisha kwetu tathmini mpya.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua hali halisi na ukweli kwamba kwa Halmashauri nyingi taratibu za Benki ya Dunia hazitekelezeki, kutokana hasa na ugumu wa kupata idadi inayotakiwa ya kampuni za kushindanisha zabuni hizo, Serikali iliomba Benki ya Dunia, ilegeze masharti yake.

Mheshimiwa Spika, ninayo furaha kulitaarifu Bunge lako Tukufu, kwamba jana tarehe 8 Julai, 2008 Benki ya Dunia, imekubali kulegeza masharti hayo kwa Halmashauri 82 hivyo kuashiria mwanzo wa utekelezaji wa mradi huu ambao tumeungoja kwa muda mrefu. Orodha ya Halmashauri hizo imeambatanishwa kwenye taarifa hii na ninaomba isomeke katika *Hansard* kama sehemu ya kauli hii, (*Tazama Kiambatanisho A*).

Hatua inayofuata kwa halmashauri hizo ni kuzielekeza kampuni za wataalamu washauri ziandae mapendekezo ya usanifu wa miradi kwa ajili ya utekelezaji. Halmashauri 17, zinaendelea kurudia tathmini ya Kampuni zilizopeleka maombi yao ya kufanya kazi za ushauri. Aidha Halmashauri 33 zitarudia kutangaza ili kupata maombi mapya ya kampuni zitakazofanya kazi hizo za ushauri. (*Makofi*).

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi yenyе matokeo ya haraka. Sambamba na juhudи za kuwapatia wataalamu washauri hizo Halmashauri, watakaofanya usanifu na kuandaa zabuni kwa ajili ya miradi ya maji katika vijiji 10 katika kila Halmashauri, Serikali imeendelea kutekeleza programu ndogo ya maji na usafi wa mazingira vijijini kulingana na mipango ya Halmashauri zenyewe ya kujenga na kukarabati miradi ya maji ambayo haihitaji utaalamu wa kiwango cha juu katika usanifu na ujenzi.

Miradi hii ni ile inayotarajiwa kuleta matokeo ya haraka ya *quickwins*. Ili kutekeleza miradi hiyo, Mwishoni mwa mwezi Juni mwaka 2007, serikali ilituma shilingi bilioni 19.25 kwenye Halmashauri na Sekretarieti za mikoa.

Fedha hizo zinatokana na mkopo wenye masharti nafuu kutoka Benki ya Maendeleo ya Asfrika (*ADB*). Kati ya hizo shilingi bilioni 18.9 zilitumwa kwa Halmashauri zote na shilingi milioni 353.5 zilipelekwa kwenye Sekretarieti za Mikoa.

Kati ya Halmashauri 121 zilizokuwepo wakati ule, Halmashauri 84 ziliwa zimetimiza masharti ya mfumo wa utoaji wa ruzuku ya maendeleo kwa Serikali za Mitaa. Halmashauri hizo zilipewa fedha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miradi ya maji na kujijengea uwezo. Halmashauri 37 ambazo hazikuweza kutimiza masharti ya kupewa ruzuku, zilipewa fedha kwa ajili ya kujijengea uwezo tu, fedha hizo ziliwa zikitumika katika mwaka uliopita wa 2007/2008 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya *Quick Wins*. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2008, Halmashauri ziliwa bado hazijatumia shilingi bilioni sita au zaidi ya 30% ya fedha zilizotumwa.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri nyingi hazijatumia fedha zao zote hadi sasa kwa sababu kubwa mbili. Kwanza, baadhi ya Halmashauri zilichelewa kuanza ujenzi na ukarabati wa mifumo ya maji kutokana na kuwa na uwezo mdogo wa kufuata taratibu za manunuvi kwa ufanisi.

Pili, baadhi ya Wilaya, Wakandarasi wa Ujenzi, hawakuitikia zabuni za ujenzi na ukarabati na ilibidi zabuni zitiishwe tena na kazi katika maeneo mengine zitekelezwe na Halmashauri zenyewe.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ambazo zimetolewa na Halmashauri hadi kufikia mwezi Machi, 2008 miradi ya maji 969 ya *Quick Wins* kati ya 1778 iliyokusudiwa kujengwa ilikuwa imekamilika. Vilevile ofisi 34 za Idara za Maji za Halmashauri ziliwa zimekarabatiwa na Ofisi nane mpya zimejengwa.

Halmashauri 12 kati ya 84, zilizopewa fedha kwa ajili ya miundombinu ya maji ziliwa zimekamilisha utekelezaji wa miradi yake. Halmashauri hizo ni Kasulu, Kishapu, Kiteto, Maswa, Manispaa ya Moshi, Jiji la Mwanza, Nachingwea, Namtumbo, Rungwe, Manispaa ya Shinyanga na Songea Vijijini.

Mheshimiwa Spika, kulingana na utaratibu wa utoaji wa taarifa za utekelezaji, taarifa za robo mwaka ilioishia mwezi Juni, 2008 zitapatikana mwisho wa mwezi Julai, 2008.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Kwa mwaka wa fedha uliopita yaani 2007/2008, Serikali iliendelea na utekelezaji wa *program* ndogo ya maji na usafi wa mazingira kupitia miradi inayoleta matokeo ya haraka. Ninayo furaha kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba tarehe 27 Juni, 2008, Serikali kupitia Hazina ilituma shilingi bilioni 11.95 kwa Halmashauri zote nchini. Fedha hizo kama ilivyokuwa fedha zilizotumwa mwezi Juni 2007, zimetokana na mkopo nafuu kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika

kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya sekta ya maji hasa kwa miradi ya *Quick Wins*.

Mheshimiwa Spika, kati ya Halmashauri 132 zilizopo kwa mwaka 2007/2008, Halmashauri 120 ndizo zilikuwa zimetimiza masharti ya kupewa ruzuku ya maendeleo na zimepewa fedha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miradi ya maji pamoja na kujenga uwezo. Halmashauri 12 hazikuweza kutimiza masharti hayo na hivyo zimepewa fedha kwa ajili ya kujijengea uwezo tu.

Mheshimiwa Spika, orodha ya mgao wa fedha hizo, imeambatanishwa kwenye taarifa hii na ninaomba isomeke katika *Hansard* kama sehemu ya kauli hii, (*Tazama kiambatisho B*).

Mheshimiwa Spika, Serikali inapenda kusisitiza kwamba kwa kuwa fedha za utekelezaji wa *program* ya maendeleo ya Sekta ya Maji zipo, mipango ya Halmashauri ya ujenzi na ukarabati wa miradi ya maji itaendelea kutekelezwa kabla ya Wataalamu Washauri hawajapatikana na hata baada ya Wataalamu hao kupatikana. Fedha zitatolewa kulingana na jinsi taarifa za utekelezaji wa miradi na matumizi ya fedha ya kila robo mwaka zitakavyokuwa zinawasilishwa na Halmashauri. Halmashauri zitakazochelewa kuwasilisha taarifa, zitachelewa pia kupata fedha.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda nichukue fursa hii kuwashukuru Washimiwa Wabunge, wananchi, Taasisi za Kiserikali na zisizo za Kiserikali, Madhehebu ya Dini, Washirika wetu wa Maendeleo na Wadau wote wa Sekta ya Maji, kwa kuungana na Serikali katika juhudzi zake za kuwapatia wananchi maji safi, salama na ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii. Kwa heshima na taadhima, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, kwa taarifa yako hiyo njema na hasa kwa uadilifu wa kuambatanisha kabisa orodha ya Halmashauri zote nchini. Itatusaidia sana kama rejea sisi Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijawaita wachangiaji, naomba kutoa ufanuzi ufuatao. Nimeandikiwa hapa kwamba Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka amekwishachangia. Hiyo siyo tafsiri sahihi ya Kanuni ya 65(1). Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, alisoma taarifa kwa niaba ya Mwenyekiti, kwa hiyo kumtaja kwangu hapa ni kwa makusudi kabisa, hakuna kosa lolote, ana haki ya kuchangia kama Mbunge wa eneo analotoka. Kwa hiyo, msije mkajiaibisha hapa kwa kusema Mwongozo wa Spika, *rulling* ndiyo hiyo, anayewasilisha taarifa kwa niaba, kwa kweli yale maoni siyo yake, ni maoni ya Kamati.

Pili, Mheshimiwa Mohamed Said Sinani, amenitaarifu kwamba yeye ndiye alikuwa awe mchangiaji wetu wa kwanza, jana tulipomtamka hakuwepo ukumbini,

mwanaye alikuwa amepata ajali kule Dar es Salaam. Sasa amerejea jana usiku kwa sababu hiyo, ingawa hamumuoni kwenye orodha, itabidi nimtambue na kwa kweli nimpe haki aanze yeche.

Kwa hiyo, mpangilio ataanza Mheshimiwa Mohamed Said Sinani, Mheshimiwa Emmanuel Jumanne Luhahula, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama na Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka.

Tunaanza na Mheshimiwa Mohamed Said Sinani.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali ywa Mwaka 2008/2009 – Wizara ya Nishati ya Madini

(Majadiliano yanaendelea)

MHE. MOHAMED SAID SINANI: Mheshimiwa Spika, ahsante na ninakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie hoja hii ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninaomba kwa niaba ya wananchi wangu wa Mtwara Mjini, niishukuru Serikali kwa jitihada iliyozifanya mpaka nasi tukapata umeme katika Manispaa yetu. Lakini wanassema hawatakuwa na raha ikiwa ndugu zao katika Wilaya nyingine za Masasi, Tandahimba, Newala, Nachingwea na mahali pengine katika Mikoa hii miwili, hawajaunganishiwa umeme. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hayo nimefarijika baada ya kusoma hiyo hotuba ya bajeti ya Nishati kwamba mkataba kati ya Serikali au na Wizara husika, utatiwa saini mwezi Julai na kwamba baada ya mkataba huo kutiwa saini umeme utapatikana katika Wilaya nyingine. Hili nalo naishukuru Serikali, tunaomba kwamba mpango huo uendelee kama ulivyopangwa. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, pia ninapenda kutoa shukrani kwa Serikali kwa katuona sisi watu wa Kusini katika suala zima la umeme hususani baada ya kutangazwa kwamba hata vijijini kutakuwa na umeme na kwamba gharama zake ni shilingi haitazidi 60,000/= mpaka 80,000/=. Hilo nalo tunalipongeza kwa kuwajali wanavijiji wetu ili nao wapate umeme. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninatoa pongezi kubwa kabisa kwa Wizara, pongezi kwa Wafanyakazi na wataalamu wa TPDC kwa jinsi wanavyochapa kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo na baada ya kutoa shukrani hizo, ninapenda pia kuipongeza Serikali kwa kuvalia njuga suala la *IPTL* na inaonekana katika hotuba hii Serikali inataka na inaendelea kufanya mazungumzo na *IPTL* ili gharama zipungue katika *capacity charges* na gharama nyingine ili kuwaondolea mzigo wananchi wa nchi hii, nawapongeza kwa hilo pia.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, ninapenda sasa kuingia katika suala moja la madini ya chumvi. Chumvi ni madini muhimu sana, mimi naamini hata katika jiko la Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri, kuna chumvi na anakula chumvi kila siku, nashangaa kwa nini wamesahau kuweka madini ya chumvi katika hotuba hii, chumvi si kitu cha kusahaulika.

Mheshimiwa Spika, chumvi si chakula tu bali ni dawa, ni dawa kwa maana kwamba chumvi ikiwekwa *Iodine* au Madini Joto, huondoa mtindio wa ubongo, pia huondoa *Goitre* yaani Matezi. Kwa hiyo, chumvi si madini peke yake bali ni chakula na pia ni dawa.

Mheshimiwa Spika, chumvi huzalishwa katika nchi hii katika mwambao wa Pwani, Uvinza na maeneo mengine na hutoa ajira kwa watu zaidi ya 20,000. Ukianzia Tanga mpaka Mtwara katika mwambao wote huo, hutoa ajira hususani kwa akina mama katika vijiji vyote ambavyo kuna majangwa haya ya chumvi au kuna fukwe za chumvi, sasa sidhani kama hili ni suala la kupuuzwa.

Mheshimiwa Spika, nikisoma hotuba hii, wameandika wachimbaji wadogo, wachimbaji wadogo watafanyiwa hivi, wachimbaji wadogo watasaidiwa lakini sioni mahali popote wazalishaji chumvi wametajwa ingawa wanaweza kusema ni wachimba Madini lakini chumvi haichimbwi ila huzalishwa kwa kutumia maji ya bahari na mwanga wa jua, malighafi ni maji ya bahari na mwanga wa jua na kwa kufanya mradi huu au kazi hii ya kuzalisha chumvi hakuna athari kwa mazingira. Nilitegemea hapa kwamba nao wangewepo katika kuwaelimisha, kuwapa mikopo na kuwasaidia kwa namna moja au nyingine. *UNICEF* kidogo imesaidia lakini si kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninapenda Waziri atakapokuwa anajibu hoja hizi, atuambie kama wazalishaji wa chumvi nao wamo katika mpango wa kukopeshwa au wapo katika mpango wa kupewa mafunzo.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi katika nchi hii, chumvi huzalishwa takribani tani 150,000 lakini *demand* ya chumvi katika nchi hii ni karibu tani 400,000 na chumvi nyingine huagizwa kutoka nje. Kwa hiyo, huligharimu Taifa kuagiza chumvi kutoka nje wakati kulikuwa hakuna haja. Kama wazalishaji hao wangesaidiwa, wakapewa mafunzo, mikopo na nyenzo za kufanya kazi, wangeweza kuzalisha chumvi ya kutosha kwa matumizi ya hapa nchini na nyingine kusafirisha nchi za nje na kulipatia Taifa fedha za kigeni lakini naona kwa muda mrefu wamewekwa pembeni. Naomba hawa wazalishaji wa chumvi wadogo na wakubwa na wao watiliwe maanani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wazalishaji wa chumvi wamekabiliwa na kodi nyingi, kuna kodi zilizoorodheshwa hapa, kuna *royalty* yaani mrahaba 3%, ushuru wa mikoko, leseni za madini, VAT kwenye chumvi, VAT kwenye Madini Joto na Ushuru wa Kijiji, hii orodha ya kodi ni kubwa mno.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, ushuru wa Mikoko, chumvi inapoanza kutengenezwa, kwa kawaida huenda sehemu nyingine kukawa na Mikoko michache ambayo itakatwa lakini kuna maeneo mengine hakuna mikoko kabisa. Sasa Mikoko inayokatwa, inakatwa kwa mara moja siyo kila mwaka. Sioni kama ni halali kumtoza mzalishaji chumvi ushuru wa Mikoko miaka yote yaani kila mwaka alipe ushuru wa Mikoko. Kama hivyo ndivyo, ingebidi yule anayekata miti kujenga nyumba basi na yeye alipe ushuru miaka yote. Amekata Mikoko kwa wakati ule tu ambapo anaanzisha shamba la chumvi au eneo la kutengeneza chumvi, robo ekari au eneo dogo zaidi ya hapo.

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida chumvi hutengenezwa katika jangwa la chumvi ambalo hakuna mti, lakini wakati mwingine wanalazimika kukata Mikoko michache, sasa kuwatoza kodi ya Mikoko kila mwaka, naona si halali.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Wizara ya Madini izungumze na Wizara husika, waondoe ushuru huu wa Mikoko kwa sababu kuna watu wengine ambao hukata mti, wakajenga nyumba basi nao watozwe kodi kila mwaka, jambo hili naona si halali.

Mheshimiwa Spika, halafu kutoza VAT katika *Iodine* au Madini Joto, naona pia ingefaa Wizara ilishughulikie suala hili ili hii kodi iondolewe kwa sababu *Iodine* ni dawa, dawa ambayo huondoa *Goitre* na Mtindio wa Ubongo. Kwa hiyo, nawasihi kodi hii nayo iondolewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, chumvi kama nilivyokwishesema ni chakula, unapoweka ushuru sawasawa na madini mengine kama dhahabu na na kadhalika, naona pia hili ni tatizo kwa sababu kodi hizi zitawafanya wananchi hawa washindwe kutengeneza chumvi. Wakishindwa kutengeneza chumvi ajira zitakuwa hazipo, itabidi nchi hii iagize chumvi kutoka nje jambo ambalo kwa kweli itakuwa ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, nimeona leo nisimame nizungumzie suala la chumvi kwa sababu limesahaulika kabisa kwani katika bajeti mwaka jana halikutajwa na mwaka huu pia haikutajwa. Kwa hiyo, ninaomba suala hili liwemo au Wizara inayohusika ilishughulikie.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo kwamba tunaagiza chumvi kutoka nje kwa mfano chumvi ya unga yaani *free flowing salt* au *table salt*. Teknolojia hii iko hapa Kenya tu, ingewezekana hawa watu wangepelekwa Kenya, wakajifunza jinsi ya kutengeneza chumvi hii ambayo tungeepukana na kuagiza chumvi kutoka nchi jirani. Ni aibu kuagiza chumvi wakati sisi tuna fukwe, tuna maji ya bahari na jua lipo! Sioni sababu kwa nini chumvi iagizwe kutoka nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala hili nimeona leo nilizungumzie hapa kwako na sina lingine la zaidi na kwa kuwa watu wanaotaka kuchangia ni wengi, nimeona niishie hapo.

Mheshimiwa Spika, nami naunga mkono hoja hii, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mohamed Saidi Sinani, tunakupa pole na kumtakia ahueni kijana wako.

Sasa ninamuita Mheshimiwa Emmanuel Jumanne Luhahula, wakati huo ajiandae Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga.

MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunilinda na ambaye ametufanya tuwepo katika siku hii ya leo.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Makamishna wote na Watendaji katika Wizara, kwa kuanda hotuba hii ambayo mimi nimeiona ni faraja sana kwangu na kwa wananchi wa Wilaya ya Bukombe. Mungu awabariki sana na naomba mtekeleze na kutimiza yote mliyosema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niende kwenye suala la nishati. Ninaipongeza pia Serikali, nimekuwa na ombi langu na malalamiko, kwa muda mrefu bajeti zote mbili zilizopita, tumekuwa tukiongelea suala la umeme katika Makao Makuu na Wilaya ya Bukombe. Lakini naipongeza Serikali kwa sababu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 45 – 46, ameeleza bayana jinsi ambavyo Wilaya ya Bukombe itakavyohudumiwa na mpango wa Benki ya Afrika.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu hapa kwa sababu hata mwaka 2006 tulipata kwenye bajeti, mwaka 2007 wakasema pia, lakini sasa naomba Serikali ihakikishe kwamba tunateua Wakandarasi haraka kama mlivyoeleza kwenye hotuba yenu kwamba kuanzia mwezi huu kwa sababu upembuzi yakinifu umeshakamilika kazi iliyobaki ni ya kuteua Wakandarasi.

Mheshimiwa Spika, ninaamini mmetusaidia kama umeme utafika kwa muda muafaka kwa sababu wana Bukombe tuna shida na tulikuwa tukieleza shida yetu mara nyingi na kila wakati tuliposimama kuhusiana na suala la nishati tulisema. Kwa hiyo, ninaomba sana tuhakikishe suala hili tunalikamilisha na ninaamini maisha bora kwa kila Mtanzania yatafikiwa kwa sababu tatizo kubwa tulikuwa nalo ni la umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, umeme huu unatoka maeneo ya Ilogi, ninajua tutakapokuwa tunapata umeme huu, haifaidiki Bukombe peke yake bali hata Jimbo la Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, litafaidika kwa sababu ninaamini utapita katika vijiji vya Lunguya, Segese na Ikinda, ninaamini ni maeneo ambayo yanapitia umeme kwa ajili ya kuja Bukombe.

Mheshimiwa Spika, nina uhakika kwamba hata katika mchanganuo mliondika pale, vijiji nilivyovitaja ni Lunguya, Segese na Ikinda ni vijiji vilivyo katika Jimbo la Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, Wilaya ya Kahama haviko katika Wilaya ya Bukombe ili baadaye visije vikasomeka kwamba Bukombe tumeendelea kuwapa umeme vijiji vingi sana, niliona hilo nilifafanue.

Mheshimiwa Spika, sasa kuna kila dalili ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Ninaomba sasa wawekezaji basi katika Wilaya ya Bukombe mkisikia umeme umekamilika, ninaamini kwa sababu wanateua Wakandarasi mwezi huu, umeme utakamilika mapema ili wawekezaji waliokuwa wanaogopa kufika pale kwa sababu ya kukosa nishati ya nishati, tunawakaribisha sana na wananchi wa Bukombe tunawaahidi ushirikiano, karibuni tutafanya kazi kwa pamoja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, niongelee suala la madini. Katika suala la madini, nataka nizungumzie vipengele vifuatavyo, ninaanza na *STAMICO*. Ninapongeza Wizara kwa kuliona hili kwa kuiondoa *STAMICO* kwenye Mashirika yaliyokusudiwa kubinafsishwa. Mmesema kwamba mmeshapeleka maombi yenu kwenye ngazi za maamuzi, tunashauri *Consolidated Hold Cooperation (CHS)*, wanaoshughulikia sual hili na *TRA* wahakikishe kwamba Shirika hili wanalipa nafasi kwa sababu limeshindwa hata kujiendesha vizuri kwa sababu lipo *specified*. Tunaomba sana liachiwe haraka liwe huru ili lifanye kazi. Tunaamini *STAMICO* wakiwezeshw na wakapata nafasi hata ya kujiendesha, wataweza kukopa. Tuna hakika kwamba *STAMICO* ikiwezeshw, mambo mengi ya madini katika nchi yetu yatakwenda vizuri.

Ndugu Mwakalukwa, Mkurugenzi wa *STAMICO*, nikuombe kwa sababu hali ya shirika lako inakwenda vizuri, utembelee Bukombe, uje ukutane na wachimbaji wadogowadogo waliopo katika Wilaya yangu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la watafiti. Leo ni safari ya tatu katika Kikao cha bajeti kwenye Wizara hii ninaposimama, ninazungumzia suala la Watafiti. Nimekuwa na masikitiko makubwa sana hasa katika Jimbo langu kwa sababu wapo Watafiti ambao wamefanya kazi ya utafiti katika maeneo kwa muda mrefu sana, zaidi ya miaka 10 wanafanya utafiti na kila ninapowauliza Serikali hawatoi majibu ya kueleweka.

Mheshimiwa Spika, wapo Watafiti katika eneo la Nyakafuru wa Kampuni ya *Resolute*, wamefanya utafiti muda mrefu sana lakini hakuna majibu yanayotokea pale. Ninapenda kuiomba Serikali safari hii watuambie, niliuliza katika bajeti iliyopita tukasema hawa kwa sababu wamekuwa wakitafiti na eneo lile limetafitiwa zaidi ya miaka 10 wako pale, kama wamekosa ninaomba na ninaishauri Serikali eneo lile waliachie na leseni zao zitakapokamilika wasipewe leseni tena ili eneo lile tuwape wananchi wachimbaji wadogowadogo wa Wilaya ya Bukombe kwa sababu ninaamini mkakati ni mzuri sana.

Mheshimiwa Spika, nimesoma *Action Plan* ya STAMICO, wana mpango mzuri sana lakini bado Ilani ya Chama cha Mapinduzi, ina mkakati mzuri sana na wachimbaji wadogowadogo, ninaomba hawa watu waacie, haiwezekani wanatafiti muda mrefu hivyo lakini pia inapofikia katika hali hii, ninafikiri tatizo liko kwenye Wizara husika. Wizara husika inawezekana wataalamu hamtembelei maeneo yale, wale watu wanatafiti tu wenye we wanachimba, wanachukua *sample*, wanakwenda na mwisho watakacholeta ripoti ofisini ndicho tunachukua. Wakisema leo hatukupata, tunasema sawa! Naomba sana Waziri utakapokuwa unahitimisha, uniambie leseni zao hizi zikikamilika usiwave nyine tuwape wachimbaji wadogo wa Bukombe.

Mheshimiwa Spika, lakini wapo watafiti wengine ambao kwa kweli wanafurahisha, iko kampuni ya TANZAM, wanaofanya utafiti katika Hifadhi ya Kigosi Myowosi, ni kampuni ambayo kwa kweli siku tulipotembelea kule na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, walinfurahisha sana. Wapo pale muda mfupi sana lakini walielezea hatua wanazokwenda nazo na wakaeleza ule ukweli lakini bado nimeona hata kwenye hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati naye amegusia sana suala la TANZAM na *Tan Can Mining Company Limited*. Ninaomba sana tuwe na watafiti ambao wana nia nzuri na nchi yetu siyo watafiti ambao wako kwa ajili ya kujinufaisha.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana suala hili na hasa la watafiti ambao wako katika eneo la Nyakafulu, wamechukua leseni nyangi sana, wana eneo kubwa sana lakini haina tija na haina faida katika Wilaya na wananchi wa Bukombe.

Mheshimiwa Spika, niongelee suala la wachimbaji wadogo wadogo. Ninaipongeza sana Serikali kupitia Waziri na Naibu Waziri, Kamishna kwani walifika kwangu. Waziri alimtuma Naibu Waziri, walifika na Kamishna, kwa kweli kulikuwa na mgogoro wa wachimbaji wadogo wadogo lakini niitumie nafasi hii kuwapongeza kwa dhati kwa sababu eneo la Nyakasaluma lililokuwa linaleta mgogoro na wanaoleta mgogoro ni hawa hawa wa *Resolute*, waliopo Nyakafulu lakini tuliweza kutoa kibali ili wananchi wa Bukombe waweze kujipatia riziki. Tunaomba sana muendelee na moyo huo!

Mheshimiwa Spika, lakini si hivyo tu bado mmeonyesha nia nzuri ya kuwasaidia wachimbaji wa eneo la Katente ambao ni SACCOS ya Katente. Kwa kweli ni mpango mzuri sana ambao ninaamini hata wananchi wangu wanafurahi. Kwa hiyo, ninaomba sasa ikiwezekana Wilaya ya Bukombe kwa sababu haina mgodi mkubwa, tuwezeshe Wilaya ile, tuitenge tu yote iwe ya wachimbaji wadogo wadogo, tusitoe maeneo yote yawe ya wachimbaji wakubwa, kama wanatafiti miaka 10 na zaidi hawapati basi liwe eneo la wachimbaji wadogo wadogo na hii ni kwa sababu pengine baadhi ya watafiti wengine hawafanyi kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, niongelee suala la madini kwa ujumla. Madini sasa hivi inawezekana ukawa ni uti wa mgongo wa uchumi wetu Tanzania. Ninasema hivyo kwa sababu gani? Madini soko lake halina utata ni soko ambalo liko dhahiri, soko lake linatofautiana na soko la mazao ya chakula na mazao ya biashara kwa sababu leo hii pamba kule kwangu watu mpaka sasa hivi hawauzi kwa sababu bei ni ndogo lakini

dhahabu inazidi kupanda juu. Dhahabu tunaweza tukaweka *stock* tutakuja tuuze kwa bei ya juu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali kwanza ifanye mpango na hili suala nililiongea hata mwaka 2006, Serikali ifanye mpango wa kuwapa hatimiliki wananchi maeneo yao ili waweze kumiliki ardhi hizo wanapokuja wawekezaji angalau 2% ili na wao ziweze kuwasaidie.

Lakini la pili, Serikali iingie ubia na makampuni yanayokuja kuchimba madini katika nchi yetu. Mtaji wetu ni ardhi, mtaji wetu ni madini, wale wanakuja na vyombo kwa nini tunashindwa kutoa 50% kwa 50%? Ninaishauri Serikali iliangularie suala hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la tatu, tutumie watafiti wa Tanzania, tuitumie *STAMICO* na tukiitumia itatuambia kwa uhalisi, *reserve* iliyopo katika eneo husika. Wawekezaji wanapokuja, wanajua idadi ya *stock* tulionayo katika eneo husika.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tunatumia *STAMICO* na makampuni ambayo wanashirikiana nayo. Nimeona kwenye hotuba ya Mwenyekiti katika ukurasa wa tano, wameeleza kwamba *STAMICO* imekuwa ikishirikiana na *TANZAM* 2000, *Geo Can Resources Limited* na *Tan Can Mining Company Limited*, inaonyesha kampuni hizi ambazo zimekuwa zikishirikiana na *STAMICO* ni kampuni nzuri tena wanasema zinatoka Canada. Mimi ninaamini kwamba inawezekana uongozi wa kampuni hizi ni mzuri, tunaomba mshirikiane nazo lakini mzipe uwezo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nilitaka nitoe ushauri kwa ajili ya Kamati na Tume tunazounda, tuwe na usiri. Unajua tunaweza kufika hatua Tume au Kamati ikiundwa ikakosa usiri mambo yanaweza kuvuja na baadaye ikatokea nafasi ya kuanza kurushiana maneno, fulani katoa siri, fulani katoa siri, lakini lazima tuangalie ili tuweze kuipeleka nchi yetu mahali pazuri sana. Naamini tukifanya hivyo, uchumi katika nchi yetu utaboreka.

Mheshimiwa Spika, la mwisho niongelee kuhusu wakulima wa pamba. Ni kweli bei imeshuka sana, tunaomba Serikali iliangularie hili. Mwaka jana bei ilikuwa Sh. 500/=, mwaka huu imekuwa Sh. 400/=, wakulima mpaka leo hawajaanza kuuza. Tunaomba Serikali iandae mkakati wa lazima kama ilivyofanya kwenye korosho iangularie na Kanda ya Ziwa. Lakini nawaomba wakulima wa Wilaya ya Bukombe na sehemu nyingine, yapo maeneo ambayo mfumo wa stakabadhi ya mazao unatumika kwa mfano, Lubunga, Nyasato, naomba wakulima wauze kwa mfumo huu, utawasaidia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nilisema la mwisho lakini la mwisho zaidi ni kuhusu madini. Katika maeneo ambayo madini yanachimbwa, hakujaonyesha mabadiliko makubwa kwa wananchi wake. Ukiangalia maeneo kama ya Arusha ambako kuna Mlima Kilimanjaro, mbuga za wanyama, wananchi wa kule wana mabadiliko, kwa nini tunakotoa madini

tusibadilike? Katika kubadilisha mfumo wa sheria, naomba waangalie hilo kwa kutoa percent kwa wananchi wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja hii na nashukuru sana. Naomba utafiti yashirikishwe makampuni ambayo ni marafiki na wawekezaji amba ni marafiki wa Tanzania wanaotuletea hali nzuri katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili nami niwe mmoja wa wachangiaji wa bajeti hii ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, kama ada, nianze kwa kumpongeza Waziri, Naibu wake na watendaji wote wa Wizara, kwa kazi nzuri waliyofanya.

Aidha, napenda vilevile niipongeze sana Kamati ya Mheshimiwa Jaji Boman, kwa kazi nzuri sana waliyofanya ya kutafiti hii sekta ya madini na kushauri nini kinahitajika kufanyika ili Serikali iweze kufaidika zaidi kutokana na rasilimali hii muhimu ambayo Mwenyezi Mungu ametujalia.

Mheshimiwa Spika, napenda sasa niendelee kuchangia kwanza, suala la *refinery*. Tulifanya makosa kama nchi kufunga *refinery* yetu ya *Tipper* na toka tumefunga tunazungumza kila siku kwamba tunataka kuifungua, sasa tutaifungua lini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo ni suala zima la bomba la mafuta kutoka Dar es Salaam kwenda upande wa Magharibi wa nchi. Ni kitega uchumi muhimu sana lakini inashangaza siku zote tunazungumza habari ya kutafakari, kufanya usanifu na kadhalika. Tusidhani kwamba tupo wenyewe sisi Tanzania, nchi jirani ambayo ina bandari katika bahari ya Hindi, wenyewe tayari bomba lake limekwishafika Kisumu, lilikuwa Eldoret limefika Kisumu na sasa linaelekea Magharibi zaidi. Sasa angalia utapokuja kutengeneza bomba lako utaweza kweli kushindana na mwenzako ambaye tayari yupo huko? Bado tunaongea, bado tunaongea, hili ni jambo muhimu sana kiuchumi, tulipe nafasi yake, tulitengenezee mkakati wa haraka.

Mheshimiwa Spika, baada ya hilo, sasa nakuja kwenye matumizi ya gesi asilia. Gesi asilia tunayo, tumekuwa nayo toka miaka ya mwanzoni mwa sabini pale Songsosongo. Matumizi ya kwanza yalikuwa kutengeneza mbolea, ilianzishwa na kampuni inayoitwa *KILAMCO* (Kilwa Amonia Company) haikuweza ku-*take off*. Mpaka leo tunaendelea kupata gesi nyingi sana lakini matumizi yake ni kidogo sana. Ndiyo tumeifikisha Dar es Salaam tunaitumia pale kuendesha mashine zile za Songsosongo *Gas* pamoja na haya matumizi mengine yaliyokuja ni katika viwanda vichache.

Mheshimiwa Spika, katika moja ya maswali niliyouliza Serikali hivi karibuni ni kwamba, inafikiria nini kuhusu matumizi ya gesi asilia hususan kwa matumizi ya

majumbani na kuendeshea magari? Wamesema kwamba ati wanaanza kufanya uchunguzi kwa magari mia mbili, kwa nini magari mia mbili! Kwani teknolojia ya kuendesha magari kwa gesi hatuna haja ya kugundua gurudumu! Gurudumu lipo ni kiasi cha kuli-*perfect* kulingana na mazingira yetu. Kama hatuna huo utaalalm, India kwa kuanzia wanaendesha magari yao kwa kutumia gesi twende tukaazime wataalamu huko.

Mheshimiwa Spika, kidubwana kinachotakiwa kuwekwa kwenye gari ili ubadilishe kutoka kwenye matumizi ya mafuta kwenda kwenye gesi, kinagharimu karibu milioni moja na mafundi wapo. Hii gesi inawekwa kwenye mitungi kama ile inayotumika kwa gesi ya matumizi ya nyumbani. Sasa kigumu ni kipi katika suala hili mpaka tunaambiwa tunaanza na magari mia mbili? Kigumu ni nini mpaka tunachelewa hivyo wakati ambapo nchi yetu inapita wakati mgumu wa bei za mafuta kuwa juu wakati gesi tunayo chini?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali ituletee *master plan* ya matumizi ya gesi haraka sana na tuone tatizo liko wapi? Kama tatizo ni fedha na huu ni mpango ambao utatusaidia kuondokana na makali ya kupanda kwa bei za petroli, twende *World Bank*!

Mheshimiwa Spika, juzi Mheshimiwa Rais ambaye yuko Japan ameongea na Rais wa Benki ya Dunia, yule Rais wa Benki ya Dunia kwa habari tunazozipata, amekubali kuisaidia Tanzania kuipa takriban dola, nisiseme tarakimu kwa sababu naweza kusema uwongo, lakini tumepewa fedha baada ya Mheshimiwa Rais kuzungumza na Rais wa Benki ya Dunia. Hizi fedha zije kutusaidia katika sekta ya miundombinu ambayo ni pamoa na mambo kama haya. Sasa tuchangamke na tutengeneze mkakati wa jinsi gani tunaweza kuitumia gesi yetu.

Mheshimiwa Spika, gesi yetu tunaweza kuitumia kwa kutengeneza mbolea, kuiuza nchi za nje kwa utaratibu wa *Compressed Natural Gas (CNG)*, tukapata fedha za kigeni. Vilevile katika matumizi ya kutengeneza umeme, gesi yetu bado inatuzalishia kwa ujumla wake mpaka leo hii hazizidi *MW250*. Hiyo maana yake ni kwamba, unachukua Songas ina *MW180*, hiyo mpya ya sasa hivi iliyoko pale *TANESCO* ambayo ni ya Serikali ina *MW100*, nitabadilisha tarakimu zangu kwa kujumlisha hizi, ile ya Tegeta ina *MW45* na kule Mtwara kuna kama *MW18* lakini wanatumia *MW6* tu.

Mheshimiwa Spika, gesi hii inaweza kuzalisha *megawatts* nyingi zaidi na kama hatuwezi kutumia sisi hapa nyumbani *tu-export*! Nchi za jirani wana matatizo ya umeme, sisi Mungu katujalia vyanzo vingi vya umeme lakini hatuna mikakati na mipango ya muda mrefu ya kutumia rasilimali yetu hii kwa maendeleo ya nchi yetu, naomba Hili tulitilie mkazo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia upande wa gesi, sasa nataka nije kwenye sekta ya umeme. Nilipongeze Shirika la *TANESCO* kwa kuwekeza katika kutengeneza njia za msongo mkubwa kuelekea Kaskazini Magharibi ya Tanzania. Njia hizi zitaondoa uzito wa mzigo ambao ile *National Grid* ya sasa ilikwishaanza kuelemewa. Njia hizo zitafika mpaka Kabanga ambako kuna mradi mkubwa wa *nickel*

ambao ungechelewa kuanzishwa kwa sababu ya ukosefu wa nguvu za umeme. Kwa hiyo, kwa hili pongezi kwa *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, pongezi kwa *TANESCO* vilevile kwa kukatisha mkataba na *Dowans*, lakini vilevile kuna mikataba mibaya zaidi kama ule wa *IPTL*. Mkataba huu ni wa miaka ishirini, hivi ni dharura gani kweli ya miaka ishirini? Ulikuja chini ya utaratibu wa *emergency power, sasa emergency power* ya miaka ishirini? Yaani upo kwenye *emergency* ya miaka ishirini kweli?

Mheshimiwa Spika, lakini mbaya zaidi chini ya mkataba huu, sisi ndio tunaotengeneza zile mashine, ile mitambo tunaitengeneza sisi kwa gharama yetu. Yule mwekezaji katuletea mtambo, kauweka pale. Ni wajibu wetu sisi tuutengeneze unapoharibika na kuhakikisha kwamba unafanya kazi. Mtambo ule leo hii ni mzuri zaidi kuliko ulivyokuja kutokana na gharama zetu sisi na bado anatuchaji *capacity charge!* Sasa nasema Serikali hebu imalizane na huyu jamaa, tena amekwishaonekana kuwa ni tapeli! Alituambia amewekeza shilingi takriban milioni themanini kumbe amewekeza shilingi hamsini elfu tu?

Mheshimiwa Spika, lakini tumeendelea kumlipa kwa utaratibu wa kwamba amewekeza shilingi milioni themanini kumbe kawekeza shilingi hamsini elfu tu! Kwa hiyo, huyu ni mwizi, ametuibia! Sasa sijui tuweke mguu chini, tuzungumze naye kwa maana ya kwamba sisi tuna nguvu, tufike mahali tumalizane naye. Zile mashine tuzichukue ziwe zetu na hatimaye tuzibadilishe zitumie gesi.

Mheshimiwa Spika, wakati nikiwa katika eneo la umeme, pale Mjini Tabora, Jimbo langu linazungukwa na takriban Kata sita mpaka nane ambazo hazina umeme nazo ni Malolo, Uyui, Itonjanda, Misha, Itetemiya, Kalunde pamoja na Ndevelwa na nyingine, lakini hizi zipo Mjini. Nyaya za umeme zenye msongo mkubwa zinapita kwenye Kata hizi. Ili Kata hizi zipate umeme, wanachohitaji ni *transformers* tu. Tukiweka *transformers* kama vile pale Usoke kwenye umeme unaotoka Tabora kuelekea Urambo, pale wameweka *transformer* tu wameshusha umeme, pale Mabama wameweka *transformer* wanashusha umeme. Sasa kwa mantiki hiyo hiyo, kwenye Kata hizi zinazozunguka Tabora tunachohitaji, ni *transformers* tu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, sasa nije kwenye madini. Kama nilivyosema awali, naipongeza sana Kamati ya Jaji Bomani. Kusema kweli nimepitia ripoti zao, wamefanya kazi kubwa sana kiasi kwamba hatuhitaji kazi nyingine tena kuliko hii ya Jaji Bomani na Kamati yake. Kinachohitajika sasa ni kutunga sheria inayoendana na mapendekezo ya Mheshimiwa Jaji Bomani.

Mheshimiwa Spika, Jaji Bomani ameeleza mambo yote *in fact* nilifikiri katika hadidu za rejea kama haikuwemo ingekuwa vizuri sana kama wangeambiwa vilevile watuletee na rasimu ya sheria mpya. Kwa sababu leo tungkuwa tunaangalia ile rasimu ya sheria mpya na kwa kiasi gani imeweke mapendekezo yao. Mapendekezo yao takriban yote nayakubali mathalan tuondoe vivutio vya kodi, mrahaba upande, tukifanya haya tutaongeza pato la Taifa haraka sana. Yaani ni kulala na kuamka tayari sisi tuna

fedha nyingi. Tutaondokana na matatizo ya Serikali kutegemea kodi za pombe na wavuta sigara!

Mheshimiwa Spika, tuna eneo hili zuri tu ambalo tulikuwa tumeliacha. Wawekezaji wenzetu wanachukua fedha wanakwenda nazo. Nimesoma katika taarifa ya Jaji Bomani, kitu ambacho sikukiona nadhani nilikuwa nasoma haraka haraka. Kuna eneo linaitwa *windfall profit tax*, sikuona hilo. Sasa nasisitiza toka makampuni haya yaliposaini mikataba mpaka leo bei ya dhahabu imepanda kutoka takribani dola mia mbili hamsini kwa *ounce*, mpaka leo tunazungumzia dola mia tisa kwa *ounce* moja! Ndiyo kusema hawa jamaa wao wanapata *windfall profit*, kwa nini sisi tusiweke kodi katika hiyo? (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kuna nchi moja inaitwa Mongolia, mwaka 2006 iliweka kodi ya *windfall profit* kwa watu wanaonunua *commodities* zao na hakukuwa na kitu. Walikubaliana mambo yakaendelea. Kwa hiyo na sisi tutakapozungumza na hawa wanaosema mkianzisha kodi zenu, mkileta mambo yenu mapya, sisi mtuache, angalieni mbele, msiangalie nyuma, haiwezekani na wao tuzungumze nao. Ni suala la *win win situation*. Wanatuhitaji, tunawahitaji, kwa hiyo wao wasidhani kwamba tunawahitaji sana.

Mheshimiwa Spika, vilevile kama wanadhani tunawahitaji sana mstari wa mwisho kabisa ni kwamba pamoja na kwamba sheria inasema hatutachukua kwa nguvu mali zao lakini ikifika mahali tunashindwana, tunaweza ku-*nationalize* ule mradi, tuwalipe *fair compensation*. Kwa maslahi ya nchi, tunaweza kufika huko, wakitufikisha huko lakini kwanza tuzungumze nao kwamba, sisi tunaondoa vivutio vyote vyaya kodi, kwa kweli hawavihitaji! Tunapandisha mrahaba kwa sababu katika nchi nyingine zinazotuzunguka wanafanya hivyo na nchi nyingine duniani wanafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, kabla sijamaliza, kuna haja ya kuunda Mamlaka ya Maendeleo ya Madini ili isimamie sekta hii ya madini. Lakini tuunde pia na Mamlaka ya Umeme ili isimamie eneo la umeme. Tukifanya hivyo, tutapunguza mzigo kwa Wizara maana sasa hivi Wizara imezidiwa, imelemewa, inafanya mambo ya utawala, mara huku madini *licence*, mara huku umeme, sasa kutakuwa na *licence* za umeme, tuunde mamlaka zinazofanana na *TRA* ambayo inakusanya kodi. Kwenye Wizara hii, Mamlaka itakayosimamia maendeleo ya madini na moja itakayosimamia maendeleo ya umeme.

Mheshimiwa Spika, shughuli zote za kila siku za mambo ya leseni za madini na umeme zifanyike huko, Wizara ibakie na wajibi wa kuratibu na kushughulikia masuala ya kisera na kisiasa kufuatana na sekta hizi mbili. Tukiunda vyombo hivi viwili tutaisaidia sana Wizara. Bila kufanya hivyo, Wizara hii imelemewa na haiwezi, kwa kweli ni Wizara kubwa na ina mambo mengi sana! Njia ya kuisaidia ili iweze kufanya kazi vizuri ni kuiundia Mamlaka hizi mbili ili zichukue kazi kubwa za kusimamia sekta ya madini na umeme.

Mheshimiwa Spika, nimekwenda haraka haraka sana kwa sababu dakika kumi na tano, kwa kweli ni ndogo. Sasa nataka nirudi kwenye hii ripoti ya Jaji Bomani. Kwa kuwa ripoti hii siyo siri, matarajio yangu ni kwamba, vyombo vyahabari vitaitangaza kwa wananchi wote ili waweze kuitafakari na kuielewa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofî*)

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, sijui nianze kwa kupongeza lakini kwa kweli nasita. Labda nianze kwa kumpa pole Mheshimiwa Waziri na nimwombee Mwenyezi Mungu amsaidie, hiyo Wizara yake kwa kweli ni Wizara ambayo kwa maneno mengine naweza kusema kwamba imekaa vibaya. Kwa hiyo, namwomba Mungu amsaidie, asiingie kwenye jinamizi la ufisadi, la kupenda rushwa au kutotekeleza madaraka yake na majukumu yake sawasawa. Hizo labda niseme ndiyo salaam zangu za mwanzo.

Mheshimiwa Spika, siwezi kuanza kwa kupongeza kwa sababu kwa kweli, nina kero kubwa ya umeme kuanzia Makao Makuu ya Mkoa wa Ruvuma, Jimbo la Peramiho, Wilaya ya Namtumbo na maeneo mengine ambayo nitayaeleza.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba pia nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge, wamekuwa mahiri katika kuwakilisha Mabunge yao sawasawa ndani ya Bunge letu Tukufu na kwa kweli wamekuwa wakijenga hoja za kuwakilisha wananchi wao kwa ufasaha mkubwa sana, naamini hata mimi nafanya hivyo kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Peramiho. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, toka bajeti ya mwaka 2006, nimekuwa nikimweleza Waziri mwenye dhamana ya Nishati, mshangao wangu katika suala zima la kupeleka nishati ya umeme yenye kuaminika katika Makao Makuu ya Mkoa wa Ruvuma kwa maana ya Songea na katika maeneo mengine ya Wilaya ambazo ziko ndani ya Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, niseme tu naishukuru na kuipongeza Serikali kwa kuzingatia sana suala hilo kwa kuwaokoa ndugu zetu wananchi wa Wilaya ya Mbinga angalau wao sasa hivi, kwa miaka mingi walikuwa kwenye giza na sasa wapo kwenye mwanga.

Mheshimiwa Spika, lakini haiingii akilini kwa takriban sasa miaka arobaini na kitu toka tumepata uhuru, Mkoa wa Ruvuma kwa maana ya Wilaya ya Songea na Jimbo la Peramiho, katika Halmashauri ya Wilaya Songea, haijapata umeme wa *grid* kwa miaka arobaini na saba, haiingii akilini. Lakini Wilaya ya Songea, ni Wilaya ambayo ipo mionganoni mwa Mikoa ambayo ni *big four* katika nchi yetu ya Tanzania kwa maana ya kulisha chakula kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, nafikiri kwamba, kwa jukumu kubwa ambalo Mkoa wa Ruvuma, Wilaya hii ya Songea na Jimbo la Peramiho likiwemo ndani tumepewa na

Taifa, kipaumbele cha kupeleka umeme, kingefanywa katika Mkoa huo, Wilaya hiyo ya Songea na Jimbo la Peramiho likiwemo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashangaa sijui Serikali inataka kuniambia nini, hebu fikiria huko Jimboni Peramiho, nimepigiwa simu toka jana naambiwa, msimu wa kuuza mahindi umefika, Serikali imeomba kabisa mahindi yetu yote tusiyauze nje ya Mkoa wa Ruvuma au nje ya nchi, tupeleke kwenye Hifadhi ya Chakula ya Taifa kwa wito maalum kwamba, nchi isije kuingia katika janga la chakula. Tunakubali na tunafanya hivyo, lakini ikifika kwenye suala la mgawo wa umeme Kusini, kitabu cha Mheshimiwa Waziri anasema:-

“Usambazaji wa umeme pamoja na Songea, Namtumbo kwa grid ya Taifa utachukua muda mrefu”.

Mheshimiwa Spika, hebu nisaidie hapa leo nifanye nini na Waziri mwenye dhamana hii ya Nishati katika nchi yetu ya Tanzania?

Mheshimiwa Spika, tunapoamka asubuhi, nchi ina njaa, tutaambiwa kwamba sasa Songea, Peramiho, Namtumbo hebu tunaomba kabisa mtusaidie tupate chakula lakini tunapokuja upande huu wa pili, itachukua muda mrefu na anasema kwamba Serikali ya Uswizi wamethibitisha ufadhili, sijui ndiyo huo wa muda mrefu hata sielewi na anasema kwamba, ufadhili huo una thamani karibu ya dola milioni sabini na viji ambavyo vinapita kutoka huko Makambako mpaka huko Songea, vitafikiriwa.

Mheshimiwa Spika, nakubali, ninazo Kata zangu za Wino na nakwambia chanzo cha umeme wa *grid* kutoka Makambako kwenda Songea ni Kata yangu ya Wino. Kata ya Wino, ina *NGO* yake kubwa inaitwa *WIDA* na wao walishafanya mawasiliano na wenzetu wa Uswizi na wakaahidi kupeleka umeme Kata ya Wino lakini baadaye Serikali ikaona afadhali kuweka *grid* ya Taifa kutoka Makambako mpaka Songea ikiwemo Kata ya Wino, Mahanje na Madaba, ndiyo tulisema kwamba tutaweka *substation* pale.

Mheshimiwa Spika, ngoja niseme kitu kimoja hapa, halafu utanilewa vizuri, mwaka 2006 nilipomhoji Waziri kuhusu suala hili la umeme wa *grid* na kupeleka umeme Peramiho, alinijibu hivi naomba ninukuu, hii ni *Hansard* ya Ofisi yako, tarehe 18 Julai, 2006, akaniambia:-

“Naomba kumjibu na kumpa ufanuzi Mheshimiwa Jenista Mhagama kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Mhagama, Mji wa Peramiho na Mji wa Songea, ni muhimu kwa Serikali yetu na Serikali imepanga kwamba katika mwaka huu wa fedha 2006/2007, kazi ya kujenga na kufikisha umeme Peramiho itafanyika”. Makofi yameandikwa hapa. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Spika, sitaki kumtaja huyo Waziri aliyekuwa kipindi hicho lakini ndiye huyu huyu aliyeo sasa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2006/2007, 2007/2008, leo ni mwaka 2008/2009, Mheshimiwa Waziri anakubaliana nami kwamba Bunge hili kupitia hiyo Wizara wamejenga tabia ya kuwadanganya wananchi wa Peramiho na wako tayari kuwaomba radhi kwa kauli hizi ambazo hazikuwa za kweli? Si ya kwangu haya, zimeandikwa hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nasikitika sana, bajeti ya mwaka 2006/2007 zilitengwa Sh. 2.8bn/= kwa ajili ya kufanya *extension* ya umeme wa *grid* kutoka Makambako kwenda Songea. Umeme ukifika Songea, nina hakika Peramiho umefika, Sh.2.8bn/= sijui zimefanyiwa kazi gain, hakuna kinachoelezwa.

Mwaka huu zimetengwa Sh.3.8bn=, mradi unahitaji Sh. 70bn/=, kwa hali hii je, tutafika? Ama leo mnataka kutuambia, tuwaambie wananchi wa Mkoa wa Ruvuma, litakapofika na sisi suala la kulisha Taifa, tuanze kuwa na kigugumizi mpaka mtuletee umeme? Kwa sababu haya ni mambo ya kupeana, kutiana moyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Namtumbo mwaka jana, Kiwanda cha Sigara kilichangia kwenye kodi ya Taifa Sh. 90bn/. Sigara haziwezi kutengenezwa kama Wilaya ya Namtumbo hawajalima tumbaku. Wakulima wa tumbaku wa Wilaya ya Namtumbo wanakaa kwenye giza lakini wanachangia pato la Taifa la Tanzania kwa kiasi kikubwa. Haki iko wapi, hakuna haki! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashangaa, miaka arobaini na saba, kuna kigugumizi gani kwa Serikali yetu, tatizo ni nini? Tunapozungumzia Mikoa ya Kusini, sasa hivi ikianza kuzungumzwa Kusini inakwenda Mtwara, Lindi inaishia hapo, ikaja Nyanda za Juu Kusini inakwenda mpaka Njombe kwa Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza mwenzangu angalau mambo yake si mabaya, lakini ukishafika Njombe, Ruvuma hatujijui tupo Nyanda za Juu ama tuko Kusini ya Mwambao, tumebaki kituo ambacho hakina mwenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, afadhali wenzetu wa Rukwa wenzetu kumeanza kupambazuka, *Inshallah*, wenzetu wameona juu, naamini kabisa mambo yao si haba. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nayasema haya kwa uchungu mkubwa. Naomba sana Waziri aniambie, mwaka jana ndiyo maana nilikuwa nasema, kumbe niwaambie Waheshimiwa Wabunge, haya mambo ya kuwaomba hawa Mawaziri watusindikize Majimboni, hayana maana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwaka jana, wewe ni shahidi, nilimwomba Mheshimiwa William Ngeleja akiwa Naibu Waziri, akawaambie wananchi wa Peramiho, ni lini atawapelekea umeme, nikaenda naye. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, tulifanya mkutano mkubwa, akawapa ahadi nono, akawapa matumaini, kuwa na imani ni kuwa na mategemeo na matarajio kwa mambo yajayo.

Lakini nasikitika kusema safari ile imeishia kwa hali hii ninayoizungumza hapa ndani leo. Naomba ...

SPIKA: Mheshimiwa, hujasema baada ya mkutano wa hadhara kulikuwa na nini. (*Kicheko*)

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, naomba uzilinde dakika zangu.

Mheshimiwa Spika, namtakia kila la kheri Mheshimiwa William Ngeleja na Mheshimiwa Malima, nitapunguza shilingi kwa kuvunja kanuni, kwa kila Idara ya Wizara yake bila kujali kwamba, mshahara huu haumhusu yeye mpaka niambiwe mwaka huu umeme wa *grid* kutoka Njombe ukapita Wino, Madaba na Vijiji vyangu vingine vyote vya Lgewisenga na sehemu nyingine utafanikiwa? Nijue kama umeme Peramiko mwaka huu utakwenda kwa sababu hizo ni ahadi zilizo katika *Hansard*, hizo ni ahadi za Mheshimiwa Waziri na hivyo vyote vinaonekana kwa maandishi na kwa kweli nasikitika sana.

Mheshimiwa Spika, naomba wananchi wa Songea wapewe matumaini kwa kuzalisha na kulisha nchi hii kwa kupelekewa umeme. Tumechoka kupokea majenereta yaliyokwishatumika. Sisi ndiyo tunayapokea kila siku wakati sisi ndiyo tegemeo la nchi hii ya Tanzania, tumechoka, nasema tumechoka Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo, naomba sana wakati wa majumuisho, nipatiwe majibu ya msingi.

Mheshimiwa Spika, naomba kusema siungi mkono hoja hii. Naomba kusema simpongezi Waziri ila nampa pole kwa sababu kwa kweli haya ni mapambano, ahsante sana. (*Kicheko/Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Naona Waziri alikuwa akiandika andika hapo, naona anayo majibu.

Sasa namwita Mheshimiwa Ole-Sendeka, ajiandae Mheshimiwa Raynald Mrope na nadhani baada ya hapo ni Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi mchana wa leo ili niweze kutoa mchango wangu kwa niaba ya wananchi wa Simanjiro kwa bajeti ya rafiki yangu, Waziri wa Nishati na Madini, kwa kuzingatia mazingira ya Simanjiro na mazingira ya Taifa letu na mahitaji ya Simanjiro na mahitaji ya Watanzania kwa ujumla wao.

Mheshimiwa Spika, Waswahili wanasema:-

“Chanda chema uvishwa pete na si stahiki ya kichwa cha jogoo kuvishwa kilemba”.

Kwa mantiki hiyo, naomba nichukue nafasi hii ya mwanzo kabisa, kuishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kwa mambo mengi muhimu na mazuri kabisa ambayo

wamekuwa wakiwafanya Watanzania kwa muda wa uhai wake wa miaka hii karibu mitatu sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini nimeona nishukuru kwa sababu kwa mara ya kwanza tangu uhuru wa Tanganyika, Wilaya ya Simanjiro, Makao Makuu ya Wilaya, Orkesumet, tunatarajia wakati wowote katika wiki ijayo, *bulb* ya kwanza itawaka Makao Makuu ya Wilaya ya Simanjiro. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii inadhihirisha usikivu wa Serikali yetu na umakini wa Serikali katika kushughulikia mambo ya msingi hasa ahadi zake za Ilani ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Simanjiro, wamepata matumaini hasa kwa vijiji hivyo viwili ambavyo umeme utawaka. Lakini ni imani yangu pia kwamba Serikali iliyotusaidia ya Sweden ambayo pia ndiyo iliyosaidia Wilaya ya Ukerewe, Serikali yetu itaendelea kuishukuru kwa jinsi ambavyo wamekuwa wakisaidia miradi ya maendeleo. Bado wananchi wa Wilaya ya Simanjiro, kwa maeneo mengi, wanatarajia awamu ya pili ya mradi huo, uendelee katika vijiji vile ambavyo vilikuwa vimesahaulika au vimepitwa kulingana na utekelezaji ambao kidogo ulikuwa na mushkeli katika vijiji vya Ngage na Ngage B na Loiborsoit, kitongoji cha Engurash na Viji vya Lendenai, Naberera, Lengijape na awamu ile nyingine ule umeme uliokuwa unapitia Wilaya ya Arumeru ambao ulitarajiwa kupita katika vijiji Oiborkishu, Losunyai, Terraz, ili kuweza kutoa umeme kwa upande wa Magharibi mwa Wilaya ya Simanjiro. Kwa hiyo, naishukuru Serikali kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili ambalo napenda kuishukuru Serikali na hasa nimshukuru kipekee Mheshimiwa William Ngeleja (Mb.), Waziri wa Nishati na Madini, kwa uamuzi wa kijasiri alioufanya hivi karibuni wao na Bodi ya *TANESCO* wa kuvunja mkataba japokuwa nimeona neno kusitisha. Sasa wataalamu wa lugha watatusaidia baadaye, kuvunja mkataba na kusitisha mkataba, labda pengine Mheshimiwa Waziri baadaye atatueleza tofauti yake ni nini, ili aweze kustahili kupokea pongezi hizi. Kwa sababu ninapenda kusikia neno kuvunja mkataba na *DOWANS*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu tulikwifashanya maamuzi hapa na watu wazima wenye akili timamu wanapokutana katika mazingira huru na ya haki, wakalijadili jambo na kufanya uamuzi, busara inawatwika wajibu wa kutetea na kuyasimamia maamuzi waliokwisha kuyafanya.

Mheshimiwa Spika, tulifanya maamuzi katika Bunge lako Tukufu, kazi yetu ya sasa ni kudai utekelezaji wa maamuzi tuliyoyafanya kufuatia Ripoti ya Tume ya Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, si kujadili upya wala siyo kusaka utakaso katika

milango ya uani. Suala muhimu ni kuwa Watanzania wanasubiri taarifa ya Serikali juu ya utekelezaji wa Maazimio 23 na Azimio moja ni hili ambalo Mheshimiwa William Ngeleja na Bodi ya *TANESCO* wamefanya la kuvunja mkataba huo.

Mheshimiwa Spika, nasema huu ni mwanzo mzuri na ninataka niwahakikishie kabisa kwamba laiti hata Baba wa Taifa, marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere angekuwepo hapa, angefurahi. Kwa sababu gani? Marehemu Mwalimu Nyerere, mwaka 1962, katika Kitabu cha TANU na Raia, alipokuwa akizungumzia juu ya namna bora ya Watanzania kunufaika na utajiri wa nchi yao, alisema mambo haya na kwa ruhusa yako, naomba kunukuu kwenye hotuba yake, mwaka 1962, miaka miwili kabla mimi sijazaliwa. Mwalimu alisema hivi:-

“Leo tumeanza kupiga baragumu la pili na baragumu hili, ni baragumu la kuongeza utajiri wa nchi yetu kama vile mwanzo tulimwomba kila mwananchi kushiriki na wenzake kuondoa umaskini. Swalii ambalo hatuna budi tuijulize ni hili. Tunawomba kila raia kufanya kazi kwa bidii ili kuondoa umaskini wa nani? Umaskini wa viongozi wa TANU au wa watumishi wa Serikali au wa watu wachache wenyewe elimu au nguvu au bahati au ujanja? Narudia au ujanja au shabaha yetu ni kuondoa umaskini kwa kila mtu kama vile shabaha yetu ya kwanza ilivyokuwa kuleta uhuru na heshima kwa kila mtu?” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, nimeona ninukuu maneno haya ya Baba wa Taifa, Marehemu Mwalimu Nyerere ili kutahadharisha juu ya njama za siku hizi zinazoenea za wajanja wachache kutumia nafasi zao kujineemesha na kuyapuuza maslahi ya Watanzania kwa ujumla wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini Waswahili wanasema:-

“Usiulize sana mahali ulipoangukia ni vizuri kutazama mahali ulipojikwaa”.

Mheshimiwa Spika, ukiona mikataba hii ambayo leo Mheshimiwa William Ngeleja anashughulika nayo, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda, anashughulika nayo, Mheshimiwa Rais wetu mpandwa, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, anashughulika nayo, ni lazima tuijulize ni wapi tulipojikwaa na si wapi tumeangukia.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa ni kutotimiza wajibu wetu kwa kuchagua viongozi waaminifu au watendaji waaminifu na wenyewe uzalendo na ambao uzalendo wao na uaminifu wao umejidhihirisha. Katika Mwongozo wa Chama cha CCM wa mwaka 1981 katika ukurasa 104, unasema Chama kuongoza maana yake, naomba kunukuu:-

“Chama kuongoza maana yake ni kuhakikisha pia kuwa madaraka muhimu ya Serikali na ya Mashirika ya Umma yanakabidhiwa kwa watu ambao pamoja na uwezo

wao wa kitaalam ni wenye msimamo wa kizalendo na waaminifu kwa Chama na kwa wakulima na wafanyakazi wa Tanzania” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, tatizo linalotukumba leo na ambalo linatuadhibu katika mikataba hii mibovu ambayo leo tunaipa jina la ufisadi kutokana na watu wachache kujineemesha kwa kile ambacho hawakustahili, ni sisi kupuuza mambo yetu ya msingi ya kuhakikisha kabisa kwamba watu tunaowakabidhi dhamana hii uaminifu wao, uzalendo wao hautiliwi mashaka kwa namna yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Bodi ya *TANESCO* kwa ujasiri huo na naipongeza Serikali kwa uamuzi huo iliyofanya kwa *DOWANS*. Nataka waende kwa *IPTL*, nataka waende *ALSTOM*. *ALSTOM* wamechukua fedha zetu bila wao wenyewe kufanya kazi. Wameweka maboya tu ya mitambo pale Mwanza na hatimaye tukawalipa mabilioni ya fedha na fedha hizo za Watanzania zimepotea na walioitungiza kwenye mikataba hiyo bado wana nafasi katika Wizara hizo. Ningefarijika leo kusikia kwamba hao wanaohusika katika kutuingiza kwenye mikataba hiyo, wamekaa pembedi ili tuitakase safu yetu na kuwa na timu ambayo inaaminika katika mambo ya msingi yaliyobainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama chetu na Sera za msingi za Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukifanya hivyo, hapatakuwa na nafasi tena ya watu wachache kuendelea kubeza baadhi ya maamuzi ambayo tunayo kwa sababu ujasiri huo wataukosa. Ujasiri wa leo, wanaupata kwa sababu wana fedha nyingi ambazo hazina kazi.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchukua nafasi hii, kipekee kuwapongeza na kuvishukuru Vyombo vya Habari, nchini wamekuwa mstari wa mbele kufichua ufisadi unaofanyika na mikataba mibovu. Waandishi hao kwa kweli wanastahili pongezi. Hata mikataba ya *IPTL* ilikwishaandikwa kwa muda mrefu, mikataba ya *DOWANS* ilikwishaandikwa kwa mufa mrefu na sasa nataka niwapongeze hao ambao wanaendelea na msimamo huo na ambao hawayumbi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kwa dakika zilizobaki, nzungumzie suala la uwiano wa maendeleo ulio sawa na kudhihirisha kwamba uwiano wa maendeleo ulio sawa huleta matumaini yaliyo sawa katika nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, tukianza kuwatumikia Watanzania kwa uwiano ulio sawa, tutawapa matumaini yaliyo sawa na kwa maana hiyo, tutadumisha amani na mshikamano ndani ya nchi yetu na hakuna mtu ambaye atanung’ unika.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa nimefanya dhambi kubwa sana nisipotumia nafasi hii kuzungumzia mambo machache katika Tume ya Bomani.

Mheshimiwa Spika, kama kuna Tume iliyofanya kazi iliyowagusa wapiga kura wangu wa Mererani, ni Tume ya Jaji Mark Bomani. Imefanya kazi ya kuheshimika na ninapenda kuiomba Serikali izingatie mapendekezo yote ya Tume hiyo ya Rais iliooongozwa na Jaji Mark Bomani na wameeleza dhiki wanayoipata wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo wa *Tanzanite* pale Mererani wanapewa mita 50 kwa 50, lakini *geology* ya uchimbaji wa madini ya *Tanzanite* inadai uchimbe mgodi kwenda mshazari siyo kwenda *vertically*, unatakiwa kwenda *horizontally* katika *angle* ya nyuzi 45, unatakiwa kwenda mshazari. Katika mazingira hayo unapokuwa umepewa eneo la mita 50 kwa 50, huwezi kuchimba madini ya *Tanzanite*. Hatutakuwa tukitengeneza mazingira muafaka na ushindani ulio sawa unapowapa wachimbaji wadogo wa *Tanzanite* maeneo madogo ya kuchimba wakati yale makampuni makubwa ya kigeni yanapewa maeneo makubwa.

Mheshimiwa Spika, naunganana na Tume ya Jaji ya Mark Bomani, kwa pendekeso walilolitoa la kuhakikisha kwamba madini ya vito yanachimbwa na Watanzania pekee yao lakini nafikiri kwa kuanzia tuanze na *Tanzanite*. *Tanzanite* ni madini ya pekee ambayo yamebeba heshima na jina la Tanzania pekee, hakuna mahali pengine ambako unaweza kupata *Tanzanite*. Tukiwaachia watu wachache wachimbe madini hayo na kwenda kuyaweka kwenye *stockpile* kwenye nchi zao, ni hujuma kwa nchi yetu. Mimi nataka niwaambie, tutakuja kuyajutia haya. Ni afadhali kutokea sasa Serikali iangalie uwezekano wa kufidia hao wawekezaji wakubwa waondoke ili wapishe wachimbaji wadogo waendelee kuchimba madini ya *Tanzanite*.

Mheshimiwa Spika, malalamiko yaliyopo katika uchimbaji wa madini ya vito. Wachimbaji wadogo hawapati huduma muhimu zinazohitajika, hawapati vifaa vyta kisasa vyta kuchimbia, lakini bado nataka niwaambie kuchimba *Tanzanite* huhitaji mitambo mikubwa, kunahitajika uchimbaji mdogo ili jambo hili liweze kuwa endelevu. Kwa hiyo, lazima tufike mahali tuangalie mahali ambapo tulijikwaa na tulijikwaa pale ambapo tuliwapa wageni waweze kuchimba madini hayo. Mimi bado ninasema hata ikilazimu kuendelea kupata wafadhili, huyo mgeni anayechimba madini ya *Tanzanite* apewe pungufu ya asilimia 50.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mererani ambao wanachimba madini ya *Tanzanite* na Naisinyai, nataka niwahakikishie kabisa hakuna chochote cha maana wanachokipata wao kwa wawekezaji waliopo pale. Kinachofanyika ni kuhamishwa kwa madini yale. Wananchi wa Naisinyai katika Kitongoji cha Emishiye hawana maji, hawana shule nzuri, hawana huduma muhimu, maji wanayoyatumia, watoto wanaozaliwa, wanapinda miguu na Mkemia amekwishathibitisha kabisa kwamba maji

yale hayafai kwa matumizi ya binadamu lakini majirani zao wapo watu wanaozalisha madini kwa mabilioni ya shilingi.

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia suala la ajira kwa wazalendo wanaoajiriwa katika migodi hii litazamwe ili kuhakikisha kwamba Watanzania wenye elimu na walioajiriwa katika migodi ya wawekezaji wakubwa wanalipwa mishahara inayolingana na wenzao wenyе taaluma inayolingana na yao wanaotoka katika nchi za kigeni.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kabisa ukiangalia wazalendo walioajiriwa, wanalipwa kima cha chini na mgeni mwenye elimu ndogo kuliko ya kwao analipwa fedha nyingi zaidi.

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia niungane na Tume ya Jaji Mark Boman, kwamba wale wanaopitishwa kwenye *X-Ray* katika migodi hiyo mikubwa, *X-Ray* hizo zikaguliwe ili zifulikane kama zina athari kwa maisha ya wale wanaofanya kazi pale ili ikiwezekana kuzisitisha mara moja na wale wenyе migodi watafute namna bora ya kulinda madini yao kuliko ilivyo sasa ambapo kila asubuhi na jioni na kila kukicha wanapita katika *X-Ray* na madhara yake wakati mwingine vijana wanalamika kuwa wanadhirika.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri Wizara ya Nishati na Madini, ikajithibitishia usalama wa mitambo hiyo ili kuwapa Watanzania matumaini. Kutofanya hivyo ni kuendelea kuwapa Watanzania mashaka kwamba Serikali haikuwasikiliza kwa kiwango stahiki.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, ahsante sana.

Sasa ni nafasi ya Mheshimiwa Raynald Mrope, atafuatiwa na Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba wakati huo huo Mheshimiwa George Simbachawene, ajiandae.

MHE. RAYNALD A. MROPE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii adimu ili nami niweze kuchangia kidogo juu ya Wizara hii ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze ndugu yangu, Mheshimiwa William Ngeleja, pamoja na Naibu Waziri wake pamoja na Katibu Mkuu. Nasema nawapongeza kwa sababu mwanzoni kwa kweli nilikuwa nimejiandaa kupinga hoja lakini hivi karibuni kwa kweli kumekuwa na sababu nyingi, safi sana ambazo zimenifanya niunge mkono hotuba hii moja kwa moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu katika mchango wangu wa tarehe 16 mwezi Juni, nilitoa kilio kikubwa cha wananchi wa Masasi ambao kwa wakati ule walikuwa wanapata umeme kwa muda wa masaa manne tu. Leo ninavyozungumza, wanapata umeme kwa masaa matatu kuanzia saa tisa usiku mpaka saa 12 asubuhi, sasa haya ni mambo gani? Ndio! Kweli katika hali hii, mtu unaweza kuunga mkono hoja? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini nitawaelezeni baadaye mambo gani ya ajabu kayafanya ndugu William Ngeleja yanayonifanya niweze kuunga mkono hoja yake. Katika mchango wangu labda ninukuu tu *Hansard* ya tarehe 16 nilisema kwamba:-

“Ninachokiomba ni uunganishaji wa kilomita 32 kati ya Nyangao na Ndanda zilizobakia na Waziri wa Nishati aiombe GNT yaani Government Negotiating Team ikutane mara moja ili mkataba kati ya Artumas na Serikali ukamilishwe ili tuweze kupata umeme wa uhakika”.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka kusema kwamba kwa namna ya ajabu kabisa Mheshimiwa William Ngeleja, aliitisha hiyo Kamati ya *GNT* kukutana tarehe 30 mwezi Juni. Sasa *speed* ya namna hii, haijapata kutokea, tulizungumza tarehe 16 tayari tarehe 30 Kamati nzito kabisa ilikutana na juhusisha Wizara nzima ya Nishati wakiwemo *TANESCO, TPDC*, Wizara ya Fedha (Hazina), akiwepo Kamishna wa Sera na Fedha za Nje. Pia wenzetu kutoka Canada kwa upande wa Artumas walikuwepo na washauri kutoka Jumuiya ya Madola nao tulikutana kuanzia tarehe 30 mpaka tarehe 5 mwezi Julai, kuhusu suala hili la umeme kukosekana katika Wilaya yangu ya Masasi.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri, mimi ni Mbunge pekee niliyekuwepo katika Kamati ile. Ndiyo maana nikasema kwamba ninaunga mkono hoja kwa sababu naamini kabisa vijana hawa William Ngeleja na Mheshimiwa Adam Malima, ni *Boys II Men* wa Marekani yaani unawaona kama *boys* lakini wanaelekea utu uzima, ndivyo wanavyofanya mambo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa tulivyokuwa katika mkutano ule juzi tu, nilielezea juu ya mateso makubwa wanayopata wananchi wa Masasi, Nachingwea, Ruangwa, Newala na Tandahimba kwa kukosa nishati hii toka pale *Mnazi Bay*. Nilielezea vizuri kabisa hali ilivyo na kila mmoja alisikitika. Katika kusikitika huko, wakaamua tufanye mpango madhubuti ambao ndiyo utatatua tatizo tulilonalo. Kwa hiyo, kuanzia wakati huo, niliona mwanga katika lile tanuri. Ndiyo maana nasema kwa kweli inawezekana kutakucha yaani “kuchele” katika eneo hili kwa mambo yote yanayohusiana na umeme.

Mheshimiwa Spika, maamuzi yaliyofanyika pale, ni kwamba kazi ya ujenzi wa Nyangao mpaka Ndanda yaani kuweka nyaya, nguzo, vikombe na kadhalika itaanza mara moja na ilikadirwa kukamilika tarehe 30 mwezi Machi. Kazi ya ku-*upgrade* sehemu ya Mnazimmoja mpaka Nyangao, tulikubaliana ikamilike mwezi Januari. Kazi ya kuweka

transformer kwa upande wa Mtwara ili kuongeza nguvu katika uzalishaji wa umeme, nayo tulikubaliana kwamba ikamilike ifikapo tarehe 30 mwezi Aprili, halafu kazi iliyobaki ya kuhakikisha kwamba umeme wa Masasi unabadilishwa kutoka 11KV mpaka 33KV, kazi hii ikamilike katika miezi mitatu, Aprili – Juni, 2008.

Mheshimiwa Spika, sasa maana yangu ni kusema kwamba mradi mzima utaweza kukamilika mwakani hasa hasa ifikapo tarehe 30 Aprili tunategemea unaweza ukakamilika ikifika mwezi Juni, eneo lote la Masasi umeme huu utapatikana. Ndiyo maana nikasema kwamba hapa ni lazima tuunge mkono hoja hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ila kilichobaki kikubwa wahakikishe kwamba zinapatikana fedha shilingi bilioni tano kutoka Hazina. Shilingi bilioni tano hizi, zinaweza kutoka katika mfuko wa bajeti yetu ya *Mnazi Bay* ambayo ni ya shilingi bilioni 7.5. Kwa hiyo, zikitolewa hizi shilingi bilioni tano mara moja maana yake ni kwamba kazi hii inaweza kuanza. Ninavyoona kwa jinsi shida ilivyo kubwa kule, leo jioni tukipitisha bajeti yake, kesho aanze kutoa hela ziende katika kufanya kazi hii kwa sababu kwa kweli kuna mateso makubwa sana kwa watu wa Masasi, Nachingwea, Ruangwa na nyine nilizozitaja na inawezekana tu ikiwa fedha hizi zitatoka mara moja ili kuhakikisha kwamba tunasambaza umeme katika maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, hakuna njia nyine ya urahisi kusema kwamba zinunuliwe *transformer* kwa ajili ya maeneo haya itakuwa ni gharama kubwa na bei ya mafuta sasa hivi nimesikia Masasi imeshafika 2500 kwa lita. Sasa kuendesha majenereta hayo itakuwa ghali sana. Kwa hiyo, ni afadhali tuharakishe upatikanaji wa fedha hizi ili kazi hii iweze kuanza. Tunaelewa kwamba mara baada ya bajeti, siku kadhaa zanapita kabla ya kuweka saini, lakini mimi naomba watumie njia zote za kimapinduzi na ndiyo maana nimewaita *Boy II Men*, watumie njia za kimapinduzi zipatikane hizo fedha kesho kazi hiyo ianze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili nililotaka kuzungumzia ni kuhusu matumizi bora ya gesi. Katika wiki hii niliyokuwa Arusha, nimejifunza mambo mengi sana. Nilikutana na wataalamu wa kila aina wa mambo ya gesi. Kama nilivyosema, kulikuwa na wataalamu kutoka *Commonwealth* na kadhalika. Kusema kweli hawa wataalamu wengi walisema kwamba inaonekana kama Tanzania haina nia ya kutumia vizuri gesi yake.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu sasa hivi shughuli ambayo tunayoweza kuifanya mara moja ni kuichimba gesi ile na kutengeneza gesi iliyoyeyushwa *CNG*. Hii *CNG* yaani *Compressed Natural Gas*, ni fedha taslimu. Hata hapa nje ya Bunge, wenzetu wa *TPDC* wametuonyesha kwa kutumia *CNG* ndiyo unaweza kuendesha magari, unaweza kutumia majumbani na ndiyo unaweza kutumia kwa vitu vingi. Kwa hiyo, tutafungua uchumi kwa namna ya pekee ambayo haijawahi kutokea kuliko kwa hivi sasa kusubiri mpaka kiwanda cha mbolea kije kukamilika. Kiwanda cha Mbolea, kitatuchukua si chini ya miaka mitatu ambapo kutengeneza *CNG* katika mwaka mmoja tunawenza kufanya hivyo. Kwa hiyo, Serikali badilini mwelekeo mhakikishe kwamba mara moja

tunakamilisha mipango ya kutumia gesi yetu hii na iyeyushwe iwe *CNG*. Tukifanya hivyo, tutaweza kuibua mambo mengi sana yatakayotufaa katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema viwanda vya mbolea, viwanda vya *cement* vitakuja baadaye lakini kwa wakati huu, la muhimu ni kwanza, tutumie gesi yetu kwa ajili ya umeme. Naelewa kwa sasa hivi kwa pale Mtwara peke yake, tunaweza kuzalisha kiasi cha *MW 30* lakini gesi iliyopo pale inaweza kuzalisha *MW 300* ambazo zinawenza kusambazwa kwenye Gridi ya Taifa, jamani mambo haya ndiyo kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, halafu la pili kwa umuhimu iwe *CNG* na tatu iwe ya mbolea na nne iwe ya sementi. Tukifanya hivi, nchi yetu itabadiika hasa zaidi kiuchumi. Nchi nydingi sasa hivi zenyenye mafuta na nchi nydingi zenyenye gesi, zinafanya mipango mikubwa.

Mheshimiwa Spika, hata pale jana katika mchango wake Mheshimiwa Getrude Mongella ambaye ni Rais wa *Africa Union*, alisema ni lazima tufanye mipango ya kuuza gesi yetu nje ya nchi. Sasa hilo sikuliona katika hotuba ya Waziri, nataka kulisisitiza tuwe na mipango ya kuuza gesi nje ili nchi yetu iweze kupata manufaa ya gesi iliyopo kwa wingi hivi sasa. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nataka kusema kwamba katika suala hili la gesi kwa upande wa wenzetu wenye madini wanapata mrahaba lakini hakuna mpango wowote wa kulipa mrahaba. Kwa hiyo, naomba Waziri aweke suala hilo la mrahaba kwa wote wanaotoa gesi ili nao wanufaikie.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, tayari muda wako umekwisha.

MHE. RAYNALD A. MROPE: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, naunga mkono hoja hii. (*Makofit*)

SPIKA: Mheshimiwa Raynald Mrope, ahsante sana.

Nitamwita sasa Mheshimiwa Kabuzi Rwiomba atafuatiwa na Mheshimiwa George Simbachawene lakini kwa kuweka uwiano baada ya hapo, nitamwita Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa.

MHE. KABUZI F. RWIOMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja nyeti iliyo mbele yetu. Napenda nikiri kwa furaha kabisa kwamba huu ni mwaka wangu wa saba katika nyumba hii Tukufu. Nilikuwa sijawahi kuunga mkono hoja ya Nishati na Madini kwa sababu ya mazingira niliyokuwa nayo. Lakini kwa bajeti na jinsi ilivyowakilishwa, nitaeleza sababu. Kwa mara ya

kwanza naunga mkono bajeti hii, naunga mkono kabisa kwa nguvu zangu zote na ninazo sababu tatu za msingi ambazo zimenifanya niunge mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sababu ya kwanza, katika ukurasa wa 77, naishukuru Serikali na Mheshimiwa Waziri na wenzake, wameweza kutaja Kata zangu 13 kwamba zitapewa umeme na zimetajwa, ziko kwenye ukurasa wa 77. Kwa kweli ilikuwa ni ndoto. Ni ombi la muda mrefu, ni kilio cha muda mrefu, lakini wamesema sasa kwa njia ya *MCC* wanapeleka umeme, nashukuru sana. La pili ni ripoti hii ya Kamati iliyoundwa na Rais ya Mheshimiwa Jaji Bomani. Jana nimeipitia kidogo kwa haraka haraka na nilikuwa nimekasirika kwa nini ilikuwa imekuja imechelewa. Lakini imegusa karibu kila kitu, malalamiko yote kuhusu madini, imegusa karibu kila kitu, kwa kweli sikuona sababu kwa nini nianze kugombana na Serikali wakati ninayoyahitaji yameletwa. Namshukuru Mheshimiwa Rais, nafikiri yeye amemaliza kazi yake, kilichobaki ni kwa Mheshimiwa Waziri na wenzake kulileta kama Mheshimiwa Malecela alivyosema kwamba liletwe Bungeni tulijadili tulipitie. Kwa hiyo, nashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatu ni watendaji wa Ofisi ya Wizara ya Nishati na Madini. Kwa kweli nimekwenda, wamenipa ushirikiano, nilikuwa nafuatilia suala la umeme, kuna Mzee Mrindoko, Magambo, Wakea pamoja na mama mmoja na wengine, walinipokea vizuri wakanipa maelekezo, nikaona kwamba kuna dalili ya umeme. Kwa hiyo, wanafanya kazi vizuri sana na ni waadilifu. Hiyo ilinipa moyo na watu wangu wa Busanda nilipokwenda nikawaeleza kwamba kuna kitu kinakuja. Nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, labda niseme kuhusu hii ripoti. Ripoti hii nadhani kuna haja ya kuiangalia na kuifanyia haraka. Katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 31, napenda niseme kwamba mimi sikubaliani nao. Ametoa mpaka mwezi wa Aprili kwamba sheria itakuwa inafanyiwa kazi, anawapa mwaka mzima waendelee kuchimba. Nadhani Mheshimiwa Waziri haelewi wenzetu wanafanyaje kazi. Wenzetu hawafanyi kama sisi tunavyofanya Kiswahili. Ukiwapa mwaka mzima, hesabu ni miaka miwili *they are working 24 hours*. Wanapokwenda mle mgodini kwanza wanaondoa simu, hakuna kupiga simu ni kufanya kazi masaa 24 wanachimbua.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri akimaliza atoke hapa aende akatembelee mgodi wa Geita, *Barrick* na migodi mingine. *Barrick* ukienda juu utaona kama hakuna mgodi pale, lakini nenda kule chini ni wazi, wanachimba sasa hivi kama wako Geita. Sasa unawaambia tuendelee mpaka mwezi wa Aprili, tuanze sasa hivi. Kuna mambo ambayo humu yametajwa ambayo hayahitaji kusubiri, yanahitaji kufanyiwa kazi, nikukubaliana nao tukaelewana, wananchi wakaenda vizuri.

Mimi nasema hivyo kwa uchungu kwa sababu maeneo ninayotoka naogopa hata kusema kwamba natoka Geita. Nikisema natoka Geita watu watafikiri nina nafuu, lakini wakifika kwangu inakuwa aibu. Kuna Wabunge wametembelea, wameona huruma. Watu wengi, hakuna huduma, hakuna maji, hakuna barabara, shida tupu! Unasema unatoka Geita! Lakini kitabu kimetaja hata suala la mrahaba ukurasa wa 167 waliokuwa wanaikataa, kitu *impossible* mrahaba kugawana, wameeleza vizuri kwamba kuna haja ya kuliangalia hili suala kwamba watu wanapokaa kama nchi nyingine wanazofanya ziende

kule, sio lazima kugombana na wale wawekezaji. Vimetajwa vitu vingi na maeneo makubwa, wametaja kwa nini wachimbaji wadogo wasipewe maneno hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba sana, nafikiri ni *typist* alikosea. Mheshimiwa Waziri ana akili nyingi, nadhani alikosea hebu rekebisha hapo kwamba tuanze sasa hivi. Nilikuwa naomba tuanze sasa hivi na ninaomba kama walivyoomba asubuhi hii iletwe haraka tujadili ikiwezekana tuyunje siku moja tujadili. Hii ni muhimu sana kwa maisha ya Watanzania. Hatuwezi kuendelea kusubiri tena mwaka mwingine wenzetu wanaendelea, wana kitu wanaita *high grading* na wanachukua zile *juice places* ndizo wanachukua wewe utabaki na nini? Mheshimiwa Ngeleja nakuomba usije ukaingia katika eneo la watu ambalo utakuja kupigwa, kaburi lako litakuja kupigwa fimbo kuwa na wewe uliharibu. Wewe sasa hivi unakwenda vizuri na sisi tulishaona kwamba tutapigwa viboko kwa sababu tulikuwepo kwenye uongozi na tukayaharibu mambo. Sasa hebu nyoosha vizuri hapo.

Mheshimiwa Spika, lingine linahusu umeme. Nashukuru sana Mheshimiwa Ngeleja aliwahi kwenda kule kwenye maeneo yangu na nilikuwa naomba tukitoka hapa, kwa kuwa ana kazi nyingi, niende na Mheshimiwa Naibu wake tukawahakikishie wananchi kwamba umeme utakuja. Kuna maeneo yametajwa Bukori, Nyarugusu, Kamena, Rwanmwasa, Katoro, Butundwe yote mpaka Bukondo na Nungwe. Naomba uhakika wa hii *MCC Challenge* kwa sababu tunatakiwa tuanze na huu ni *grant*, najua *grant* kutoka Marekani sasa tumepewa twende haraka.

Kwetu wanasema: “*Mfwa wimbwa unyobwagushushe.*” Mchuzi wa mbwa hunyewa ungali moto, usichelewe chelewe. Wazinza wanasema sayansi ya wafugaji wanasema eti “*Ente eyomusazi etemwa alo yagambirwa.*” Yaani kama baba yako unamwona ni wa mashaka mashaka au wakati mwingine hawapi hata nyama, kitoweo hata nyumbani haleti, lakini anageuka geuka akikwambia kwamba, akiwaambia wanangu leo tunakula ng’ombe mniamwuliza ni ng’ombe gani? Yule pale! Funga kamba, chinja haraka, kwa sababu ikipita nusu saa atageuka, hamtakula nyama siku hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa hii tuliyopewa tusichezecheze, kama fedha zimekuja nitasikitika, humu umeandika halafu wanasema fedha tena zipo, ni *grant* hii zikiondolewa ni tatizo. Naomba tujitahidi ziweze kufanyiwa kazi haraka na kama ndivyo, naomba nitoe ushauri ufuataao. Niliwahi kuwatembelea wataalamu wako, umeme unaokwenda Katoro upitie vijiji ambavyo ni vya muhimu vile vile. Unapokwenda Bukori upitie Buyagu, Nyarwanzajwa, Kamena, uende Nyamalimbe, uende Bukori halafu uende Nyaruyeye mpaka Nyarugusu halafu uende kwenye kituo cha afya cha Busanda. Unapokwenda Geita badala ya *taping point* ambayo unafikiria pale Samina wasifanyie pale *Taping* utapita porini kwenda kufika Nungwe. *Taping point* upite Msasa, uende Chibingo ndio pawe na *taping point*. Unakwenda kwenye kituo cha afya unakwenda Sekondari Nyakagomba, unakwenda Chigunga pale ndiyo kuna *diversion taping* nyingine na unakwenda Nungwe, halafu ndio unakwenda Nyechulumu kituo cha afya na unakwenda Bukondo na kisha mwingine uende Katoro, sasa utakuwa umefanya kazi nzuri na Mungu atakubariki sana. Warumi 13 wanasema: “Mamlaka yanatoka kwa Mungu usi-*abuse* nafasi hiyo.”

Mheshimiwa Spika, napenda nizungumzie wachimbaji wadogo. Wachimbaji wadogo ndio waathirika wakubwa sana kwenye maeneo yetu. Nashukuru kwenye kitabu chake amezungumza na kweli sehemu za Nyarugusu wamepewapewa na sehemu za Rwanagwasa wamepewa eneo, lakini wamepata eneo kwa mapambano makali sana na *East African Mine* mpaka wamechoma magari. Hatupendi tufikie kule. Basi tunaomba hii sheria ipite haraka hata *GGM* wawape sehemu kama Nyamatagata, imekaa wanasesma ni eneo la *GGM* lakini kama ungfanyika utaratibu kwa nini wachimbaji wadogo wasipewe na wenyewe wakajisikia vizuri?

Mheshimiwa Spika, kuna eneo lingine kama la Matabe, eneo la Matabe liko ndani ya msitu, *Berrick* ndiyo ilikuwa inafanya kazi pale, tukaomba *Berrick*, *Berrick* kwa wema wao wakawaachia wachimbaji wadogo. Sasa wamepewa wachimbaji wadogo ikawa kama wamekosea dunia haya *DC* akaja na bunduki, *RPC* fukuza, wamefukuzwa kama mbwa. Inasikitisha sana, wakati *Berrick* ikiwemo hapakuwa na maneno, wameachia, hawa wachimbaji wana mataitizo gani? Eneo lile sasa hivi kuna wachimba mkaa na wakulima, ni eneo dogo ambalo wangeweza kuachiwa, kwa nini tusiwape wachimbaji wetu? Bahati mbaya tulishaleta hoja hiyo, Kamishna wa Madini anajua, Waziri akaandika barua Maliasili, barua ikaandikwa na Waziri, Maliasili hawakujibu. Tukafuatilia wakasema imepotea. Barua ya Waziri inapotea! Kama ya Waziri inapotea, ya kwangu itakuwaje? Si itachomwa moto! Mahusiano gani hayo? Naomba hilo wakati wa kufanya majumuisho Mheshimiwa Waziri anijibu.

Hili ni suala la Matabe. Bahati nzuri, nilikuwa nanong'ona, nilikuwa nazungumza na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili akasema, lakini nadhani kisehemu kidogo ya yeze anafahamu. Naomba Mheshimiwa Naibu Waziri akija kule twende wote, naomba aje na wataalam wake wa madini na mtaalam wa mambo ya *MCC Challenge* tuweze kuangalia maeneo na yale niliyosema kuyapitisha. Lakini naomba sana wachimbaji wadogo wafikiriwe kwa sababu wachimbaji wadogo ndio wanaajiri watu wengi, fedha zinabaki hapa hapa. Sasa tunaanza kuwatupa na ni *time bomb*, kwa kweli tukiwaacha hawa watu, ndio watu wanaoweka hapa fedha. Hawa wengine siwezi kuzungumza tena sana kwa sababu nimeshalia sana kwa mateso walijonayo watu wangu wa Sagulwa hiki kitabu nilivyosoma kimenipa faraja na Rais amenipa faraja. Rais amemaliza kazi yake tusimtake Rais aje asimame humu tena, ni kazi kwetu, tukishindwa kufanya, basi ni sisi wenyewe tunaobadilisha na kuuza wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa mara ya kwanza naunga mkono hoja katika Wizara hii na naunga kwa nguvu zangu zote. Ahsante sana. (*Makofî*)

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Nishati na Madini. Lakini awali ya yote niwapongeze kwa ujumla rafiki zangu, Mheshimiwa William Ngeleja na Mheshimiwa Adam Malima kwa kupewa Wizara nzito, Wizara muhimu katika nchi hii hasa kwa kipindi hiki ambacho kila nchi inafanya biashara.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, lakini napenda tu nichukue nafasi hii kuwapa pole kwa uzito wa kazi walionayo nikiamini tu kwamba wataiweza na napenda niwatie moyo kwamba kazi hiyo wanaiweza na kwa hatua walizozifanya mpaka sasa inaashiria kwamba wana uwezo na wataiweza Wizara hiyo. Nchi hii ni ya kwetu wote. Nchi hii ni ya sisi tunaoishi sasa, lakini pia ni ya watu watakaokuja kuishi baadaye sisi tukiwa hatupo. Ukiangalia, natoa *statement* hii nzito kidogo kwa namna ambavyo naona tuna haraka na katika kila haraka tunayoifanya tunaanguka kwenye makosa.

Tunasema maneno mengi sana na tunayoyasema mengi sana hatuyatekelezi. Nikianza na suala zima la umeme na nataka nionyeshe kwa rafiki zangu hawa wawili niliowasema hapa, Waziri na Naibu Waziri kwamba wana kazi nzito kwa maneno haya. Makosa mengi ambayo yamekuwa yakifanyika ni *trend*, likitoka kosa hili linakuja kosa lingine Watanzania wanabeba mzigo. Likitoka kosa hili linakuja lingine wanabeba mzigo, sina hakika na hatua wanayokwenda kukanyaga na wao kama itakuwa salama au sio salama.

Mheshimiwa Spika, tuna makosa yaliyotokana na *IPTL*, tukajikwaa pale, watu wapo na matatizo yapo tukaenda *Songas* kuna matatizo, tumekwenda *RICHMOND* na *DOWANS* tumekuwa matatizo, tunaendelea *AGGRECO* huko *ALSTOM* ni matatizo. Sasa wenzangu hawa wanapewa mzigo huu watambue kwamba wana kazi na Watanzania wanataka matokeo ya kazi yao. Kazi yoyote unayoifanya ni lazima ilete matokeo kwa matarajio ya wanayoisubiri. Kwa kitendo cha kusitisha mkataba wa *RICHMOND* au *DOWANS* mimi nawapongeza sana Wizara. Tuendelee huku tukiwa makini kwamba mikataba iliyoingiwa ni mikataba *valid*, lakini sasa kama kuna *technical gap*, basi kuna kila haja ya kushughulikia mkataba mmoja baada ya mwingine ili tuweze kuondokana na mzigo huu ambao karibu shilingi bilioni 20 kila mwezi nchi inazipoteza kwa mikataba ya aina namna hii.

Mheshimiwa Spika, niliona niyaseme haya na niwajulishe wenzangu kwamba kwa maana ya nchi hii kuwa ya kwetu wote ya sisi tulipo sasa na wajao, basi ni vyema tukafanya mambo yetu kwa stahili ya kuangalia hata baadaye.

Mheshimiwa Spika, mimi naamini sisi wengine ni vijana wa juzi, kama nyinyi mlipoanza wazee mlioko huku ndani mngekuwa na haraka ya mambo, basi hii nchi tungeikuta imechakaa kabisa. Mimi nadhani wenzangu waone kwamba Wizara yao ndipo tunaposubiri kupata mbolea kwenye Wizara yao, ndiko tunakosubiri kupata saruji na ndiko tunakosubiri kupata gesi na mambo mengine. Kwa hiyo, ukombozi na uchumi wa Tanzania uko mikononi mwao. Maamuzi yao yanapaswa kuwa *bold*, yanapaswa kuwa na mtizamo wa kweli unaozingatia faida ya nchi lakini sio kufurahisha watu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba leo nimepata fursa ya kuwaambia rafiki zangu maneno haya huku nikiweka ushahidi kwa *public*. Ni matarajio makubwa kwa Watanzania kwamba tunaweza tukapata mafanikio makubwa tukiitumia Wizara yao kwa ufanisi na kwa matarajio ya Watanzania.

Lakini niwape tu changamoto nyingine kwamba yote tunayoyasema hapa nianze kwa mfano na *TANESCO*. Watanzania bado wanabeba mzigo mkubwa kwa gharama ambazo pengine hawazitumii. Sio Watanzania wote wanaoweza kuhesabu zile *units* kwa hivyo wenzetu hawa *TANESCO* wajaribu kutoa huduma na kuuza bidhaa ambayo ni halisi na ni haki kwa kila mtu kulipia. Mimi nina mifano mingi na mimi mwenyewe ni mtumiaji wa umeme nikiwa kabla sijawa kiongozi na hata baada ya kuwa kiongozi bado hakuna ukweli katika *readings* za *TANESCO*. Kwa hiyo, Watanzania wanabeba mzigo mkubwa.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ni pale ambapo mimi ni mteja, nimejenga nyumba yangu, nataka kuweka umeme, unaniambia nilipie nguzo, waya, *pole*, sasa katika *modern business this is too illogical*. Sasa *ownership* yangu iko wapi? Inaanzia kwenye nguzo na zile waya au baadaye tunakuja kufanya *business* gani? Maana yake hii mali ni ya kwako unaniambia nilipie mimi, nadhani kama kuna ma-*economist* na *TANESCO* ina watu wanaojua biashara, mimi nadhani wakae wafikirie hata kutumia lugha nyingine, lakini kusema mimi nilipie nguzo, waya halafu mimi sio mmiliki na hata baadaye hatuji kukatana kwa zile bili zinazokuja, awali mimi nadhani *this is a very great misconception*.

Ni maeneo ambayo Watanzania wanunung'unika na mimi huwa napenda ku-*deal* sana na maeneo ya manung'uniko, kwa nini mtu anung'unike? Tumeona hapa katika bei za umeme katika *East Africa* kwa Tanzania, Kenya na Uganda sisi tuko chini kwa hizi *rates* zetu, lakini manung'uniko yapo kwa sababu hatutumii sayansi katika kufanya biashara ya kisasa na ndiyo maana pengine hata kwenye *negotiation table* katika mikataba yetu tunaingia mikataba ambayo siku zote tunaanguka kwenye hasara tu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naomba nihamie katika jambo la pili la umeme vijijini. Naipongeza Serikali kwamba angalau jimboni kwangu umeme unaweza ukafika kupitia mradi wa *MCC*. Lakini unaweza kufika kwa sababu pamoja na kusema Waziri amesema kwenye hotuba yake kwamba ziko fedha kupitia *MCC* na mimi nimepata miradi pale wa kwenda Wota na kwenda Pwaga. Lakini tunaogopa kusema wakati mwengine ahadi hizi zinatuponza kwa wapiga kura wetu. Unaweza ukasema hapa, halafu yasitimie. Kwa hiyo, kesho utaadhibiwa kwa hilo.

Mimi ningependa Mheshimiwa Waziri anithibitishie hapa *MMC* sawa, nimekubali, fedha zipo sawa; je, lini utekelezaji wa miradi hii utaanza? Maana tuweke *commitment* kabisa kwa sababu bila ya kufanya hivyo tunapata shida kuelezea kama ilivyokuwa kwa miradi ya maji ambayo leo Waziri ndio umetolewa ufanuzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili katika mradi huo wa umeme vijijini na hasa katika huu mradi wa *MCC* ni *designing* na *planning*. Tunapokuwa tuna mambo ambayo yanafanya bila kushirikisha *Local Government* kwa maana Halmashauri zetu lazima kunakuwa na mapungufu. Maeneo haya ni ya vijijini, lakini sina hakika katika *designing* na *planning* kama yalihuisha Halmashauri za Wilaya. Kama zilihuiska, basi ni kwa kiasi kidogo sana.

Kwa mfano unasema unataka kupeleka umeme Pwaga kutoka Kijiji cha Iyengi. Uki sema unapeleka umeme Pwaga tu sio *effective* na wala sio *economic* kwa sababu unapeleka Pwaga tu *straight forward* wakati unaacha *option* ya njia nyingine kutoka Kibakwe kuititia Ikuju ambako kuna shule ya sekondari, kuna zahanati kuititia Luhundwa ambako kuna shule ya sekondari, kuna zahanati kuititia Kidenge ambako kuna kilimo kizuri, kuititia Mingui hadi Pwaga inakuwa *more economic*. Lakini ukisema unakatisha tu kwa sababu *distance* ni karibu sawa. Mimi nadhani kuna haja kabla ya kuanza kutekeleza miradi hii kuangalia namna gani tunaweza kufanya marekebisho ambayo hayataathiri gharama zake.

Mheshimiwa Spika, kuna njia nyingine ya kutoka Kibakwe kwenda Wota, Wota ni milimani na kule kumekaa vijiji viko karibu karibu kwa pamoja ni vizuri tukaambiya, maana unaweza ukute mradi unafika katika kijiji cha kwanza ukaambiya unaishia hapo, haijasemwa utafika wapi. Ni vizuri tukaambiya umeme utafika wapi. Ni afadhalii umeme ukafika kwenye *institution* kubwa kama shule ya sekondari na Wota pale tunategemea kuwa na *High School* ni vizuri tukaelezwa kwamba umeme utafika kule.

Mheshimiwa Spika, lakini wakati Waziri wakati huo akiwa Naibu Waziri katika swali langu ambalo nilimwuliza kuhusu umeme kutoka Mtera, Kisima, Chipogolo, Rudi na Masa mpaka Ipela, aliniambia kwamba ataiweka kwenye mradi wa umeme vijijini. Lakini katika bajeti hii sijaona popote aliposema hata kusema tu kwamba nipo kwenye mpango wa kupewa fedha kwa mwaka mwingine au la, sijasikia kabisa akizungumzia. Alisema uthamini ulishafanyika na makadirio ya kwamba itatumika shilingi bilioni 4.5 ningeomba anijibu wakati wa majumuisho.

Mheshimiwa Spika, nihamie kwenye madini. Napenda nichukue nafasi hii kupongeza kwa dhati kabisa kazi nzuri iliyofanywa na Tume hii ya Jaji Bomani. Kwa kweli wamefanya kazi nzuri ambayo sisi kama Bunge na Serikali kwa ujumla kweli tunapaswa kuwapongeza. Hii taarifa ni *research* ni taarifa ya kitaalam kweli kweli. Nadhani kuna haja Serikali kama ilivyoileta na yenyewe na kutambua uzuri wa taarifa hii kama ni sehemu ya bajeti hii na ikataka tujadili, kwa kweli mimi nadhani mambo yaliyomo humu ni mazuri wala sipendi kurudia. Lakini nizungumzie tu suala la nishati ya madini ya Winza kule Kibakwe ambako yamegundulika madini ya safaya katika Wilaya ya Mpwapwa.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini - Bwana Arthur Mwakapugi na Kamishna wa Madini – Dr. Kafumu. Kwa kweli tumeshirikiana vizuri sana katika kufikiria namna gani tunaweza tukafanya kazi na wachimbaji wadogo. Lakini pia niipongeze Serikali kwa kukubali ombi langu kwamba eneo lile liwe *designated* kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Ninapenda niipongeze pia Halmashauri yangu ya Wilaya na Mheshimiwa Lubeleje Mbunge mwenzangu wa Jimbo la Mpwapwa kwamba tumeshirikiana vizuri sana katika kuishawishi Serikali kukubaliana lile eneo liwe la wachimbaji wadogo.

Nilitaka kujua tu kwamba, katika mchakato mzima wa kuwagawia viwanja, basi tufanye haraka kwa sababu idadi ya watu wale inazidi kuwa kubwa. Sasa hivi

wanakwenda kwenye karibu elfu sita. Kwa hiyo, *control* yake baadaye tukichelewa kuwagawia na kuwapa leseni itakuwa ni ngumu. Mimi niseme kwamba napongeza tu ila ningependa kujua *commitment* kwamba angalau ndani ya mwezi huu mpaka mwezi wa nane tuwe tumemaliza kuwagawia wale viwanja ili kuwe na utulivu katika shughuli wanayoifanya. Shughuli wanayoifanya, kwanza kabisa napenda niwapongeze wachimbaji wale.

Napenda niwapongeze kwa sababu uchumi wa Kibakwe na Mpwapwa kwa ujumla umebadilika sasa. Ukienda Mpwapwa uliyokuwa unaifahamu mwaka mmoja uliopita sio ile ya sasa. Sasa hivi mambo yamebadilika. Kwa hiyo, nataka niseme kwamba wachimbaji wadogo hawa wana umuhimu sana katika uchumi wa nchi hii. Mimi napongeza sana. Niseme tu kwamba ningependa nijue lini basi mambo haya yanaweza kukamilika wakawa wameweza kupatiwa leseni?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya ambayo naamini kwa kiasi ambacho nilikuwa nimejiandaa yanatosha, naomba niwaachie na wenzangu. Naomba kuunga hoja mkono. Ahsante sana. (*Makofii*)

MHE. MOHAMED H. J. MNYAA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nashukuru kwa kunipatia nafasi na mimi nitoe mchango wangu. Kwanza ningependa *ku-declare interest* kwamba mimi ni mmoja katika Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini ya Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, nianze mchango wangu kwa kuiangalia *TPDC* yenyewe. Kamati kabla ya kubadilishwa ilipokuwa Kamati ya Uwekezaji na Biashara mpaka Kamati ya Nishati na Madini ya Kudumu ya Bunge, imekuwa ikitoa mapendekezo, Serikalini mara kwa mara kuhusu *TPDC* kupata *retention* ili kuweza kujiendeleza katika miradi ya maendeleo. Ni mara nyingi Kamati imesitisiza suala hilo na baadaye mwaka huu turmpata faraja kupata habari kwamba katika kikao cha Baraza la Mawaziri wameridhia suala hilo na mpango huo kuanza mwaka huu wa fedha pamoja na ule mfuko wa Hifadhi ya Mafuta.

Lakini nimeangalia katika bajeti hii, nimejaribu kusoma ukurasa wa 143 mpaka 152 sijaona kitu hicho kama kimeingizwa kwamba. Je, hao *TPDC*, hiyo *retention* itaanza mwaka huu wa fedha kama ilivyokubaliwa na Baraza la Mawaziri au kuna kikao baadaye kimebadilisha? Ningeomba Mheshimiwa Waziri atuhakikishie kwamba *TPDC* itapata hiyo *retention* kuanzia mwaka huu wa fedha ya asilimia 50. Ikiwa mauzo ya gesi yanafika kiwango cha dola milioni moja kwa mwezi na ikiwa bado *TPDC* inashindwa kuwekeza katika ile mikataba ya *PSA* ambayo ni faida kwa Serikali hii itakuwa ni hatari na wakati huo tukitilia maanani kwamba muda huu mpaka sasa hivi ni makampuni mawili yanayozalisha gesi, yaani Songsongo na *ARTUMUS*. Lakini *TPDC* tayari wana mikataba 22 Makampuni 13, ikiwa leo haya mawili hatujaweza kuwekeza: Je, haya makampuni 13 yote yakija yakianza kuzalisha gesi?

Mheshimiwa Spika, hili ni suala la kufikiria na kulifanyia kazi na kitu kimojawapo muhimu kwamba Mheshimiwa Waziri katika bajeti ya mwaka huu ni

kwamba *TPDC* ipate hiyo *retention* ya asilimia 50. Vinginevyo tutakuja kuruhusu haya mambo huko mbele, tutakuja kuchanganyikiwa, uwezo wetu utakuja kuwa mdogo, Makampuni ambayo yanazalisha gesi tayari yameshakuwa mengi, ikiwa mawili tunashindwa kuwasaidia na tukaweza kuwekeza, tutakuja kuweza wakati Makampuni yanayozalisha gesi ni mengi sana kama saba au nane, yote yakigundua gesi na kuzalisha.

Kwa hiyo, ni suala ambalo lifanyiwe kazi muda huu na Mheshimiwa Waziri aje atufahamishe hapa, ikiwa suala hili limo katika bajeti yake, mimi sikuliona na kama halimo, kwa nini lisiwemo au uamuzi wa Baraza la Mawaziri ultenguliwa? Kuna kikao kingine kilitengua? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya kama miaka mitatu hivi nyuma, yaani nakusudia bajeti ya mwaka 2006/2007, 2007/2008 na ya mwaka huu. Tumekuwa tukitenga fedha kwa ajili ya uongezaji thamani wa madini pamoja na kuwasaidia wachimbaji wadogo wadogo. Mwaka 2006/2007 tulitenga shilingi bilioni moja na 2007/2008 tukatenga bilioni nyingine na maeleo ni kwamba fedha hii ni kutia thamani madeni ya vito ili yawe na thamani zaidi na kuwasaidia wachimbaji wadogo wadogo pamoja na kuboresha mazingira ambayo wachimbaji wadogo wadogo wanakabiliana nayo, kuimarisha migodi, kujenga uwezo wa *geological survey* na kadhalika. Katika bajeti ya mwaka huu zimetengwa 2,455,000,000.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nataka kuju Mheshimiwa Waziri ana utaratibu gani kwa wachimbaji wa Mererani na kuboresha hayo mazingira ili kuepuka maafa au mazingira mabaya na mambo yaliyotokea mwaka huu ya ajali ili yasije yakatokea tena?

Je, tumeweza kufanikiwa kiasi gani? Kwa sababu tunapanga Bajeti, tunatenga hela kwa ajili ya kuyaongezea thamani madini, lakini hatupati ripoti ya kwamba madini yetu yameongezeka thamani kwa mpango wetu tuliofanya hapa nchini kwa kiasi fulani. Inabidi sasa Mheshimiwa Waziri atueleze: Je, tumefanikiwa kiasi gani katika mpango wetu kuanzia mwaka juzi na mwaka na matarajio yetu kwa mwaka huu?

Mheshimiwa Spika, suala la tatu ni hili la migogoro ya madini. Sote tunaipongeza repoti ya Mheshimiwa Jaji Bomani na tunategemea Serikali itafuata ushauri huo ili tuweze kufanikisha kuondoa matatizo haya. Lakini pamoja na ripoti ya Jaji Bomani, ipo migogoro ambayo haisababishwi au chanzo chake ni tofauti. Kwa sababu katika migogoro mikubwa inayotokea ambayo Mheshimiwa Waziri ameeleza katika hotuba ya Bajeti yake ni kwamba, ni ile sababu ya wachimbaji wadogo wadogo kuvamia migodi ya wachimbaji wakubwa na sababu nyingine aliyoitaja. Ni suala la fidia kuwa ndogo watu kuondolewa katika makazi yao ya kudumu na akapewa fidia ndogo.

Mheshimiwa Spika, hivi ni vyanzo viwili alivyovitaja katika hotuba yake kwamba ni mambo ambayo yanababisha hiyo migogoro. Lakini ipo migogoro mingine ambayo ni tofauti na hiyo aliyoitaja Mheshimiwa Waziri. Kwa mfano eneo la *RIJETI* Nyamilimila kule Geita kuna migogoro ambayo imeweza kuendelea toka mwaka 1985 mpaka hivi leo na baadhi ya migogoro hiyo imekwenda Mahakamani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano kesi Na. 177 ya mwaka 2005 na aliyeshinda kesi hiyo mpaka leo anashindwa kumilikishwa. Kamishna wa Madini aliyeko huko sijui ana kikwazo gani kummilikisha eneo lake. Ni sawasawa na kusema ni kama *contempt of court*. Inakuaje kesi imekwenda, umeshinda kesi, halafu amri ya Mahakama ya kuwa wajibu ufanywe hivi haufanywi.

Sasa migogoro kama hiyo ni Mheshimiwa Waziri kufutilia Wizara yake, kwanini kunatokea matatizo kama hayo na ndipo pale tunaposema kuna haya masuala ambayo inaonekana wale viongozi wakishirikiana na hawa wawekezaji wakubwa kuna kama njama na harufu ya rushwa ambayo inawahu hao viongozi, inawahu Wakuu wa Polisi wa maeneo hayo na wakati mwininge inawahu hata *Ma-DC*. Kule Mugusu Geita kuna mgogoro amba unahusiana na Mwenyekiti wa Kijiji hicho na *DC* wa Wilaya ile. Sasa haya leo kesho kutwa kunazuka maafa, mauaji wakati huo tunasubiri mapendekezo ya Jaji Bomani wakati yapo mambo hayhusiani na hayo, ni kwenda kuyatekeleza.

Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, haya masuala sio ya kufumbia macho, mengine ya kwenye ripoti yatakekelezwa. Kuna vijiji hivi sasa kuna hali ya mashaka, ugomvi, mgogoro amba lolote linaweza likatokea na ripoti Mheshimiwa Waziri anazo, walifika ofisini kwake.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni fidia. Nashukuru kuna Mheshimiwa Mbunge ameshukuru kwamba shilingi bilioni 400 zimetolewa kwa kulipa fidia wananchi wa sehemu zake. Lakini nathubutu kusema kwamba sio wote waliopata na wengine bado wanahangaishwa. Kwa bahati nzuri au kwa bahati mbaya, hata Jimboni kwa Mheshimiwa Naibu Waziri Jimboni kwake Mkuranga kuna watu hawajalipwa na wamekwenda mpaka kwenye Ofisi ya Mtendaji na ushahidi upo, wameharibiwa mazao yao, picha zipo na kila kitu, ushahidi wote upo, lakini mpaka leo hawajafidiwa. Kwa mfano, huko Mkuranga kwenyewe kuna mazao yameharibiwa, nyumba zimepasuka, mashamba ya mananasi, mikorosho na minazi lakini mtu hajafidiwa, kesi zipo kwa Mkurugenzi na mpaka leo hakuna kilichofanyika. Kwa hiyo, masuala kama hayo yasiachiliwe madogo madogo baadaye yakawa makubwa.

Mheshimiwa Spika, kuna hili suala la *AUPEC* amba wamekuja kuishauri Serikali zote mbili kuhusu masuala namna ya kugharamia gharama na faida zinazotokana na gesi na mafuta ndani ya muungano. Tumearifiwa kwamba kazi imeanza mwezi Juni na Mtaalam Mshauri atamaliza mwezi Agosti. Mimi namshauri Mheshimiwa Waziri yasije yakatendeka kama yale ya *JFC* kutoka mwaka 2003 na mpaka leo ikawa bado haijajulikana mapato kugawana namna gani. Ikiwa umetuahidi katika Bajeti yako hii tutakuja kukukamata tena kwenye Bajeti nyingine. Umetuambia mshauri huyu ameanza kazi mwezi Juni na anamaliza kazi mwezi Agosti, tena isijekuwa nasi hatujapata majibu kutoka Serikali ya Zanzibar Serikali haijabadilisha nini. Mheshimiwa Waziri ondoa matatizo ya migogoro. Isije kuwa kama mfuko ule ikiwa mpaka leo haijajulikana mgawanyo wa mapato kutoka Benki tangu mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo nilikusudia niliseme, ni kuhusu hii gesi. Kusema kweli hii sio mara ya kwanza kulizungumza suala hili na Serikali bado haijatupa jibu la uhakika kwamba viwanda vingi sasa hivi vinatumia gesi. Asilimia 19 ya matumizi ya viwanda yanatumia gesi katika mitambo yao na asilimia 81 ndiyo inatumia umeme. Lakini jedwali linaonyesha kwamba gharama zao zimepungua kwa kiasi kikubwa, tumeweza kuokoa fedha nyingi za kigeni kwenye hivi viwanda. Lakini mwananchi wa kawaida mpaka hii leo hajafaidika kwa sababu kufaidika kwa gesi sio lazima ile gesi ipite na upate umeme.

Kufaidika kwa gesi kama inazalishwa hapa Tanzania na viwanda vimepata kupunguza gharama zake, basi mwananchi wa kawaida faida yake hata kama yupo Kagera, Pemba au Dodoma atafaidika kwa punguzo la vifaa vinavyozalishwa kule viwandani. Ikiwa ni bati, saruji na mafuta tuone bei zimepungua. Hili tuliwahi kuzungumza hapa katika Bunge lako Tukufu, Serikali ikasema, itakuja kufafanua, lakini mpaka leo bado halijafafanuliwa namna gani hali hii ya kuwa na gesi mwananchi wa kawaida atafaidika nayo vipi ikiwa viwanda vinapata punguzo, vinapunguza gharama lakini mwananchi wa kawaida mpaka leo haoni hilo punguzo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hayo na ikiwa Mheshimiwa Waziri atanihakikishia hii *retention* ya TPDC itaanza katika bajeti ya mwaka huu, nitaunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. DORAH H. MUSHI: Mheshimiwa Spika, naomba nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii na afya njema nikaweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. Nawapongeza Mheshimiwa William Ngeleja, pamoja na mkwe wangu, Naibu Waziri pamoja na wataalam wote walioandaa hotuba hii na kuiwasilisha mbele za Bunge lako Tukufu. Bila kuwasahau wananchi wa Manyara. Natoa rambirambi zangu za dhati kabisa kwa maafa makubwa yaliyotokea katika machimbo ya Mererani. Naomba Mungu aziweke roho za Marehemu mahali pema Peponi.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze suala la maafa yaliyotokea Mererani. Sote tunajua ya kwamba maafa haya yalisababishwa na nyenzo duni zinazotumiwa na wachimbaji wadogo wadogo. Nachukue pia nafasi kuishukuru sana Serikali ya Tanzania kwa jitihada zake za kuweza kuiopoa miili ya wachimbaji walionaswa kwenye migodi na kuweza kuisafirisha kwao na kwenda kuzikwa kiheshima. Nampongeza pia Mkuu wa Mkoa wa Manyara kwa kazi kubwa na jitihada kubwa alizozifanya katika kukabiliana na janga hilo.

Mheshimiwa Spika, naomba basi Serikali ichukue hatua za makusudi kabisa kuhakikisha kwamba matatizo kama haya hayawezi kutokea tena na zaidi ya haya, Serikali iweze kuwasaidia wananchi wachimbaji wadogo wadogo waweze kupata nyenzo za kuchimbia na kutoa elimu ya uchimbaji. Hivyo naomba Wakati Mheshimiwa Waziri atakapokuwa ana *wind-up* hotuba yake, naomba alieleze Bunge lako Tukufu kwamba maafa haya yaligharimu kiasi gani cha fedha na je, Serikali inafanya jitihada gani kuhakikisha kwamba matatizo kama haya au maafa kama haya hayawezi kutokea tena?

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii tena kulipongeza Shirika la Madini la Taifa (*STAMICO*), Mkurugenzi wao Bwana Mwakalukwa pamoja na wataalam wote kwa mkakati mzuri waliouandaa na kuuwasilisha Wizara ya Nishati na Madini. Ninaamini kabisa kwamba Mkakati huu utasaidia sana kuwainua wachimbaji wadogo hasa kuwapa nyenzo na kuwapa elimu na ninaamini kabisa sasa wachimbaji wadogo wamempata baba. Kwa sababu ukiangalia kweli Serikali ilikuwa imewasahau wachimbaji wadogo ikawa inawakumbatia wachimbaji wakubwa na kusahau kwamba wachimbaji wadogo ni wawekezaji wa ndani ya nchi na pia wana uwezo mkubwa wa kuhakikisha kuinua pato la Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ichukue hatua za makusudi na za haraka kuweza kuliwezesha Shirika la *STAMICO* ili waweze kufanikisha hayo ambayo wameazimia kwa kuwasaidia wachimbaji wadogo kwa kuwapa elimu, kwa kuwaongoza na udhibiti. Pia naomba nizungumzie wafanyakazie suala la wafanyakazi wa *Tanzanite One*. Wachimbaji wa *Tanzanite One* wanafanya kazi katika mazingira mabaya sana, tunayaita mazingira hatarishi. Wale wachimbaji kwa kila siku wanafanyiwa X-Ray. Kitu ambacho ninaamini kabisa X-Ray hata kwa mtu wa kawaida, hata kwa mgonjwa sio kitu kizuri kabisa.

Ningeomba Wizara hii iangalie namna ya kuwaeleza wale wawekezaji kwa kuwashauri, watumie njia nyingine ya udhibiti kuliko kutimia X-Ray kwa vijana wetu. Vijana wetu wanaathirika sana. Wao wanachukua madini wanaondoka wanatuachia vifo vyta vijana wetu ingaweje hatujui ni kwa wakati gani athari zitaonekana, lakini sio jambo zuri kwa mtu kufanyiwa X-Ray kila siku. Naomba hilo liangaliwe sana na wananchi wa Mererani wanalamika wanasema hawataki kabisa kusikia kwamba vijana wao wanafanyiwa X-Ray kila siku. Ina madhara makubwa hata wengine wake zao wamewakimbia. (*Makofit Kicheko*)

SPIKA: Mheshimiwa Dorah, hiyo X-Ray ya Mererani inafanana na hii ya hapa Bungeni au ipo tofauti? Kwa sababu kama ni hivyo, basi hata maisha ya Wabunge yapo hatarini. Endelea lakini. (*Kicheko*)

MHE. DORAH H. MUSHI: Mheshimiwa Spika, sio kama hii ya Bungeni.

Mheshimiwa Spika, nimalizie na suala la *EPZ*. Suala la *EPZ* limeleta utatanishi. Naona kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri haipo kabisa na ninashangaa kwamba mwaka 2002 Makampuni yanayofanya biashara ya madini duniani walifanyika mkutano kule Marekani na ilionekana kwamba *Tanzanite* ilikuwa inahusishwa na Mtando wa *Al-qaida*. Sasa kwa kuyanusuru madini yetu ambayo hayapatikani mahali pengine popote duniani, ikionekana kwamba ianzishwe *EPZ Center* Mererani ili madini yaweze kupita kwenye mkondo ule. Hili lingekuwa ni jambo zuri kwa sababu ni njia mojawapo pia ya kuweza kudhibiti madini yetu.

Kwa hiyo, makubaliano yalikuwa kwamba *Tanzanite EPZ Center* iwekwe Mererani na wawekezaji waje kuwekeza kwa kuweka viwanda vyao vidogo au vikubwa

kwa ajili ya kukata madini ambayo itakuwa njia sahihi ya kuyadhibiti madini yetu katika Mkoa wa Manyara.

Lakini ninachoshangaa, mpango huu umesimama, hakuna anayetamka tena. Kwanza walikwenda wataalam Mererani na kusema kwamba wanataka kuja kuwekeza, kwa hiyo, wanahitaji kupata eneo la kutosha. Wananchi wa Mererani Mkoa wa Manyara wameshaandaa eneo la kutosha lenye ukubwa wa hekta 2,000. Lakini nimeshangaa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri sioni habari ya *EPZ* na sioni chochote kinachozungumziwa. Naomba nipate jibu wakati Mheshimiwa Waziri atakapokuwa aki-*wind-up*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, *EPZ* ni mpango mzuri utakaota ajira kwa watu wa Mkoa wa Manyara, Arusha na Kilimanjaro pia. Kwa hiyo, kama tunawapa wawekezaji wa nje madini yetu yote na pia hatuna jinsi ya kuyadhibiti, si basi *EPZ Center* iwekwe Mererani ili tuweze kudhibiti na angalau na sisi tuweze kupata ajira? Mimi kwa kweli sitaunga mkono mpaka nitakapopata jibu sahihi la kuhusu *EPZ Center*.

Mheshimiwa Spika, naona sina mengine ya kuongea, lakini sitaunga mkono mpaka nipate ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri atakapokuwa ana *wind-up* hotuba yake. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Dorah Mushi. Kwa hali ya kawaida kwa sababu tulikwishesema pengine jioni tuanze na Naibu Waziri halafu Waziri mtoa hoja. Lakini kwa sababu maalum, naomba nifanye yafuatayo: Kwanza kuna ombi maalum la Mheshimiwa Mabina ambalo nawajibika kulihehishimu, ambaye nitamwita, sasa halafu saa 11.00 ataanza Mheshimiwa Luhaga Johnson Mpina na tutamalizia na Mheshimiwa Bujiku Sakila ambaye amekuwa akisubiri sana humu ndani kuweza kuchangia. Kwa hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Mabina.

MHE. ERNEST G. MABINA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya upendeleo na namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kukubali ombi langu. Napenda niwapongeze Waziri wa Nishati na Madini, Naibu wake, Katibu Mkuu, Makamishna wote na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi wanayoifanya. Wizara hii ni ngumu, Wizara hii inahitaji umekini mkubwa na ndiyo maana unakuta kwamba tumekuwa wachangiaji wengi sana.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Geita tumekuwa na kilio kikubwa sana kuhusu wawekezaji wakubwa hawa. Umekuwa ni mfano wa kutolewa na Wabunge wengi wanaposimama lazima watatoa mfano wa Geita. Naiomba Serikali iwatupie jicho la huruma wananchi wa Geita ili kuweza kuwanusuru katika hali ya kuweza kuwa inatolewa mfano mara kwa mara.

Tunayazungumza haya kutohana na kwamba leseni ya wachimbaji wa Geita ni *special mining license*. Ina maana ni leseni kubwa ambayo imechukua eneo kubwa katika eneo lile la Geita, imechukua eneo zima la Wilaya nzima ya Geita na maeneo yake yote,

lakini kwa masikitiko makubwa ni kwamba pamoja na kwamba ina leseni kubwa, imajaribu kuchukua tena maeneo mengine ya utafiti kiasi ambacho kimewanyima hatananchi wa eneo lile kuweza kupewa maeneo ya kuweza kuchimba.

Mheshimiwa Spika, ombi langu ambalo ninaliomba, kwa sababu eneo lote ni la machimbo, ninaomba *GGM* wapewa *special mining licence*, lakini maeneo ya utafiti ambayo bado yanafanyiwa utafiti, basi wachimbaji wadogo wadogo wamilikishwe. Sehemu hizo ni kubwa, kuna Nyamwilimilwa, Kamuhanga, kuna Rwenge na maeneo mbalimbali ambayo yote yale yana dhahabu, lakini tayari yameshachukuliwa na mchimbaji huyu mkubwa ambaye ni *GGM* kwamba ni *Special prospecting license*.

Sasa ninasema hayo, angalau Waheshimiwa Wabunge waje walione tatizo hili. Nimekuja na ramani ya Wilaya ya *Geita Special license* ambayo imechukuliwa na maeneo yote ambayo imechukuliwa na maeneo yote ambayo yapo katika maeneo yale. Lakini nilichokiona ambacho nimekigundua ambapo Waheshimiwa Wabunge wanawenza wakatusaidia, Mheshimiwa Waziri alete Sheria ya Madini ili iweze kubadilishwa katika vipengele fulani fulani. Bila hivyo utakuta tutapiga kelele kubadilisha mikataba, kufanya nini, lakini bila kubadilisha Sheria ya Madini haujafanya kitu chochote. (*Makofi*)

Hiyo naomba kabisa Serikali iweze kusikiliza kwa sababu mikataba hii ilipokuwa inaandikwa hawakuandika Watanzania, wameandika wawekezaji wenyewe. Hawezi akaandika mikataba halafu akaja akajinyonga. Lazima ataangalia ni faida ipi inayoweza ikampa faida katika maeneo haya. Ni wachangiaji wengi wamesema ni jinsi gani tuweze kuboresha na kuweza kuleta pato ya Taifa katika maeneo haya. Ninaomba sana suala hili liweze kutekelezwa. Katika suala hili limekuja kujitokeza kwa sababu ya mikataba mibovu. Geita tumekuwa na matatizo ya aina nyingi na sasa hivi kuna matatizo ambayo hayatekelezeki kwa wakati.

Moja, kuna wachimbaji wa mgodi mpya na nafikiri kuna Kamati mbalimbali zimekwenda Geita, wapo pale Mahakama ya Mwanzo, wamekaa pale na wameshindwa kesi walikuwa wanakaa katika maeneo yao. Lakini kwa kutokujua sheria, wameondolewa na sheria wanasema mpaka Mahakama sijui ifanye nini. Sasa hawajui lolote, watafanya nini? Sasa ninachokiomba, kwa sababu Serikali yenye imekubali yenye kuwapeleka katika jengo lao la Mahakama ya Mwanzo, ina maana imekubali kosa, wale watu watafutiwe maeneo, kama ni kulipwa, Serikali yenye ilipe iweze kuwanusuru wale wananchi wanaokaa katika maeneo yale. Hilo ni moja (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili, wakati kampuni ya *GGM* ili fidia katika maeneo ya Nyamalembo na Katoma, kuna wananchi saba wamebaki katika maeneo yale. Ni maeneo hatari, Mgodi wa Geita ni *open cast* ina maana unakuta kwamba wanapolipua vumbi lote linawapata wananchi. Kuna familia saba zimebaki za Nyamalembo ambazo zinahitajika kufanyiwa utafiti na kufanyiwa uhamisho haraka iwezekanavyo. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, kwa sababu ni eneo lile na wachimbaji anawamudu, basi awaambie walipwe haraka zaidi waondoke ili waweze kunusuru maisha yao.

Mheshimiwa Spika, la tatu, wakati wanafanya fidia ya wananchi wa eneo la Nyamatakata kuna wananchi 72 wamebaki bila kufidiwa wakafidiwa 39 tu. Sasa kuna vigezo gani vilivyotumika kuwafidia wale wananchi 39? Naomba wananchi 72 wapate fidia yao ambayo tayari malipo yao yameshatayarishwa na sidhani kama fedha ziko wapi, lakini ninaomba wakati anafanya majumuisho nipate jibu fedha zao zipo na watalipwa wakati gani? Kwa hilo, naweza kutoa hata Shilingi.

Mheshimiwa Spika, ni matatizo makubwa ambayo yanawapata wananchi wa Geita, kuna migogoro ambayo imetokana na wananchi kutokujua sheria. Lakini kuna eneo la Mugusu, naona eneo hili lilikuwa la wachimbaji wadogo wadogo, lakini kuna mjanja mmoja akaja akachukua leseni akawafanya wale kama wale ni wafanyakazi, sasa hivi wanahangaika kuweza kutafuta maeneo.

Tumekwenda Wizarani kumwomba Mheshimiwa Waziri angalau anasuru eneo hili. Nimemwomba Naibu Waziri, wakati tutakapomala hapa kipindi cha Bunge hili, naomba tunusuru maisha ya watu wa Mugusu ili waweze kupata haki yao ya kuishi. Bila ya kufanya hivi, utakuta kuna migogoro ambayo imejitekeza, wengine watasema ni migogoro ya kisiasa na wengine watasema ni migogoro mbalimbali. Tunataka tuwe ni watu wa mmoja, hatupendi kuona huyu ana umaarufu gani au vipi tunataka kuona kwamba wote ni Watanzania na tunaishi katika Tanzania moja. Hilo naliomba sana Mheshimiwa Waziri aweze kulitilia maanani ili kuweza kuwaokoa wananchi wa Geita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Kamati ya Mheshimiwa Jaji Boman, imefanya kazi nzuri, imefika Geita, imeweza kuwaona wananchi. Lakini Kamati hizi ni nyingi mno, zimeundwa, kuna Kamati ya Kipoloka ambayo ilikuwa inadurusu sera za madini, lakini mpaka sasa hatuoni matokeo yake na hii nayo tumeletewa vitabu hivi na inawezekana tukyaweka kwenye Maktaba tukawa tunyaangalia. Lakini naomba, kwa sababu yaliyomo humu yote ni mazuri, yanaweza yakanusuru wananchi wa Geita. Geita imekuwa kama kichocheo watu wanakwenda kuangalia kule.

Mheshimiwa Spika, nafikiri ulikuwepo alipokuwa anachangia Mheshimiwa Musalika. Alisema kwamba wananchi wa Geita maisha yao yapo hatarini, unaweza ukakuta wananchi wote wakawa hali sio nzuri. Kwa hiyo, ninaomba kabisa ripoti hii iweze kuangaliwa kwa undani zaidi, lakini unakuta kwamba kuna masuala ambayo yanajitokeza mengine ya kukashifu hata viongozi wetu wa ngazi za juu, labda kama wametoa ripoti mapema. Hiyo isiweze kusemwa kwa sababu kuna baadhi ya Wabunge wenzetu hapa unakuta mnazungumza kwenye Kamati tayari anakimbia kwenye Vyombo vya Habari.

Mheshimiwa Spika, hili nilikuwa naomba kwa usalama wa nchi tujaribu kuweka siri za nchi, tusianze kukimbia katika maeneo tukaacha usalama wa nchi yetu. Nchi hii inahitajika amani na utulivu ili tuweze kuishi. Ripoti hii ni muhimu. Ni muhimu kwa wananchi wa Geita na ni muhimu kwa wananchi wote ambao wanahitaji maendeleo katika sekta ya madini. Naomba sana hali hii iweze kuokolewa na Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, sisi tuna matatizo ya umeme katika maeneo mbalimbali. Katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri amesema kwamba kuna ruzuku ambayo itatolewa kwa ajili ya umeme vijijini. Naomba pesa hizo au tozo hiyo itolewe haraka zaidi kwa sababu Sheria tumeshaipitisha na kitu gani ambacho kina sababisha mpaka sasa hivi watu hatutozi tozo hiyo ili wananchi wetu wa vijijini wakapata umeme. Mifano ipo mingi maeneo ya Nkome hawana umeme, Nzera hawana umeme, Kasamwa hawana umeme na Lubanga, Bugurula na Kamuhanga sehemu zote hizo hazina umeme. Vijiji hivi vikipewa umeme vitakuwa na maendeleo ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Mabina. Waheshimiwa Wabunge muda wa kusitisha shughuli za Bunge kwa mchana huu umekaribia sana. Niseme tu kwamba nimepata taarifa kwamba Mheshimiwa Bujiku Sakila amekwischachangia sasa kwa maandishi hii inatupa muda mzuri zaidi. Hii inatupa muda mzuri zaidi kwa hiyo itakuwa ni Mheshimiwa Mpina saa kumi na moja, baada ya hapo nitamwita Mheshimiwa Naibu Waziri na baadae mtoa hoja kwa muda wa saa moja na robo.

Baada ya tangazo hilo sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa kumi na moja jioni.

(*Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa Mpaka Saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Katibu kwa shughuli zitakazofuata, naomba kutoa ufanuzi kuhusu jambo moja nililolitamka mwenyewe saa za asubuhi pale, tuseme mchana. Nilimkatiza kidogo Mheshimiwa Dorah Mushi alipokuwa akitoa malalamiko kuhusu wachimbaji wadogo na wale akina Apolo kuwa wanapitishwa kwenye *X-Ray* kule machimboni Mererani.

Sasa nataka nitofautishe maana mimi nilisema hapa Bungeni, nimeambiwa kitaalam, kinachofanyika hapa Bungeni mnapita kwenye kitu kinaitwa *Pass-through Detector*, hiyo siyo *X-Ray* kwa maana ya *X-Ray*. *X-Ray* ni ile inayopima mpaka kuona viungo vya ndani, hiyo ndiyo mionzi na inapima hata kama kijana wa Mererani labda kameza *Tanzanite* iko ndani ya tumbo, inaonekana. Sasa, tulichonacho hapa ni tofauti kabisa. Kinagundua kisu, yaani chuma, baruti, vitu vya namna hiyo. Kwa hiyo, niliomba nitofautishe. Kwa hiyo, rai ya hawa Waheshimiwa wa Mererani kama kweli ni hiyo *X-Ray* ya kuangalia mpaka ndani kabisa kwenye mifupa, basi itabidi Mheshimiwa Waziri atusaidie kidogo kuhusu hilo.

Waheshimiwa Wabunge, sasa orodha yangu ilikuwa bado ndefu, lakini alisalia mmoja tu wa kumwita ambaye ni Mheshimiwa Mpina. Lakini, nimetaarifiwa na upande wa Serikali, wanahitaji kama nusu saa kukamilisha mambo fulani. Kwa hiyo, itabidi nimtafute msemajji mwingine. Naona aliyekuwa anafuata, Mheshimiwa Said Amour Arfi

hayupo. Kwa hiyo, wa karibu yake ni Mheshimiwa Lekule Michael Laizer. Kwa hiyo, namwita Mheshimiwa Mpina. (*Makofit*)

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwanza, kabla sijakwenda mbali, napenda tu kusema kwamba hotuba hii ya Waziri wa Nishati na Madini, siiungi mkono. Nitatumia kifungu cha 103(2) wakati ukifika cha kuondoa Shilingi katika makadirio.

SPIKA: Mheshimiwa Mpina, utaratibu ni kwanza, kudai maelezo, usiporidhika ndio unakwenda hatua ya Shilingi.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Spika, ndiyo! Nasema hivyo, nataka nipaye ufanuzi wa kutosha juu ya *line* ya umeme unaotoka Nghoboko kwenda Isengwa, Mbalagane, Lubiga na Mwandoya ili kisha sasa uweze kutoka pale Mwandoya uende Kisesa, Gambasingu, Bariadi na kisha uende Sakasaka na baadaye *Butuli Game Reserve*, pale yalipo Makao Makuu ya *Game Reserve*.

Mheshimiwa Spika, nayasema haya kwa sababu *line* hii ya umeme, nimekuwepo hapa Bungeni toka nilipoingia hapa Bungeni, nauliza maswali ya msingi na maswali ya nyongeza. Mheshimiwa Rais alipokuja kuninadi Kisesa, aliwaambia Wanakisesa umeme utafika mapema. Lakini, inavyoonyesha na inavyosikitisha Serikali yetu kulingana na bajeti hii sasa, tumezivumilia bajeti zote tatu, lakini ukiendelea kuisoma hii bajeti unagundua kwamba Serikali imetoa ahadi lakini haina mkakati wowote wa kupeleka umeme huo.

Mheshimiwa Spika, naungana na Waheshimiwa wenzangu hapa, Mheshimiwa Mhagama alilia sana kuhusu Peramiho, Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mheshimiwa Ally Salum kule Solwa, lakini kwa utaratibu huu unaoonekana, umeme huu hauwezi kufika kwa sababu Serikali inatoa ahadi, lakini haina mkakati wowote wa kutimiza ahadi zake.

Mheshimiwa Spika, nikikupeleka Meatu, Wilaya ya Meatu ina vijiji sita tu. Vijiji sita tu ndivyo vilivyopitiwa na umeme, yaani kupitiwa na umeme, siyo kwamba vina umeme, vilivyopitiwa na umeme. Vinavyopata umeme ni kijiji kimoja ambacho ni Makao Makuu tu ya Wilaya pale. Sasa Ukizungumza Kisesa ni kijiji kimoja tu, ukizungumza Jimbo la Kisesa ni kijiji kimoja tu. Lakini pale Kisesa, Kisesa kama Kisesa wawekezaji ni wengi. Watu wanataka kuweka *Ginnery* zao pale, wataka kuweka posho *mill* zao pale kwa ajili ya mazao na kadhalika. Lakini ndio hivyo, danadana za Serikali unaahidiwa hapa majibu mazuri, unaandika na barua, unajibiwa, bajeti ijayo hakuna tatizo. Lakini, ukiangalia hivi, mwenye macho haambiwi tazama na kama una akili zako, ukiisoma hii bajeti, unajua kabisa umeme huu hauwezi kufika.

Mheshimiwa Spika, ukiisoma bajeti ya mwaka 2006/2007 ni ile ile. Bajeti ya mwaka 2007/2008 ni ile ile, ni *ku-copy* na *ku-paste*. Pesa zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo mwaka 2007/2008 ni shilingi bilioni 312, mwaka 2008/2009 ni shilingi bilioni 320. Ukiangalia mfumko wa bei pale, ni sawa na hakuna tu, ni sawa na bajeti ile ile ya

mwaka uliopita. Lakini ukienda kwenye miradi ya maendeleo ambayo imekuwa ikitengwa katika umeme vijijini, miradi inayotajwa ya umeme vijijini, ukipitia hotuba ya Waziri, mwaka 2007/2008 hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini alisema; "Katika bajeti ya mwaka 2007/2008, umeme utafikishwa katika Wilaya ya Rufiji, Kilindi, Bukombe, Kilolo, Simanjiro na kadhalika." Mwaka huu bajeti inazungumza juu ya Wilaya zile zile! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukichukua bajeti, Mpango wa Umeme Vijijini, ninao hapa ambaao ulifanyiwa tathmini mwaka 2005, una thamani ya trilioni 1.2. Nenda sasa katika huyu Wakala wa Umeme Vijijini ametengewa shilingi ngapi! Mwaka 2007/2008 huyu Wakala alikuwa ametengewa bilioni 10 tu kati ya madai ya trilioni 1.2.

Mwaka huu Wakala wa Umeme Vijijini ametengewa, ukiangalia, nimesoma sana Makabrasha, lakini nimeona pale kuna shilingi bilioni 10 nyingine zinakuwa kama shilingi bilioni 20. Nikafanya hesabu ya tozo la asilimia tatu, unapata kama inaweza ikawa *around* shilingi bilioni nne au sita, inakuwa jumla ni shilingi bilioni 26 katika kutekeleza malengo ya shilingi trilioni 1.2.

Mheshimiwa Spika, huu ni mzaha kwa Serikali iliyoahidi kuwatumikia wananchi wake kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya na tena kwa Bunge linaloongozwa na Spika, wa kasi na viwango, kuwadanganya wananchi kiasi hiki. Huku ni kuwachokoza wananchi kwa sababu, ni heri asiye na matumaini kwa maana hatachukia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mkullo, alisikika katika vyombo vya habari akiongea na watu wa Soko la Hisa la Dar es salaam, akasema kuwa Makampuni makubwa ya Madini yanaripoti hasara Serikalini, lakini kwenye Makampuni yao Mama, wanaripoti faida. Akawataka hao watu wa Soko la Hisa wachukue hatua kwa Makampuni haya kwa maana wanafanya hivyo kwa maana ya kukwepa ushuru.

Hotuba hii ya Mheshimiwa Mkullo inasapotiwa vizuri na Kamati ya Mheshimiwa Rais ya Kuishauri Serikali kuhusu Usimamizi wa Sekta ya Madini. Katika Ukarasa wa 17 kipengele cha nne inasema; kodi na mgawanyo wa mapato ya mauzo ya Madini, naomba kunukuu: "Hoja ni kwamba Taifa halinufaiki ipasavyo kutokana na mapato na mauzo ya Madini. Wawekezaji ndio wanaonufaika. Aidha, Taifa linaambulia uharibifu wa mazingira, mashimo, mapango, uharibifu wa maliasili na kadhalika." Mwisho wa kunukuu. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, hakuna sehemu yoyote ambapo amelizungumza suala hili ambalo ni kubwa kweli kweli kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, lakini, hata hivyo kuna mambo ya kujiuliza: Hivi ni sahihi kwa Waziri wa Fedha na Uchumi aliyepewa dhamana na Taifa hili ya kusimamia rasilimali za nchi kutoa hotuba ya malalamiko badala ya ufumbuzi wa tatizo lenyewe? Je, sasa kama Serikali imegundua kuwa kuna fedha nyingi zimekuwa zikiibiwa na hao wenye makampuni makubwa, ni makampuni gani yanayojihusisha na udanganyifu huo? Je, ni jumla ya shilingi ngapi ambazo Mheshimiwa Waziri amezifanyia hesabu kujua

kwamba Taifa limeibiwa fedha hizo? Je, Serikali sasa imechukua hatua gani dhidi ya makampuni hayo na hatua gani ya kuzirejesha fedha hizo za Watanzania? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Sera na Sheria ya Madini, licha ya dharura kubwa ambayo imekuwepo hapa nchini ya usimamizi na uendeshaji wa migodi nchini, Wizara ya Nishati na Madini imekuwa inapiga tu danadana kuileta hii Sera ya mwaka 1997 na Sheria ya Madini ya mwaka 1998 hapa Bungeni. Matatizo ni makubwa, lakini toka mwaka 2006, tumekuwa tukielezwa tu Sheria inadurusiwa, mnadurusu mpaka lini?

Mheshimiwa Spika, Kamati nyingi za ushauri, leo miaka minne, 2009 tunaanza kujitayarisha na majimbo, leo miaka minne, Sheria inadurusiwa. Kamati zimeundwa za kina Masha, kina Bomani, za Wakaguzi kama akina Alex, zimetoa ushauri wake na hii ya mwisho ya Bwana Bomani iko *very comprehensive*. Kinachosubiriwa mpaka mwaka 2009 ni nini?

Namtaka Waziri, wailete Sheria hii ya Madini kulingana na taarifa ambayo tumeisoma ya Bomani. Hizi Sheria zinahitaji kuchukuliwa udharura wake, tuzifanyie kazi hapa Bungeni, kuna mambo makubwa ya *ku-observe* pale; mfumo wa kodi, wachimbaji wadogo wadogo, Serikali inavyoshiriki katika hii migodi mikubwa, fidia ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Sera na Sheria ya Madini iletwe tufanyie marekebisho katika Bunge hili kutokana na udharura wake. Hatuwezi kuendelea kusubiri Taifa linaendelea kafilisika, lakini watu wanasema wanendelea kudurusu tu. Mtadurusu mpaka lini?

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kusema, ninaomba sana, nimechoka na ahadi ambazo nimekuwa nikipewa na Serikali. Nainaomba sana nipewe sasa ufanuzi wa kutosha katika umeme nilioutaja unaoanzia pale *junction* ya Nhocoko, Isengwa, Mbalagane, Lubiga unakwenda Mwandoya.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa nipewe ufanuzi wa kutosha. Kama nilivyo sema, nitatumia kifungu cha 103(2) kuondoa shilingi moja katika mshahara wa Waziri kama sitapata ufanuzi wa kutosha. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mpina, kama nilivytamka, msemaji wangu wa mwisho ni Mheshimiwa Michael Lekule Laizer – Mbunge wa Longido.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii adimu ambayo niliisubiri kwa hamu sana. Kwa hiyo, nashukuru kwa kunipa nafasi niseme machache.

Mheshimiwa Spika, kabla sijasema mengine, ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutusaidia katika kipindi kigumu tuliposhitakiwa, tulipotuhumiwa na sasa tumefutiwa kesi. Tunamshukuru Mungu sana kwa sababu na sisi tulionewa sana,

tumenyanyaswa sana, hatukutendewa haki. Hata mwaka mzima tumekwenda Mahakamani hatujawahi kusikilizwa mpaka kesi imefutwa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mungu sana kwa sababu mimi na mwenzangu Mollel pamoja na wenzetu sita tumefutiwa mashitaka na nawashukuru Wabunge wenzangu, tangu tulipokamatwa, wametufariji, wametupa pole, Wabunge wote pamoja na wa Upinzani nawashukuru sana pamoja na wananchi wa majimbo yetu, Jimbo la Longido na Jimbo la Arumeru, nawashukuru sana kwa sababu walikuwa pamoja nasi mpaka kesi imekuja kufutwa wakiwa pamoja nasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na wewe, baada ya kutoa ufanuzi, kwa sababu kuna baadhi ya watu walitaka tufukuzwe Bungeni, lakini umetoa ufanuzi wa kisheria. Nami kwa kweli mtu ambaye anapenda haki, kwa kweli nakuwa pamoja naye kila wakati kwa sababu na mimi sipendi watu wanyanyaswe. Was wahili wamesema; “Mungu si Athumanî”. Lakini leo naongeza neno moja, “Mungu siyo Ole.” Sina maana ya kusema Ole Sendeka au Ole Nangoro hapa, Ole ni *Sir Name* kwa kikwetu Wamasai. Kwa hiyo, Mungu siyo Ole! (*Makofi/Kicheko*)

SPIKA: Wala siyo “Asama”. (*Kicheko*)

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Spika, wala siyo Jimbo la mwezangu pale! niingie kwenye hoja. Nimechangia bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa miaka 12 na miaka miwili iliyopita sikuunga mkono. Nilisema iandikwe kwenye maandishi kabisa kwamba siungi mkono na sikupata jambo lolote katika Jimbo langu litakalonishawishi leo niunge mkono.

Mheshimiwa Spika, tulipoingia Bungeni, Waziri wa Nishati na Madini wakati huo alikuwa Mheshimiwa Shija na Mheshimiwa Mkapa akiwa Rais. Wote wawili walitoa ahadi ya umeme Longido. Mawaziri wote waliofuatia, kila mmoja ametoa ahadi ya umeme Longido mpaka Rais wa sasa amekwenda longido amesema mtapata umeme. Kwa sababu umeme wa Longido hauna gharama nyingi kuleta umeme kutoka Namanga mpaka Longido, ni fedha chache ambazo tunazo, “Mtapata umeme.” Mheshimiwa Rais akatamka kwamba ni ye ye ndiye atakuja kuzindua umeme Longido, mwaka huu hauishi bila umeme kufika Longido.

Kwa hiyo, mzigo umetua kwangu, sasa unamlemea Mheshimiwa Rais kwa sababu ye ye ndiye sasa ameahidi. Mimi ni mtu mdogo. Kwa hiyo, kiongozi wa nchi amesema kwamba umeme utafika Longido na mpaka sasa haujafika.

Mheshimiwa Spika, ni aibu tupu ! Ukienda Namanga, Mji wa Kenya na Namanga Tanzania, ni Mji mmoja. Ni kabarabara kembamba ndio kanatenga. Lakini upande mwingine wana umeme, sisi hatuna umeme, tunawasha kibatari. Mji mkubwa kama huo ! Kwa hiyo ni aibu tupu!

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sina sababu ya kuunga mkono hoja hii mpaka nipate maelezo. Nimeona kwenye kitabu hiki kwenye majedwali Longido imo, lakini hiyo hainishawishi niunge mkono kwa sababu kila hotuba Longido imo! Imo tu kwenye vitabu! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwanza, ningependa kufahamu, hivi inakuwaje Wilaya moja kuwekewa vijiji 36 umeme? Kwenye majedwali ukiangalia, Wilaya ina vijiji 36, nyingine ina 20 na nyingine ina mpaka 40. Lakini Wilaya nyingine hazina kabisa ! Halafu cha ajabu, huyu Waziri wa Nishati na Madini ameandika Wilaya kwa majina. Wilaya ya Longido, ye ye mpaka leo hatambui kwamba ni Wilaya, akaifanya kijiji ndani ya Wilaya ya Arumeru. Kwa hiyo, siyo Wilaya.

Kwanza, kabla hatujaingia kwenye vifungu, asahihishe. Wote mnatambua kwamba Longido ni Wilaya, lakini anakwenda kuandika eti ni kijiji kimojawapo ndani ya Wilaya ya Arumeru, kama hayo si madharau! Watu wa Longido watashangaa sana eti wakisikia kwamba Longido ni kijiji cha Arumeru. Kwa nini hakuandika Wilaya ya Longido kama alivyoandika Wilaya nyingine za Tanzania, kama alivyoandika Sengerema, kama alivyoandika Geta, kama alivyoandika Mwanza? Ni Wilaya, siyo kijiji. Kwa hiyo, hapo nikaanza kupata mashaka na nimemwandikia kwamba amefanya kosa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni Madini na nianze kuzungumzia Mgodi wa Mererani, *Tanzanite*.

Mheshimiwa Spika, hii nchi ni ya kwetu, siyo ya Makaburu! Makaburu wanapewa eneo kubwa, wao eneo lao linahesabiwa kwa kilomita za mraba, lakini wachimbaji wadogo wanapewa mita 50. Hawa Makaburu (samahani kutumia jina hilo), lakini sikukosea kwa sababu mtu akinisema Mmasai, hakufanya kosa kwa kuwa mimi ni Mmasai.

Kwa hiyo, hata nikisema nao ni Makaburu, ni Makaburu! Hivi kwenda kumpa mzawa aliyekutwa pale na wageni, ukampa mita 50, yule ukampa kilomita za mraba, halafu bado unamhifadhi, bado ye ye ndiye unamjali kuliko mzawa wa Tanzania. Hilo halikutenda haki na hiyo inaweza kusababisha migogoro mpaka tunyanyue mikuki kama Zimbabwe tukadai ardhi yetu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni utafiti wa Madini katika nchi hii. Tunaomba utafiti ufanyike, tujue kwamba Madini yako wapi, tusing'ang'anie mashimo ambayo yamekwishapatikana. Inawezekana Madini yakaisha hapo, kumbe tumekalia utajiri mwengine katika maeneo mengine. Watalaan wetu waanze sasa kufanya utafiti ili tupanue uzalishaji wa Madini.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni soko. Soko la *Tanzanite* sisi hatuna. Soko la *Tanzanite* ni Kenya. Ni kwamba sisi wenye hatujawajali wachimbaji wetu, hawana masoko. Tutafute masoko ili wachimbaji wadogo wafaidike. Huu umasikini hautaondoka

kama hatujatafuta namna ya kuwasaidia wananchi ili wapate masoko. Kila siku tunalia masoko masoko, wachimbaji wa Mererani wawekewe utaratibu mzuri wa kuuza mali, wa kuuza madini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningependa kurudia kusema kwamba Longido imekaa muda mrefu bila kupata umeme, sijui tuna matatizo gani! Wilaya zinazotuzunguka, Rombo, Siha, Arumeru Mashariki, Arumeru Magharibi wana umeme, sisi hatuna. Monduli yenye ambayo tulikuwa Wilaya moja wao wana umeme. Wilaya ya Longido na Ngorongoro ziko mpakani, lakini hakuna Wilaya hata moja yenye umeme. Sasa umeme uje Longido na ukate kwenda Ngorongoro, kwenda Loliondo. Inawezekana ndiyo *shortcut*. Kwa hiyo, ukifika Longido, tawi liende mpaka Ngorongoro.

Hivi ukiwaambia Ngorongoro watumie mashine, mashine zikiharibika, kwanza kuja Arusha ni kilomita 500 kutoka Loliondo. Kwa hiyo, inahitaji wapate umeme kama wenzao wa Kenya. Loliondo iko mpakani kama Longido, lakini Kenya wana umeme, sisi hatuna umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningependa nipate majibu,, tena Mheshimiwa Waziri angetaja Longido ni lini watapata umeme ili wasikie kutoka kwake, lini wapate kwa sababu meseji zimejaa kwenye simu zangu, natumiwa meseji. “Hivi leo, Waziri anasemaje?, Hivi leo utachangia?” Nimechangia, nimewasemea, sasa imebaki ni kauli ya Serikali waseme kwamba Longido watapatiwa umeme lini?

Mheshimiwa Spika, pamoja na Wabunge wenzangu, kwa kweli mmeonyesha upendo mkubwa kwetu hata wengine wametusaidia kwa nauli kwenda kwenye kesi. Nawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru. (*Makofi*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. FATMA MUSSA MAGHIMBI: Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kidogo juu ya hoja hii. Wakati wa utafiti wowote, tunaelewa kwamba lazima kuna wananchi watapoteza mali zao. Lakini Serikali au Shirika linalofanya utafiti huo ni lazima iheshimu mali za Watanzania. Wakati wa utafiti wa gesi, Mtanzania aitwai Abdul R. Magomba aliharibiwa shamba lake. Ni siku nyingi sasa zimepita madai yake hayajalipwa.

Je, Mtanzania huyo ende akadai? Mtanzania huyo, shamba lake liko Mkuranga Kipalanganda Kitongoji cha Msasa. Msemaji wa Upinzani jana alisema kuwa kituo cha Somanga Funga hakijamalizika kwa sababu mkandarasi wa kituo hicho ni swahiba wa Kigogo mmoja. Napenda nielimishwe. Je, mkandarasi anapopewa kazi huwa haingii mkataba na serikali au wizara? Kama kaingia mkataba na wakati umepita, kwa nini asipelewe Mahakamani?

Pia, ningependa kuelimishwa juu ya *Alstom Power*, mradi huu unagharimu dola milioni 116 lakini ripoti yasema inagharimu dola milioni 130.181. Je, hii *Topographical Error* au hii tofauti hii itapelekwa wapi?

Mheshimiwa Spika, miradi mingi ya Wizara hii huwa ina fedha nyingi za kutiliwa mashaka.

Namwombea dua Mheshimiwa waziri mpya, hatatuletea ripoti za mashaka. Ahsante.

MHE. MWINCHOUM ABDULRAHMAN MSOMI: Mheshimiwa Spika, miaka miwili iliyopita nilichangia juu ya uwezekano wa kuwepo gesi eneo la Kimbiji Tarafa ya Kigamboni na Wizara kulishughulikia kwa kuwapa kazi hiyo ya utafutaji gesi/mafuta kampuni ya *PETRODEL* ya Uingereza, lakini hakuna kinachoendelea juu ya mradi huo mpaka sasa:-

(a) Je, kazi itafanyika?

(b) Lini itaanza kazi?

Mheshimiwa Spika, wananchi walioathirika na mradi wa upitishaji umeme mkali chini ya mradi wa Gridi ya Taifa wanalamika kwamba fidia waliyolipwa ni ndogo, hasa kwa kuzingatia kwamba udhamini ulifanyika 2005 na malipo ya fidia yamefanyika mwaka 2007. Hivyo, gharama za vifaa vya ujenzi vimepanda sana. Wanaomba malipo ya fidia yaendane na wakati na gharama za sasa.

Mheshimiwa Spika, upimaji ulifanywa na wanafunzi wa *UCLAS* badala ya wataalamu timilifu. Hii inawapa mashaka juu ya uhalali wa tathmini hiyo kwa kuwa zoezi zima limefanywa na wanafunzi. Wanaomba majibu ya Serikali.

Kuanzishwa kwa mfuko wa kusaidia wachimbaji wadogo wa madini, naomba fedha hizo zisitengwe kwenye machimbo ya vito, bali hata wachimbaji wadogo wa mawe nao wafaidike na mfuko.

Nalipongeza sana Shirika la Umeme Tanzania kwa juhudi zao za usambazaji umeme katika Jimbo la Kigamboni katika maeneo ya Kisoda, Kisiwani, Vijibweni, Geaulole, Chamazi. Vile vile, bado naliomba shirika hili kuchukua hatua ya kuendelea kusambaza umeme katika maeneo ya Jimbo la Kigamboni, Kilungule, Kibugumo, Tuangoma, Kibada na Mtoni Kijichi. Sehemu hizo nyingi umeme mkali umeshapita bado kuwekama *Transforma tu*.

Mheshimiwa Spika, pale Mjmwema kuna wawekezaji katika sekta ya machimbo ya mawe ambao wanamiliki maeneo makubwa sana, lakini hayaendelezwi na badala yake kuna maficho ya wezi na majambazi. Naomba kuishauri Serikali kuchukua hatua ya kuyachukua maeneo hayo kwa nia ya kuwagawia wachimbaji wadogo.

Baruti zinatumika kwenye machimbo ya mawe kwa ajili ya kupasua miamba, lakini kwa bahati mbaya sana baruti hizo hutumika na kwa uvuvi haramu. Naishauri Serikali kuendelea na juhudzi zake za kuwataka wawekezaji wa sekta hii kutumia baruti zisizowenza kutumika na wavuvi kwa uvuvi haramu. Inawezekana.

Mheshimiwa Spika, *TAZAMA* Wanazuia Halmashauri ya Manispaa ya Temeke kujenga barabara ya kutoka Mbagala *Zakham* kwenda Kingungi kwa kiwango cha kokoto/lami. Hili ni tatizo kubwa kwetu, naomba *TAZAMA* waruhusu na Halmashauri itazingatia vipimo vyao vya mipaka. Hii ni barabara muhimu sana kwa wananchi. Tupeni kibali tujenge.

TAZAMA isitishe kumwaga uchafu ovyo, *TIPER*, wananchi wanaathirika sana.

MHE. DR. DAVID MATHAYO DAVID: Mheshimiwa Spika, tarehe 21 Agosti, 2008 nilipokea barua Kumb.Na. DO/MRE/BUNGE toka kwa Mkuregenzi Mkuu wa *TANESCO* kuwa vijiji vya Same Magharibi kuwa vingewekewa umeme katika bajeti ya 2006/2007 kwa kutumia *ERT Programme Phase I* na *II*. Ahadi hiyo hadi leo haijatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, tarehe 25 Februari, 2008 nilipokea barua toka kwa Katibu Mkuu, Nishati na Madini Kumb. Na.CBD.88/286/01 kwamba tathmini ya kuweka umeme katika vijiji vya Ijinyu, Muheza, Msindo, Mbakweni, Kizungo, Dido Kijomu vitagharimu takribani shilingi milioni 321. Pia nilipewa ratiba kuwa utekelezaji utaanza April, 2008. Hadi leo sijaona utekelezaji huo ambao katika vijiji vyote kwa mujibu wa ratiba vingwekwa umeme hadi Novemba, 2008.

Mheshimiwa Spika, mimi kama kiongozi Serikalini, siwezi kupiga kelele Bungeni. Naomba nijibibiwe na wananchi wangu waelezwe vizuri. Je, uwekaji wa umeme (ratiba niliyopewa) utekelezaji utaanza lini?

Vijiji hivyo ni:-

		HT	LT Extension	Transformer	Cost(Tshs)
1.	MUHEZI	5 KM	2 KM	100 KVA	57ml
2.	MSINDO	5 KM		100 KVA	40ml
3.	MBAKWENI	5 KM		100 KVA	40ml
4.	IJINYU	<i>Underline</i>	2 KM	100 KVA	36ml
5.	KIZUNGO/ DIDO	5 KM		2X100KVA	84ml
5.	MABILIONI/ KIJOMU	<i>Underline</i>	4 KM	2 x 100KVA	63ml

Mheshimiwa Spika, niliunga mkono na naendelea kuunga mkono kwa asilimia mia moja. Naomba kuwakilisha.

MHE. GOSBERT BEGUMISA BLANDES: Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kwa kazi nzuri anayoifanya katika Wizara hii ngumu. Pia, nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara hii kwa kuchapa kazi kwa uaminifu wa hali ya juu. Wananchi wa Jimbo langu wanajivunia Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Januari, 2008, Mheshimiwa Rais akiwa Jimboni Karagwe, aliahidi kuwapatia umeme wananchi wa Jimbo la Karagwe (vijijini) kwa maeneo yafuatayo:-

- (a) Bugene – Bisheshe – Nyakayanja – Nyaishozi – Ihembe;
- (b) Bugene – Ihanda – Rwabwete – Kamagambo – Nyakagoyagoye- hadi Nyakaiga; na
- (c) Kayanga – Rukaka – Nama – Nyabwegira – Kakilo – Runyaga hadi Rwambaizi.

Ahadi hii tulielezwa itaanza kutekelezwa mwaka huu wa fedha yaani, 2008/2009. Upembuzi yakinifu tayari ulishakamilika tangu 2006 kwa kuptitia shirika la SIDA – SWEDEN. Taarifa nilizonazo ni kwamba mradi mzima unategemea kutumia Shs.10bn kwa wilaya ya Karagwe, Misenyi na Bukoba Vijijini na Muleba. Ninafahamu kuna fedha hififi zingetolewa na SIDA - SWEDEN. Je fedha hiso zimeshatolewa? Kama hazijatolewa ni kwa nini

Mheshimiwa Spika, fedha za wafadhili zina masharti magumu sana na imewezekana zisipatikane hivyo ni bora Serikali ikajipange kwa kutenga fedha *from own source* (yaani fedha zetu za ndani) vinginevyo ahadi ya Rais itakuwa hewa na hilo siyo jambo zuri kwa wananchi wa Jimbo la Karagwe, liko pembezoni. Naomba Mheshimiwa Waziri atoe kauli ya Serikali ni lini mradi huo wa umeme utakamilika kabla ya utawala wa awamu ya nne, yaani 2010.

Napenda kushauri kuwa mikataba yoyote ya Wizara hii na hasa katika *negotiation process* ihusishe *super brain* tulizonazo hapa nchini. Katika hili namaanisha kuwa timu nzima ya *negotiation* iongozwe na wataalam toka nje ya Wizara. Tunao walimu wazuri toka Vyuo Vikuu vyetu na hasa *professors* na madaktari. Mfano mzuri ni wa Prof. Issah Shivji, Prof. Fimbo na wengine wengi. Hawa wakitumiwa vizuri watatusaidia kuondokana na aibu ya mikataba mibovu kwani watu wetu (Wizarani) hawajapata *training* ya kutosha kukabiliana na wataalamu waliobobea kutoka nje. Pia, tunao wastaafu wetu amba wanao uwezo wa kutusaidia katika suala zima la mikataba mfano Majaji waliostaafu. Naunga mkono hoja.

MHE. PASCHAL CONSTANTINE DEGERA: Mheshimiwa Spika, Ninaomba nichangie hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini .

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri ambayo imefafanua kwa kina mambo yaliyotekelawa na yale ambayo yamepangwa kutekelezwa kwa mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuweka utaratibu wenyewe matumaini ya kusambaza umeme vijiji kupitia miradi mbalimbali. Hata hivyo nina machache ya kuchangia kuhusu miradi iliyopangwa kutekelezwa Wilayani Kondoka katika mwaka wa 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, katika jedwali Na.9 ukurasa wa 76 ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Wilaya ya Kondoa ni moja ya Wilaya zilizopangiwa kupatiwa umeme kupitia mradi wa *MCC*.

Mheshimiwa Spika, nasikitika kusema kuwa Wilaya ya Kondoa kwa ujumla na hususani Jimbo la Kondoa Kusini imepangwiwa miradi michache na midogo sana. Katika orodha hiyo ni vijiji viwili tu vya Dalai na Hamai vimepatiwa mradi katika Jimbo la Kondoa Kusini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, ninaomba nimshauri Mheshimiwa Waziri anisaidie yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Hamai kwa taarifa kimekwisha patiwa umeme, hivyo ninaomba mradi wa kijiji cha Hamai uhamishiwe kijiji jirani cha Churuku.

Mheshimiwa Spika, naomba vijiji vya Mapango, Igunga na Mwailanje viongezwe katika miradi inayotekelawa chini ya mradi wa *MCC*.

Mheshimiwa Spika, vijiji vyote hivi nilivyopendekeza viongezwe viko karibu sana na njia kuu ya umeme wa gridi ya Taifa, hivyo gharama ya kufikisha umeme katika vijiji hivyo ni ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi ya kuchangia. Naunga mkono Hotuba ya Waziri.

MHE. HASSAN CHANDE KIGWALILO: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini - Mheshimiwa William Mganga Ngeleja na Naibu Waziri - Mheshimiwa Adam K. Malima kwa nyadhifa walizopata. Nina imani kubwa kwamba Wizara imepata viongozi waadilifu na ninawatakia kila na kheri katika majukumu hayo mazito. Aidha, nawapongeza kwa hotuba nzuri, pia ninampongeza Katibu Mkuu na wataalam husika.

Mheshimiwa Spika, nimeisoma hotuba ya bajeti ya Wizara husika, sikuona maelezo kamilifu ya namna ya umeme wa *Mnazi Bay* utavyoletwa Wilaya ya Liwale – kama vile *Time Frame*, Kampuni gani itayohusika na kupeleka umeme Liwale umbali wa *Kms 136* kutoka Nachingwea, lini zitaanza kuwekwa nguzo na ni kampuni gani

itahusika? Je, mkataba wa kazi hiyo umeshatiwa sahihi? Kama bado, kwa nini? Je, fedha za kugharamia mradi huo zimepatikana? Kama bado hali halisi ikoje?

Mheshimiwa Spika, nikiwa kama Mbunge wa Wilaya ya Liwale, ni muhimu kufuatilia kwa karibu namna Wilaya hiyo itavyonufaika mapema na mradi wa umeme wa *Mnazi Bay*, kwani majenereta yanayotumika kuzalisha umeme Liwale sasa yamechakaa na kama umeme wa *Mnazi Bay* utachelewa, hali ya uzalishaji wa umeme wa majenereta Liwale utazidi kuzorota.

Kwa vile kutoka Nachingwea kwenda Liwale ni kilometra 136 na hakuna nguzo hata moja ilioanza kuwekwa kuelekea Liwale: Je, Serikali haioni kuweka mikakati madhubuti hivi sasa ni muhimu sana ili umeme utakapofika Masasi, Ndanda na Nachingwea tayari pawe na nguzo kwenda Liwale ili umeme huo ufile Liwale? Ninaomba Mheshimiwa Waziri atoe maelezo kamili atapokuwa anafanya majumuisho leo jioni.

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Serikali au *TANESCO* kwa kutupatia *Spares* mara kwa mara za kukarabati majenereta ya Wilaya ya Liwale. Ninaomba na kushauri Serikali iendelee kutuma *spares* na mafundi husika ili kuyakaribati majenerata hayo ya Liwale kila inapobidi.

Ninawashukuru watumishi wa *TANESCO* Liwale japo kuwa majenereta hayo ni chakavu, wanafuatilia *spares* mara kwa mara. Ninaomba Serikali ituunge mkono kwa kutupatia *spares* kila inapobidi ili Liwale iendelee kuwa na umeme hadi hapo umeme wa *Gas Mnazi Bay* utapofika Liwale.

Ahsante. Ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. GAUDENCE CASSIAN KAYOMBO: Mheshimiwa Spika, naanza na pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Ngeleja na Naibu wake Mheshimiwa Malima kwa kazi nzuri wanayoifanya wakishirikiana na wafanyakazi wote wa Wizara hiyo.

Mheshimiwa Spika, naipongeza na kuishauri Serikali kwa kuwajali sana wananchi wa Mbinga. Mji wa Mbinga ulianza kupata umeme kwa kutumia jenereta dogo la Halmashauri toka tarehe 7 Septemba, 2007. Jenereta mbili mpya zimewasili. Patakuwa na ucheleweshaji wa kufunga kwa sababu ujenzi wa sehemu ya kuweka machine ulikosewa.

Kuhusu umeme, yapo matatizo yafuatayo: Sio kweli kwamba mifumo ya usambazaji umeme katika Mji wa Mbinga umekalimika. Ukarabati wa mifumo ya zamani tu iliyofanywa na *MECCO* ndiyo iliyofanywa tofauti na ilivyosomwa ukurasa wa 13 wa hotuba wa Mheshimiwa Waziri. Sehemu kubwa ya mji wa Mbinga mifumo hiyo bado. Hivyo wananchi watalazimika kulipa gharama nyingi sana kupata/kuvuta umeme. Serikali ilitoa Shilingi milioni 500. Je, zilifanya kazi gani? Inafaa kufanya uchunguzi.

Baada ya jenereta mbili mpya kufanya kazi, napendekeza ili jenereta ndogo ninayotamka sasa ipelekwe mji mdogo wa Maguu. Sina wasiwasi na Halmashauri kutoa jenereta hiyo ikatumika Maguu, mradi tu *TANESCO* waendelee kuiendesha kama ilivyofanya Msanga. Naomba Wizara ifikirie na ifunge kwa dharura utoaji wa umeme mji mdogo wa Maguu. *It is a viable project.*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kujua maendeleo/utekelezaji wa majibu ya Wizara kwa hoja nilizotoa wakati wa kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais – Dodoma. Nukuu majibu ya Wizara ya tarehe 23 Machi, 2006 Kumb.Na.EB.83/447/01/10. Wachimbaji wadogo bado mpaka sasa maeneo hayo hayajatengwa rasmi. Naelewa na nashukuru wapo waliopata leseni, kinachotakiwa ni tamko kwamba eneo hilo ni la wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, eneo dogo tu la Mbalawala Kata ya Ruanda sasa linafanyiwa utafiti na *NDC*. Kuna maeneo mengine ya Ngaka na Mbanwa. Naomba *GST* watusaidie ili tuje kiasi gani mali iliyoko.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa kituo cha umeme Nakatute. Sioni mahali popote pakitajwa, lini maendeleo yake? Nitafurahi kupata majibu kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme wa gridi, naomba umeme huu ifikiriwe pia kuweza kufika katika miji midogo ifuatayo: Ruanda, Matiri, Maguu na Litembo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwezeshaji wa wachimbaji wadogo, *DIT* walinieleza kuwa wanaweza kutengeneza zana za watu hao. Naomba mfuatilie. Naomba hatua zilizoainishwa ziingie Mbinga kwa wachimbaji wa Ngemba mbili, Masungwa, Makoro na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utengenezaji vito, *South Korea* wana utalaam juu ya mambo hayo, mawasiliano nao yaanzishwe. Pale *South Korea* pia wanayo *Museum* kubwa sana ya madini ya aina yote. Ni sehemu ya utalii, mafunzo na burudani. Ni vizuri kuwa na sehemu kama hiyo hapa nchini kwa sababu sisi tuna madini ya kila aina. Inawezekana *South Korea* wanaweza kutusaidia juu ya hili pia.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kutupa umeme Mbinga. Naomba usambazaji uboreshwe. Naunga mkono hoja.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana, Mheshimiwa Waziri, akiwa Naibu Waziri akijibu swali langu juu ya umeme, kutoka – Mtera – Kisima – Chipogoro Wiyenzele, Mtamba, Rudi, Masa Hadi Ipera kuwa tathimini ilikwishafanywa na kwamba gharama ni Shilingi bilioni 4.5 na kwamba *RFA* ndiyo jibu la tatizo langu. Je, kwa nini mradi huo haujatajwa wala kutengewa fedha katika bajeti ya 2008/2009. Naomba maelezo.

Mheshimiwa Spika, Miradi ya *MCC*, *design and planning* yake haikuhusisha *local government* na hivyo vijiji vingi vimerukwa bila sababu na Mheshimiwa Waziri. *We must be careful*, miradi hii itakuwa *effective* na *more economic* kama itapita kwenye vijiji badala ya kupita porini. Mfano *MCC* – Kibakwe wanataka umeme utoke Iyenge (Kijiji) – hadi Pwaga (Kijiji) badala ya kutoka Kibakwe – Ikuyu ambako kuna *Sec.* – Luhundwa (*Sec.*) – *then* Pwaga (*Sec.*) na umbali wa *line* hizi karibu sawasawa.

Mheshimiwa Spika, kabla ya utekelezaji wa miradi hii, naomba wataalamu waangalie uwezekano wa kufanya mabadiliko ili mradi hayabadili gharama. Naunga mkono hoja.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Nishati na Madini - Mheshimiwa William Ngeleja, Naibu Waziri - Mheshimiwa Adam Kighoma Malima na viongozi wote wa Wizara kwa kazi nzuri ya maandali ya bajeti ya mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini ukurasa wa 214, aya ya 45 Mheshimiwa Waziri amesema kuwa bei ya nguzo moja ni Sh.153,017/=

Mheshimiwa Spika, siyo kweli hata kidogo, kwani *TANESCO* wanauzu nguzo moja kwa Sh.1,374,000/=. Bei ambayo mwananchi wa kawaida asiyé Afisa katika ofisi au mfanyakia hawezi kumudu. Mheshimiwa Waziri arekebishe kauli yake au aeleze bei halisi za nguzo ili wananchi wasilanguliwe na *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, Ukurasa wa 23 Mheshimiwa Waziri amezungumzia suala la uhusiano wa *TANESCO* na *IPTL* na kwa *capacity charges* inayolipwa na *TANESCO* kwa *IPTL* ni zaidi ya kiasi kinachostahili kufuatana na ukokotolewaji kwa kutumia mtaji (*equity*).

Mheshimiwa Spika, Kama kilichosemwa na Mheshimiwa Waziri ndio ukweli wenywewe, kwa nini *TANESCO* wanaendelea kuilipa *IPTL*?

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuongezeka kwa shughuli nyingi za utafutaji, uchimbaji na biashara ya madini kuongezeka wananchi walitegemea pato la Taifa kuongezeka maradufu na siyo kwa asilimia ndogo ilivyo katika taarifa ya Mheshimiwa waziri. Hii inaonesha ni kwa jinsi gani wachimbaji wakubwa wanavyotuobia. Serikali ituambie mikakati madhubuti kuthibiti uwizi huu wa wazi kwa Taifa.

Mwisho, naunga mkono hoja.

MHE. VUWAI ABDALLAH KHAMIS: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri Mheshimiwa William M. Ngeleja na Naibu Waziri - Mheshimiwa Adam Malima kwa kazi nzuri, pia kwa mashirikiano na watendaji wa Wizara pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara yao.

Mheshimiwa Spika, nishati kwa Tanzania ndio tegemeo kubwa la uchumi wetu. Kwa hiyo, naiomba Serikali kusimamia vyema hasa kwa bajeti hii baada ya kupitishwa na ni vyema Tanzania tukatumia wazalendo na uzalendo juu ya sekta za nishati zote.

Mheshimiwa Spika, umeme kwa Zanzibar na Tanzania Bara, kwa nini kuwe na tofauti ya malipo? *EWURA* kwa nini kwa sasa isiondoe tatizo hili? Kwa kweli naiomba Serikali iliangalie haraka na pia litatuliwe iwe *TANESCO* ya Ari mpya, Nguvu na Kasi Mpya.

Mheshimiwa Spika, miradi ya ndani ya nchi yetu hutupatia ajira kwa wananchi wetu, pia Serikali kupata pato, lakini bado hatulianglii vizuri. Kwa hiyo, naiomba Serikali wachimbaji wa madini wote waangaliwe hasa hawa wadogo wadogo wapewe nguvu kubwa sana hasa kwa bajeti hii na sisi Wabunge tutaitipisha kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magogoni na mimi mwenyewe.

Naunga mkono hoja hii.

MHE. DAMAS P. NAKEI: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa W. Ngeleja - Waziri wa Nishati na Madini na Naibu Waziri - Mheshimiwa Malima kwa maandalizi mazuri yaliyozaa hotuba nzuri. Nampongeza pia Mheshimiwa Rais J. Kikwete kwa kuunda Kama/Tume kuchunguza mikataba ya madini. Taarifa ya Tume ya Bomani ni mkombozi wetu katika eneo hili la madini.

Mheshimiwa Spika, tunayo taarifa ya kuwepo *uranium*. Tuambiwe kuna mpango gani wa umeme wa *Nuclear Power* hapa nchini? Japan wanatumia 80% *nuclear power*, 20% ndio mengineyo kama makaa ya mawe na maji kuzalisha umeme. Tuchukue mfano huu wa Japan.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliahidi kufikisha umeme katika vijiji vya *RIRODA* mwaka 2002/2003. Lini ahadi hii itatekelezwa? Mradi wa *Electricity TV* umepita juu ya vijiji vya Muwada, Vilima vitatu, Madunga Kati. Naomba umeme huo ushushwe kwa wananchi wa sehemu hizo pamoja na Gidas jirani na Bereko.

Mheshimiwa Spika, baada ya maombi hayo naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

MHE. BUJIKU PHILIP SAKILA: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wake na watendaji wote walioshiriki katika uandaaji wa hotuba hii. Ni hotuba nzuri, yenye matumaini kwa wananchi wengi wa Jimbo la Kwimba, nawapongeza sana na kwa niaba ya wananchi wote watakaofikiwa na umeme husika.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie kutoa ufanuzi katika masuala mawili. Je, Mheshimiwa Waziri anaposema Mwamashimba itapata umeme ana maana ya kitongaji cha Mwamashimba au Tarafa ya Mwamashimba? Katika Wilaya ya Kwimba hatuna kijiji cha Mwamashimba. Tulivyonavyo ni:-

Mheshimiwa Spika, Shule mbili za Mwamashimba (Msingi na Sekondari. Shule hizi zimo katika kijiji cha Sanga Kata ya Fukalo. (Kijiji hiki hakijaorodheshwa).

Mheshimiwa Spika, kipo Kitongoji cha Mwamashimba kimo katika Kijiji cha Bupanwa Kata ya Bupumwa. Kipo Kitongoji cha Butigiyi yalimo Makao Makuu ya Tarafa ya Mwamashimba yenye Kata tano. Katika Kitongoji cha Butigit kimo kituo cha Afya kinachotumia jina la Tarafa (mwamashimba) na Kitongoji cha Butigit kimo katika kijiji cha Bupamwa ambacho hakimo katika orodha iliyotajwa katika jewali Na.12. Je, hasa ni vijiji vipi vilivytengwa? Naomba orodha iwe bayana.

Mheshimiwa Spika, ufanuzi wa pili ni chanzo cha umeme huo na gharama yake. Taarifa za awali zilikuwa zikionesha kuwa kwanza umeme ungepoozwa katika kijiji cha Mabuki (Misungwi) na kutoka hapo ungesambazwa kuelekea maeneo mengine pamoja na Hugumatwa, Mwabujo, Sangu na Kwingineko kama Nyamilama.

Mheshimiwa Spika, naomba kufahamishwa, umeme utafikaje Hugamlwa kutoka Mabuki bila kupita Rumele. Iwaje Rumele isiwemo katika orodha? Ni kwa namna gani umeme utafika Ngamilama bila kupertia Malemve Jojiro, Gatulina. Shigunhulo? Mbona vijiji hivi havijafikiriwa? Umeme uliotajwa unakwenda hadi Nyamilama kwa upande mmoja na Hungumalwa kwa upande mwengine. Je, vijiji vya Ilula na Mwankulwe imeshindikana kabisa kuongezwa? Ni vitu yenye watu wengi na wenye uwezo wa kuvuta umeme iwapo gharama zitapunguzwa kidogo. Je, vijiji hivi kama haitawezekana kabisa kuiongeza? Vinaweza kufikiriwa kwa siku za karibuni?

Mheshimiwa Spika, napenda kwa dhati kumpongeza na kumshuru kwa dhati Mheshimiwa Waziri na watendaji wa Wizara hii kwa kuwa safari hii wameonyesha kuwa wako makini. Nimekuwa nikiomba umeme kila mwaka tangu 1996 kwa ajili ya maeneo yaliyotajwa hadi mwaka huu. Mwaka huu nashukuru nia hiyo inaonekana.

Ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri ni kuelezea kiasi kilichotengwa kitatumika kwa shughuli zipi za mradi huu. Mradi huu utaanza lini na kukamilika lini? Serikali inataraja kuwa ifikapo mwisho wa mwaka huu wa fedha, utakapokuwa unamalizika mradi huu utakuwa umefikia hatua gani. Naomba ufanuzi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. HERBERT JAMES MANTANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na viongozi wa Taasisi zote chini ya Wizara hii kwa kumsaidia Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoka ushauri na mapendekezo katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, bei za mafuta zinatishia maendeleo ya nchi, viwanda, kilimo, usafiri. Ughali wa maisha kwa wananchi na hivyo kudumaza uchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa kutoanza haraka na kuendeleza matumizi ya gesi asilia katika matumizi ya gesi viwandani, majumbani na katika magari kwa kasi, ni sawa na Serikali kufungia macho tatizo la bei za mafuta na kutojali mikakati ya kuinua uchumi wa Tanzania. Hakuna sababu za msingi kutoipatia *TPDC* fedha za kutosha kuanzisha miradi hiyo. Kiasi kilichotolewa kuanzisha ni kidogo sana!

Njia iliyo wazi ya kuiwezesha *TPDC* ni kupata mgao halisi wa sehemu ya mapato ya mauzo yote ya gesi, Songsongo, *Mnazi Bay* na hatimaye Mkwanga ili iweze kutekeleza miradi muhimu ya maendeleo niliyotaja hapo juu, pamoja na uwezo wa kuhifadhi mafuta ya dharura na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini itoe mchango wake katika kuanzishwa kwa uzalishaji wa *biodiesel*. Tanzania bado ina ardhi kubwa na ina nafasi ya uzalishaji wa mazao ya *jetrofa* (Mbono) na viwanda kuzalisha dizeli. Tatizo ni kubwa mahusiano na ushirikiano mzuri wa kitaifa kati ya vyombo mbalimbali vyenye majukumu tofauti. Kwa mfano, Wizara ya Ardhi, Wizara ya Kilimo ina mamlaka na kilimo, taasisi ya utekezaji (*TIC*) nayo ina mahusiano na wawekezaji. Hivyo kukosa mahusiano kunasababisha migongano, ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi muhimu ya kitaifa. Miradi ya *biodiesel* ni changamoto muhimu katika kupambana bei za mafuta Soko la Dunia. Serikali ikamilishe sera, mwongozo, kanuni za uwekezaji ili miradi hii ianzishwe.

Mheshimiwa Spika, jengo la *Mafuta House* sasa limepewe jina tofauti. Hivi Wizara imeridhika na hatua hiyo? Dhamira ya awali ilitosha kuweka heshima na *TPDC* katika sekta ya mafuta na hivyo kujenga kumbukumbu sahihi. Wizara ya Nishati na Madini itueleze imeridhika vipi kubadili Jina la Jengo lile? Kushindwa kuzuia hilo kutokea kusiwe tena kigezo cha kufanya *TPDC* ishindwe kuita ule mnara wa ofisi zao kuitwa *Mafuta Tower*. Turejeshe heshima ya awali ya sekta kuweka jina linaloweza kurudisha hadhi iliyopotezwa ya *Mafuta House*.

Mheshimiwa Spika, miradi yote ya uzalishaji umeme ni muhimu kupitiwa upya. Nilipata nafasi ya kuusoma mkataba wa uzalishaji umeme kati ya *TANESCO* na *IPTL*. Mradi una kurasa nyingi zenyelengo la kumfanya mshiriki (*TANESCO*) ashindwe kufanya tathmini halisi ya makubaliano hasa katika eneo la *formula* ya ukokotoaji wa malipo.

Hii inaridhisha dhamira ya kufanya ukokotoaji kuwa mgumu na kutoa mwanya wa kuwezesha malipo kuwa makubwa kuliko dhamira ya mshiriki wa mkataba (*TANESCO*) wakati wa majadiliano kabla ya kuingia mkataba. Hali hiyo imejitokeza katika viwango vya uwekezaji halisi kama ambavyo Wizara sasa imegundua kuwa umekuwepo udanganyifu.

Mheshimiwa Spika, je, Tanzania imenufaika vipi na makataba kati ya *TANESCO* na *ALSTOM POWER RENTALS*. Je, kampuni hii imezalisha kiasi gani cha umeme na kiasi gani kimetumika kule Mwanza kabla ya muda wa mkataba kwisha?

Mheshimiwa Spika, je, Serikali inayo majukumu gani katika mikataba ya *Alstom Power Rentals, IPTL, DOWANS* na *AGGREKO* katika jukumu la Kuondoa na kusafirisha mashine zao baada ya mikataba yao ya uzalishaji wa umeme wa dharura kuisha?

Mheshimiwa Spika, Huduma za Ofisi za *TANESCO* Wilayani. Wilaya ya Muheza inahudumiwa kijiografia na Ofisi ya Wilaya Muheza na sehemu nyingine na Ofisi ya *TANESCO* Korogwe hasa Kata za Songa, Potwe na Bwambwera zilizoko Wilaya ya Muheza.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu umeiathiri Wilaya ya Muheza kwa kupata huduma duni toka Ofisi za *TANESCO* Korogwe. Kwa mfano:-

- (i) Ahadi za Wizara hata kwa kuweka *transforma* tuu pale Songa tangu mwaka 2005/2006 haijatekelezwa.
- (ii) Mameneja wawili wa Ofisi ya *TANESCO* Korogwe, aliyekuwepo 2005 – 2007 na aliopo sasa, wamenithibitishia kwamba kwa upande wao eneo la Muheza lililopo chini yao hajawahi kupata hata mradi mmoja chini ya mpango wa *MCC*. Kwa upande wa *TANESCO* Muheza nashukuru sana miradi ya *MCC*, ipo ya kuridhisha. Naiomba Wizara na *TANESCO* waangalie hali niliyoileza hasa ya huduma duni toka *TANESCO* Korogwe kwa Wilaya ya Muheza.

Mheshimiwa Naibu Spika nina maombi maalum. Wahisani na wananchi binafsi wamegharamia uvutaji wa umeme katika maeneo mbalimbali kutokana na *TANESCO* kushindwa kwa muda mrefu. Mfano:

- (i) Kituo kipyta cha Polisi Muheza (Wizara ya Mambo ya Ndani imegharamia);
- (ii) Zahanati ya Magoda Kata ya Lusanga (Taasisi ya Dini imegharamia); na
- (iii) Maeneo ya Michungwani (Wananchi binafsi na Taasisi za Dini zimegharamia zenyewe).

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais atafungua *Muheza High School* tarehe 18 Julai, 2008. *TANESCO* Muheza wanataka Shilingi Milioni 30 kufikisha umeme hapo shulen. Shule ni ya Serikali. Naomba Wizara na *TANESCO* zisaidie shule hii ya Taifa ipate umeme fedha za *MCC* au vyombo vingine kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Spika, kwanza, nashauri mapendekezo ya Kamati ya Rais yatekelezwe haraka, ni juu ya Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Spika, Tatizo la Umeme Mkoani Kigoma: Mabadiliko ya Baraza la Mawaziri ni ya nia njema, lakini mabadiliko hayo pia yanaathiri utendaji na inapunguza tija hasa katika maamuzi na baadhi ya miradi inaathirika.

Mheshimiwa Spika, kufuatia ahadi ya Mheshimiwa Rais tarehe 29 Agosti, 2005 *Kigoma Centre* aliahidi umeme wa gridi ya Taifa kwenye Wilaya mbalimbali ikiwemo Mbinga na Kigoma. Ninasema mabadiliko yanaathiri utendaji na baadhi ya miradi inaathirika kwa mfano ufuatao:

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya 2006 – 2007, Waziri wa kipindi hicho Mheshimiwa Msabaha alilieleza Bunge hili kuwa *ADB*, *African Development Bank* itafadhili umeme wa grid ya Taifa kutoka Tabora – Kaliua – Urambo – Kigoma. Nguzo zitawekwa kufuata reli kutoka Tabora - Kaliua Urambo mpaka Kigoma na baadaye Wabunge wa Mkoa wa Kigoma tulikutana na Mheshimiwa Msabaha akatueleza mradi ulivyo na anahakikisha kuwa *ADB* wanafadhili mradi. Tulimwuliza ikiwa *ADB* hawatatoa, alisema ni ahadi ya Rais, lazima itekelezwe hata kwa pesa za ndani.

Mheshimiwa Spika, *Bajeti ya 2007 – 2008*, ilikuja picha tofauti chini ya Waziri mwingine Mheshimiwa N. Karamagi, yeye alikuja na mrdi wa Geita – Bulyankulu mpaka Nyakanazi, kwamba umeme wa grid ya Taifa utatoka Geita – Bulyankulu mpaka Nyakanazi.

Kwa maana hiyo Kibondo na Kasulu zingepata umeme wa gridi kabla ya Manispaa ya Kigoma. Cha kusikitisha au kushangaza Waziri huyo hakutoa maelezo ya hatua ya mradi wa 2006/2007 chini ya ufadhili wa *ADB*. Nilipomwuliza wakati wa kuitisha vifungu, Waziri huyo alijibu kwamba mradi ule wa 2006 – 2007 haukuwa (viable) mzuri kwani umeme ungefika Kigoma ukiwa mdogo. Swali langu ni moja ina m aana bunge linaweza kuletewa taarifa ya miradi iliyotengewa fedha bila *feasibility study*? Au wafadhili gani wanatoa pesa bila kupewa uhakika wa mradi? Je, hizo *feasibility study* (upembizi yakinifu) hautumii pesa? Au haukufanywa kabla ya mradi?

Mheshimiwa Spika, bajeti ya 2008/2009 imekuja na mambo mapya, uk.16, kuna maelezo mafupi sana yanayosema, Kigoma imetengewa shilingi bilioni 13.8 kwa ajili ya ufungaji wa mitambo na mitambo hiyo ni yenye uwezo wa kuzalisha MW6 na ufungaji huo wa mitambo unatarajiwa kukamilika 2009 mwishoni. Huu ni mkakati wa muda mfupi.

Maelezo hayo hayasemi pesa zimetoka wapi, mitambo itanunuliwa lini? Hakuna maelezo ya Kasulu wala Kibondo.

Mheshimiwa Spika, ukirejea ukurasa wa 48, inaelezwa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Ngeleja kuwa pesa za *MCC* shilingi milioni 53.7 za Kimarekani zitatumika kujenga kituo cha kuzalisha umeme kwenye mto Malagarasi cha MW8 kwa ajili ya Kigoma, Uvinza na Kasulu. Hapa Kibondo haitajwi au haipo Kigoma.

Hatujaambiwa pesa zitapatikana lini na Mradi unaanza lini. Ninachojua mimi pesa za *MCC* zimeanza kusikika toka naingia Bungeni mkataba umesomwa Februari, 2008. Wala hazitatolewa shilingi milioni 698 zote zitatolewa kwa awamu. Maana yake ni kwamba kwa pesa zinatolewa kidogo kidogo, itategemea wanaofanya maamuzi mradi upi uanze kati ya mingi inayofadhiliwa na *MCC*.

Mheshimiwa Spika, sitashangaa mwaka 2008/2009 tukiletewa mradi mpya na hii ya nyuma ikafa kama ilivyo kawaida. Kwani hata Waziri wa Nishati na Madini wa sasa hajaelezea hatua ya mpango wa mradi tulioambiwa na Mheshimiwa Karamagi wa mwaka 2007/2008 ule wa gridi *extension from Geita – Bulyankulu, Nyakanazi*, kaja na yake mapya. Ndio maana nashawishika kuwa tatizo la miradi kutokuwa endelevu ni mabadiliko ya baraza mara kwa mara. Kwani toka mwaka 2005 – 2008 Baraza limebadilika mara nne na kuvunjwa kabisa mara moja. Pamoja na kwamba Baraza zima ndio hupitisha maamuzi, lakini inagemea ushauri wa Waziri husika kadri aonavyo yeye inafaa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ukurasa Na.49, ameleezea usitishwajiwa wa Mkataba wa *Richmond/Dowans* kuanzia tarehe 1 Agost, 2008. Ametoa maeleo mafupi sana mpaka leo Serikali haijataja wamiliki. Swali hili halihitaji kujibiwa.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 46 kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya pamoja na kwamba Waziri ametoa *statement* kuwa kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya utaendelea kutekelezwa kulingana na maelekezo ya Ilani ya CCM, kwa kadri ya upatikanaji wa fedha. Maneno hayo hayatoshi, hakuna mpango, mikakati madhubuti ya kupeleka umeme Makao Makuu ya Wilaya. Wala hakuna *time frame* ya utekelezaji. Tunachoshwa na maneno ya kiasisa, hawahitaji utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, *TPDC*, kutokana na sheria tuliyopitisha ya petroli ya 2008, *TPDC* inatakiwa ianze kuagiza mafuta kwa wingi (*Bulk procurement*) haraka iwezekanavyo, hii itasaidia kupunguza ongezeko halali la bei ya mafuta inayopanda kila siku. Nashauri Serikali ingalie uwezekano wa kutoa ruzuku kwenye mafuta. Hili jambo linawezekana, kwani tunasamehe pesa nyingi sana za kodi kwa wawekezaji, tuache tabia ya kusamehe kodi. Ruzuku itasaidia kupoza bei ya mafuta na kupunguza mfumko wa bei za bidhaa mbalimbali kutokana na bei ya uzalishaji na usafirishaji kuwa juu.

Mheshimiwa Spika, mipago mingi ya Serikali haina *time frame*. Miradi mingi inatajwa kwa lugha za kuvutia na kutia matumaini, lakini utekelezwaji wake ni mgumu sana kwani Serikali haina mikakati ya kupata fedha. Hii ni changamoto, tuangalie Sekta mbalimbali ikiwemo ya madini, bado haijaweza kuisaidia nchi kimapato. Serikali aingalie vyanzo mbalimbali na ichukue maoni ya Kambi ya Upinzani kwenye hotuba ya bajeti ya Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, *Power System Masterplan PSMP*, ukurasa wa 18, imeonyeshwa mipango ya muda wa kati na muda mrefu maeleo hayo yamejitokeza mara kadhaa na mradi wa *Stiglers George (MW 158)* unatajwa tu karibu katika kila hotuba,

mipango haina *time frame*, kuna taarifa kuwa *feasibility study ya stiglers George*, awali ulifanyika (1985) na mpaka leo tunaandika tu bila utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali iwe naeleza angalau kwa mafungu. Kifungu cha *OC*. Katika Wizara hii, zimeombwa Sh. 362,922,265,600/= za maendeleo Sh. 320,067,385,600/. Matumizi ya kawaida Sh.42,854,880,000/=, Sh. 33,051,639,000/= ni mishahara na Sh. 39,549,241,000/= ni matumizi mengineyo. Sh. 39,549,241,000/= ni nyingi sana, lakini hazitolewi maelezo.

Mheshimiwa Spika, Wakati Waziri Mkuu akijibu hoja, alimtakia Mheshimiwa Ngeleja kutafuta *appropriate time* kutoa *statement* ya Serikali juu ya Kiwira, nasisitiza jambo hilo lifanyike kama ilivyoshauriwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Pete M. Pinda.

MHE. DR. ALI TARAB ALI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nanukuu baadhi ya malengo ya Sera ya Taifa ya Mazingira. Sera hii ina lengo la kufanya mazingira kupewa kipaumbele katika kila maamuzi muhimu kwa ajili ya kupata maendeleo endelevu, usalama wa afya za watu na utumiaji mzuri wa rasilimali kwa ajili ya kupata mahitaji yote muhimu ya waliopo na wanaokuja. Pia lengo lingine ni kulinda na kuhifadhi mazingira kama vile maji, ardhi na hewa ambavyo vyote ni muhimu kwa maisha yetu.

Maelezo haya yanaonyesha jinsi gani mazingira yalivyo muhimu katika kila kipengele cha maendeleo ya maisha ya mwanadamu na hakuna mafanikio yoyote bila ya kuweka mbele mazingira.

Licha ya faida kubwa zinazopatikana na uchimbaji wa madini, lakini kutokana na ongezeko la machimbo hayo inapelekea kuweka mazingira katika hali ya hatari. Mfano mzuri ni sehemu za Shinyanga, Mwanza na Musama. Wengi wa wakazi wa sehemu hizi wanategemea kilimo na ufugaji katika maisha yao yote. Uongezekaji huo wa mashimo unapelekea kupunguzwa kwa ardhi ambayo ni sehemu muhimu katika uzalishaji na ufugaji na hii imepelekea kuongezeka umasikini kwa kiasi kikubwa ambaa umechangiwa na uharibifu wa mazingira.

Mabaki ya mawe yatokanayo na madini yana mchanganyiko wa *sulphur oxide* ambapo inapochanganyika na maji inapelekea kufanyika kwa tindikali aina ya *sulphuric acid* ambayo huleta athari kubwa kwa mazingira, binadamu na wanyama.

Mfano, katika Nyakambale, Geita, maji yaliyopo katika kijiji hicho yameathiriwa zaidi na tindikali hili ambalo athari yake huwa ni kubwa kwa wanavijiji na wanyama wao kama vile ng'ombe. Wengi wa wanyama hawa hufa kutokana na maji hayo ambayo sio salama. Pia, wanavijiji hulalamika sana kutokana na kushindwa kutumia maji hayo ambayo hayaaminiki, sio kwa kunywa, lakini hata kutumia majumbani.

Mheshimiwa Spika, tunasikitishwa na *Environmental Impact Assessment (EIA)* ambaa ndio wahusika wakuu wa kushughulikia hifadhi ya mazingira, lakini uwepo wake

hauonekani, hasa kwa usalama na afya ya jamii. Mazingira yanaharibiwa na maisha ya watu yako hatarini, lakini *EIA* imekaa kinya. Je, kazi yake sasa ni nini?

Mheshimiwa Spika, *Cyanide* ni sumu ambayo inapatikana katika uchimbaji wa madini ya dhahabu (*waste water*). Maji haya machafu huenda moja kwa moja kwenye vyanzo vyta maji kama vile sehemu za ndani na jirani ya Ziwa Victoria, ambayo huleta athari kubwa kwa binadamu na viumbe wengine wanaotumia maji hayo.

Uchimbaji mkubwa wa madini (*large scale mining*) hasa uchimbaji wa dhahabu unaofikia tani 20 unapelekea kuweka shimo kubwa ambalo huhatarisha maisha. Mfano ni lile shimo lililopo Geita ambalo linafika mita 600. Hii inapelekea maporomoko ya ardhi (*land slides*) lakini pia inapelekea maafa ya mara kwa mara na hatujui Wizara imechukua hatua gani juu ya tatizo hili.

Aidha, sehemu kubwa za Geita ni jangwa, ambayo ni hatari kwa maisha ya mwanadamu na kwa viumbe wengine ambao misitu hiyo huwa ni makazi (*habitat*) yao. Lakini pia, misitu ni muhimu kama ni chanzo cha mvua, lakini kubwa zaidi inasaidia kupunguza kiwango cha *carbon dioxide (CO₂)* ambayo athari zake ni kuongezeka kwa joto duniani.

MHE. DR. GUIDO GOROGOLIO SIGONDA: Mheshimiwa Spika, hongera kwa hotuba nzuri. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, Wilayani Chunya wachimbaji wadogo wadogo hunyanyaswa sana na wakati mwingine huondolewa kwa kufukuza na kuzuiwa kuendelea na shughuli za uchimbaji ili kusije kukatokea vurugu na mfarakano kama yanayotokea maeneo mengine, siyo vyema maeneo yakatengwa rasmi kwa ajili ya wachimbaji hao wadogo wadogo huko Wilayani Chunya.

Mheshimiwa Spika, kwenye Jimbo la Songwe wananchi waliitikia wito wa kushiriki katika kuchimbia nguzo za umeme umbali wa kilomita 29. Mradi ulianza mwaka 2003, lakini hadi sasa nyaya bado hazijaanza kutandikwa. Nashauri mradi huo uendelezwe ili wananchi wasije wakavunjika moyo.

Mheshimiwa Spika, Wilayani Chunya yapo matatizo kadhaa yanayohusu uchimbaji madini na usambazaji umeme, mipango ingefanyika Waheshimiwa Mawaziri kupanga safari kutembelea huko.

MHE. HEMED MOHAMMED HEMED: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake iliyojaa matumaini kwa Watanzania kwa kunufaika kwa mali yao iliyomo ndani ya tumbo la ardhi, pia na mgongo wa ardhi ya nchi yao.

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu nitoe mchango wangu katika hotuba hii iliyopo mezani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madini, Tanzania ni nchi iliyobahatika kuwa na aina mbalimbali za madini ukilinganisha na nchi zote za Bara la Afrika. Pamoja na wingi wa madini tulionayo, bado madini yetu hayajamsaidia mwananchi wa nchi hii na hata mrahaba unaopatikana katika madini yetu ni mdogo sana. Hii inathibitisha madini yetu inawasaidia wawekezaji zaidi amba o huzinufaisha nchi zao jambo ambalo nchi yetu sisi maskini.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili linasababishwa na ubovu wa mikataba iliyopo. Hivyo basi Serikali inapaswa kuiangalia tena mikataba ili kuondoa dosari zote ambazo zinatoa mwanya kwa wawekezaji wa nje kuzitajirisha nchi zao kuliko Tanzania yenye.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafuta na gesi asilia, kwa kuzingaia Muungano wetu, mafuta na gesi ni mali ya Muungano. Tunaiomba Serikali itujulishe hali ya mapato ya mafuta na gesi asilia. Pia na mgao wa fedha iliyopata Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo nasema ahsante.

MHE. ALI KHAMIS SELF: Mheshimiwa Spika, Serikali kuanzia Agosti, 2008 itakuwa imeshaachana na Mkataba wa *DOWANS* hali ambayo kwa hiari kidogo sana italipunguzia mzigo shirika la *TANESCO*. Je, ni lini sasa Serikali itaondokana na mikataba mizito ya *IPTL* na mengineyo yenyе gharama za uendeshaji kubwa (*Capacity Charge*)?

Mheshimiwa Spika, nadhani ipo haja *TANESCO* kufikiria ufinyu wa bei ya uungaji wa umeme kwenye nyumba. Gharama kubwa inawapunguzia uwezo wa wananchi kuwa wateja wa *TANESCO*. Gharama zikiwa ndogo *TANESCO* ingelipata wateja wengi.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ina mchango mkubwa katika kuhakikisha uhifadhi wa mazingira katika kubuni nishati mbadala badala ya makaa na kuni. Imezoleka kila leo kuzungumza uhifadhi wa mazingira, lakini hatua madhubuti ya kulikabili suala hili kwa Serikali halipo na kama lipo basi ni la hiari kidogo .

Mheshimiwa Spika, umefika wakati sasa Wizara itueleze ni mkakati gani utachukuliwa ili tupate nishati mbadala ya bei nafuu ili wananchi wa Tanzania amba o ni maskini waweze kuitumia. Ahsante.

MHE. PROF. IDRISA A. MTULIA: Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri Ngeleja, Naibu wake, Mheshimiwa Adamu Malima, Katibu Mkuu na watendaji wa ngazi zote katika Wizara ya Nishati na Madini, kwa kutuletea bajeti nzuri inayowafikia wananchi wengi hususan wale “*Marginalized*” mfano Rufiji, kwa sababu hiyo ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, pili, naishukuru Serikali kwa kutupatia umeme Makao Makuu ya Wilaya ya Rufiji yaani mji wa Utete. Aidha, kupata umeme wa *grid* kwa vijiji vya Mohoro, Nyamwage, Ikwiriri, Kibiti, Bungu, Nyamisati na Jaribu.

Mheshimiwa Spika, tatu, tunashukuru wakulima wetu waliokatiwa mazao yao ili kupidisha njia ya umeme, wote wamelipwa fidia zao, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, ombi, kwa kuwa bomba la gesi na nguzo za nyaya za umeme zinapita katika vijiji vifuatavyo navyo havipo katika *program* ya kupata umeme huu wa Songas, naomba vijiji vifuatavyo vipatiwe umeme navyo ni Kiwanga, Chumbi, Utunge, Nyanda-Katundu na Kindwitwi kabla ya kuingia Utete.

Mheshimiwa Spika, nne, kuhusu ujenzi wa Mradi wa Stiegler's George, *Hydropower (Mw 2400)*. Tunaomba Serikali iharakishe kuwapa moyo wawekezaji waliojitokeza na matumaini ili waanze kazi mara moja kwa mpango wa "BOT".

Mheshimiwa Spika, umeme ndio maendeleo ya Taifa. Viwanda vyetu havizalishi na bidhaa zetu bei zake ziko juu kwa sababu ya *tariff* ya umeme wa viwandani na hautoshi. Bidhaa hizo sio *competitive* katika masoko ya Dunia. Rufiji itashukuru sana kama mradi huu utaanza mapema.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Mheshimiwa Waziri Ngeleja, atengeneze historia ya kusimamia Stiegler's Project na kumaliza tatizo la umeme Tanzania na kuwa na uwezo wa kuuza umeme nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, tano, ugunduzi wa *petroleum*, Kwinga wa Jongo, Kibiti Rufiji, ni faraja kwetu. Tunaiomba Serikali ifanye haraka kuhimiza uchimbaji wa mafuta hayo ili tunufaikie wote wakati huu mgumu.

Mheshimiwa Spika, sita, hongera kwa kuifufua *STAMICO*, kama chombo cha Taifa cha kudhibiti uchimbaji, usafirishaji na uuzaaji wa madini nchini.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja pamoja na angalizo lifuatalo:

Katika kitabu chenye ripoti ya *CAG – MARCH, 2007*, imetaja matumizi ya fedha za Serikali bila kutumia nyaraka kamilifu (*Questionable Payments*), jumla ya fedha zilizotumika hivyo ni bilioni 67.8/=, Wizara zote lakini Wizara ya Nishati na Madini peke yake imetumia bilioni 46.5/=, (68%) ya matumizi hayo.

Mheshimiwa Spika, ombi, Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, wajizatiti na kufuta dosari katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

MHE. DR. LUKA J. SIYAME: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kutoa maelezo mafupi kuhusu Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara na viongozi wa Taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Madini na Nishati kwa kazi kubwa ya kutayarisha hotuba yenyе kueleza mambo mengi sana kuhusu nishati na madini nchini. Hata hivyo, nasita kuunga mkono hoja kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mbozi, hususani Jimbo la Mbozi Magharibi, haijafikiriwa katika hata eneo moja la uendelezaji au uanzishaji wa miradi ya nishati, hususani ile ya umeme na madini;

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mbozi Magharibi, lenye eneo la kilomita za mraba 6,275, lina Kata kumi na moja (11), vijiji takribani tisini na tano (95), halina umeme kabisa kasoro kwenye mji mdogo wa Tunduma na kijiji cha Mpemba (Katete) ambayo kwa bahati tu vimepitija na mkonga wa umeme kutoka Zambia. Hata hivyo, umeme wa vijiji hivyo viwili ni wa kukatikakatika.

Mheshimiwa Spika, katika mkutano wa kumi na moja (11) wa Bunge lako Tukufu, hapo tarehe 10 Aprili, 2008, niliuliza swali kuhusiana na tatizo la umeme Tunduma. Jinsi linavyoathiri usalama wa raia pale, kurudisha nyuma shughuli za maendeleo, kukwamisha uvutaji wa maji kutoka kwenye visima vinavyotoa maji pale na pia kusababisha mashine za majokofu ya *mortuary* kutofanya kazi kwenye kituo cha Afya Tunduma.

Mheshimiwa Spika, nikaelezea kuwa kutokana na ahadi ya aliyekuwa Waziri Mkuu, katika ziara yake hapo mwezi Oktoba, 2007, kwa wananchi kuwa maji na umeme visipopatikana hadi kufikia 2010, basi Mheshimiwa Rais na Mbunge wa sasa, wasichaguliwe tena, ni vyema Serikali ikatekeleza ahadi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kinyume chake, hata ile *Transformer* ya umeme iliyokuwa imefungwa ili kupeleka umeme kwenye *mortuary* ya pale Tunduma na Kituo cha Afya kwa jumla, imeondolewa na kwenda kufungwa sehemu mpya inayojengwa na watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, *transformer* hii ilipelekwa pale baada ya maombi maalum niliyofanya baada ya tukio la udhalilishaji wa watu waliokuwa wakihifadhiwa kwenye *mortuary* ya Nakonde, upande wa Zambia. Napenda kujua ni kwa nini *Transformer* ile imeondolewa pale na kupelekwa kwenye eneo jipya la mji ule na nini hatma ya *mortuary* ile na majokofu yake? Majibu ya Meneja wa TANESCO, Tunduma ni ya kijeuri. Hatumbui tatizo la maiti zinazooza pale Tunduma zikiwa kwenye *mortuary* ile.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maji sasa hivi imechimba visima viwili vyenye maji mengi pale Tunduma na kuweka *inversion pump* za umeme, ambazo zimeshindwa kufanya kazi ya kupandisha maji kwa ajili ya matumizi ya mji huo. Ni kwa vipi Transformer hiyo, kama ilionekana haifai pale *mortuary*, isipelekwe kwenye matumizi ya kuvuta maji?

Mheshimiwa Spika, hayo ni kwa uchache tu. Naomba, nipewe uhakika wa mambo hayo machache na angalau ahadi ya utekelezaji wa utafiti wa nishati na madini Wilayani Mbozi, hususan Jimbo la Mbozi Magharibi ambalo halina shughuli yoyote ya viwanda kutokana na giza kuu lililotanda kule.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

MHE. ERNEST G. MABINA: Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongozi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Makamishna wote wa Nishati na Madini, kwa uteuzi na utendaji kazi wao mzuri sana ndio maana bajeti imewasilishwa kwa ustadi mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, namuomba Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, afanye hima ya kuleta Sheria ya Madini hapa Bungeni kwa kuwa iliyopo sasa hivi haitoshelezi au haikidhi mahitaji na kuleta tija kwa wananchi wanaokaa maeneo ya wachimbaji.

Mheshimiwa Spika, tumeng'ang'ania kubadilisha mikataba yetu, lakini haya ni matawi, Sheria ndio shina. Hivyo lazima tuboreshe kwanza Sheria ya Madini ili wananchi wetu waweze kuwa na manufaa kwa rasilimali ya nchi yetu, badala ya kuwaachia wawekezaji kutoka nje mali ya nchi hii bila gharama yoyote. Itafikia wakati wawekezaji hawa wakachukua mikopo huko nje na kuja kuonyesha dhamana ya mikopo hii kwa kuonyesha viwanja vyetu. Hii ni kashfa kubwa kwa nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, hali hii inasababisha kuwa na malalamiko, manung'uniko kwa wananchi wa Geita na kutokuwepo haki yao ya kuishi hasa kwa kutatua migogoro nusu nusu tu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuyaona haya yanawatesa wananchi wa Geita, naomba haya yafuatayo:-

(i) Kijiji cha Nyakabale kina wakazi ambao wamezuiliwa na mgodi wa *GGM* na mbaya zaidi mgodi unatupa takataka eneo la juu la kijiji cha Nyakabale. Mvua zinaponyesha uchafu wote unajaa kijijini na kusababisha eneo hilo kutokufaa katika shughuli za kilimo na hata maji ya kunywa, ni shida sana. Hivyo kijiji hiki kihamishwe na wananchi wake wapewe fidia haraka iwezekanavyo ili kupisha shughuli za mgodi;

(ii) Kuna wananchi sabini na wawili (72) wa eneo la Nyamotagata hawajalipwa fidia wakati wenzao 39 wameshalipwa, hawa kulikoni?;

(iii) Wakati wakilipa fidia kwa wananchi wa Katoma na Nyamalembo, kuna wananchi saba wamebaki katika maeneo hatari sasa, wafidiwe haraka ili waweze kuondoka;

(iv) Kuna Watanzania wanalala nje kwa kutojua Sheria, wakafukuzwa katika maeneo yao mpya ya *mine*, naomba sana suala hili litiliwe maanani na kuwapa fidia ili waweze kujipatia makazi ya kudumu kuliko kukaa nje ya Mahakama ya Mwanzo ya Kalangalala. Ni aibu kwa Serikali na Chama cha Mapinduzi kwa ujumla;

(v) Wawekezaji hawa wakubwa kama wana *Special Mining Licence*, wasiruhusiwe kuchukua *Prospecting Mining Licence (PML)*, ili kutoa fursa kwa wachimbaji wadogo wadogo na ili kuwaokoa wananchi wa Geita ambao maeneo yao makubwa yamechukuliwa.

(vi) Mfuko wa Nishati Vijijini (*Rural Energy Fund (REF)*). Tozo kwa wazalishaji wote wa umeme ifanyike haraka zaidi ili fedha zipatikane kuwezesha kusambaza umeme vijijini.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Spika, kwanza, nchi yetu ina rasilimali nyingi za madini lakini pamoja na Tume kuundwa bado rasilimali hizo hazijawasaidia Watanzania. Kwa mfano, madini ya makaa wa mawe (*911:0 million – Tons*) lakini hadi leo, Serikali haijaweza kuingia mkataba na makampuni ya uchimbaji wanaoweza kuzalisha umeme.

Hivi sasa Serikali ya Msumbiji, imeingia ubia na kampuni ya Australia kuchimba na kuzalisha umeme, kwa hiyo, kama Tanzania itachelewa kidogo tu, Tanzania itanunua umeme kutoka Msumbiji na wawekezaji watashindwa kuwekeza kwenye mgodi wetu, kwani hawatakuwa na soko.

Mheshimiwa Spika, nashauri *NDC* na kampuni yao ya pamoja ya Australia wakabidhiwe Mchuchuma ili wazalishe umeme haraka.

Mheshimiwa Spika, pili, kuweka akiba ya rasilimali. Nchi yetu pamoja na kuwa na rasilimali za aina nyingi lakini Serikali hadi leo haijaweka mpango wa kuweka akiba ya rasilimali hizo. Kwa mfano, hivi sasa maeneo mengi yanachimbwa dhahabu, Serikali haisemi bei ya Tani 2,222 zilizopo, katika kipindi cha miaka 15 – 25 tunakusudia kuchimba kiasi gani na kufika maeneo gani?

Aidha hatujui wataalamu wangapi watahitajika katika kuzalisha idadi hiyo ya dhahabu. Hivyo hivyo, kwa *Uranium* ambayo haijasemwa ipo kwa kiwango gani na kadhalika. Kuendelea kutoa leseni kwa watu mbalimbali hakusaidii kuondoa umasikini bali uharibifu wa rasilimali tu.

Mheshimiwa Spika, tatu, kuwawezesha Watanzania. Serikali imekuwa ikitoa viwanja vya utafutaji wa madini, lakini kwa kuwa wachimbaji hawa hawajui kiwango cha mali iliyopo, matokeo yake raia kuuza maeneo haya kwa bei ndogo kwa wawekezaji wa nje. Nashauri wananchi wawezeshwe kwa kupewa utaalamu, mtaji na mikataba yao ipate idhini ya wataalamu badala ya kuwachia wao wenyewe tu.

Mheshimiwa Spika, nne, kupunguziwa majukumu Waziri. Kumekuwa kuna uchelewaji wa kusaini leseni za watafutaji na wachimbaji, nashauri Sheria ibadilishwe ili madaraka yake yahamishiwe kwa Kamishna. Hii pia itamuondolea Waziri matatizo ambayo yamekuwa sugu ndani ya Wizara hii na pia kupunguza mlundikano wa watu wanaongojea kupatiwa leseni zao.

Mheshimiwa Spika, tano, kuimarishe kwa takwimu za rasilimali zilizoko ardhini. Serikali lazima iimarishe Idara ya Survey ili iwe na uwezo zaidi wa kujua rasilimali za nchi. Katika nchi nyingi hasa zilizoendelea Idara kama hii huwa inaundwa, inapewa fedha za kutosha ili kudhibiti rasilimali za Taifa. Leo Idara za Survey za nje, zina taarifa nyingi za nchi yetu kuliko hata idara yetu. Hii ni hatari na nashauri Idara hii iwezeshwe.

Mheshimiwa Spika, sita, kuzuia kusafirisha malighafi za madini. Serikali bado haijaweka mazingira ya kudhibiti na kuongeza thamani ya vito vyetu. Ni muda muafaka kuwasaidia wawekezaji raia kuanzisha viwanda vya kuchonga vito ili kupanua wigo wa kodi na kuongeza ajira.

Mheshimiwa Spika, saba, gesi, mgawanyo wa mafuta yatokayo na gesi baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Zanzibar limekuwa tatizo. Nashauri Waziri aje na majibu ya kutosheleza kwani hili suala litaleta mgogoro ndani ya muungano. Aidha suala la *TANESCO* kutoa bei kubwa kwa Shirika la Umeme Zanzibar hadi kusababisha umeme kupanda Zanzibar, jambo hili linahitaji kuangaliwa upya hasa ukizingatia kuwa Zanzibar ndio walioelekezwa kwenye mradi huu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa kutegemea kupata majibu muafaka.

MHE. ABDUL J. MAROMBWA: Mheshimi Spika, nianze kuchangia hotuba hii kwa kuunga mkono kwa asilimia mia.

Mheshimi Spika, napenda kuchukua fursa hii, kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na uongozi wote wa Wizara ya Nishati na Madini kwa kazi kubwa mnayoifanya, kuisafisha Wizara hii ambayo kwa wananchi wa kawaida wanaiona imejaa ufisadi. Ongezeni bidii ili kuifanya iwe ni kigezo cha utendaji bora wa kazi na kuliletea Taifa letu faida kubwa inayotokana na madini pamoja na nishati tulizonazo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu Wilaya ya Rufiji haijapata umeme. Hii inatokana na kutopitiwa kwa gridi ya Taifa ya Umeme. Lakini tangu gesi ianze kuzalishwa kule Songosongo, matumaini ya kupata umeme yameongezeka. Hadi sasa tayari nguzo, nyaya na transfoma zimefungwa katika vijiji zaidi ya saba katika Wilaya ya Rufiji. Tunaishukuru Serikali kwa hatua hii kwani inatupa faraja kubwa kuwa umeme utapatikana hivi karibuni. Ninaombwa Serikali kuwa ikamilishe kazi hii ili umeme uanze kuwaka katika miji ya Mohoro, Utete, Nywamwage, Ikwiri, Kibiti na Bungu.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri aeleze ni lini nguzo zitaanza kuwekwa kutoka Bungu hadi Mkuranga ili umeme huu uungane na ule wa gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali itusaidie kupeleka umeme katika kiwanda cha kusindika samaki pale Nyamisati. Kiwanda hiki ni kikubwa na kinamilikiwa na Halmshauri ya Wilaya ya Rufiji. Lakini kwa kuwa kinatumia *diesel*, kiwanda hiki hakifanyi kazi.

Mheshimiwa Spika, umeme huu unapokwenda huko Nyamisati kutoka Bungu ambako kwa sasa unaishia, utasaidia kupata umeme kwa shule tatu za sekondari. Shule hizi ni Mlanzi, Mahege na Nyamisati inayomilikiwa na WAMA. Taasisi hii ya WAMA inayoongozwa na Mke wa Rais, Mama Salma Kikwete inamiliki shule hiyo ya Nyamisati ambayo itakuwa na Kidato cha Kwanza hadi cha Sita.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuishukuru Serikali kwa kulipa fidia waathirika wote waliopitiwa na njia ya umeme. Ila kuna dosari ambazo zimejitokeza kuhusu baadhi ya wadai kutolipwa fidia kutokana na vitabu vyao kutopitishwa/kutoonekana. Naiomba Serikali iwalipe wananchi hao ili kero hii iondoke.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Spika, napenda kuendelea kuchangia Wizara yako kama kawaida yangu. Kwa muda wa miaka kumi na mbili (12) sasa nimekuwa nikichangia na kuomba umeme kwenye Wilaya ya Longido. Nasikitika Serikali imetoa ahadi tangu mwaka 1996 mpaka leo hatujapata umeme.

Mheshimiwa Rais ametoa ahadi ambayo wananchi wa Longido wanaulizia kwamba mbona Rais ametudanganya? Aliwaambia ye ye mwenyewe atakuja kuzindua umeme Longido. Mheshimiwa Waziri, naomba kwenye majumuisho yako, ueleze kabisa wananchi wa Longido wasikie kauli yako kwamba watapata umeme lini?

Mheshimiwa Spika, masikitiko ni mengine, kuna kauli ya Serikali kwamba ifikapo mwaka 2010, kila Makao Makuu ya Wilaya, watapatiwa umeme lakini naona utekelezaji ni mdogo sana. Hivi kupeleka maeneo mengine umeme mpaka vijiji thelathini na sita (36) huku maeneo mengine ya Wilaya zingine hawana umeme, ina maana gain?

Mheshimiwa Spika, kwa muda wa miaka miwili iliyopita, nimekataa kuunga mkono hoja ya Wizara hii kwa sababu nimekosa imani kuhusu ahadi ambazo hazitekelezwi.

Mheshimiwa Spika, kwenye majedwali umeandika kila Wilaya na vijiji vyake lakini umeona Wilaya ya Longido haina hadhi ya kuwa Wilaya jambo ambalo Serikali inatambua kwamba ni Wilaya. Naomba usahihishe kwani ni kuidharau, kuiweka kwenye vijiji vya Arumeru ambapo hatujawahi kuwa Wilaya moja. Bajeti ya leo, imeturudisha nyumba hatuwezi kuona Wilaya yetu iko huko.

Mheshimiwa Waziri, hakuna Mbunge ambaye ameелеza kwamba hatagombea Ubunge kama umeme hautafika Jimboni kwake. Lakini mimi nimetangaza kabisa kwamba nimechoka na kuwadaganya wananchi kuhusu umeme. Hatua niliyochukua ni maamuzi magumu na nimeamua kuacha kabisa Ubunge kwa ajili ya kukosa umeme Jimboni Longido.

Mheshimiwa Spika, naomba uwaeleze watu wa Longido, ni lini umeme utakwenda Longido. Nilikuwa na mengi ya kuongea lakini nipe ufanuzi wa hayo machache.

MHE. PROF. M. MWANDOSYA: Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea naomba nitumie nafasi hii kumpongeza kwa dhati kabisa, Mheshimiwa William Ngeleja, kwa hotuba yake nzuri, ya kina, ambayo imetoa ufanuzi wa masuala mengi na kutoa matumaini kwamba nishati hasa ya umeme, utachochea maendeleo ya Taifa letu. Mwenyezi Mungu ametujaalia sana na raslimali ya madini. Kuitumia vema raslimali hiyo kwa manufaa ya wananchi wa kizazi hiki na kizazi na vizazi vijavyo ndiyo shukrani tunayoweza kutoa kwa Rabuka. Nampongeza vile vile Mheshimiwa Adam Malima, na pia Arthur Mwakapugi, Naibu Waziri na Katibu Mkuu sawia.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, katika jimbo la Rungwe Mashariki, *TANESCO* imefanya kazi kubwa kueneza umeme vijijini. Hata hivyo, imeacha kazi zilizosimama kwa muda mrefu, kazi ambazo zilianza kutekelezwa na nyngine zilifika hatua kubwa na nzuri ya utekelezaji. Ni kwa sababu hiyo, inaonekana kama vile fedha zilizotumika kununua na kuweka vifaa kama vile nguzo na nyaya, zimepotea bure. Maeneo husika ni kama yafuatayo:-

Kwanza, umeme Mbambo/Ntaba- Ipinda. Mbambo iko Wilaya ya Rungwe. Umeme wa KV 33 upo kati ya Mbambo na Ntaba, ambayo iko Wilaya ya Rungwe. Ntaba na Ipinda ni umbali wa kilometra 12 hivi. Ipinda iko Kyela. Tayari nguzo zimesimikwa kutoka Ntaba mpaka Ipinda. Nyaya zimewekwa umbali wa kilometra 7 hivi. Vikombe vile vile vipo kwa kilometra 5 hivi yote haya yalifanyika miaka mitano iliyopita. Mradi umeachwa, nguzo zinaanguka, nyaya zinaibiwa. Haitoi sura nzuri kwa shirika na Serikali. Ikumbukwe pia kwamba njia hii ni ya pili kuunganisha Wilaya za Kyela na Rungwe hivyo kutoa njia mbadala ya kuunganisha Wilaya hizi. Mwaka 2006 Mbunge wa Kyela aliuliza swali kuhusu mradi huu mdogo, Waziri alijibu *TANESCO* ingetekeleza kwa shilingi milioni 25 za wakati ule.

Pili, *TANESCO* vile vile imesimamisha nguzo kwa zaidi ya miaka minne katika maeneo yafuatayo; Mwakaleli – Mpombo, Isange – Mbigili, Mwakaleli – Matamba na Kandete – Luteba. Miradi yote hii inahusu umbali usiozidi kilometra tano kwa kila eneo.

Mheshimiwa Spika, kila mwaka kwa mfululizo wa miaka mitano nimerudia ombi hili na kila mwaka nimeahidiwa kuhusu utekelezaji. Mwaka 2007, wakati wa majadiliano kuhusu hoja hii, baada ya kuwasiliana na Dr. Idris Rashid ambaye nampongeza kwa kazi kubwa na ngumu anayoisimamia, aliniahidi kwa maandishi kwamba *TANESCO* ingekamilisha miradi hiyo kwani ilanzishwa na *TANESCO*. Naamini Waziri atazingatia haya ambayo ni maombi ya wananchi wa Rungwe Mashariki.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Spika, kuhusu kusambaza umeme kutoka Itigi – *Mgandu Complex*, mradi huu awali ulikisiwa kugharimu shilingi bilioni 1.2 mwaka 2006, lakini sasa mwaka 2008 umekadiriwa kugharimu shilingi bilioni 3.

Nimekuwa nikifuatilia kwa karibu sana mpango huu na hata Mheshimiwa Waziri alijionea mwenyewe alipofika Mgandu (Mitundu) tarehe 8.8.2007 jinsi *Mgandu Complex* ilivyokaa kiuchumi na azma ya wananchi wa maeneo hayo. *Mgandu Complex* kuna Tumbaku, Mbao (Mninga) (Miyombo), Asali, Nta na mazao mchanganyiko. Alizeti, Ufuta, Dengu na kadhalika. Pia ni sehemu muhimu kwa ufugaji na mbuga ya Hifadhi ya Mhesi/Rungwa. Minara ya *Celtel* tayari imewekwa na *Vodacom* wako njiani.

Nilipokuwa Dar es Salaam kwenye vikao vya kamati mwezi Mei/Juni nilifika Wizarani na kugundua kuwa mradi huu haukuwekwa kwenye *memorandum* ya Bajeti ya mwaka 2008/2009 ya Wizara ya Nishati na Madini, lakini nikaahidi kwamba *separate arrangement* itafanyika kuuweka kwenye mpango *separate* wa mfuko wa nishati vijijini ili mradi uanze walau kwa shilingi bilioni 1.5 kwa mwaka 2008/2009 na shilingi bilioni 1.5 kwa mwaka 2009/2010. Niliridhika na maelezo hayo.

Lakini ninaomba *commitment* ya Serikali walau kwa kauli ndani ya Bunge ili wananchi wanaosubiri kwa hamu waweze kusikia. Wanahitaji kufungua viwanda vidogo vidogo.

Mheshimiwa Spika, uhaba wa mita za umeme bado unasumbua wananchi na kuwaacha waombaji wapya kusubiri miaka bila mafanikio ya kupata umeme pale Itigi na Sanjaranda. Nashauri tatizo hili lishughulikiwe kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, bei ya kuvuta umeme kuingiza ndani ni shilingi 550,000/=, huu ni mzigo mkubwa kwa wananchi. Serikali ione uwezekano wa kushusha gharama hii ili wananchi wengi wapate nishati hii muhimu kwa matumizi yao na ufunguzi wa viwanda vidogo vidogo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Litman Mines* – Mgandu. Je, Serikali inafahamu kuwa kuna uchimbaji usio rasmi (haramu) wa madini ya dhahabu kwenye mlima wa Litman ndani ya hifadhi ya Mhesi, *Mgandu triangle?* Wananchi wamekuwa wakilalamika kuwa uchimbaji huu unafanywa kinyemela na wawindaji kwa kushirikiana na wafanyakazi wa wanyamapori kwenye mlima huo ambapo wananchi au watu wengine hawaruhusiwi kusogea maeneo hayo. Machimbo hayo yaliwahi kufanywa na Wajerumani na kusimama walipoondoka, lakini hivi sasa yanachimbwa na wajanja bila utaratibu rasmi huku wakipewa ulinzi na wafanyakazi wa wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali na hasa Wizara hii ifuatilie ili ijue kuna nini mlima wa Litman – Mgandu.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Hifadhi ya Taifa ya Mafuta, kumekuwepo na ongezeko la bei ya mafuta kila kukicha sababu tu yanaletwa na watu binafsi. Serikali iharakishe haraka iwezekanavyo kuiwezesha *TPDC* kuagiza mafuta ili iweze kuwauzia watu binafsi. Kwa njia hii hao *TPDC* watakuwa wana-control bei. Vile vile kuwa na hifadhi yetu ni muhimu hata ikitokea dharura tunakuwa na akiba pamoja na Serikali kuridhia kuwa na uanzishwaji wa hifadhi ya mafuta ya Taifa nchini lakini swali langu ni lini mchakato wa utekelezaji wa kuwa ni hifadhi ya mafuta utakamilika? Naomba jibu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa usambazaji umeme vijijini, umekuwa ni hadithi kuhusu kupeleka kwenye vijijiji. Maendeleo hayawezi kupatikana bila kuwa na umeme wa uhakika hata kule kwenye umeme vijijini, mfano Moshi Vijijini ikifika jioni saa kumi na mbili taa haziwaki umeme ni hafifu. Ushauri wangu ni kuwa huu mkakati uzingatie kupeleka umeme wa uhakika ambao utaweza kutumika viwandani hata vidogo ili wakulima wa *process* mazao yao kule. Uangalie pia uwezo wa kupeleka gesi mpaka vijijini, mpango huu usiishie tu mjini. Tumechoka na kusikia Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi imeahidi umeme, utafika? Sasa hii Ilani itatekelezwa lini? Tuache siasa, tuhangaike na maendeleo kwa Watanzania wanayoyasubiri kwa hamu.

Mheshimiwa Spika, Shirika la umeme *TANESCO*, ningependa kujua mpaka leo *TANESCO* walikusanya kiasi gani kutoka *RICHMOND/DOWANS* zile dola 10,000 ambazo walikuwa walipe kila siku kwa kutotimiza au kutokamilisha mtambo wakati muafaka? Fedha hizo zilikuwa ni *fine*.

Mheshimiwa Spika, bei za umeme zinapanda kila siku na haziwezi kushuka, Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake katueleza hata nguzo za umeme zinaagizwa kutoka *South Africa*, hili ni jambo la aibu. Tanzania kuna ardhi kubwa yenye rutuba, kama si kuchezea fedha za walipa kodi, ni sababu zipi zinapelekea shirika kuagiza nguzo kutoka *South Africa*? Au huu ulikuwa ushauri kutoka *Net Group Solution*?

Mheshimiwa Spika, siku za hivi karibuni kuwekuwepo na matukio mengi ya nyumba za watu kuwaka moto na matukio mengi ya moto yanatokana na vifaa feki vya umeme. Inaleta hasara kubwa vitu kuungua hata wengine kupoteza maisha, ushauri ni kuwa ili kuwa na uhakika wa vifaa hivi, *TANESCO* itoe wakala *at least* katika kila Mkoa mahali (duka) ili watu waweza kununua vifaa kwa uhakika ili kuondokana na matatizo haya ya kuunguliwa vifaa na nyumba.

Kuhusu *STAMICO*, bila kuiwezesha *STAMICO* hatuwezi kuwasaidia wachimbaji haswa wadogo. Tumeona juzi wanavyonyanyaswa na wachibaji wakubwa. Ni lazima tuangalie jinsi ya kuwatunza hawa vijana. Shirika hili la *STAMICO* likiwezeshe wa litawenza kutoa elimu kwa wachimbaji hawa waweze kuongeza uchimbaji kwa kutumia teknolojia za uchimbaji na uchenjuaji wa madini kwa kuwafunza na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, *STAMICO* inadai shilingi milioi 171 kutoka *PSRC* wakilipwa deni hili kwa kiasi kikubwa itawasaidia sana katika kutekeleza mipango iliyojipangia na hatimaye kuwasaidia wachimbaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, kwa msisitizo shirika la *TPDC* liwezeshwe ipasavyo ili liweze kufanya utafiti bila matatizo yoyote. Ukizingatia kwa sasa gesi asilia imegundulika nchini, tusije tukawapa wawekezaji tukaingia kwenye mikataba mibovu kama ya madini ya dhahabu ambayo kwa sasa inatugharimu kiasi kikubwa hata kupelekea Mheshimiwa Rais kuunda Tume ya kuchunguza migodi ile. Hiki ni kitu cha kuangalia mapema.

MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Makamishna, Wakurugenzi na Mameneja wa Wizara kwa hotuba ilioandalialiwa kitaalamu. Mheshimiwa Waziri ameanza vizuri. Nampongeza kwa ufuutiliaji wa ahadi za Serikali, ni Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Hongera, *keep it up.*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia eneo la umeme vijijini hususan Wilaya ya Rorya. Wilaya mpya ya Rorya ina Tarafa nne, Kata 21 na vijiji 10. Vijiji vya Wilaya ya Rorya vilivyokuwa vinapata umeme ni tisa tu kuanzia mwaka 1961 hadi mwaka 2000. Kuanzia mwaka 2001 – 2005 kutokana na jitihada za Mheshimiwa Mbunge wa Rorya kupitia Chama cha Mapinduzi, vijiji (vituo) 10 viliweza kupatiwa umeme hivyo kufanya vijiji (vituo) vinavyopata huduma za umeme kuwa 19. Mpango wa umeme vijijini katika Wilaya na Jimbo la Rorya liliandaliwa na Mheshimiwa Mbunge mwaka 2005 kwa lengo la kwanza, matumizi katika kilimo, ufugaji, viwanda; pili, matumizi ya nyumbani, biashara, shulenii, Zahanati, vituo vya Afya, matumizi ya maji kwa ajili ya binadamu na tatu, migodi ya Madini – Rorya inayo madini mengi ambayo utafiti unaendelea.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza meneja wa *TANESCO* Mkoa wa Mara na Meneja wa Wilaya kwa jitihada zao za kufanikisha miradi ya umeme katika vijiji vy Rorya kama ifutavyo, kwanza, miradi ya Benki ya Dunia (*ERT*) mwaka 2005 – 2007, kupeleka umeme Masonga na Sota na mradi wa umeme vijiji vya Bukama – Nyorombo, Nyamtunga, Mrore, Kisumu, Nyamchabakenye na Kibuyi, miradi hii yote ilitengewa shilingi milioni 724.6.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2008 Mheshimiwa Waziri aliniahidi kuwa miradi hii imehamishwa *REA*. Napenda kumpongeza Mtendaji Mkuu wa *REA* kwa ushirikiano wake na jitihada zake katika kuhakikisha Tanzania itatokana na giza hasa vijijini, nampongeza kwa azma hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za *REA* vijiji 7 vya Rorya viliingizwa katika miradi mipyä itakayopatiwa huduma za umeme mwaka 2008/2009. Vijiji hivyo ni Masonga, Mirore, Nyarombo, Nyamtinga, Kisumu, Nyamchabakenye na Kibuyi.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Wilaya ya Rorya walipokea kwa furaha miradi hii, ombi maalum ni kuwa naomba Mheshimiwa Waziri atamke hapa Bungeni kuwa miradi niliyotaja ipo ingawa haikutajwa katika hobuta ya Bajeti ya mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Wilaya ya Rorya wapewe upendeleo maalum kuhusu huduma za umeme kwa kuwa kati ya vijiji 98 ni vijiji 19 tu ndiyo vinapata

huduma za umeme, wananchi wako tayari kulipia huduma za umeme hivyo maombi ya vijiji 7 na ahadi ya Mheshimiwa Waziri itekelezwe katika kipindi cha mwaka wa fedha 2008/2009 na Wilaya ya Rarya inatoa mchango wa Pato la Taifa katika sekta ya uvuvi. Jumla mialo 34 ya wavuvi haina umeme.

Mheshimiwa Spika, ombi, umeme upelekwe Sota, Kibuyi na Rwangenyi kwa kuanzia.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Naomba nipaye majibu.

MHE: JOHN S. MALECELA: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Nishati na Madini kwa hotuba yake yenye kina na uchambuzi wa kutosha. Naanza mchango wangu kwa kuunga mkono hoja.

Baada ya hayo natoa mchango wangu kama ifuatavyo, kwanza ni kuhusu msaada kwa wachimbaji wadogo. Wizara iwe na fungu maalum la kusaidia wachimbaji wadogo hasa katika kununua mitambo ya kuwasaidia kwenye shughuli zao. Pia hawa wachimbaji wadogo wapewe semina na mafunzo ya mara kwa mara ili kuwaongezea uwezo na pia kutunga sheria za kuwalinda.

Mheshimiwa Spika, ahadi za Wizara ya kuwa umeme toka *Mvumi Mission* hadi vijiji vya Makang'wa na Mlowa Barabarani, ahadi ilikwishatolewa na Wizara na Fedha shilingi milioni 400 kwa mradi huo, ingawa hadi sasa haujatekelezwa, nina imani kubwa kwa Waziri Mheshimiwa William Ngeleja kuwa sasa mradi huu utatekelezwa.

Kuhusu umeme vijijini nina matumaini kwamba Serikali itaweka ratiba ya uhakika ya kupeleka umeme vijijini, Wilaya kadhaa kila mwaka ili kuzipa Wilaya zote matumaini. Umeme kutokana na jua, Tanzania ina uwezo mkubwa wa kutumia nishati hii mfano mzuri wa kuiga ni nchi ya Malta ambayo ina sheria ya kulazimisha nyumba zote za kuishi zinapojengwa kuwa na nishati ya jua.

Mheshimiwa Spika, Mererani kwa muda mrefu kumekuwa na matatizo ya mara kwa mara kati ya wachimbaji wakubwa na wadogo. Naiomba Wizara kumaliza tatizo hili ili lisiwe donda ndugu kwa Taifa. Kuhusu Chuo cha Madini Dodoma, kipanuliwe ili kiwe Chuo Kikuu maana uchimbaji wa madini Tanzania unapanuka haraka na kuifanya Tanzania kuwa na mahitaji makubwa ya wataalam wa ngazi za juu.

Mheshimiwa Spika, namtakia kheri Waziri Mheshimiwa William Ngeleja katika kutekeleza kazi yake ngumu. Pia nawapa hongera Mheshimiwa Waziri na watendaji wake wote kazi ngumu wanazotekeliza.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. VICTOR K MWAMBALASWA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja. Baada ya hapo nachangia sehemu ndogo sana. Kuna *project* inayochangiwa na Serikali ya Norway ya kuongeza mipaka ya Tanzania baharini kwa

kiasi cha *nautical mailes* 200. *Project* hii inatakiwa iwe imekamilika na kupelekwa UN mwezi Mei, 2009 pamoja na kuongeza mipaka ya nchi, pia nchi itafaidi raslimali zingine kama gesi, mafuta na uvuvi katika eneo hilo. Sasa *project* hii iko chini ya Wizara ya Ardhi, lakini ikifanikiwa, Wizara ya Nishati na Madini ndiyo itafaidi sana.

Naomba sana Waziri wa Nishati na Madini amsukume mwenzie wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi ili Serikali itoe mchango wake wa dola milioni 2.6. Serikali ya Norway imeshatoa mchango wake wa dola milioni 4.6. Kama *project* hii haitapelekwa mwezi Mei, 2009 basi Tanzania itakosa fursa hiyo milele. Nchi zote duniani zenyе bahari zinatengeneza *project*.

MHE. MOHAMEDI RISHED ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kukupongeza wewe pamoja na Naibu Waziri wa Nishati na Madini, wataalam wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba hii Bajeti ya mwaka 2008/2009.

Kwanza niseme naunga mkono hoja. Pili nilichangia wakati wa hotuba ya Bajeti mwanzo wa Bunge hili, leo nachangia mambo yanayohusu Jimbo langu, kuna miradi ya maji ambayo imekamilika lakini ina subiri umeme (*transforma*) miradi yenye iko kwenye vijiji vifuatavyo, Mradi wa Maji Kijiji cha Kimang'a, Mradi wa Maji Kijiji cha Mikinguni, Mradi wa Maji Kijiji cha Madanga, Mradi wa Maji Kijiji cha Kambona na *Transfoma* kwenye Kijiji cha Kipumbwi.

Mheshimiwa Spika, niliandikia barua kumuomba Mheshimiwa Waziri umeme kwenye kijiji cha Kimang'a, Masaika, Mkalamo na Kigurusimba. Naomba ombi langu lizingatiwe na nitashukuru ukinijibu.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Mheshimiwa William Ngeleja (Waziri), Mheshimiwa Adam Kighoma Malima (Naibu Waziri), Katibu Mkuu, pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa Bajeti hii nzuri yenye mwelekeo wa kuboresha sekta ya Nishati na Madini hapa nchini ingawa Mkoa wa Singida maombi yake hayajapata kipaumbele katika Bajeti kama nitakavyoeleza katika mchango wangu kama ifuatavyo nitahitaji maelezo ya wakati akijibu hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme kijiji cha Mgongo na Kata ya Msingi Tarafa ya Kinampanda. Naipongeza Serikali kwani baadhi ya Makao Makuu ya Tarafa, Jimbo la Iramba Magharibi yana umeme muda mrefu. Baada ya kuona umeme upo Shelui na Kinampanda tuliomba tupatiwe umeme Kijiji cha Mgongo chenye wakazi wengi ikiwemo kituo cha Afya, Shule ya Sekondari, Shule ya Msingi, Machimbo ya dhahabu na wakazi wengi. Ninasikitika ombi hili halijapata fedha, naomba Waziri awaeleze wananchi.

Mheshimiwa Spika, vile vile baada ya umeme kuwepo Kinampanda, Makao Makuu ya Tarafa tuliomba umeme uende Kata ya Msingi umbali wa kilometra mbili tu eneo lenye Chuo cha Maendeleo ya Wananchi, Sekondari, Zahanati, Shule ya Msingi na

wakazi wengi wenye shughuli mbalimbali za uzalishaji mali, ombi hili halipo ndani ya Bajeti pia Waziri atueleze ili wananchi tusikate tamaa na Serikali yetu.

Kuhusu umeme Sepuka na Ihanja, ni muda mrefu sana hadi sasa kuwa tukiahidiwa kupatiwa umeme katika Makao Makuu ya Tarafa mbili nilizozitaja hapo juu pamoja na Mbunge wa Jimbo la Singida Kusini kufuatilia kwa karibu sana.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa jitihada zetu hazikuzaa matunda kupata fedha kwenye bajeti hii tunamtegemea Mheshimiwa Waziri ndugu yetu na mwanangu atupe maelezo yatakayotutia moyo pamoja na wananchi wa Sepuka na Ihanja kwani nguzo sasa zimeanza kuoza tangu ziliposambazwa.

Kuhusu umeme Kintiku na Chikuyu, pamoja na maeneo tajwa hapo juu kupitiwa na umeme wa gridi bado maeneo hayo hayana umeme, wanaona nguzo na nyaya zikipita. Jimbo hili la Manyoni Mashariki linasikitisha sana kwani halina umeme eneo lolote, sijui Serikali inasema nini kumnusuru Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwani ana mtihani na wapiga kura wake. Majibu pekee ya Waziri ndiyo yatamnusuru kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme kwenye Machimbo ya Dhahabu Londoni na Sambaru, nampongeza Mheshimiwa William Ngeleja, Waziri wa Nishati na Madini, aliwahi kutembelea machimbo haya ya Londoni (Manyoni) na Sambaru (Singida Kusini) na alishuhudia hali halisi ya kukosa umeme maeneo ambayo yana uzalishaji mkubwa. Tunaomba tuelenze umeme utaletwa lini ili wawekezaji waweze kuvutika. Waziri afafanue hili.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadodo kuwezeshe, tunashukuru Mungu kwani kati ya mikoa iliyopata neema ya kuwa na madini yenyenye thamani ni pamoja na Mkoa wa Singida. Vile vile tunawapongeza sana wachimbaji wadogo wadogo wanavyojitahidi kuwekeza kwenye madini.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kwa uongozi wa Mkoa wa Singida chini ya Mkuu wa Mkoa Mheshimiwa Parseko Kone, jinsi wanavyojitahidi kutafuta wawekezaji wakubwa ambao watakuwa wabia na wachimbaji wadogo katika machimbi ya Londoni na Sambaru. Kwani wanategemea kumpata mwekezaji wa kutoka Urusi ambaye atakuwa mbia na wawekezaji wetu wadogo kwa kuwapa vifaa vya uchimbaji na vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kumuunga mkono Mkuu wetu wa Mkoa ili mwekezaji huyu aweze kufika haraka kuwanusuru wachimbaji wetu wadogo katika maeneo niliyotaja hapo juu. Mheshimiwa Waziri atambue juhudzi za Mkuu wa Mkoa wetu ili apate moyo wa kuwakomboa Wanasingida.

Kuhusu machimbo ya Mlima Sekenke na Mgongo, kwa kuwa wachimbaji hawa hawajapata mwekezaji wa kufanya nao kazi na kuwasaidia vifaa, naiomba Serikali iwakopeshe wachimbaji hawa wadogo wadogo ili wapate vitende kazi ambavyo

vitasaidia kufanya kazi yao kwa urahisi na kuinua pato la nchi na vipato vyao kwa manufaa ya jamii kwa ujumla. Benki zipewe maelekezo au mfuko maalum Wizara itoe. Nitategemea Waziri atatoa maelezo ili wachimbaji wazalendo wanufaike.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Singida una Tarafa 21 lakini mpaka leo hii ni tarafa 10 ambazo zina umeme angalau makao makuu ya tarafa na kijiji kimoja au viwili, tarafa 11 hazina umeme naomba Serikali kuititia takwimu hii ijipange vizuri ili iweze kuona namna itakavyotupatia umeme kwani sifa za tarafa hizi kupata umeme zipo. Waziri akitueleza tutashukuru sana na wananchi watajua kuwa tunatoa taarifa mara nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, umeme wa upepo. Naipongeza Serikali kutambua kuwa Mkoa wa Singida unaweza kutengeneza umeme wa upepo. Kwa kuwa tayari Mkuu wa Mkoa amepata kampuni za kuwekeza basi aungwe mkono katika harakari zake za kupata mwekezaji wa kutengeneza umeme wa upepo kwani uongozi wa Mkoa wetu kwa niaba ya Wanasingida wana uchu wa maendeleo sana, jitihada hizi Serikali iziunge mkono.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba nimalizie kwa kupongeza sana jitihada za Mheshimiwa William Ngeleja na Naibu Waziri Mheshimiwa Adam Malima na watendaji wote ambazo zinaonekana kuititia utendaji wao, kujibu maswali Bungeni na hotuba ya Bajeti hii. Ninawaombea Mungu awape afya, nguvu na mshikamano katika kutekeleza Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuunga mkono Bajeti hii huku nikingojea majibu ya mchango wangu.

Kuhusu bili za umeme, bado kuna tatizo la usomaji wa mita za umeme kwani upo ushahidi wa kutosha baadhi ya watumiaji wakubwa wa umeme bili zao kuwa ndogo na watumiaji wadogo bili zao kuwa kubwa, tunaomba hili lifanyiwe utafiti hasa mijini ili kuondoa migogoro kwa wateja wa *TANESCO* isiokuwa na tija. Nategemea Waziri atafafanua.

Mheshimiwa Spika, kuna mgogoro wa umiliki wa mita pale mwenye nyumba kukosa uwezo wa kuingiza umeme kisha mpangaji kuingiza umeme kwa jina lake, pale atakapojenga nyumba yake anamnyima mita alioingiza kwa jina lake na gharama yake mfano Ndugu Jafari Juma Kuwingwa, mkazi wa Manyoni Mjini amenyimwa mita yake na mwenye nyumba ambaye ni mtumishi wa *TANESCO*, Waziri atoe tamko kuondoa mgogoro huu ambaeo umeanza kutoa dhana potofu kuwa wananchi wanadhuluiwa kwa vile mwenye nyumba ni mtumishi wa *TANESCO* ili iwe fundisho pia na maeneo mengine pia.

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kuieleza Serikali kuwa kuna tatizo kubwa la wateja kuchelewa kupata umeme baada ya kukamilisha malipo ama pale wanapohitaji baada ya kumaliza ujenzi wa nyumba zao. Naiomba Serikali sasa itafute mbinu au mkakati wa kuwapa wateja umeme mara wanapohitaji kwani wanapochelewa kupata umeme nyumba zao hukosa soko. Nitashukuru Waziri akitoa ufanuzi.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wote wa Wizara kwa kuandaa na kuwasilisha hotuba nzuri ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2008/2009. Pamoja na hayo nina mambo machache ambayo ningependa kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusu ukamilishaji miradi ya umeme Mbozi. Jimbo langu la Mbozi Mashariki lina miradi mitatu ya umeme ya muda mrefu sana ambayo haijakamilishwa. Miradi hiyo ambayo ilianza kati ya mwaka 2001/2002 ni kama ifuatavyo, Ruanda – Iyula – Idiwili kilometra 26, Mahenye – Igunda kilometra 5 na Vwawa – Hasamba kilometra 13.

Mheshimiwa Spika, kama unavyoona miradi hiyo ina karibu miaka 7 sasa bado haijakamilika. Nguzo za umeme zilishachimbiwa muda mrefu, na nguzo nyingine zimeanza kuoza na nyingine kuunguzwa na mioto pori. Aidha, wananchi wa maeneo hayo ambaao walipewa matumaini ya kupatiwa umeme sasa wamekata tama.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikiliuliza swal hili hapa Bungeni mara kadhaa lakini majibu yake yamekuwa yakinutaka tuvute subira. Lakini wananchi hawa wataendelea kuvuta subira hadi lini ? Mwaka huu mwezi Februari nilimwandikia Waziri Mheshimiwa William Ngeleja, barua nikintaka anieleze ni lini hasa miradi hii itakamilika. Hata hivyo nasikitika kwamba bado sijajibiwa. Sasa kuitia Bunge hili nataka kupata majibu juu ya ni lini sasa miradi hiyo itakamilika?

Mheshimiwa Spika, malipo kwa *IPTL*, katika ukurasa wa 23 wa hotuba yake Waziri amesema vizuri kwamba uchunguzi umegundua kwamba *equinity* halisi iliyotumika ilikuwa shilingi 50,000/= kwa maana hiyo, malipo ambayo *TANESCO* imekuwa ikilipata *IPTL* kama *capacity charge* ni zaidi ya kiasi kilichostahili!

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri anatuambia kwamba huo ndio msingi wa mgogoro wa sasa ambaao Serikali/*TANESCO* na *IPTL* wanaendelea kujadili! Hapa inashangaza sana na naomba maelezo. Uchunguzi umefanyika na umegundulika kwamba *IPTL* wanalipwa pesa nyingi sana kwa maana kwamba kiwango cha *equinity* kilichotumika ni kikubwa sana ambacho kinainufaisha *IPTL* kinyume na kiwango halisi cha shilingi 50,000=/. Kama imegundulika hivyo kwa nini *TANESCO* iendelee kuilipa *IPTL* kwa makosa? Malipo yasimamishwe au kiwango halisi kitumike.

Mheshimiwa Spika, Gridi ya Taifa. Wilaya ya Mbozi imekuwa ikitumia umeme kutoka Zambia umeme ambaao siyo wa kutegemewa sana kutoptaka na kukatika katika sana na hivyo kusababisha hasara kubwa sana kwa watumishi. Kwa kuwa tayari umeme wa Gridi umefika Mbeya tunaiomba Wizara ituunganishe kwenye Gridi ya Taifa na hasa ukizingatia Miundombinu yote ya kuiunganisha Mbozi kwenye gridi ilishakamilika muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, umeme nuru (*Solar power*). Kwa kuwa wananchi wengi hasa vijijini wanahamu kubwa ya kujiwekea umeme nuru (*Solar Power*). Lakini wanatatizwa na bei kubwa hasa *panel za solar*, Wizara inaombwa ifanye jitihada za dhati ili kuona kwamba bei zake zinapungua. Kwa sasa bei za umeme huo ni kati ya shilingi milioni moja hadi milioni 20. Ni Watanzania wachache sana wanaweza kumudu bei hizo. Aidha, upatikanaji wa vifaa hivyo ikiwezekana upatikana kwenye Makao Makuu ya Wilaya zote nchini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SAVELINA S. MWIJAGE: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia Wizara hii kwa manufaa ya wananchi wangu wa Mkoa wa Kagera ambao wana matatizo ya umeme kwenye mkoa wao.

Kwanza kama Serikali inavyojua kuhusu umeme wetu unavyotoka nchi jirani hatuna vifaa vyta kuweza kuzalisha umeme kwenye mkoa wetu na Mkoa una vyanzo vingi vyta kuweza kuzalisha umeme, wananchi waliahidiwa kupata umeme kwa bei nafuu, wananchi walifurahi sana wananchi walijiandaa kufunya *wiring* kwenye nyumba zao, je, Serikali inawasaidiaje watu wa vijiji? Je, gharama zake zitapungua au hapana?

Naomba maelezo je, ni kwa nini Serikali inapenda kuipunguzia au kuwapunguzia wawekezaji wa madini kutoka nje hisa zao? Na wakisha fika hapa pamoja na kupunguziwa wanakuwa jeuri kwa wananchi wetu na je, wachimbaji wadogo wa Bulyanhulu, Serikali inawasaidiaje hasa machimbo ya Bulyanhulu Geita ambao walishakuwa sugu kwa ujeuri. Mikataba ibadilishwe ya wachimbaji wote wa gesi na madini.

Pili, napenda kujua mashimo matatu ambayo yamechimbwa *Mnazi Bay* viko wazi siku nyingi hivi Serikali haioni kuwa ni hasara kubwa sana je, ni kwa nini havifanyikazi Watanzania wakafaidika na gesi hiyo. Kuhusu mafuta Serikali ina mikakati gani kila mkoa unajipangia bei yake je, Serikali inajua au hapana?

Mheshimiwa Spika, nawapongeza kwa kufunga mikataba hewa na Wizara hii iendelee hivyo kwa kazi nzuri sana nilikuwa nashauri kuhusu nguzo kutoka nje ni kwa nini Wizara isifungue kiwanda hapa kwetu kuhusu miti, tunayo miti wanazalisha hapa ili wananchi waweze kujivunia raslimali zake kuliko kununua nguzo kwa bei kubwa sana. Ikumbukwe Kagera tuko kwenye hali ngumu. Mganda akiamua tutalala gizani hivi Serikali ina mpango gani kwani mtegemea cha nduguye hufa masikini. Naomba nipatiwe majibu mazuri, ni mtihani mkubwa kwa wana Kagera. Kwa hayo naomba kuwasilisha na nawatakia Bajeti njema kwa kuwajibu Wabunge pamoja na Kambi ya Upinzani maoni pamoja na ushauri.

MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA: Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa William Ngeleja, Waziri wa Nishati na Madini, Naibu Waziri Mheshimiwa Adam Malima na wafanyakazi wa Wizara ya Nishati na Madini kwa hotuba nzuri na kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, nina masuala mawili ya kuchangia mwaka 2004/2005 wananchi wa Wilaya za Bunda na Serengeti walikubali sehemu ya ardhi yao ili *line* (njia ya umeme) iweza kupita. Hata hivyo pale *wire* za umeme zilipita juu ya nyumba zao au mazizi ya ng'ombe, wananchi walikubali kuhama ili kupisha *line* ya umeme lakini kwa makubaliano kuwa watalipwa fidia.

Mheshimiwa Spika, hadi leo miaka mitano iliyopita wananchi hawajalipwa hata senti moja ya fidia. Tafadhali naomba majibu ya Waziri kuwa ni lini wananchi hawa watalipwa fidia yao?

Mheshimiwa Spika, mji wa Mugumu umepatiwa umeme lakini sio mji wote. Sehemu ya Romotonga bado iko gizani kwa kisingizio kuwa hamna *transforma*. Hii imeleta kero kwa wananchi wa Mugumu wanaishi Morotonga wanabaguliwa. Tafadhali naomba jibu kuwa ni lini *transforma* hii itapelekwa ili wananchi wa Morotonga wapate umeme? Nimelalamika sana lakini hadi leo sijapata jibu.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru Wilaya ya Serengeti imepatiwa umeme. Lakini hadi sasa ni sehemu au vijiji vichache ndivyo vimepatiwa umeme. Tafadhali tunaomba umeme upelekwe kwenye vijiji vingine vipate umeme.

MHE. DR. EMMANUEL J. NCHIMBI: Mheshimiwa Spika, nampongeza kwa dhati Mheshimiwa William Ngeleja, Waziri wa Nishati na Madini kwa hotuba yake nzuri iliyogusa kwa kina sekta yote ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Songea Mjini niishukuru sana Wizara ya Nishati na Madini kwa kutafuta fedha zaidi ya dola za Kimarekani milioni 70 ambazo ni sawa na shilingi bilioni 80 za Tanzania kwa ajili ya mradi wa kupeleka umeme wa gridi ya Taifa Songea na Namtumbo. Mradi huu pia utaboresha mifumo ya usambazaji umeme.

Mheshimiwa Spika, hali ya umeme katika Jimbo la Songea Mjini imekuwa ya kusua sua kwa muda mrefu. Songea imekuwa itegemea umeme wa jenereta amba ni chakavu na miundombinu dhaifu, mgao wa umeme umekuwa sehemu ya kawa ya maisha ya watu wa Songea. Athari kubwa ambayo imekuwa wazi ni kushindikana uanzishaji na uendelezaji wa viwanda vidogo, vya kati na viwanda vikubwa. Kutokana na ukweli huo wananchi wa Songea wanapata faraja ya pekee kwa ukombozi huu.

tunaomba Wizara isimamie kwa karibu kasi ya mradi huu ili kukidhi matarajio ya Serikali na ya wananchi wa Songea.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo machache naunga mkono hoja asilimia mia moja.

MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI: Mheshimiwa Spika, napenda kwanza kuipongeza Wizara hii pamoja na Mashirika yaliyopo chini yake kwa jitihada wanazofanya kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kuhusu ukuaji wa huduma za usambazaji wa nishati na ukuaji wa shughuli za madini. Hivyo naunga mkono hoja hii.

Hata hivyo ninayo maoni yafuatayo, miradi wa kupeleka umeme Bahi, kwa kuwa Wizara inatekeleza mradi wa kupeleka umeme Bahi na kwa kuwa Wilaya ya Manyoni tumeomba umeme katika miji midogo ya Kintinku, Chikuyu na Kilimatinde, na kwa kuwa kutoka Bahi hadi Kintinku ni kilometra 10 tu, tunaomba ushauri mradi huu usiishie mpakani (Bahi) bali uruke mpaka wa Dodoma/Singida na kufikisha umeme Kintinku (kilometra 10 kutoka Bahi), Chikuyu (kilometra 25 kutoka Bahi) na Kilimatinde (kilometra 35 kutoka Bahi). Ombi hili liliwasilishwa Wizara ya Nishati na Madini tangu mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mipango ya nishati mbadala, hotuba ya Bajeti imeeleza mipango ya Wizara hiyo kutoka ukuzaji wa nishati mbadala kama umeme juu, umeme wa upepo, biogesi na kadhalika. Suala hili tulunge mkono kuomba Wizara iongeze kasi. Umeme wa juu kwa mfano, tatizo lake ni bei ya vifaa vyake ni kubwa mno, na Watanzania wengi hawawezi kumudu. Wizara iweke mkakati wa kutatua tatizo hili kwa kuondoa kodi zote za zana hizi na hata kuweka utaratibu wa ruzuku kama mbolea kwani umeme ni nyenzo muhimu sana katika kukuza uchumi.

Kuhusu uwezeshaji wa wachimbaji wadogo, hotuba imeahidi kuendelea kusaidia wachimbaji wadogo, aidha, Wizara imekuwa inatoa leseni kwa wachimbaji wadogo wa Sembaru na Londoni (Manyoni) tunashukuru sana hata hivyo tunaomba kasi iongezwe katika kuwasaidia wachimbaji wadogo kuhusu mafunzo, kupata zana za kisasa na soko la uhakika. Naomba kuunga mkono hoja.

MHE. BRIG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI: Mheshimiwa Spika, katika hotuba iliyowasilishwa na Waziri suala la usambazaji umeme katika Jimbo la Mlalo haikugusia Tarafa ya Mtæe.

Katika mradi wa awali wa kupeleka umeme Mlalo, mradi huo ilikuwa ukamilike kwa kufikishwa umeme Mtæe kuititia vijiji vya Makose, Rangwi, Sunga hadi Mtæe. Aidha, *line* nyingine iliotokea Lukozi hadi Viti ilikuwa iendelezwe hadi Manolo Kibaoni na kuunganishwa na Sunga hadi Mtæe. Mradi huu ulikatishwa bia kukamilika wananchi walihamasishwa, wakaweka nyaya kwenye majengo yao wakingojea umeme wa gridi uwafikie, sasa ni miaka 10 toka mradi huu usitishwe. Wananchi wa Mtæe wanaona

wamepuuzwa wakati maeneo mengine Tanzania yanaendelea kupata umeme kama mpango wa Wizara hii wa mwaka 2008/2009 unavyoonyesha.

Napenda kuunga mkono hoja lakini ni budi mradi huu ufahamike utakamilika lini.

MHE. STEPHEN M. WASIRA: Mheshimiwa Spika, usambazaji umeme katika vijiji na shule za sekondari, zinazopitiwa na umeme wa gridi, Bunda mjini ndiko chanzo cha umeme uendao Mugumu, Makao Makuu ya Wilaya ya Serengeti na pia Ukerewe. Umeme uendao Mugumu unapitia vijiji vya Misisi, shule ya sekondari ya Sazera, vijiji vya Mcharo na Changuje, palipo shule ya sekondari ya Sizaki ambako inajengwa hosteli ya wasichana ambayo inahitaji umeme.

Vijiji vya Kinoleli, ambako kuna *transforma* lakini umeme hausambazwi. Kijiji cha Salama A kina *transforma* lakini sekondari ya Salama A kuna *transforma* lakini sekondari ya Salama iliyoko Serae Kati ambako Wajapani wanajenga hosteli ya wasichana ambayo inahitaji umeme. Kijiji cha Sanzate pia kinapitia na umeme wa gridi lakini hakuna umeme. Shule za sekondari za Chamwino, Mihingo na Mikomarino, shule ya sekondari ya Hunyani na kijiji cha Hunyeni. Shule ya Sekondari ya Kabasa na Kijiji cha King'ombe, naomba vifikiriwe kupewa umeme. Eneo hili liko kilometra 3 - 4 kutoka Bunda ambako kuna umeme. Shule ya Sekondari ya Guta na Kijiji cha Nyabaho, kwenye chanzo cha kusukuma umeme kinahitaji umeme.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. FATMA ABDULHABIB FEREJI: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja hii kama ifuatayo, katika hotuba ya Waziri, ukurasa wa 44 na 45 kwa upande mmoja na ukurasa wa 50 kuna maelezo ya kutatanisha kuhusiana na majukumu aliyopewa Mshauri kutoka United Kingdom wa kampuni ya AUPEC anayezishauri Serikali zetu mbili kuhusiana na mgawanyo wa gharama na mapato katika sekta ya mafuta na gesi asilia.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri Waziri akalieleza Bunge lako hili Tukufu, Mshauri huyo anashauri kuhusu mafuta na gesi asilia au mafuta tu?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mafuta na gesi asilia ni masula ya Muungano, je, baada ya ushauri kutolewa na kukubaliwa na Serikali zetu mbili, je, Zanzibar nayo itapata mgao wake wa gesi asilia ilioanza kutumika kutoka Songsongo toka Julai, 2004. Naomba Waziri atupe ufanuzi wa kina katika hili.

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu kwamba Serikali itazingatia vema taarifa ya Kamati ya Rais ya kuishauri Serikali kuhusu usimamizi wa Sekta ya Madini ili Watanzania wafaidike na madini kama raslimali yao.

Mheshimiwa Spika, suala la kung'ang'ania kupenda mrahaba kutoka kwa wawekezaji kama njia ya kuongeza pato kutoka kwenye madini halitoshi. Ni vyema Serikali ikaangalia uwezekano wa *ku-review tax regime* ya sekta ya madini na

kuhakikisha kwamba wawekezaji wanatozwa kodi inayostahili ili wananchi wafaidike na raslimali ya madini yao. Watanzania lazima wahahakikishiwe kwamba madini yatakuwa mkombozi wa matatizo yao ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza wizara kwa kuvunja mkataba kati ya *TANESCO* na *Richmond/Dowans*. Angalau Watanzania watapa nafuu kidogo.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, kwanza nakupongeza kwa hotuba yako nzuri yenyе ufanuzi wa kina kuhusu Wizara yako. Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono hoja hii naomba kuchangia maeneo yafuatayo, kwanza ni kuhusu sekta ya kilimo, kwa kuwa Wilaya ya Mpwapwa kuna madini aina ya Ruby/Safaya katika kijiji cha Winza na *Blue Copper* katika kijiji cha Mlembule na Tambi na kwa kuwa wachimbaji wadogo wadogo wa maeneo hayo wanakabiliwa na tatizo la mitaji kwa ajili ya ununuzi wa vitendea kazi, kwa kuwa vyombo wanavyotumia wachimbaji wadogo wa Winza ni duni sana na vyenye tija ndogo: je, Serikali imeweka mkakati gani wa kuwasaidia mitaji na kuwapatia mikopo kwa kuwa wanashindwa kupata mikopo kwenye mabenki kutokana na masharti magumu?

Je, Serikali imeweka mkakati gani wa kuhakikisha kwamba wawekezaji wakubwa hawawanyanyasi wachimbaji wadogo? Je, Serikali imefanya utafiti ni hekta ngapi ambazo zina madini aina ya Ruby/Safaya katika Kijiji cha Winza Wilayani Mpwapwa na *Blue Copper* katika vijiji vya Mlembule na Tambi Wilayani Mpwapwa. Je, Serikali ina mpango gani wa kutafuta wawekezaji wa kuchimba madini aina ya Jasi (*Gypsum*) katika kijiji cha Msagali – Wilayani Mpwapwa.

Kuhusu sekta ya umeme, je, ni vijiji vingapi katika Wilaya ya Mpwapwa vitakavyopatiwa umeme kwa fedha za *MCC* (mpango wa *MCC* wa kusambaza umeme vijijini)? Kwa kuwa nguzo nyangi za umeme unaokwenda Mpwapwa, Kongwa na Kibakwe kukatika katika hasa kipindi cha mvua, je, Serikali imetenga shilingi ngapi za ukarabati? Je, vijiji vya Berege, Mima, Mzase, Chunyu, Lupeta, Mbori, Godegode, Nghambi, Chitemo, Msagali, Tambi Wilayani Mpwapwa vitapatiwa umeme katika Bajeti ya mwaka 2008/2009? Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza gharama za umeme ili kupata wateja wengi kuliko hali ilivyo sasa na gharama ni kubwa sana?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa bei ya mafuta inapanda siku hadi siku na kufanya gharama ya vitu vingine kupanda bei na hata gharama ya maisha kupanda, je, Serikali imeweka mkakati gani wa kudhibiti mfumuko wa bei ya mafuta ya dizeli, petroli, mafuta ya taa na kadhalika?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. GIDEON A. CHEYO: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa William Ngeleja, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nishati na Madini na Mheshimiwa Adam Kighoma Malima, kuteuliwa kuwa

Naibu Waziri wa Wizara hii. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri ya uwasilishaji mzuri.

Mheshimiwa Spika, katika kuunga mkono hoja hii napenda kuchangia maeneo machache hasa kwa lengo la kumkumbusha Mheshimiwa Waziri kuzingatia na kutoa majibu kwa maombi yaliyokwisha wasilishwa Wizarani kwake.

Umeme Wilaya ya Ileje unaotumika katika baadhi ya maeneo ya Wilaya ya Ileje unatoka Zambia kupitia Wilaya ya Mbozi. Matatizo ya kukatika katika kwa umeme yaliyoelezwa katika aya ya 27 ya hotuba ya Waziri, kuhusu umeme Sumbawanga, ni sawa na hali ya Ileje. Sasa swalij, makubaliano ya Waziri Mheshimiwa William Ngeleja na Waziri wa Zambia kuhusu ufumbuzi wa matatizo ya umeme Sumbawanga yatahusu pia Wilaya ya Ileje? Wakati wa kupitisha Muswada wa Umeme nilimuomba Mheshimiwa Waziri kuzingatia suala hili. Nitafurahi kupata jibu.

Mheshimiwa Spika, makaa ya Mawe ya Kiwira sehemu kubwa ya mgodi wa makaa ya mawe ya Kiwira iko ndani ya Wilaya ya Ileje. Nimekwisha wasilisha ombi kwa Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, nipatiwe maelezo ya kina kuhusu hali halisi ya umiliki na uendeshwaji wa mgodi huu. Wana-Ileje tukiwa wadau muhimu wa mgodi huu nadhani tuna haki ya kupata taarifa sahihi na kushirikishwa kadri iwezekanavyo.

Aidha, tunatumaini mradi wa kuzalisha umeme kutoka mgodi huo, kama ilivyoelezwu katika aya ya 93 ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri, utaongeza kasi ya kusambaza umeme katika Wilaya ya Ileje. Wana-Ileje bado hawajafaidika kabisa na kuwepo kwa mgodi huo ndani ya Wilaya yao, ukiondoa ajira ya wana-Ileje wachache katika mgodi huo.

Mheshimiwa Spika, maporomoko madogo madogo ya maji ya Jotoardhi. Katika aya ya 51 ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri, imeelezwa kwamba ufatifi umefanyika katika eneo la Songwe kuhusu somo hilo hapo juu. Ningependa kufahamu ni Songwe ipi maana jina hilo lipi katika Wilaya ya Mbeya Vijijini, Mbozi, Ileje na Kyela. Sasa eneo lipi hasa? Wilayani Ileje yapo maporomoko madogo madogo ya maji, kama vile Lusalala, kata ya Sange, ambayo yangeweze kutumika kuzalisha umeme. Je, wataalam wanazo taarifa hizo? Natumaini wakala wa nishati vijijini utaelekeza nguvu zake katika kubaini vyanzo kama hivi.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huo mdogo, napenda kumaliza kwa kuwatakitia kila la kheri katika utekelezaji wa Bajeti ya Wizara na naunga mkono hoja.

MHE. ZAINABU M. VULU: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa William Ngeleja, Naibu wake Mheshimiwa Adam Malima, Katibu Mkuu na watendaji wao wote.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri hakika imeweza kutupa changamoto katika sekta zote na pia tumeweza kupata taswira ya suala zima la umeme na madini nchini kutokana na taarifa kuhusu usimamizi wa sekta ya madini.

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe shukrani zangu kwa niaba ya baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Pwani kwa kupatiwa umeme, maeneo hayo ni Bungu, Kibiti, Muharo na Utete, Wilaya ya Rufiji. Umeme huu wa barabarani ni hatua moja mbele ya maendeleo kwani umerahisisha kwa wananchi wenyewe uwezo kuvuta na kuweka majumbani na hasa ukizingatia kwamba gharama zake ni nafuu. Tunapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ningeomba kupata maelezo ya maeneo mengine kwa kuanzia Wilaya hiyo hiyo ya Rufiji. Kuna bandari ya Nyamisati, shule ya sekondari ya Mahege, Mlanzi na pia kuna Kiwanda cha kuhifadhia samaki hapo Nyamisati, je, ni lini mradi wa umeme utafika huko, kwani bandari ni muhimu kwa Mkoa wa Pwani ikiwa ni kiungo cha abiria na biashara kwa watu wa Mafia.

Vile vile kiwanda kimesimama muda mrefu sasa kikipata umeme basi pia itakuwa ukombozi kwa wanachama kwa maana ya kupata ajira. Pia naomba Mheshimiwa Waziri anipatie maelezo ni mikakati gani ambayo Wizara imeweza katika kuitisha nyaya za umeme kwenye daraja la Mheshimiwa Mkapa ili na maeneo mengine waweze kupata umeme. Kwa kuwa Kibiti, Muhoro, Bungu tayari kuna umeme wa barabara na barabara hiyo ni kubwa je, ni lini nguzo za umeme zitaanza kuwekwa kuanzia Bungu kuelekea Mkuranga (ningependa kujua nguzo na umeme huo utafungwa lini).

Mheshimiwa Spika, mbali ya matatizo hayo kwa Rufiji ni vyema Mheshimiwa waziri anipe utaratibu wa Wizara wa uwekaji umeme wa barabara kuanzia Kibaha hadi Chalinze, umeme katika Wilaya ya Kisarawe, na maeneo mengine ya mkoa wa Pwani. Baada ya maelezo hayo ambayo natarajia kupata majibu, pia naomba kutoa ushauri kwa Wizara kuhusu utoaji wa elimu ili kuwandaan na kuwawezesha kisaikolojia, kiuchumi, wananchi wanaoishi maeneo ya madini na gesi, elimu hiyo na ushirikishwaji huo wa wananchi na wawekezaji utasaidia kupunguza migogoro. Baada ya maelezo hayo napenda kuunga mkono hoja.

MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kwanza kuunga mkono hoja ya Bajeti ya Waziri wa Nishati na Madini.

Pamoja na hayo ninayo michango ya mambo machache kama ifuatavyo, *Nyamongo Gold Mine* wanapelekewa umeme toka jimbo langu la Musoma Mjini. Pamoja na kazi hiyo nzuri, yapo matatizo yaliyojitekeza katika jimbo langu nayo ni wananchi wanalamikia fidia waliyoipata ilikuwa ndogo sana na uthamini ulifanywa kwa kumlinda mwekezaji huyo wa Nyamongo na ninaamini Mheshimiwa Waziri taarifa hiyo anayo. Napenda kujua ni kwa kiasi gani suala hili limeshughulikiwa na kama Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuja Musoma Mjini wasikilize wananchi hao ambao hawakufurahishwa na utaratibu mzima wa uthamini wa mali zao.

Pili Mheshimiwa Spika, gharama za usambazaji wa umeme zimekuwa juu sana kwa kuwa *TANESCO* wanakwepa majukumu yao ya gharama na badala yake wanamrundikia mtumiaji azilipe kabla hajapewa umeme, ningependa kujuu ni lini gharama hizo zitaanza kubebwa na *TANESCO* wenyewe au la mwananchi alipe gharama hizo zipunguzwe kwenye bili yao ya kila mwezi.

Ahsante Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

MHE: EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Spika, awali naomba nimpongeze sana Mheshimiwa William Ngeleja na Naibu wake Mheshimiwa Adam Malima, kwa kushirikiana vyema na viongozi wengine wa Wizara na kuanza kufanya maamuzi mazito na mazuri ya kulisaidia Taifa. Aidha, nawapongeza kwa Bajeti nzuri.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha Bajeti hii, naomba kuchangia mambo yafuatayo, kwanza ni kuhusu wachimbaji wadogo Kahama. Serikali haijabaini maeneo yanayofaa kutengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Hii imekuwa ahadi toka mwaka 1996, walipoondolewa maeneo ya Bulyanhulu eneo hilo lilipotolewa kwa Barrick. Hivi sasa wako wananchi zaidi ya 100,000 walipo Kakola bila kazi. Uwepo wa kundi kubwa la watu wasio na maeneo ya kufanya kazi ndicho chanzo cha migogoro isiyokoma baina ya Serilali na Barrick Bulyanhulu.

Mnamo Februari, 2007 Mheshimiwa Nazir Karamagi katika kutatua mgogoro na vurugu za wananchi aliahidi kwamba Serikali itasaidia upelekaji wa umeme Kakola kuititia *BGML*, itasaidia katika usimamizi wa ukarabati wa barabara ya Kakola – Kahama unaofanywa na Barrick kwa mujibu wa makubaliano ya mwaka 1997 (kati ya Idara ya Ujenzi na *Kahama Mining Co. Ltd*) na itasimamia upatikanaji wa maeneo ya wachimbaji wadogo Kahama. Wananchi walipaswa wajijunge katika vikundi.

Mheshimiwa Spika, ahadi hizi zilitolewa hadharani. Wananchi waliambiwa utekelezaji wake utachukua mwaka mmoja hadi mwaka 2008. Naomba sana Serikali itimize ahadi yake hii.

Kuhusu umeme vijiji – Segese, naishukuru sana Wizara hii kukubali kuingiza Kijiji cha Segese katika mradi wa umeme Bukombe. Naomba sana mchakato ufanyike haraka ili vijiji vyote vitakavyopata umeme katika mradi huu vipate umeme kabla ya mwaka 2010 kama ilivyo kwenye Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapainduzi mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nishati mbadala, kutokana na ongezeko la bei ya mafuta, gharama za maisha zipande na uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Wizara isaidie miradi ifuatayo, *TPDC* waweke stock ya mafuta, nishati mbadala – *biogas* na gesi hasa mijini, usambazaji wa teknolojia ya mafuta mazito ya motopoa na kubadili injini za gari kutumia gesi badala mafuta.

Mheshimiwa Spika, manufaa/miundombinu ya maeneo ya madini, Serikali itumie dola milioni 7 zinazotolewa na Barrick kama *advance tax* kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya maeneo ya migodini. Wananchi wa Kahama wamekuwa wakilalamikia vumbi katika barabara ya Kahama – Kakola. Mheshimiwa Rais aliahidi Oktoba 2007 alipotembelea Kahama kuwa barabara hiyo itatengenezwa kwa teknolojia rahisi ya *Molasis* ili kuondokana na vumbi. Hili linawakera sana wananchi. Aidha, limekuwa likiwakera hata Barrick wenywewe. Tunaomba fedha za *advance tax* (dola milioni 7) zilizolenga kuboresha miundombinu ya maeneo ya migodini zitumike kwa lengo hilo.

Barrack agreed to start paying this advance tax in order to get the social licence. The money has to be used to improve infrastructure in the mining areas and the mining division in the Ministry so as to reduce unnecessary public complains against Barrick. Don't dump this money into the consolidated fund.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE: PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Spika, umeme utokao Mbala – Zambia mpaka Sumbawanga, Tanzania uhudumie vijiji vikubwa njiani kama vile kijiji cha Kasesya, Tatanda, Sopa, Matai, Msanzi, Katuka, Matanga na Mtimbwa. Nashukuru sana kuwepo katika mpango wa kupewa umeme mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atamke wazi kuwa nguzo zitaanza kuwekwa mwezi upi? Umeme wa Mpanda Mjini mashine zake ni spana mkononi hivyo naomba sana tutafutiwe vipuri vya uhakika wakati ambapo wanatafutiwa mashine zingine.

Mheshimiwa Spika, Rukwa tunaomba umeme wa gridi. Bila umeme mazingira yataendelea kuharibiwa.

Kuhusu Madini naomba sana upimaji mpya ufanywe Wilaya ya Nkasi ambapo haujafanywa. Mheshimiwa Waziri hivi sasa Wazungu wanachimba madini ya vito Wilayani Nkasi na wana uhakika na maeneo na wameanza kuomba kuyamiliki.

Mheshimiwa Spika, Mpanda kunachimbwa dhahabu; na baadhi ya wafanyakishara wamehodhi maeneo. Wapo waliomiliki vitalu bila kuvifanya kazi, matokeo yake wawekezaji wameshindwa kuwekeza kwa vile maeneo yameshikwa na watu hawa wanakaa Dar es Salaam ambao ni Wahindi. Vibali vyote vya aina hii naomba mvifute.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE: MWANAWETU S. ZARAFI: Mheshimiwa Spika, wakati wa kuchimba gesi ya Songsongo kuna mafuta ambayo wachimbaji hawa huyakusanya hadi kufika tani mia nane ndipo huwauzia *TPDC* na hufika meli kuchukua. *TPDC* huyafanya nini? Hutengeneza mafuta ya aina gani, dizeli, petroli, mafuta ya taa au mafuta gani? Kama

hutengeneza mafuta, je, ni rasmi? Kodi na utaratibu mwingine wa kisheria unaenda sawa sawa.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukiona tarehe mbalimbali zenyе kutia matumaini ili umeme wa uhakika upatikane Kilwa, lakini hadi leo hakuna kitu. Tungependa tujue tatizo ni nini, kwa nini mkandarasi anafanya kazi nusu nusu na anaangaliwa tu? Kama hana uwezo hadi leo hii hamjagundua au anaogopwa.

Ningependa kujua ni lini umeme wa *Songas* utapatikana kuwa wa uhakika Kilwa? Katika kuitia mikataba ya mradi wa Songosongo, iwe kurekebisha mikopo ya kupunguza *capacity charge* tu, bali iangalie pia ni jinsi gani na Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa pamoja na wananchi wake wananaufaikaje (siyo *social support* tu ambayo mwekezaji hutoa pale anapojisikia) kwa nini wenzetu wa *Mnazibay* Mkataba wao unamanufaa kwa wananchi wake. Kwa nini Kilwa? Naomba mliangalie hili.

MHE: DR. BINILITH S. MAHENGЕ: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa maandalizi ya hotuba nzuri. Kwa niaba ya wananchi wa Makete natoa shukrani kwa Serikali kwa kuingiza mpango wa kupeleka umeme Tandala – Ikonda Hospitali katika mpango wa *MCC*. Mradi huu utasaidia sehemu zifuatazo kupata umeme ambazo ni Ndulamo, Kisinga, Mago, Lupalilo, Lupalilo sekondari, Ikonda Hospitali, Chuo cha Walimu Tandala na Mjini Tandala.

Ombi maalum (*special request*) kwa kuzingatia vigezo vya matatizo yaliyopo katika Wilaya ya Makete yaani tatizo la UKIMWI na uchumi duni unaoikabili Wilaya ya Makete, ambapo uchumi duni ndio msingi wa kuenea kwa UKIMWI, uliosababisha Wilaya kuwa na yatima 13,000 tunaomba Serikali ifanye yafuatayo, Serikali itoe kipaumbele cha kuanza kutekeleza mradi wa umeme wa *MCC* kupeleka Ikonda mwaka huu yaani mwezi huu wa nane. Kupelekwa kwa umeme kutawawezesha wananchi kupunguza umaskini na hivyo kuondokana na UKIMWI. Pia Serikali ipeleke umeme kwenye vijiji vilivyopitiwa na nguzo za umeme kutoka Mbeya kwenda mjini Makete vijiji hivi ni Ujuni, Nkenja, Isapulano na Mpangala.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali ipeleke umeme katika kata ya Mfumbi, kata hii inapakanan na Wilaya ya Mbarali na Mbeya Vijijini ambapo Wilaya hizo zingine zina umeme pande zote, lakini kipande kidogo cha Makete umeme unapita, wananchi walinda nguzo tu.

Kuhusu umeme vijijini (*rural electrification*). Serikali iweke kipaumbele cha kupeleka umeme vijijini. Umeme ukipelekwa vijijini Serikali inaweza kutegemea mambo yafuatayo, kuongeza pato la wananchi, kwa wananchi kutumia umeme kwenye shughuli za uzalishaji, kuweza kuongeza uzalishaji katika kilimo kwa kutumia pampu za umeme kwenye kilimo cha umwagiliaji na saa za kazi kwa wafanyabiashara zitaongezeka, na hivyo kuongeza uzalishaji. Hii ni kutokana na mazingira mazuri ya kuwepo umeme.

Kuhusu vyanzo vya umeme, naipongeza Serikali kwa kuweka mto Rumakali katika mpango wa kuzalisha umeme katika mpango wa muda mrefu. Napendekeza

Serikali pia ione uwezekano wa kutumia vile vyanzo nya mito midogo kuzalisha umeme wa *small scale hydropower, small hydropower generation*, itasaidia Serikali kusambaza umeme kwa kasi katika vijiji na hivyo kufikia azma yake ya maisha bora kwa kila Mtanzania. Naunga hoja.

MHE: MKIWA A. KIMWANGA : Mheshimiwa Spika, nami napenda kuchangia hoja hii ya Wizara ya Nishati na Madini.

Kwanza napenda kumpongeza Waziri pamoja na Naibu wake kwa kuleta hotuba ya Wizara yao pamoja na maneno mazuri tunaomba utekelezaji kama ulivyowasilishwa.

Mheshimiwa Spika, mimi napenda kwanza kuchangia suala la madini kwani tangu Kamati teule zianze kufutilia masuala ya madini zote zinatoa taarifa lakini taarifa hizo haziwafikii wananchi kwa wakati, huchukua muda mrefu na hatimaye huwa kimya. Je, hali hii ni mpaka lini? Pia napenda kufahamu kuhusu suala la mchanga wenye madini ambaao ulikuwa ukienda nje kutenganishwa madini na mchanga, je, mpaka hii leo mchanga huo bado ukienda au mmesitisha?

Naomba wakati wa majumuisho unijibu suala hilo. Pia ningependa kuhaftahmu, nilisikia mtambo wa mashine ya kutenganisha mchanga na madini kinajengwa Mwanza, je, hii ni kweli? Kama ni kweli basi naomba uniambie ujenzi huo umefikia wapi? Pia napenda kuishauri Serikali kuwa wawekezaji wa madini watenge ongezeko la kuchangia maendeleo katika maeneo husika. Itakuwa ajabu kama hali za migodini, kwa wakazi wa maeneo hayo kuwa bado duni, hii ni aibu sana.

Mheshimiwa Spika, Wizara naiomba iwe mstari wa mbele kuhakikisha ubora wa wananchi hawa, pia maji wanayotumia watu hawa ambaao wanaishi kando kando ya migodi kwani waoshao dhahabu hutumia maji yenye dawa ambayo yana athari kwa wananchi.

Napenda pia kuchangia upande wa nishati, katika ukurasa wa 52 Ibara ya 101 katika hotuba ya Waziri ameongelea umeme nuru ambaao uko Mkoani Mwanza na umeleta mafanikio ya mradi wa majoribio na yataendelea kutekelezwa Mkoa wa Mara na kwingineko.

Kwanza napenda Waziri anisaidie kujua umeme nuru na katika Mkoa wa Mwanza majoribio yamefanyikia wapi? Je, Serikali haioni ni busara kama kuna mradi mpya wa maeneo husika wakashirikishwa Wabunge wa maeneo hayo, ili kuepuka mshangao.

Mheshimiwa Spika, naomba pia miradi ya umeme katika Jiji la Mwanza eneo la Wilaya ya Ilelema ambako ni Wilaya mpya, baada ya mgawanyo wa Wilaya. Tunaomba umeme maeneo ya Kiseke, Kangae, Bugogwa, Kahama na hata Busweru na Igombe. Imejengwa Halmashauri mpya ya Wilaya ya Ilemela. Hata katika Wilaya ya Sengerema pia umeme ni muhimu. Jimbo la Sengerema, pia Buchosa.

Tunaiomba *EWURA* kuzingatia katika suala la mafuta, hali ni mbaya huko mikoani. Mwanza mjini mafuta ya taa ni shilingi 1500/= chini ya hapo ni shilingi 1,400=/. Je, *EWURA* hawalioni hilo? Mwananchi dhaifu atamudu kweli? Dizeli ni kama inavyojulikana kwa sasa ni shilingi 2000/= kwa lita mwananchi dhaifu atamudu? Tuonaomba washitueni *EWURA* ili wafanye kazi. Meno tuliwapa sasa hatujasikia kama wameuma.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima nakuomba mdogo wangu majibu ya kunipa mwanga na ya matumaini. Hongera kwa mtoto wa kike Mungu ampe maisha mema na marefu. Ahsante.

MHE: NURU A. BAFADHIL: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuchangia hotuba hii. Pili, napenda kumpongeza Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii kwa umakini na ufuatiliaji wake wa karibu.

Napenda kujikita katika suala zima la umeme. Miaka 48 ya Uhuru Watanzania wanazidi kuwa wachache katika matumizi ya umeme. Hutokana na kupanda bei kwa umeme siku hadi siku watumiaji wa nishati hii wanapungua. Hii inapelekea hata baadhi ya wananchi katika baadhi ya sehemu kutumia Kinyesi cha ng'ombe, magogo kwa ajili ya kuwashia moto ili uweze kuwamulika usiku. Huu utaratibu wa utumiaji wa kinyesi cha ng'ombe au magogo hupelekea kusababisha hatari za moto katika baadhi ya nyumba wakati mwingine wengine hupoteza maisha kwa moto huo na baadhi ya watu wanapoamka huwa na macho mekundu ambayo huambiwa ni wachawi kutokana na imani za kishirikina.

Mheshimiwa Spika, kupanda kwa bei ya umeme pia kunaathiri maisha ya kila siku. Ukipandisha bei za umeme ni dhahiri gharama za uendeshaji sehemu mbalimbali utapanda. Mfano umeme unapopanda viwandani, bei ya bidhaa kadhaa nazo hupanda kiasi cha kumfanya mwananchi hususani mwenye kipato cha chini kushindwa kumudu maisha yake. Kupanda kwa umeme pia ndio chanzo cha kufivunga baadhi ya viwanda hutokana na kushinndwa kuzalisha.

Mheshimiwa Spika, naomba mjibu hoja atueleze hivi Serikali yetu ina mpango gani wa kushusha bei ya umeme ukizingatia kuwa Serikali ina mkakati wa kupeleka umeme vijijini. Kwanza tujiulize iwapo mjini ambapo mzunguko wa fehda una afadhali tofauti na vijiji, je, mwananchi anayeishi kijijini atamudu kulipia umeme wakati mjini zoezi la kata kata umeme limeongezeka siku hadi siku kwa watumiaji wa nishati hii?

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kuhusu madini katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 32 aya 62 ameelezea sehemu zilizotengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo. Naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri, je, wale wachimbaji wadogo wa Kigwasi – Kalalani, Kata ya Mashewa Wilaya ya Korogwe vijijini hawajapewa leseni za uchimbaji mdogo unaoendelea katika machimbo hayo niliyotaja.

Mheshimiwa Spika, kuna vitendo vya kinyama vinavyotendeka katika maeneo hayo ya Kigwasi. Kuna raia wanafanyiwa unyama kama vile kupigwa risasi, kupigwa hadi kuumizwa na wengi hata kulawitiwa na hao wanaojiita walini wa wamiliki wa mgodi huo. Mgodi huu unajulikana kwa jina la *AAPS* lakini kuna wawekezaji ambao wameweka kibao chao cha umiliki kwa jina la *Amazon*. Mheshimiwa Waziri atueleze mmilikaji halisi wa mgodi huu ni yupi *AAPS* au *Amazon*?

Mheshimiwa Spika, nashangaa watu wanapigwa, wanaumizwa lakini wanaitwa vibaka. Sasa vibaka hupelekwa mahakamani hujibu mashtaka au watu huchukua sheria mkononi mwao. Naomba kupata maelezo ya kwa nini hawa wachimbaji wadogo wadogo wasipangiwe sehemu zao ambazo hawataingiliwa na hawa wawekezaji huwanyang'anya sehemu zao. Hiki ndio chanzo cha migogoro mingi ya ardhi kutokana na dhuluma inayofanyika kwa wachimbaji hawa wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, inaelekea kuna baadhi ya wawekezaji wanaomba ardhi kuwekeza katika uchimbaji wa madini ni ujanja tu. Hawana malengo ya kuchimba ila tu huwekeza kupata mikopo ya mabilioni ya pesa kwa faida yao binafsi.

Mheshimiwa Spika, hii migodi inakuwa kama stempu tu ya kupatia mikopo katika mabenki mbalimbali. Wawekezaji hawa wanatuachia mashimo au mahandaki. Naiomba Serikali iangalie suala zima la hawa wawekezaji ambao wana malengo ya kuvuna kile wasichopanda.

MHE: MATHIAS M. CHIKAWE: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuwapongeza Waziri Mheshimiwa William Ngeleja na Naibu wake Mheshimiwa Adam Malima kwa kuteuliwa kushika nyadhifa zao wanazistahili.

Naomba nichangie maeneo mawili ya Bajeti hii. Umeme Nachingwea unatoka kwenye mitambo iliyopo Masasi. Mitambo hiyo kwa sasa ni mibovu. Matokeo yake ni kuwa hakuna umeme Nachingwea na kutokana na hilo hakuna maji Nachingwea maana maji yanategemea pampu zinazoendeshwa kwa umeme. Suluhisho la tatizo hili ni kuwekwa jenereta Nachingwea. Umeme wa *ARTUMAS* una muda mrefu kufikia Nachingwea. Hatuutegemei umeme wa *ARTUMAS* kabla ya kipindi cha mwaka mmoja. Kwa sasa dawa ni jenereta.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wachimbaji wadogo/wakubwa, Wilaya ya Nachingwea imebahatika kupata madini mengi ya kila aina. Aidha, sasa hivi kuna *rush* ya wachimbaji wadogo katika sehemu kubwa ya Wilaya. Kuna dalili za vurugu za hawa wachimbaji wadogo kutokea. Nashauri na kupendekeza kuwa Wizara ipeleke wataalam wa madini ili wakafanye mambo muhimu yatakayoweza kutuliza hali ya tafrani Wilayani. Lakini la muhimu ni kutenga eneo la wachimbaji wadogo wadogo ili nao wapate sehemu ya kuchimba na kukimu maisha yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja ya Wizara hii.

MHE: ALHAJ PROF. JUMA A. KAPUYA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wao na timu yote ya Wizara kwa hotuba nzuri ilijoja matumaini.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Wizara ni kuhusu kusambaza umeme katika vijiji cha Kaliua. Naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, wataalam wake wa umeme wakiongozwa na Kamishna wa Nishati, Ndugu Mrindoko na bila kumsahau Mkurugenzi Mkuu wa TANESCO Ndugu Dr. Idrisa Rashid kwa ushawishi wao kwa Serikali ya Sweden hadi ikakubali kuongezea nguvu mkondo wa umeme uendao Kaliua toka Urambo ili uwe wa *three phase*. Umeme huu sasa utakidhi matakwa ya viwanda vinavyojengwa Kaliua na vinahitajiwa kujengwa. Mpaka hivi sasa karibu kiwanda cha *Ginnery* ya pamba unakamilika.

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Waziri, pamoja na shukrani hizo bado tunaomba tatizo la kusambaza umeme pale Kaliua. Tuna maeneo muhimu yafuatayo, Shule ya Sekondari "A" Level ya Kaliua, Shule ya Sekondari ya "O" level ya Ushokola, kituo cha Afya cha kisasa na ni kikubwa sana na kina vifaa vya kisasa, eneo lote la soko ambalo ndio wafanyabiashara wote wanafanya shughuli zao na kuishi na kijiji cha Ulinduanoni ambako kunajengwa chuo cha VETA, shule ya sekondari ya "O" Level inayojengwa na Kanisa la Moravian.

Mheshimiwa Spika, pia kuna shule inajengwa ya "A" level inayojengwa na Kanisa la Wasabato na shule za msingi tano zilizoko mjini Kaliua.

Mheshimiwa Spika, wote hawa ni watumiaji walioko tayari kabisa, lakini tukiwaachia shughuli ya kusambaza waifanye wao hawataweza kutokana na gharama kuwa kubwa sana. Naomba wao waachiwe gharama za kuingiza umeme katika taasisi zao au nyumba zao tu. Nakuhakikishia umeme utaleta mageuzi makubwa ya kiuchumi katika eneo letu na kwa hiyo, kusaidia uharaka wa kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania. Lakini pia watakuwa ni wachangiaji wakubwa katika pato la TANESCO.

Mheshimiwa Spika, nashukuru na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja lakini narudia, tafadhali sana, wakati wa kupekeka *third phase* Kaliua tukamilishe na usambazaji katika maeneo niliyoainisha pale juu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

MHE: JANETH M. MASSABURI: Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu yake ya wataalam kwa kuandaa hotuba nzuri ya Makadirio ya Bajeti kwa mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa masikitiko makubwa kwa kuomba jambo moja sugu kama ifuatavyo, kumekuwa na matatizo makubwa ya kutopatikana kwa umeme katika maeneo yaliyoko pembezoni mwa Mkoa wa Dar es Salaam na hasa eneo la Chanika (Videte) mpaka Msongola Jimbo la Ukonga. Pamoja na Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete alipoahidi mbele ya wananchi wa Kata ya Chanika mnamo mwezi Machi 2006 mpaka leo umeme haujapatikana.

Mheshimiwa Spika, naiomba tena na tena Serikali kupitia Wizara hii ya Nishati na Madini kupitia kwa Mheshimiwa William Ngeleja ambaye ndiye mwenye dhamana ya Wizara hii aweze kuhakikisha umeme unapatikana bila ucheleweshaji usiokuwa wa lazima. Naomba maeneo haya yazingatiwe. Kata ya Chanika (Videte) kuelekea Kata ya Msongola, Kata ya Kitunda kuelekea Kivule, maeneo haya katika Jimbo la Ukonga Wilaya ya Ilala. Kata za Pembamnazi, kata ya Kisarawe II na Kata ya Chamazi ziko Wilaya ya Temeke. Kata ya Goba na Mbezi Jimbo la Ubungo na Kawe.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri afanye ziara ya kukagua maeneo haya ili aweze kuona hali halisi n kuelewa ukubwa wa tatizo ulivyo. Idadi ya wakazi ni kubwa sana na wimbi la uhalifu umehamia maeneo hayo, kutokana na giza la ukosefu wa umeme. Narudia tena Mheshimiwa William Ngeleja na tunaimani na wewe na Naibu Waziri Mheshimiwa Adam Malima. Ni aibu Mkoa wa Dar es salaam hauna umeme jamani ! Kila la kheri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE: RIZIKI OMAR JUMA: Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuchangia hoja hii kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na watendaji wake wote kwa kujitahidi kupanga mikakati madhubuti ya kuhakikisha kuenea kwa umeme Tanzania. Kwanza naomba niende moja kwa moja kwenye nishati.

Mheshimiwa Spika, naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri je, wale wananchi wa Kipumbwi Wilaya ya Pangani ambao ndani ya Bunge hili walihidiwa kuwekewa *transfoma* ifikapo mwezi Agosti, 2007 hadi leo hivi hata hawakutajwa katika hotuba yake? *Transfoma* hiyo ni gharma ya shilingi milioni saba tu kwa kauli iliyotolewa ndani ya Bunge hili ama ndio tunaendelea kuwadanganya wananchi na kuwakatisha tamaa.

Mheshimiwa Spika, lazima tukumbuke kwamba umeme ni mategemeo kwa kila sehemu kwa maana hiyo umeme ni maendeleo. Bila umeme ajira zinapungua, kwani shughuli nyingi za maendeleo zinahitaji umeme hivyo naomba tuwe na mkakati madhubuti wa kuwafikishia wananchi huko vijijini nishati hii muhimu. Pia itasaidia kulinda mazingira, lakini bila umeme vijijini mazingira yataendelea kuharibika kwa sababu hakuna nishati mbadala. Shule za sekondari zinalazimika kuwa na maabara bila umeme, haiwezekani hivyo uhaba wa wanasayansi Tanzania utaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Spika, wazee wenyе macho mekundu vijijini wataendelea kuuwawa kutokana na kuendelea kutumia kuni na hatimaye kuitwa wachawi.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ihakikishe utekelezaji wa usambazaji wa umeme vijijini na kwa gharama nafuu ili kuwaondolea wananchi umaskini kwani kiza ni unyonge, kiza kikitawala na umaskini hushamiri.

Mheshimiwa Spika, maandiko yatekelezwe yasiishie vitabuni.

MHE: DUSTAN D. MKAPA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kuunga mkono hoja hii ya Wizara ya Nishati na Madini. Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa William Ngeleja kwa hotoba yake nzuri sana ya Makadirio na Matumizi ya fedha kwa mwaka 2008/2009. Pia napenda nimpongeze Naibu Waziri wake Mheshimiwa Adam Malima kwa kumsaidia vizuri Waziri Mheshimiwa William Ngeleja na pia naomba nimpongeze Katibu Mkuu wa Wizara hiyo pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa kuandaa Bajeti hii nzuri.

Mheshimiwa Spika, Wilayani kwangu Nanyumbu ni giza tupu, Wilaya haina nishati ya umeme. Hivyo kukosekana kwa nishati hii kunadumaza maendeleo. Itakuwa ni mzaha kuhimiza maendeleo Wilayani kama umeme Wilayani haupo.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 imeelekeza kuongeza kasi ya kupeleka umeme vijiji kuitia mfuko wa nishati vijiji. Hivyo naiomba Wizara ya Nishati na Madini ifanye juhud za makusudi kupeleka nishati ya umeme Wilayani Nanyumbu.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini ukurasa wa 46 inaeleza juu ya mikakati ya Wizara kupeleka umeme makao makuu ya Wilaya. Miji mikuu ya Wilaya hizo ni pamoja na Wilaya yangu ya Nanyumbu. Hata hivyo hotuba ya Waziri haikutanabaisha kwa undani zaidi juu ya mpango huo, hivyo namwomba Waziri awaeleze wananchi wa Nanyumbu wategemee lini kuupata umeme huo? Naoimba Wizara kuitia wakala wa nishati vijiji na hasa mfuko wa nishati vijiji tupatiwe nasi ruzuku ili tupate umeme. Aidha, mfuko wa *MCC* au *JICA* vinaweza kufadhili uletwaji wa umeme Wilayani Nanyumbu.

Mheshimiwa Spika, Wilayani Nanyumbu kuna baadhi ya maeneo yana madini na vijana walikuwa wanajitafutia riziki kama wachimbaji wadogo wadogo. Hata hivyo vijana hao wamesitishwa uchimbaji kwa maelezo kwamba wanachimba ndani ya hifadhi ya msitu wa uwindaji wa Lukwika. Hivi ni nani ananufaika na madini hayo? Naomba Wizara itoe maelekezo au wananaufaika kwenye Hifadhi hiyo?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. LUCAS L. SELELII: Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja ya Wizara hii kwa sababu nimesubiri kwa hamu ahadi ya kupata umeme toka Nzega – Puge – Ndala. Ahadi hii imekuwa tangu mwaka 2003/2004 katika taarifa ya ziara na Rais Mstaafu Mheshimiwa Benjamin Mkapa. Ahadi ya Rais mwenyewe na Ilani ya Uchaguzi. Ahadi yako mwenyewe, kumbuka ziara ulioifanya ulipokuwa Naibu Waziri katika maeneo ya Ndala na Bukene, Bajeti ya mwaka 2006/2007 na mwaka 2007/2008 tuliamiwi tusubiri hadi Bajeti hii ya mwaka 2008/2009 subiri, subira, imetosha tunataka umeme Puge/Ndaga mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, upandaji wa bei ya umeme mara kwa mara hasa kutokana na kipengele cha *capacity charges* ambayo ipo hadi kwa mlaji (*bill*). Toeni kipengele hicho katika makampuni ya jenereta *IPTL/SONGAS/APGUM* na kadhalika. Huyu Mtanzania anayelipia *capacity charges* za makampuni ambayo mikataba yao ina utata ni dhuluma. Ondoa kipengele cha *capacity charges* kwenye makampuni yote.

Mheshimiwa Spika, kuhusu gharama ya kuunganisha umeme toka nguzo hadi nyumbani ni kubwa kuliko uwezo wa wananchi, ipunguzwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kupata majibu ya kuniridhisha hasa juu ya umeme wa Nzega – Puge - Ndala upatikane mwaka 2008/2009 la sivyo katika vifungu shilingi ya Waziri naitoa kwa kutumia kifungu 103(2).

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja.

MHE. MGENI JADI KADIKA: Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kunipa afya njema na kuniwezesha kuchangia hotuba hii kwa maandishi. Napenda kumpongeza Waziri na Naibu wake pamoja na wote walioshiriki katika kuandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, umeme ni kitu ambacho kinaleta maendeleo katika nchi yoyote duniani, nchi ambayo haina umeme haina maendeleo wala haileti maisha bora kwa wananchi wake na uchumi unasua sua.

Mheshimiwa Spika, bila umeme hakuna elimu, afya, viwanda, maji na kazi za ofisi. Kwa kweli nyanja zote hizi zinahitaji umeme. Kwa kweli ni jambo la kusikitisha kuwa wananchi walio vijijiini asilimia 80 bado wako kizani. Kuna uchumi mkubwa lakini wako nyuma kwa ukosefu wa umeme, kuna mifugo mingi lakini hakuna viwanda vyta kusagisha nyama, hakuna viwanda vyta maziwa, kuna samaki wengi lakini hawana viwanda vyta samaki na mengi mengineo. Shule wanafunzi hawapati kusoma kwa sababu hakuna maabara, je, ni lini umeme utazalishwa angalau mikoa ya Tanzania ifikie asilimia 50?

Naipongeza Serikali kwa kufuta mkataba wa *Dowans*. Madini ni mali yetu lakini hatufaidiki na madini yetu zaidi wanaofaidika ni wageni. Serikali itunge sera ili wazalendo wa nchi hii na wao wafaidike.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo wadogo nao watengewe eneo na wao wajipatie maisha bora na kukuza uchumi wa nchi yao. Kuliko kuwapa wachimbaji wakubwa ambao pato kubwa hupeleka kwao na kuikosesha nchi hii faida kubwa ya madini yao.

Mheshimiwa Spika, nawatakia kila la kheri Waziri na Naibu Waziri na Mwenyezi Mungu awape maisha marefu na waongoze nchi hii kwa usalama na awaepushe na balaa, *Amini*.

MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA: Mheshimiwa Spika, nampa Mheshimiwa Waziri kwa hotuba zuri. Umeme wa Zambia kwenda Sumbawanga umepitia Jimbo la Kalambo, umeme huu ni wa wasiwasi, naomba tupate umeme katika vijiji vya Matai, Kasanga, Kasesya, Sopa, Msanzi, Katuka na vijiji vinavyopitiwa na umeme huo.

Mheshimiwa Spika, naomba basi umeme wa majaribio wa umeme nuru utekelezwe ili vijiji nilivyovitaja uweze kukamilika kama *alternative source*.

Kuhusu uchimbaji wa makaa ya mawe wa Rukwa eneo la Namwele unafanywa na kampuni binafsi ya *Upendo Group*. Nia ya mradi huu pamoja na kuuza mkaa kiwanda cha Sementi Mbeya ni kuzalisha umeme ili kuongeza uwezo wa umeme Mkoa wa Rukwa. Waziri hukulisema hili inashangaza kama huna taarifa na takwimu za mradi huu.

Mheshimiwa Spika, madini ya vito na dhahabu mkoani Rukwa havijatiliwa maanani ili uchumi wa mkoa na nchi uweze kuongezeka. Lipo tatizo la kuhodhi maeneo ya madini na wajanja wachache hili ni kosa. Yapo madini ya *Zinc mwambao* wote wa Ziwa Tanganyika hakuna uwezekano wa kuyachimba kwa sababu hakuna umeme hakuna barabara, reli na mtaji.

Mheshimiwa Spika, yapo madini ya *phosphates* eneo la Karema madini haya yangeongeza ubora wa kilimo lakini Wizara iko kimya kabisa hivi tutajikoa lini tuwekeze katika madini haya?

Mwisho nataka maelezo umeme katika Jimbo la Kalambo. Uchimbaji Madini ya Mkaa wa mawe Namwele, *Zinc na phosphates*.

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Waziri na Naibu Waziri kwa hotuba mzuri na kwa kazi nzuri iliyofanyika toka wateuliwe. Nawashukuru sana *TANESCO* kwa kuwa leo nimepewa taarifa kuwa jenereta kutoka Lindi zimeingia Tunduru leo.

Ufumbuzi wa kudumu kwa tatizo la umeme Mji/Wilaya ya Tunduru ni aidha, kuunganishwa na gridi ya Taifa au kuunganishwa gridi ya umeme ya Kusini inayomilikiwa na kampuni ya *ARTUMAS* au kuendelea kuwashawishi *Kanyan Capital* kujenga *min-hydro power plant* mto wa Muhuwesi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashauri yafuatayo, kwanza kwa kuzingatia hali ya Kijiografia na mtawanyiko wa vijiji na idadi ya watu, nashauri fikra zielekezwe zaidi kuiunganisha Tunduru kwa gridi ya Kusini (*ARTUMAS*) umbali kutoka Masasi hadi Mangaka (Makao Makuu ya Wilaya ya Nanyumbu) ni kilometra 54, Mangaka – Tunduru ni kilometra 139. Lakini umbali huo una mlolongo wa vijiji vikubwa sana zaidi ya 20 ambavyo vitahitaji umeme mwingi. Lakini umbali toka Namtumbo hadi Tunduru ni kilometra 202, pia sehemu kubwa ni pori na vijiji vikubwa ni takriban 10.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa umeme wa *ARTUMAS* tayari upo wakati ule wa gridi ya Taifa bado hata Songea haujafika hali hiyo inatoa unafuu zaidi kwa Tunduma kuunganishwa na Grid ya Kusini. Hata hivyo bado *min-hydro power plant* miradi unaotarajia kufanywa na *Kayan Capital* ni mradi mzuri kwetu endapo utaungwa mkono na Serikali.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

MHE. JUMA ABDALLAH NJWAYO: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa William Ngeleja na Naibu wake Mheshimiwa Adam Malima, pia watendaji wote wa Wizara ya Nishati na Madini kwa changamoto wanazokutana nazo na hatua wanazochukua kukabiliana na changamoto hizo.

Mchango wangu ni kama ifuatavyo, nasikitika sana na ucheleweshwaji wa *Power Plant* ya Somanga – Funga. Hivi tatizo ni nini? Kwa nini mradi huu haukamiliki? Ningependa kupata maelezo ya kina kwa nini hatua za dhafi zisichukuliwe haraka ili wananchi wa Wilaya za Kilwa, Rufiji na kadhalika wanaondokana na umeme usio wa uhakika wa kutumia jenereta zilizochoka.

Mheshimiwa Spika, Wilaya za Tandahimba, Newala, Masasi, Mtwara vijijini hukosa maji kwa kutokuwa na jenereta nzima. Ikumbukwe maji ndio uhai wa binadamu. Ombi langu ni kuwa hatua za dharura zichukuliwe wakati huu tunaposubiri mradi wa gesi asilia wa *Mnazibay* ili zipelekwe jenereta za kuokoa hali ya tatizo la maji.

Mheshimiwa Spika, ipo tabia imejitokeza sasa kwa wauzaji wa mitungi ya gesi (motopoa) kutotoa risiti kwa mauzo ya mitungi hiyo. Huu ni ujanja wa kuikosesha Serikali mapato. Wizara hii lazima iandae mkakati wa kudhibiti ujanja wa wauza mitungi ya gesi.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali ione uwezekano wa *TANESCO* kuweka *luku* kwa watumiaji wote wa umeme nchini. Hii itapunguza malalamiko ya wizi wa umeme unaofanywa na baadhi ya wafanyakazi wasio waaminifu pia itapunguza gharama za ajira ya wasoma mita na bugudha za wasoma mita kwa wateja wa umeme ikiwa ni pamoja na rushwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DR. WILBROD P. SLAA: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo, kwanza ni kuhusu Meremeta na *Tangold*.

Mheshimiwa Spika, kama Bunge hili lilivyoarifiwa mara kadhaa kuwa Meremeta ilikuwa mali ya Serikali ya Tanzania na ilipofilisika shughuli zake zilipokelewa na *Tangold Co. Ltd.* Leo katika hotuba nzima ya Waziri hakuna mahali wala sentensi hata moja inayozungumzia shughuli za *Tangold* wala manufaa yake kwa Taifa hili. Kwa

vyovyyote vile maelezo kuwa Meremeta na *Tangold* zinafanya kazi ya jeshi na hivyo shughuli zake haziwezi kujadiliwa hadharani si ukweli na wala si sahihi.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kuchimba dhahabu, kuuza dhahabu na mapato kuingizwa Serikalini au jeshini haiwezi kuwa lenyewe kuzuia Bunge kujadili wala la Meremeta na *Tangold*. Kamati ya Jaji Mark Bomani inasema; “haikupata maelezo ya kina na ya kuridhisha kuhusiana na uanzishwaji, umiliki na ufilisi wa kampuni ya Meremeta na hatimaye uanzishwaji wa Kampuni ya *Tangold* zilizosajiliwa nje ya nchi.” Hapa kwa kweli kama Bunge limehoji haikupata majibu, Kamati ya Rais haikupata majibu na inapendekeza uchunguzi wa kina ambaa utatumia tena fedha za Watanzania jambo ambalo sikubaliani nalo. Serikali imesema ni ya Serikali, haiwekani Serikali isiwe na majibu mpaka uchunguzi.

Mheshimiwa Spika, iwapo sitapata majibu ya kuridhisha nitaomba Bunge liunde Kamati Teule kujua ukweli wa jambo hili. Ikumbuwe *BOT* ililipa shilingi bilioni 155 kulipa madeni ya Meremeta wakati Meremeta ni mali ya Serikali kwa asilimia 50 tu! Pia Mheshimiwa Waziri ni lazima alieleze Bunge hili kwa nini Serikali imedanganya Bunge kuwa Meremeta ni mali ya Serikali, wakati nyaraka *Brela* na sasa Kamati Teule ya Jaji Mark Bomani imethibitisha kuwa Serikali imekuwa ikimiliki asilimia 50 tu.

Mheshimiwa Spika, baada ya mgodi wa Buhemba kufungwa, Serikali inatoa kauli gani kuhusu wafayakazi 127 wanaodai shilingi milioni 282? Haiwezekani Serikali iwashdulumu watu wake wakati imelipa watu wasiojulikana kupitia *NEDBANK* ya Afrika Kusini. Waziri atupe mkakati na ratiba iliyowazi kuwalipa watumishi hao.

Mheshimiwa Spika, wakati anahitimisha hoja yake, kuhusu ubinafsishaji wa *Kiwira Coal Mines Ltd* kuwa Kampuni ya *Tanpower Resources Ltd*. alisema Waziri wa Nishati na Madini atatolea maelezo ya kina suala hili. Kwa mshangao mkubwa hotuba ya Waziri nayo haisemi chochote kuhusu kampuni hii. Hii ni pamoja na Kamati Teule ya Jaji Mark Bomani ukurasa wa 119 kusema kuwa Serikali ichukue hatua za haraka kuchunguza uhalali wa taratibu zilizotumika za kubinafisha mgodi huo, malalamiko ya wafanyakazi ya kupunjwa mafao yao na uchaguzi wa Mto Kiwira, Serikali ichunguze uhalali wa matumizi ya shilingi bilioni 13 kwa ajili ya kukarabati mgodi na uzalishaji na Serikali ichunguze madai ya uuzzwaji wa mali za mgodi na utekelezaji wa masharti ya ubia.

Mheshimiwa Spika, haya ndiyo yaliyotufanya ubinafishaji huu toka mwanzo. Hivyo sikubaliani na hoja ya uchunguzi wa kina ambayo dhahiri itakuwa matumizi mabaya ya fedha za umma, labda tu kama tunaanzisha uchunguzi wa kuficha ukweli. Mambo yafuatayo yako wazi, aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini kwenye Bunge la Bajeti mwala 2004/2005 Mheshimiwa Daniel Yona alitoa taarifa kwa Bunge kuhusu hali ya Mgodi wa Kiwira (*Hansard*).

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi alieleza kuwa mitambo ya Kiwira imechakaa/imechoka; alikuwa anatafutwa mbia toka China; jitihada hizo hazikuzaa matunda na kuwa *PSRC* imefunga milango kwa wawekezaji wengine kwa hali hii ni

dhahiri kuwa Waziri Daniel Yona alikuwa na alitumia *inside information* ambayo alitumia kufanikisha malengo yale na ya Mheshimiwa Benjamin Mkapa kujiuzia hisa 70% na baadaye kufikia 85% ya hisa za Kiwira.

Mheshimiwa Spika, *Anbem* ya Mheshimiwa Benjamin Mkapa imeshiriki kikamilifu katika mjadala wa kununua hisa za Kiwira japo baadaye walirudisha hisa 200 kwa *Tanpower Resources Ltd.* Kampuni ya *Tanpower Resources* imesajiliwa tarehe 29 Desemba, 2004 na Rais Benjamin Mkapa alikuwa mwanahisa kupitia Kampuni ya *Anbem* ilioanzishwa naye na familia yake mwaka 1999.

Mheshimiwa Spika, cha kushangaza, majadiliano na mchakato wa *Tanpower Resources Ltd.* kuchukua asilimia 70 ulianza tarehe 15 Desemba, 2004, yaani wiki mbili hata kabla ya *Tanpower Resources Ltd.* kuandikishwa rasmi *Brela* (nyaraka ninazo).

Mheshimiwa Spika, cha kutisha zaidi, mwaka 2005 wakati Mheshimiwa Daniel Yona na Mheshimiwa Benjamin Mkapa na Kampuni zao wakijua fika kuwa wanununa hiso hisa wakiwa na dhamana ya kulinda mali na raslimali za Taifa, kampuni ya *Tanpower* ikaingia makubaliano na Serikali yaani “Yona raia anaingia mkataba na Yona Waziri! Haya ni maajabu.

Mheshimiwa Spika, sheria ya maadili ya umma ya mwaka 1995 (*RE*) vifungu vya 12 na 12(a) viko wazi kabisa. Suala la *inside information trading* nayo iko dhahiri, kwa vile Mheshimiwa Daniel Yona mwenyewe ndiye aliyekuwa anaandikiwa kama Waziri na Kampuni yake ya *Tanpower* naye kujibu kama Waziri. Hivyo basi, Waziri alieleze Bunge lako Tukufu lini Serikali itachukua hatua dhidi ya wahusika. Si suala la uchunguzi, *records* zote ziko Serikalini, sheria ilivunjwa inajulikana, Waziri anatoa kauli gani kuhusu mkataba uliosainiwa kati ya *Tanpower Resources Ltd.* na *TANESCO*? Je, *capacity charge* itakayolipwa na Watanzania ina manufaa gani kwa wananchi wanaotumia umeme; kwa uchumi wa nchi?

Mheshimiwa Spika, kwa vile inaonekana dhahiri mkataba huo una dosari zile zile za *IPTL, Richmond/Dowans* Serikali itavunja lini mkataba huo ili usiathiri wananchi wetu ambao tayari wameelemewa na gharama kubwa za umeme?

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja, labda nkipata maelezo ya kina na hatua za dhati za Serikali kuhusu mambo hayo hapo juu, na ikiwa lazima kwa yote mawili nitaomba Bunge liunde Kamati Teule.

MHE. JUMA SAID OMAR: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya na hivyo kushiriki kikao cha leo.

Mheshimiwa Spika, madini ni sekta muhimu sana ambayo ikisimamiwa vizuri inaweza kuchangia asilimia kubwa kuliko ilivyo hivi sasa katika Pato la Taifa na hivyo kusaidia kukuwa kwa uchumi wetu. Sekta ya madini haijachangia vya kutoka katika Pato la Taifa. Kutowajibika kikamilifu, kwa baadhi ya watendaji wa sekta ya madini pia kunachangia kapatikana kwa mapato yasiyotosheleza.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya Taifa letu yanategemea sana kupatikana kwa umeme wa kutosha mijini na vijijini jambo ambalo hadi hivi sasa bado halijafikiriwa. Tunahitaji viwanda kwa usindikaji wa mazao mbalimbali yakiwemo ya wakulima na yale ya baharini. Bila ya umeme wa kutosha viwanda haviwezi kujengwa. Wawekezaji wa ndani na wa nje hawawezi kuelekeza katika ujenzi wa viwanda ikiwa hapana umeme wa kutosha na wa kuaminika. Serikali ina mkakati gani wa makusudi utakaohakikisha kwamba umeme wa kutosha unapatikana nchi nzima mjini na vijijini?

Mheshimiwa Spika, umeme ni muhimu katika maeneo mbalimbali yakiwemo katika shule, hospitali, wafanyabiahsara wakubwa na wadogo walioko mijini na vijijini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa kupatikana kwa umeme katika nchi bado ni tatizo lakini pia gharama za kuufikisha umeme majumbani ni kubwa mno kiasi kwamba wananchi wengi katika hayo maeneo ambayo tayari umeme umeshafika wanashindwa kuugharimia. Hivyo ni vema Serikali ikalionna tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, mafuta ni nishati nyingine muhimu kwa maisha ya kila siku kwa kila Mtanzania na wengine na katika suala zima la maendeleo ya nchi yetu. Mafuta yanatumika katika shughuli zote za usafiri ikiwa ni pamoja na nchi kavu, angani na majini. Bila ya mafuta usafiri wa aina yoyote hauwezi kufanyika na hivyo kusababisha kudumaa kwa maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, bei za mafuta zinapanda bila ya mpangilio maalum na sasa imekuwa kero kubwa kwa wananchi hasa wale wenye kipato cha chini. Usafiri wa wananchi pamoja na usafirishaji wa mazao mbalimbali ya wakulima pamoja na bidhaa nyingine umekuwa mgumu na wenye gharma kubwa. Serikali inasema nini kuhusu kupanda mara kwa mara kwa bei ya mafuta?

MHE. PAUL P. KIMITI: Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa jinsi unavyendesha kikao hiki. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu akisaidiwa na watendaji wake wakuu na watumishi wote kwa maandalizi mazuri ya hoja hii. Mheshimiwa Waziri ameanza vizuri na naunga mkono hoja yake hii.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri anipatie maelezo katika maeneo yafuatayo, pamoja na kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuwashakikishia wana Sumbawanga kuwa umeme Sumbawanga utakuwa historia mwishoni mwa mwaka 2008, naomba tuthibitishie kama kitu gani kimekubalika na majirani zetu Zambia kuwa watakuwa hawatuleti tatizo lingine. Wakati tunasubiri hadi Desemba, je ahadi za kupatiwa jenereta ni lini zinakuja kutupunguzia adha hii.

Pia mfuko wa nishati vijijini umesua sua sasa ni mwaka wa tatu, bila chochote kile kufanyika. Je, tatizo ni lipi ambalo Waziri anadhani limetufikisha huko na kwamba hilo hilo lisiwe tena mtego wa kushindwa kuanzisha mfuko wa kuwaendeleza wachimbaji wadogo wa madini. Mheshimiwa Waziri asikubali kuchelewesha maamuzi ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, namwomba pia Mheshimiwa Waziri afuatilie upatikanaji wa ramani ya madini kwa nchi nzima, naelewa kuwa kwa sasa ramani inayotumika ni ile ilioandaliwa na Warusi miaka 50 iliyopita. Huu ni wakati muafaka kwa taasisi zako zikiwemo *STAMICO* kwa kutumia Chuo cha Madini waende nchi nzima kufuatilia *maping* upya, yenye madni na viwango vilivyomo kwenye maeneo hayo. Vifaa vyta kisasa viro inaweza kutupatia ukweli wa nini tulichonacho ardhini. Ningombwa wataalamu waangalie kama kweli eneo la Sumbawanga lina madini ya *Burma Ruby* na *Emmarald* ili wachimbaji wadogo wasiendelee kupoteza nguvu zao.

Mheshimiwa Spika, kutokana na gharama kubwa ya umeme na hasa matumizi yake, nashauri mambo mawili, kwanza ufanyike msako mkali kuona wezi wa umeme katika maeneo ambayo yana majengo makubwa lakini nalipa kidogo na pili, Serikali inanze maandalizi ya kuwataka waletao *bulbs* hapa nchini waingize zile ambazo hazitumii umeme mwingu (*energy server*). Hili lianzesha mapema ili zile *bulbs* za zamani zilizomo nchini zianze kupungua pole pole.

Mheshimiwa Spika, mwisho Mheshimiwa Waziri anaelewa kuwa *IPTL* kwa muda mrefu imekuwa kibambikiza madai makubwa kwa *TANESCO* na kutuongezea mzigo wa gharama bure. Naelewa pia kuwa sasa kuna kesi mahakamani ya ugomvi huo huo kati ya *IPTL* na *VIP engineering*. Je, ni kwani nini mpaka sasa Serikali imeshindwa kufikia uamuza wa kuinunua *IPTL* kama maamuza ya nyuma yaliyokwishaalezwa humu Bungeni na kwa nia ya kuongeza usimamizi wetu wenyewe wa *IPTL*, juu ya *capital charges*.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ameanza vizuri, ushauri unaletwa kwako na Waheshimiwa Wabunge kwa kuwa wanakuamini, tumia nafasi hii kujipanga namna ya kutekeleza maombi yao awamu kwa awamu. Naelewa kuwa uwezo wa kutekeleza hayo yote yanayoombwa, yatategemea uwezo wa Serikali kuiwezesha *TANESCO* kuyafanya hayo yote, hata wawekezaji wapya wakiingia, bado Serikali itahusika kubeba mzigo mkubwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba niipongeze kwa dhati Kamati Teule ya Madini ilioongozwala na Mheshimiwa Jaji Mark Bomani kwa kazi nzuri walivofanya kwa manufaa ya nchi hii. Tuifanyie kazi taarifa hii ili iwe ni faraja kwa maisha ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JUMA H. KILLIMBA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri mwenye dhamana na Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa William Ngeleja, Naibu Waziri Mheshimiwa Adam Kighoma Malima, Katibu Mkuu wa Wizara na watumishi wote wa Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni nyeti sana hasa kutokana na majukumu iliyonayo, hivyo ni muhimu tunapojadili Wizara hii ni dhahiri tunajadili masuala muhimu ya maslahi ya nchi, kisiasa, Kijamii na uchumi.

Mheshimiwa Spika, moja ya raslimali ya kujivunia kutoka wa Mungu ni raslimali ya madini, raslimali hii, tumebahatika nchini mwetu kwa kuwa na maeneo mbalimbali yenye madini ya aina tofauti ya thamani mbalimbali, tunayo dhahabu, almasi, *Ruby*, *Tanzanite*, *Green jemaline*, *Nilcon* na kadhalika. Huu ni utafiti usiohitaji gharama yoyote mbali na ile ya uchimbaji na utayarishaji wake.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa ili upate madini niliyoyataja vinahitajika vitu kadhaa katika kufanikisha, inahitajika teknolojia, mtaji mbali ya upatikanaji wake ambapo kwa kiwango kikubwa ardhi ndiyo inayohusika kutunza madini haya.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kuona kwamba ni jinsi gani raslimali hii muhimu inavyotumika na kapatikana kwa kasi bila uhakika wa uzao wa faida kwa nchi yetu. Hebu tujiulize hivi baada ya miaka hamsini ijayo Tanzania itakuwa bado inayo dhahabu ya kutosha kama iliyvo kule *North Mara*, Buzwagi, Bulyanhulu, Geita, Lusu (Nzega) na kadhalika *Tanzanite* ya kule Mererani na madini ya aina zote, ni dhahiri katika miaka hiyo, madini yatakuwa yametoweka na je, hali yetu ya maendeleo itakuwa vipi kutokana na pato (faida) iliyotokana na raslimali hii tuliyopokea kutoka kwa Mungu? Nadhani tutakuwa tumefukarishwa kwa mara nyingine na huu ukoloni mamboleo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umaskini wetu tulionao wa kuwa na *capacity* ndogo kuhusiana na mtaji na hata teknolojia lakini sasa yatupasa kusimama imara na hatuna sababu ya kuendelea, kulia eti sisi ni maskini ni umaskini upi wakati raslimali tunaiachia kwenda kwa wajanja ughaibuni ni dhambi kubwa kuendelea kuomba kwa Mwenyezi Mungu kuondolewa umaskini tuonao, inasikitisha kuona hali ya utumwa kupitia raslimali yetu unaendelezwa kama ule walitumikishwa mababu zetu na kudhalilishwa ndani ya ardhi yao na hata kuuza kwenye soko la utumwa ilhali wao ni wanadamu wanaostahili heshima sawa na binadamu wengine.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili naomba katika zama hizi jambo la faraja kama tutasema sasa basi tumbaki na dhahabu/madini yetu. Kusema huko iwe ni kwa kuihuisha mikataba yote inayohusu sekta hii ya madini kama ambavyo Mtukufu Rais alivyochukua jukumu la kuunda tume ya kuishauri serikali kuhusu usimamizi wa Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Spika, naomba mapendekezo yote ya Tume yafanyiwe kazi mara moja ili kuokoa kile kidogo tulichobaki nacho.

Kuhusu sekta ya umeme, nafahamu sekta hii ndogo ya umeme tayari sasa imeshahusisha *private sector*, kwa kuwa ni dhahiri tumejifunza kutokana na matukio mbalimbali kuhusu sekta binafsi utendaji wake ulilingia dosari katika siku za hivi karibuni hasa kutokana na ubovu wa utekelezaji wa mikataba. Hili ni jambo la faraja kama tutafanya kwa uhakika katika kuhakikisha tunazikwepa mbinu zozote zile zenyenye kutaka

kuififisha sekta hii ya umeme. Wizara ihakikishe inasimamia kikamilifu juu ya kuona wale wote wenye nia ya kuwekeza katika sekta hii basi wawe na sifa zote zile zinazoweza kuhakikisha nishati hii muhimu inamfikia kila Mtanzania ili kuendana na hali ya sasa ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii nimkumbushe Mheshimiwa Waziri juu ya miradi ya jimbo langu la Iramba Magharibi, ule mradi wa kijiji cha Mgongo (kituo cha Afya), kijiji cha Kitusha, kijiji cha Simbalungwala, Kijiji cha Kibigit na vijiji vyote vile vilivyopo jimboni kwangu vinavyopitiwa na umeme uliopozwa naomba vipatiwe umeme kwani ni gharama ndogo sana katika kuwapatia umeme.

Mheshimiwa Spika, nasikitika kwa kiwango cha Bajeti ya fedha ya Wizara hii kushuka mwaka hadi mwaka, mwaka 2006 Wizara ilitengewa shilingi bilioni 465, mwaka 2007 shilingi bilioni 353 sawa na upungufu wa shilingi bilioni 111, na mwaka 2008 shilingi bilioni 362, ongezeko la shilingi bilioni 9 ya mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, thamani ya fedha inashuka ongezeko la mahitaji kupitia Wizara hii umekua mwaka hadi mwaka. Naiomba Serikali kuona umuhimu wa kutenga fedha zaidi ili kuizidishia ufanisi Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. AMEIR ALI AMEIR: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na uzima na kuniwezesha kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, nimpungeze Mheshimiwa Waziri kwa jinsi alivyoiwasilisha hotuba yake kwa ustadi kabisa. Pia nimpungeze Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wake kwa ushirikiano wanaompa Mheshimiwa Waziri pamoja na kuandaa hutuba hii nzuri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uzuri wa hotuba hii nimeona nichangie kidogo umeme wa Zanzibar. Suala la umeme ni la Muungano lakini Zanzibar ni sehemu ya Muungano na wananchi wanaoishi Zanzibar ni wananchi wa Tanzania. Leo iweje Watanzania wanaoishi Zanzibar wapate ongezeko wa asilimia 168% kulipa umeme na Watanzania wanaoishi Bara walipe 21.7%?

Mheshimiwa Spika, kutokana na ongezeko hili tunawaambia nini ndugu zetu wa Zanzibar, hawana haki ya kutumia umeme huu? Kwa sababu kutokana na kupanda kwa bei mwananchi aliyekuwa analipa shilingi 5000/= kwa mwezi sasa itabidi alipe si zaidi ya Shilingi 17,000/=, kwa hali yoyote atashindwa kuutumia umeme.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri aniambie VIPI atawasaida ndugu zake wa Zanzibar na kipi kimesababisha upandaji huu, na nini kimekusudiwa kwa Watanzania wanaoishi Zanzibar?

Mheshimiwa Spika, naoimba Serikali kuptitia kwa Waziri warudishe bei hii iwe sawa na Watanzania wanaoishi Bara ukizingatia hawa wote ni Watanzania.

Mheshimiwa Spika, bei ya petroli wananchi tunawaambia Serikali haina uwezo wa kumiliki, kwa sababu bei inapangwa na wanaozalisha je, umeme unaozalishwa Tanzania Bara tutaambiwa viyi Watanzania wanaoishi Visiwani Zanzibar? Suala hili la umeme wa Zanzibar lisiangaliwe kwa utani, ni lazima liangaliwe kwa umakini. Kwa sababu wengine wanachekelea hali hiyo ingawa nao wamo wanaumia, lakini sasa imekuwa ndiyo ajenda kwenye majukwaa.

Mheshimiwa Spika, wazee wa zamani walisema tahadhari kabla ya hatari, kwa hiyo, naiomba tena na tena Serikali kurudisha bei ya umeme Zanzibar hili linawezekana liko ndani ya uwezo wetu.

Mheshimiwa Spika, udumu Muungano, idumu Tanzania, udumu udugu wetu na mashirikiano yetu. Mungu ibariki Tanzania na watu wake.

MHE. JOEL N. BENDERA: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpungeza Mheshimiwa William Ngeleja, Waziri wa Nishati na Madini na Mheshimiwa Adam Malima, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na wataalam wa Wizara hii kwa kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii hasa katika kipindi hiki kigumu cha misukosuko. Aidha, napongeza sana hotuba ya Wizara hii.

Mambo muhimu ninayotaka kuishauri Wizara hii, kwanza ni kuhusu *TANESCO* – sekta ya umeme. Tatizo lililopo sasa la wananchi kushindwa kuwekewa umeme kwenye nyumba zao kwa visingizio vya *service charges* na kukosa mita. Ni jambo la kusikitisha sana kwamba jimboni kwangu kero ya wananchi kucheleweshwa kuwekewa umeme imekithiri. Jimboni kwangu kuna zaidi ya wananchi 50 hadi leo hawajawekewa umeme licha ya kulipa kila kitu kwa visingizio vya mita na nguzo na kadhalika. Nashauru jambo hili litafutiwe ufumbuzi wa kudumu. Korogwe sasa wananchi wengi wamepoteza imani na *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, ni muda mrefu vijiji vifuatavyo vimeahidiwa umeme lakini ni zaidi ya miaka 10 sasa havijapata umeme. Vijiji hivyo ni Kwameta, Rwengeri Darajani, Kilole, Mzee, Bagamoyo na Kwasemangube. Kwa hiyo, vijiji vyote nilivyotaja umeme unapita juu au upo kilometa moja toka kijiji kilipo. Kijiji cha Kwameta na Kwasemangube 70% ya nyumba za wananchi zimekwishafanyiwa *wiring*. Naomba sana vijiji hivyo sasa vipatiwe umeme. Vijiji vingi nilivyovitaja vinahitaji *transforma* tu. Nasisitiza vijiji hivi sasa vipatiwe umeme hasa tukianzia na Kwameta.

Mheshimiwa Spika, Jimbo langu la Korogwe Mjini lina sekondari nane, baadhi ni Ngombezi sekondari, *Old Korogwe* Sekondari, Kwirole Sekondari, Chifu Kimeri Sekondari, Kwamdelwa Sekondari na Kwamsisi Sekondari.

Mheshimiwa Spika, sekondari hizi zote hazina umeme. Chakusikitisha ni kwamba sekondari zote hizi umeme upo mita 50 hadi kilometra moja tu jambo ambalo halihitaji fedha nyingi. Kinachohitajika ni nguzo chache na *transforma* tu.

Naomba sana Wizara iwe na mkakati maalum wa kununua *transforma* ili umeme upelekwe kwenye maeneo yetu. Katika dunia ya leo shule hizi za sekondari zinahitaji sana umeme. Naomba sana shule zangu hizo zipatiwe umeme. Bei ya kuwekewa umeme ni kubwa sana. Wananchi wanashindwa kwa sababu gharama ni kubwa sana napendekeza na kushauri *TANESCO* itafute njia ya kupunguza gharama hizo. Mimi naamini wananchi wengi wanapata fursa ya kuweka umeme ndani ya nyumba zao *TANESCO* watapata mapato mengi zaidi, hebu tutazameni upya gharama za kuweka umeme.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kusambaza umeme mji wa Korogwe, naomba nitoe masikitiko yangu makubwa sana kwa hali mbaya iliyopo mjini Korogwe ya kusambaza umeme. Mji wa Korogwe unawakazi wapatao 54,000. Ni mji unaokuwa sana lakini maeneo mengi hayana umeme. Maeneo hayo ni Mtonga, mtaa wa Msambiazi juu, mtaa wa Zungwati, mtaa wa Kwasemangube, mtaa wa Kwamkole, mtaa wa Kwamzololo, mtaa wa Bagamoyo, mtaa wa Kambi ya Maziwa na mtaa wa Majengo. Nyumba nyingi zimekwishafanya *wiring* kwani tatizo ni *TANESCO* kwa kukosa nguvu na vifaa muhimu vinavyohitajika kuingiza umeme.

Naomba Waziri anapohitimisha hoja yake anitafutie jibu la kwa nini Korogwe umeme unakatika katika mara kwa mara?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

MHE. OMARI S. KWAANGW': Mheshimiwa Spika, hii ndio hoja yangu pekee katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 hadi 2010 kwa sababu ndiyo ambalo limesemewa katika mitaa na vijiji kwa pamoja vipatavyo 48 katika hoja ya usambazaji wa umeme katika kukuza mji mpya wa Mkoa wa Manyara – Babati.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maombi ya wananchi hao wa Babati Mjini katika hotuba yangu ya kwanza Bungeni niliisemea, pia nimewasiliana kwa kiwango kikubwa na Wizara yako na *TANESCO* na mara zote pamoja na swali langu namba 399 nipewa matumaini ambayo bado sijayapata.

Mheshimiwa Spika, kwa mara ya mwisho siku chache tuliwasiliana na Mheshimiwa Waziri na kunipa matumaini zaidi kwa kunipa pole kwa hili kutokutumia kwa muda sasa kwa kuniambia kuwa hoja ya Bajeti ya Wizara yake sasa itapata majibu ya hoja yangu. Nilipata matumaini ya kweli. Nimesoma hotuba mara mbili na majedwali yote na hasa jedwali namba 10 ambako nilitazamia kuona Babati katika fungu la kwanza la kuboresha miundombinu ikiwa pamoja na mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro na Arusha. Babati ni mji mpya wa Makao Makuu ya Manyara. Unahitaji kuendelezwa kutokana na idadi kubwa sasa ya watu kuhamia Babati.

Mheshimiwa Spika, pili nilitazamia pia kuwa katika mradi wa *ADB* ambapo Mkoa wa Arusha vijiji vyake kwa wingi vinaonekana tena kwa sababu mradi wa usambazaji wa Gridi – Babati ulifadhiliwa na *ADB - Electricity IV* kama sikosei.

Mheshimiwa Spika, kituo cha umeme wa Gridi cha Babati kina uwezo wa *Megawatt 32* na kinahudumia Babati, Kondoa, Mbulu, Karatu na Kiteto na nadhani matumizi yote hayazidi *Megawatt 5*. Hivyo umeme upo, tatizo ni usambazaji tu. Vinginevyo *substation* ile haitasaidia kukuza uchumi unaotegemewa kwenye maeneo haya ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, kulingana na maelezo ya *TANESCO*, usambazaji wa umeme kwenye maeneo hayo utagharimu shilingi milioni 440 (23.8.2007) kwa kupeleka umeme kilometa nane kwa njia ya kilovolti 0.4 na utaweza kuhudumia wateja 300 wa uhakika. Naomba tufungue mapato hayo kwa matumizi hayo.

Mheshimiwa Spika, nina imani na kauli ya Mheshimiwa Waziri kuwa Bajeti yake sasa itajibu hoja hii kikamilifu. Hivyo kwa kuwa sikuona mahali popote kwenye hotoba na majedwali yote ambapo Babati kama makao Makuu ya Mkoa mchanga imetajwa kwa vijiji husika, naomba basi unisaidie maelezo ili niondokane na hoja hii ambayo sasa ni kero na adha kubwa kwangu na kwa wananchi wa Babati Mjini.

Mheshimiwa Spika, maelezo haya marefu yanaonyesha uzito wa jambo hili kwangu. Naunga mkono hoja yake ili apate pia moyo na ujasiri wa kutatua shida hii.

Mheshimiwa Spika, namtakia Waziri, Naibu wake, watendaji na Mkurugenzi Mkuu wa *TANESCO* kila la kheri.

MHE. DR. SAMSON F. MPANDA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Wilaya ya Kilwa wanasononeka, wasomi tunao tena walio bobea lakini hawawekwi kwenye Bodi ya Nishati na hii inapelekea kutokamilika kwa mradi wa Somanga Funga. Kwa nini hadi leo hii tunapozungumza asilimia 10 zilizokuwa zikamilishwe kwa kipindi cha mwaka mzima bado hazijakamilika. Mheshimiwa Waziri akumbuke kuwa wananchi wa Kilwa ndio walinzi wakuu wa mazingira ya nishati hiyo. Pia suala la mrahaba linakuwa kitendawili kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2006 niliomba kupatiwa umeme kutoka Somanga Funga – Kituo cha (*MV6*)Somanga Funga kilichopo kata ya Kinjumbi majirani wa kata hiyo ni Miteja, Tingi, Mingumbi, Chumo na Kipatimu mbona haijawekewa fungu lolote?

Mheshimiwa Spika, mkandarasi *Shapria* ambaye anatakiwa kumaliza asilimia 10 ya mradi wa Somanga Funga anachukua muda mrefu na Waziri hajalionna hilo?

Mkandarasi huyu ametimuliwa na *Tanroad* kujenga barabara ya Tingi – Kipatimu. Mheshmiwa Waziri anangoja nini?

MHE. BENEDICT OLE NANGORO: Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Waziri na Naibu wake kwa taarifa na Bajeti nzuri. Sekta ya madini na sekta ya nishati ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi na watu wetu. Kwa sababu ya umuhimu mkubwa na changamoto zinazokabili sekta hizi mbili, kuna haja ya kutenganisha nishati na madini ili kila sekta ipate uangalizi na msukumo wa kutosha. Hivyo nishati isimame kama Wizara na madini isimame pia kama Wizara inayojitegemea.

Kuhusu madini, sera na sheria zinazotumika zijali na kuthamini sura ya fursa sawa kwa wote (*equal opportunity policy*). Hadi sasa upendeleo mkubwa umetolewa kwa watu wa nje (wageni) na ubaguzi dhidi ya wenyeji katika maeneo ya mikopo, misamaha ya kodi na hata hifadhi ya usalama wao na mali zao. Wachimbaji wote wa nje na ndani, wakubwa na wadogo wawe na waonekane sana mbele ya sheria. Kwa njia hii wote watashindana wakiwa katika uwanja sawa (*level playing field*).

Mheshimiwa Spika, kuhusu nishati, *TANESCO* ihimizwe kupunguza gharama za umeme kuwezesha walaji kumudu kulipia gharama za bidhaa hii muhimu. Katika huduma za umeme, Wilaya ya Kiteto ipo chini ya Mkoa wa Dodoma na hivyo inanufaika na programu ya *MCC*. Naomba vijiji vya Matui, Ngusero na Dosidosi ambavyo vinapaswa kunufaika na mpango wa *MCC* viwekwe kwenye ratiba ya mwaka 2008/2009, ni rahisi umeme kuvutwa kutoka Mrijo chini ama Zoisa Wilayani Kongwa.

MHE. PHILEMON NDESAMBURO: Mheshimiwa Spika, ununuzi wa umeme wa *Luku*, una utata mkubwa. Leo ukinunua umeme wa shilingi 10,000/= unapewa *unit 70* baada ya siku tano ukinunua tena umeme wa shilingi 10,000/= unapewa *unit 40* na hakuna hata wakati mmoja ununuzi wa shilingi 10,000/= utakuwa sawa. Yapo malalamiko mengi na wengi kufikia kusema *TANESCO* wanaiba. Kwa nini VAT na gharama nyingine zisiwekwe kwenye kila *unit*, ili kuondoa tatizo la bei tofauti tofauti kila unaponunua umeme?

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Kilimanjaro, kuna umeme umesambazwa kila mahali lakini umeme huu haufaidishi wakazi wa Kilimanjaro kwa kiwango kikubwa. Umeme ni dhaifu sana na wakati mwengine wala huwezi kuwasha *tube light*. Sababu ni kuwa hakuna *transforma* za kutosha. Tungeomba ziwekwe *transforma* za kutosha ili umeme wa kutosha upatikane. Kutokuwa na umeme wa kutosha, hata mita hazitembei na *TANESCO* inakosa mapato.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina aina nyingi za madini na hata mengine bado hayajagunduliwa yalipo. Kwa sasa mchango wa madini katika Pato la Taifa, ni kidogo sana na sio kweli kuwa haya madini hayaleti fedha bali tunaibiwa. Kabla hatujakuwa na uwezo wa kuziba hii mianya ya wizi ingekuwa faida kwa Taifa hili kutotoa vibali kwa uvumbuzi mpya na kuanza kuziba mianya ya wizi na kurekebisha mikataba tuliyio nayo

sasa. Pia *not to renew* mikataba ya sasa mpaka tujipange kwanza. Ni heri hayo madini yabaki huko ardhini kuliko yanavyoibwa kwa sasa. Kizazi kijacho kitakuja faidi.

MHE. FRED T. MPENDAZOE: Mheshimiwa Spika, mwaka 2007 Agosti, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Kikwete alizindua mradi wa *Mwadui Community Diamond Partnership (MCDP)* ambao unalenga kuwaendeleza wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, Wizara iahidi kuhamasishwa wachimbaji wadogo na wafanyabiashara wa almasi wa Mkoa wa Shinyanga kujiunga na kuanzisha *SACCOS* ili iwe rahisi kwao kunufaika na mradi wa *MCDP* baada ya uzinduzi, katika vikao mbalimbali wadau mbalimbali ikiwemo Serikali (Wizara ya Nishati na Madini) walikubaliana kwamba Serikali iongeze jitihada na mkakati wa kupata wabia (*partners*) wengine kutoka mashirika mbalimbali nje na ndani ya nchi watakaoshiriki katika utekelezaji wa miradi mbalimbali iliyokuwa imependekezwa kwenye *MCDP*.

Kwa kuwa wananchi katika vijiji nane vinavyozunguka mgodi wa Almasi wa Mwadui (*WDL*) wamehamasishwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu ilikishirikiana na Mgodi wa *WDL*. Naiomba Wizara iwaeleze wananchi je, Serikali imefikia hatua ipi katika kutafuta wabia (*partners*) wengine na ni wabia wangapi wako tayari kushiriki katika utekelezaji wa miradi ya *MCDP*.

Aidha, naiomba Serikali itoe *commitment* kwa wananchi wa vijiji vya Songwa, Buchambi, Bugarika, Masagara, Ufenini, Nyenze na Ng'wigumbi kwamba Serikali itaendelea na utekelezaji wa mradi wa *MCDP*.

Mheshimiwa Spika, nilishaiomba Serikali ipeleke huduma ya umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya ya Kishapu. Kwa sasa umeme uko kilometra tatu tu toka Makao Makuu ya Wilaya na gharama yake si zaidi ya shilingi milioni 70. Kufikisha umeme makao makuu kutainufaisha pia shule ya sekondari Kishapu pamoja na hospitali ya Wilaya inayojengwa.

Aidha, naiomba Serikali ifikishe umeme shule ya sekondari Kawawa, Mipa, Bubiki na Ng'wigumbe kwani umeme upo karibu sana na kufikishwa umeme kutaboresha elimu inayotolewa kwenye shule hizo.

MHE. KAIKA S. TELELE: Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Ngorongoro ilianzishwa mwaka 1979. Kwa takriban miaka 30 wilaya hiyo haina umeme wa gridi ya Taifa wala umeme wa jenereta. Mpango wa *TANESCO* wa kupatiwa Wilaya hiyo umeme ni hadi 2015. Lakini kwa mujibu wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005, ni kuwa ifikapo mwaka 2010 Makao Makuu ya Wilaya zote Tanzania Bara ziwe zimepata umeme.

Mheshimiwa Spika, lakini wananchi wa Ngorongoro walifarajika mno Mheshimiwa Rais alipowatembelea tarehe 20 Machi, 2007 na kuahidi wananchi wa Ngorongoro kuwa watapa umeme wa gridi ya Taifa lakini kabla ya umeme wa Gridi

aliagiza watu wa *TANESCO* kupeleka umeme wa jenereta kuanza wakati umeme wa Grid ukiandaliwa. Sasa ni zaidi ya mwaka na hakuna dalili ya umeme wowote kupatikana Loliondo ambayo ni Makao Makuu ya Wilaya ya Ngorongoro licha ya Mheshimiwa Mbunge (mimi Telele) kumuona na kumwandikia mara nyingi bila mafanikio. Pia nilifuatilia Wizarani na *TANESCO* Makao Makuu bila mafanikio.

Mheshimiwa Spika, imeelezwa katika hotuba yake ya Bajeti katika ukurasa 46 kuwa miji mikuu ya Wilaya za Ngorongoro, Kibondo, Nanyumbu na Nkasi inatafutiwa fedha kwa ajili ya kupeleka umeme katika Wilaya hizo. Je, ni kutoka washirika wapi wa maendeleo misaada na mikopo hiyo inatafutwa au ni kutoka katika vyanzo vyetu wenyewe? Ni lini fedha hizo zinatarajiwa kupatikana?

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Ngorongoro inahitaji umeme wa haraka kwa sababu zifuatazo, kwanza utalii ni mkubwa katika Wilaya ya Ngorongoro na kuingizia Taifa shilingi bilioni nne kwa mwaka, Ngorongoro ni Wilaya ya mpakani na Jamhuri ya Kenya ambapo mikutano ya ujirani mwema na biashara mbalimbali za mpakani zinafanyika, madini yanapatikana na hivyo hitaji la umeme linakuwa kubwa na kuwa maporomoko ya maji ya mto Pinyiny na ulikwishafanyika utafiti na wataalam wa *TANESCO* na kugundulika kuwa ule ungeweza kutosheleza mji wa Loliondo na Wasso.

Mheshimiwa Spika, pia *the Great North Road* Arusha – Musoma kupitia Ngaresero/Loliondo kwa kiwango cha lami itakapopita pale itachochea shughuli nyingi za kiuchumi na kwamba hitaji la umeme haikwezeki.

MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA: Mheshimiwa Spika, Jimboni kwangu Buyungu yapo madini aina ya Chokaa ambayo yanatumika kwa mambo mengi yakiwemo kutengeneza *POP* za hospitali, chaki, kusafishia ngozi, kujenga nyumba na kadhalika. Lakini sehemu kubwa ya madini hayo yapo katika hifadhi ya Moyowosi. Wizara yako itatusaidia kuhakikisha kwamba madini hayo yaendelezwe ili wananchi wajipatie Kipato?

Mheshimiwa Spika, nimefarijika kuona tangazo la zabuni ya kununua jenereta za umeme za Kigoma, Kasulu na Kibondo. Bado nina imani kwamba ufumbuzi wa kudumu ni miji hiyo ya Kigoma, Kasulu na Kibondo pamoja mji mdogo wa Kakonko kuunganishwa kwenye Grid ya Taifa.

Kwa mji mdogo wa Kakonko, naomba jenereta zinazoagizwa zikifika, basi utusaidie jenereta moja ya zamani ifungwe Kakonko wakati tunasubiri umeme wa gridi.

MHE. STEPHEN J. GALINOMA: Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza binafsi Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri Mheshimiwa Adam Malima, Katibu Mkuu, Kamisha na timu yao yote kwa kazi nzuri hadi sasa na Bajeti fasaha. Naunga mkono hoja.

Pili, naomba kusisitiza kile ambacho umebainisha kwamba yapo mapungufu makubwa katika udhibiti wa shughuli za madini. Pia nimepitia taarifa ya Kamati Teule

ya Jaji Mark Bomani na napenda kukubaliana kwa jumla na mwelekeo wa mapendekezo ya msingi, hasa *thrust* kuhusu ushirikishi wa wanavijiji katika maeneo yenyе madini. Kwa mara ya kwanza vijiji na wilaya watafaidika na utaratibu huo mpya.

Tatu, hii inaniletä katika suala la uchimbaji mdogo mdogo katika jimbo langu la Kalenga na hususan kata ya Ifunda na Wasa ambako imethibitishwa kitaalam kwamba kuna dhahabu inayotosha uchimbaji mdogo mdogo. Kwa maana hiyo nashauri kama nilivyokwishafanya kimaandishi mambo mawili, kwanza wenye leseni watatu wanaotoka nje wafutiwe leseni zao na pili, maeneo ya Ifunda na Wasa yatengwe maalum kwa uchimbaji mdogo mdogo, majina ya makapuni hayo yanafahamika Wizarani. Wananchi wenyewe wataamua kama utafiti uendelee vipi.

Mheshimiwa Spika, mwisho naungana na Wabunge wengi waliochangia kwamba gharama za kuingiza umeme kwenye nyumba za watu binafsi ni kubwa mno na ingefaa zipunguzwe na kuhusu *REA* ni vyema kazi hii ikaonekana kuwa inafanyika katika jimbo langu. Orodha zilizoko katika ukurasa wa 75 na pia miradi ya *MCC* ukurasa wa 79 hazijumuishi Kiponzelo, Magulilwa na Igula. Ningombà vijiji hivyo viingizwe katika aidha, *REA* au *MCC*.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine napongeza Bajeti nzuri na juhudì zinazofanyika kuondoa pale ambapo pana mapungufu. Naunga mkono hoja.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Waziri, Mheshimiwa William Ngeleja, Naibu wake, Mheshimiwa Adam Malima na katibu Mkuu Arthur Mwakapugi.

Mheshimiwa Spika, katika swalı langu la nyongeza namba 171 tarehe 8 Julai 2008 nilisema mradi *132 KV* Makambako, Songea naona fedha zinazogawiwa ni kidogo kidogo hivyo unaweza kuchukua muda mrefu mpaka wananchi wa Namtumbo kupata umeme na hii itakuwa tunaenda nje ya ahadi ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Hivyo naomba nifahamishwe kama ilivyosemwa katika hotuba ya Waziri kuhusiana na mradi huu, haikufafanuliwa vizuri hizo dola milioni 70.4 ndio zitakuwa zinatolewa namna zinavyotolewa sasa kwa mfano mwaka 2007/2008 zilitoka bilioni 2.8 na mwaka 2008/2009 bilioni 3.862. Fedha za nje (*SIDA*) sasa kama mtiririko wenyewe ndio huu wa utoaji fedha unaweza kuchukua miaka mingi kukamilika.

Naomba Serikali ifikirie kuwekeza fedha za ndani tupate jenereta ya kuanzia wakati tunasubiri mradi wa *132 KV* umalizike ambao *time frame* yake hatujui. Namtumbo kuna *activities* nyingi ambazo zinahitajika umeme ili kazi ziende haraka kama uchongaji madini ya *Uranium* ambapo kuna makampuni makubwa yapo kule mawili yanafanya kazi hiyo. Tunaomba tuelezwe upatikanaji wa jenereta ya kuanzia itapatikana?

Kwa kuwa kuna kazi zinazoendelea za uchorongaji madini ya *Uranium* ni vyema sera na sheria hiyo ikakamilishwa haraka sababu madini haya ni makali na yana madhara,

hivyo yanaweza kukosewa *handling* yake na kuwapa madhara makubwa wananchi wetu kwani imeshaanza kujitokeza tabia ya wananchi kuchukua mchanga wa madini hayo na kuyaweka ndani ya nyumba zao. Naunga mkono hoja.

MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE: Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa William Ngeleja, Waziri wa Nishati na Madini kwa kuwasilisha hotuba ya Makadirio ya Matumizi ya fedha ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2008/2009 kwa ufasaha mkubwa.

Nianze kwa kuishukuru sana Serikali kwa uamuzi wa kutekeleza ahadi yake ya mwaka jana ya kupeleka umeme *Matema Beach* kutoka Ipinda. Umeme huo utapitia vijiji muhimu katika kilimo na uzalishaji wa kokoa na mpunga na katika utalii vijiji vya Mpunguti, Makwale, Ngyeke na Matema. Aidha, umeme huo utaboresha kwa kiasi kikubwa huduma muhimu zitolewazo na hospitali ya Matema inayoendeshwa na KKKT. Ombi langu maalum kwa Serikali ni kuupa mradi huu kipaumbele kwani milingoti ya umeme ya mradi huu iliwekwa miaka mingi na baadhi imedondoka na kuvunja imani ya wananchi kwa Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa kuamua kusitisha Mkataba na *Richmond/Dowans*. Tatizo langu ni ujumbe wa *TANESCO* uliofikishwa kwa Watanzania kwamba uamuzi wa kusitisha mkataba huo hautokani na uamuzi wa Bunge hili bali ushauri wa wataalam wa sheria wa *TANESCO*! Ni vema Mheshimiwa Waziri akatoa ufanuzi hapa, je, *TANESCO* wana maana kuwa ushauri wa wataalam wao wa sheria ungetaka mkataba huo uendelee, *TANESCO* wasingetekeleza maamuzi ya Bunge ya kusitisha mkataba huo?

Mheshimiwa Spika, hao wataalam wa *TANESCO* walikuwa wapi wakati *TANESCO* inatuingiza kwenye mkataba huo wa kitapeli? Je, kulikuwa na ulazima gani kwa *TANESCO* kutafuta ushauri wa wanasheria wa kulipwa baada ya Bunge kuthibitisha kwa vielelezo kuwa mkataba huo ulikuwa batili na baada ya *TANESCO* yenewe kupewa ushauri wa kina na Kampuni kubwa ya wanasheria ya *Houston Texas* mwaka 2006?

Mheshimiwa Spika, je, *TANESCO* wanaelewa faida za kusimama nyuma ya maagizo ya Bunge na hasara za kujipeleka mbele yake bila msingi wa maamuzi ya Bunge? *TANESCO* inapata faida gani kwa uamuzi huu wa kusitisha mkataba kuutenganisha na maagizo ya Bunge?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. WILLIAM V. LUKUVI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja! Bajeti hii ni nzuri sana na imetekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa vitendo, haijawahi kutokea Bajeti yoyote kuweza kuwa na miradi mingi ya umeme kama hii ya mwaka 2008/09. Hongereni sana!

Mheshimiwa Spika, miradi ya *MCC* itaweka umeme katika jimbo langu la Ismani. Nimefurahi sama kwani jimbo langu ndilo lenye bwawa la Mtera na *Ruaha National Park*. Hivi sasa jimbo langu lina umeme kijiji kimoja tu. Naomba sana mradi wa *MCC*

uchukue vijiji vingi zaidi kwani vijiji vyangu viro karibu karibu sana hususan tarafa ya Ismani na endapo vijiji vingine vitashindikana kabisa kuchukuliwa na *MCC* naomba sana Mheshimiwa Waziri ambaye ni msikivu sana anisaidie kuviwaka katika *REA*. Bila nishati nchi haiendi, nawapongeza sana sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, wataalam wote wa *TANESCO* na *MCC* kwa utendaji wao uliotukuka. Naomba ahadi ya *REA* kwa mwaka 2009/2010 nipewe kwa maandishi bila kusemwa ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Napaenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa William Ngeleja, kwa hotuba nzuri, pia Mheshimiwa Adam Malima, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara na watendaji wote wa Wizara hii, kwa ushirikiano wa hotuba nzuri yenye kueleweka.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii kwa kumpongeza kwa hatua nzuri ya kuvunja mkataba na *Richmond* na *Dowans*, naunga mkono ili Wizara iweze kuipanga upya na wananchi wawe na imani na Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wengi wamejua kwamba *TANESCO* ni chombo chao ambacho kitafikisha huduma ya umeme mpaka vijijini. Kwa hiyo, naiomba Serikali na hasa Wizara ifanye mambo yafuatayo:-

Kwanza kuifutaia madeni yote yanayodaiwa Shirika hili, pili, Serikali kuchukua madeni yote yanayotokana na mitambo iliyokopwa kwa muda mrefu toka uhuru ili *TANESCO* iweze kuijiendesha na kuingia kwenye soko la ushindani na tatu, *TANESCO* ipewe uwezo wa kutekeleza miradi ya hapa hapa nchini ambayo wanajipangia kama vile mradi wa Mchuchuma (MW 400) mradi wa Ruhuji (MW 358) na kadhalika, kama ilivyo kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, nimetaja miradi hii kuna sababu ukiondoa Mchuchuma miradi mingine iliyobaki inatokana na maji ambayo duniani kote imekubalika ndiyo yenye bei nafuu kuliko njia nyingine yoyote ya kutoa nishati ya umeme.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Waziri kwa kutambua suala la kupeleka umeme vijijini. Ningependekeza Wizara itoe ratiba ya kupeleka umeme vijijni Kiwilaya ili Wizara ijue kuna uwiano zaidi angalau kwa kila mwaka vijiji viwili au vitatu kwa kwenda bila ratiba itaonekena utekelezaji wake mgumu hasa kwa kuanzia Ndala, Bukene katika Mkoa wa Tabora. Gharama za kuunganisha umeme zirekebishwe ili wananchi waweze kuzitumia nafasi hizi kwa kujiletea maendeleo.

Kuhusu *Luku* ziwekewe umuhimu wa pekee ili kuondokana na madai ya kukimbizana na bili iwe ni lazima si hiari na iwekewe kwenye mkataba na kuingiza umeme, kama ilivyo matumizi ya simu za mkononi. Naunga mkono.

MHE. HAMZA A. MWENEGOHA: Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kusema nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wote wa Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, kama Serikali haitaweza kuwekeza kwenye uchimbaji wa madini basi ni dhahiri kwamba nchi haitaweza kufaidika kwa madini yetu, kuwekeza katika madini kutaifanya Serikali isiwe na uwezo juu ya maamuzi ya makapuni ya madini.

Mheshimiwa Spika, kuna desturi mbaya ya mashirika ama makapunini kusema kuwa makampuni haya yanaendeshwa kwa hasara, pamoja na hasara wanayopata, makampuni haya yanaendelea kufanya kazi kwa miaka kadhaa. Itungwe sheria ambayo itasema wazi kwamba kama Kampuni inatangaza hasara kwa miaka mitatu mfululizo basi kampuni hiyo ifunge shughuli zake hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka nizungumzie wachimbaji wadogo wadogo. Kwanza kabisa wachimbaji wadogo wadogo haiwezekani kuwa wanafukuzwa kila wakati mchimbaji mkubwa anapotokeza wachimbaji wadogo wadogo hufukuzwa na mara nydingine hata bila ya kulipwa fidia. Tabia hii hajengi bali inabomoa ari ya wananchi kujichimbia madini wao wenyewe.

Kuhusu umeme vijiji, Serikali imekazana sana kueneza umeme katika miji mikuu ya Mkoa na Miji Mikuu ya Wilaya. Kama Serikali haitachukua hatua za makusudi za kueneza umeme vijijini haraka, basi mambo yafuatayo yatatokea.

Kwanza uhamiaji wa watu toka vijijini kwenda mijini utaongezeka kwa kasi kubwa sana kuliko ilivyo hivi sasa, pili, kukosekana umeme vijijini kunadumaza maendeleo ya nchi nzima. Hakutakuwa na maendeleo ya kisayansi na teknolojia kwenye shule, tatu, hospitali, vituo vyta afya na zahanati haziendeshwi kisayansi kutokana na kutokuwa na umeme na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, sasa napenda kuzungumzia umeme katika wilaya ya Morogoro Vijijini. Kwanza ni vyema kuelewa kuwa Wilaya ya Morogoro Vijijini hajumuishi Manispaa ya Morogoro. Hivi sasa Wilaya ya Morogoro Vijijini ina mpango wa kuhamia vijijini, halali panapoitwa Mvuga ambapo ni katikati ya wilaya ya Morogoro Vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo wilaya nzima ya Morogoro Vijijini haswa ni tone tu la bahati mbaya, Ngerengere kwa sababu ya kuwepo kwa Jeshi ndiyo maana umeme umefikishwa hapo.

Mheshimiwa Spika, hapa sina budi kuishukuru Serikali kwa kuiweka Morogoro Vijijini katika mradi wa *MCC*. Katika mpango huu umeme unategemewa kufikishwa hadi Kitongoji cha Kangazi, katika Kijiji cha Mtamba, Kata ya Kisemu, tarafa ya Matombo.

Mheshimiwa Spika, kutoka hapo Kangazi hadi Mvuha ni umbali wa kilometra 18 tu. Hapa Mvuha ndipo yalipo Makao Makuu ya Wilaya. Hivi sasa hapo Mvuha panajengwa Hospitali ya Wilaya, vile vile Makao Makuu ya Halmashauri ya Morogoro Vijijini sasa yanajengwa. Hii ni pamoja na majengo na nyumba mbalimbali za viongozi.

Hali kadhalika, wananchi wanaoishi Mvuha, ambapo pia ni soko kubwa sana la mazao mbalimbali. Hapa pia pana hospitali za *mission*, zahanati ya Serikali, kuna Chuo na Shule ya Sekondari. Hawa wote wanashangaa kuona umeme wa *MMC* unaishia kilometra 18 tu kutoka Mvuha.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe ombi rasmi la umeme ufikishwe Mvuha. Hapa ndiyo Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa wapo wawekezaji wa mashamba ya miwa na viwanda vya sukari. Hawa wote wapo tayari kusaidia kueneza umeme kutoka Mvuha kuelekea Duthumi, Bwakila chini, Mngazi hadi Kisaki. Huko kote wawekezaji wanangojea umeme huu wa Makao Makuu.

Mheshimiwa Spika, mimi nimekuwa naomba umeme huu wakati wote. Nina amini kuwa Serikali ni sikivu yenye kuelewa na yenye kupendelea maendeleo. Naunga mkono hoja.

MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA: Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara na Taasisi/Mashirika yake kwa kazi muhimu inazofanya.

Mheshimiwa Spika, naomba umeme kitongoji cha Nhelegani, Kizumbi ambako ndiko hata Mbunge wa sasa anaishi bila umeme.

Kuhusu tatizo la nguzo za umeme nchini, napendekeza tuanze kutengeneza nguzo za sementi (*cement*); nchi zingine zinafanya hivyo. Hakuna haja ya kuagiza nguzo toka nje.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa naona sitapata nafasi ya kuchangia kwa kuzungumza, nawasilisha tena kwa maandishi maombi ya umeme, mtandao wa umeme uenee Kata zote kumi na tatu za Manispaa ili kila shule ya sekondari sasa zaidi ya 28 ipate umeme. Swali lini, hii itakamilishwa? Naomba majibu.

Mheshimiwa Spika, Nhelegani tumeomba umeme kwa muda mrefu. Lini tutapata? Huku ndiko anaishi hata Mbunge wa sasa. Naomba majibu.

Mheshimiwa Spika, Bugayambelele na *Shinyanga Airport* unahitajika umeme lini utafika? Naomba majibu. Pia kiwanda tarajiwa cha *cement TANDEM Ltd.* cha Shinyanga wamekwishalipa gharama za *Survey* ya kupelekewa umeme kwa ajili ya kuzalisha *cement* eneo la Kizumbi-Nhelegani. Lini *survey* itafanywa ili walipe gharama za kuunganishiwa umeme ili waanze uzalishaji wa *cement* baadaye mwaka kesho. Naomba jibu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa bei za umeme hapa kwetu zinaonekana kuwa chini ukilinganisha na nchi jirani (majedwali yalivyoonyesha), lakini uwezo wa wananchi kulpia (*purchasing power*) uko chini bado. Umeme unaweza kushushwa bei kwa kufuta mizigo isiyostahili kutoka *IPTL, Richmond/Dowans, Songas, Aggreco* na kadhalika. Suala siyo kufuta tu mikataba bali pia kuwafanya warudishe walichochukua bila stahili huko nyuma ili umeme ushuke bei na *TANESCO* iwekeze zaidi.

Mheshimiwa Spika, matatizo makubwa katika sekta ya madini yanaanza kwenye sera ya madini ambao ndiyo msingi mkubwa wa mengine yote. Pamoja na mapitio yanayofanyika ya sera, kazi hii haitaleta manufaa kamilifu bila ya kutamka kwenye sera kuwa Tanzania ni nchi yenye madini mengi na ya aina mbalimbali, madini hayo yote ni mali ya Watanzania wote na madini hayo ni kwa faida na manufaa ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, huu ungekuwa utangulizi stahili wa andiko la sera mpya ya madini kama hayo matatu (a – c) yakizingatiwa. Dira ya Taifa kwa sekta ya madini ingewekwa hivi katika sera, “kuwa na sekta endelevu ya madini inayoendeshwa kwa viwango bora vya Kimataifa kwa maendeleo ya Taifa na watu wake wote” (*Draft vision statement I propose*).

Mheshimiwa Spika, hivyo, dhima/dhamira ingewekwa hivi; “Serikali kusimamia na kushiriki katika kuendeleza sekta ya madini” kwa kuwezesha ushiriki wa sekta binafsi, taasisi/mashirika ya umma na wananchi kwa jumla katika uchimbaji wa biashara endelevu ya madini kwa faida ya Watanzania wote kwa kuzingatia uwiano stahili wa mapato kwa wadau husika.” (*Draft mission statement I propose*).

Mheshimiwa Spika, haya yakizingatiwa yatakuwa ni msingi mkuu wa mapendekezo mazuri na muhimu ya Kamati ya Rais kuhusu usimamizi wa sekta ya madini. Sera ndiyo dira ya mengine yote, tusikosee tena!

Sera ya sasa na sheria pia havitambui wananchi katika maeneo yenye madini kama wamiliki, watunzaji na wafaidikaji wa madini. Si sahihi wananchi kugawiwa pipi kwa hiari ya mwekezaji.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. FATMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Spika, napenda kutoa hongera kwa Bajeti, ni nzuri. Kusudi langu ni kuomba umeme katika Wilaya ya Ruangwa, Nachingwea, Liwale. Umeme huo utapatikana tu iwapo umeme wa *Mnazibay* (*ARTUMAS*) utaunganishwa Nyangao na Ndanda ili kuunganisha nyaya za umeme zilizo tayari huko Masasi ambako unamwaga umeme Nachingwea na Ruagwa.

La pili, ni kumaliza mradi wa umeme wa Somanga Funga ambao upo kwa Songosongo ambao utapeleka umeme vijiji vya Kilwa, Wilaya ya Rufiji, Wilaya ya Mkuranga na Kibiti na kadhalika mradi huu umalizike unaleta upinzani Kilwa.

La tatu, wachimbaji wadogo wadogo wa Ruangwa, wa madini wapo vile vile ila wanakosa nyenzo za kufanyia kazi. Kuna madini ya aina kadhaa zikiwemo dhahabu, *green to maline*, *green sofa* na rangi mbalimbali za nyumba na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, tunaomba wasaidiwe nyenzo, wawekewe maeneo yao ili kusiwe na mgongano na wachimbaji wakubwa wakubwa. Tunaomba mrahaba kwa gesi ya Songsongo na gesi ya Mtwara wapewe Halmashauri husika. Mbona mbuga za wanyama za *TANAPA* zinatoa mrahaba kwa jamii, kwa nini sio gesi nayo pia ni maliasili. Suala hilo pia lifikiriwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

MHE. BALOZI ABDI H. MASHANGAMA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wa Wizara na Taasisi kwa hotuba nzuri ambayo naiunga mkono mia kwa mia, naomba Waziri anifafanulie au anihakikishie yafuatayo:-

Kwanza ni kuhusu umeme vijiji. Nimemwandikia na kuzungumza na Mheshimiwa Waziri mara nyingi kuhusu haja ya kufikisha umeme tarafa ya Mlola wilayani Lushoto hasa miji midogo ya Malibwi, Makanya, Mlola, Ngwelo na Kwekanga. Nilipata matumaini na wananchi wa Tarafa ya Mlola wanayo matumaini makubwa kwamba kwa kuanzia umeme utafika Malibwi kutoka kwemakame na Ngwelo kutoka Mlalo masafa ya umbali wa kilometa kama tano hivi 2008 hadi 2009. Je, Mheshimiwa Waziri anawaambia nini wakazi wa Tarafa ya Mlola?

Mheshimiwa Spika, ibara ya 101 ukurasa wa 52 wa hotuba kuhusu *mini-hydropower generation*. Wilaya ya Lushoto ni wilaya ya milima yenye mvua nyingi, maporomoko mengi na mito mingi inayofaa kuzalisha umeme kama ilivyofanyika Kijiji cha Kinko. Kwa mtazamo huu kwa mfano vijiji vyote katika kata za Makanya, Mlola, Malibwi, Ngwelo, Gare, Kwai, Ubiri na kadhalika zingenufaika na umeme wa *mini-hydro*. Je, Waziri atajumuisha kata hizi katika mradi wa *mini-hydro* na umeme nuru?

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme kusambazwa katika shule. Vituo vya afya zahanati, *police posts*, taasisi za umma na binafsi ambazo haziko mbali na *line* za umeme kwa mfano sekondari za Kitala, Ngulwi, Lushoto, Yoghoi, Magamba, Gare, Balozi Mshangama, Masange, Mkuzi Juu, Kwai, Kwemashai, Ngwelo, Malibwi na kadhalika, msimamo wa Serikali ni upi kuhusu *electrification of rural schools clinic and communities*?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MBARUK K. MWANDORO: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja ya Wizara ya Nishati na Madini. Awali ya yote, ningependa kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na

wataalam wa Wizara na taasisi zake kwa hotuba nzuri na utekelezaji mwema wa Ilani ya uchaguzi na ahadi ya za Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, ningependa kutoa shukrani maalum kwa Serikali kwa kutekeleza ahadi yake ya kuweka umeme Kijiji cha Mkinga na Makao Makuu ya Wilaya ya Mkinga – Kasera.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo ningependa kusisitiza umuhimu wa kuwekea umeme vijiji vya Daluni, Gombero na Kwale ambavyo vimeainishwa kupata umeme chini ya akaunti ya *MCC*. Ahadi ya vijiji hivi kupatiwa umeme ni ya muda mrefu sana na hivyo vijiji hivi vinastahili kupewa kipaumbele maalum itakapofika hatua ya utekelezaji wa mradi wa *MCC*.

Mheshimiwa Spika, ningependa kurudia maombi yetu ya siku nyingi ya kuwekewa *transforma* mpya badala ya iliyoungua Kijiji cha Manza na Songoro. Aidha, narudia ombi letu la muda mrefu la kuwekewa *transforma* ya kugawa umeme katika Kijiji cha Menjamenye, Mkinga.

Mheshimiwa Spika, halikadhalika pamekuwepo maombi mengi ya kuwekewa umeme katika shule kadhaa za sekondari na zahanati Wilayani Mkinga. Pamoja na uhaba wa rasilimali unaokabili nchi yetu, umeme kwa shule za sekondari na zahanati ni muhimu pengine hata umuhimu huo ambayo kwa shughuli za viwanda vidogo vijijini.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa jitihada inayofanya kuendeleza sekta ya petroli. Ninafaraja kwamba Wilaya ya Mkinga ni mionganini mwa maeneo ambako utafiti wa gesi ya asili na mafuta ya petroli unatarajiwani kufanyika, kutokana na kasi kubwa ya kuongezeka kwa bei ya mafuta duniani, kuna umuhimu mkubwa sana wa kuharakisha mchakato wa utafiti na uchimbwaji wa gesi na petroli ili kuerekana na janga la mfumuko wa bei (*imported inflation*).

Mheshimiwa Spika, kuna haja kubwa ya kufikia muafaka rasmi baina ya pande mbili za Muungano kuhusu utaratibu wa uchimbaji wa gesi na petroli katika upande wowote wa Muungano ili tusiendelee kujikwamisha zaidi katika kutumia na kufaidika na rasilimali hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya uwezekano wa kuwa na gesi/mafuta ya petroli katika mwambao wa Bahari ya Hindi. Wilaya ya Mkinga dalili za kuwepo mafuta pia zimejionesha katika milima ya Usambara Mashariki katika Kata ya Kigongoi. Pamekuwepo taarifa za unyevunyevu na michuruziko yenye harufu ya petroli/mafuta ya taa katika eneo hilo. Nashauri Wizara na *TPDC* ifanye utafiti wa awali kuhusu uwezekano wa kuwepo kwa gesi asili na au mafuta ya petroli katika kata ya Kigongoi, Wilaya ya Mkinga.

Mheshimiwa Spika, katika kata hiyo hiyo ya Kigonga na maeneo ya karibu ya Kata ya Daluni na wilaya ya Korogwe yapo madini ya aina nyingi lakini ambayo mpaka sasa ni wachimbaji wadogo, ambao wamekuwa wakichimba kwa tija ndogo sana.

Nashauri jitihada za kufanya utafiti (*prospecting*) zipewe msukumo maalum. Aidha, wachimbaji wadogo katika eneo hilo wafikiriwe kwa uwezeshaji chini ya *Mineral Revolving Fund* na mifuko mingine.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Tume ya Mheshimiwa Jaji Mark Bomani kwa taarifa yake nzuri. Nashauri kwamba Serikali iyakubali mapendekezo ya Tume hiyo na kuyatekeleza mapendekezo hayo ipasavyo mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo hiyo, ipo hoja kwa Serikali kudurusu mikataba yote ya uchimbaji na uendelezaji wa gesi asilia ambayo Serikali yetu (au taasisi zake) imewekeana na wawekezaji kama vile *SONGAS* na *ARTUMAS*. Aidha, ni muhimu hatua za mabadiliko ya mitambo ya *IPTL* kutumia gesi asilia na Serikali kununua mtambo huo zitekelezwe haraka.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Bajeti ya Serikali ya mwaka 2008/2009 haikuleta mabadiliko ya kodi kwa mazao ya petroli, kuna hatari kubwa ya uhalifu wa kuchakachua na athari zake kuendelea. Hivyo, kuna umuhimu mkubwa sana wa kuongeza udhibiti katika uagizaji na usambazaji wa bidhaa za petroli. Mapendekezo ya kuimarisha na kuiwezesha *TPDC* kutekeleza yanayotarajiwa na pia *EWURA* ishirikiane kwa karibu zaidi na *TBS* katika udhibiti wa ubora wa bidhaa za petroli.

Mheshimiwa Spika, nafarijika na napenda kusisitiza kuhusu hatua za uimarishaji *STAMICO* kama ilivyopendekezwa na Kamati ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

MHE. FUYA G. KIMBITA: Mheshimiwa Spika, nianze kuwapongeza Waziri Mheshimiwa William Ngeleja, Naibu Waziri Mheshimiwa Adam Malima, Katibu Mkuu, pamoa na watendaji wengine wote kwa kuwasilisha hotuba ya ki-digital! Hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe maoni yangu kwenye maeneo yafutayo, sekta ya nishati. Napongeza hatua zilizochukuliwa lakini bado tunahitajika kuwa makini zaidi kwa *speed* yetu ni ndogo kufanya maamuzi na mbaya zaidi maamuzi hayo yaliyochelewa wakati mwingine baadhi yake kuwa maamuzi mabaya/hafifu hasa kwa kuzingatia maslahi ya Taifa. Mfano hai ni kwenye baadhi ya mikataba ya ajabu sana. Tunazo aina nyingi sana ya vyombo vya uhakika lakini hatujavitumia.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana kuona hadi leo hatujaweza kuiwezesha *TPDC* kuwa na uwezo wa kushiriki kikamilifu katika maeneo yanayohusika mfano kwenye gesi, bado hapati gawio la asilimia tuliyokubaliana na mbaya zaidi kuna mikanganyiko kwenye uagizaji wa mafuta hapa nchini kwani tulikubaliana tuiwezeshe *TPDC* ili iweze kuagiza mafuta lakini cha kushangaza ni kuona kwenye kitabu cha hotuba kuwa *EWURA* wametangaza zabuni sasa hapa nia njema kwa *TPDC* ipo?

Naomba maelezo! Ni kwa nini ile kazi ya usambazaji/uuzaji wa CNG tulisema/tulipendekeza *TPDC* ndio wafaye hiyo kazi lakini kwa sababu ambazo henzieleweki gawio la asilimia 50 tuliypendekeza wapewi *TPDC* bado hawapewi na matokeo yake wameshindwa kutekeleza/kufanya hiyo kazi na hivyo kampuni ya *Pan African* ndio watakaofanya hiyo kazi, je, hapa maslahi kwa Taifa yapo? Bei ya mlaji itakuwa juu hivi sio sawa hata kidogo, ninahitaji majibu mazuri!

Kuhusu sekta ya madini, kwenye sekta hii kuna matatizo makubwa mno na kinachohitajika hapa ni moyo wa uzalendo kwani mtaji tayari upo ambao ni lazima yenye ya madini lakini mikataba yetu na hao wawekezaji ni mibovu sana! Hivi hata haya madini ya vito ni lazima wachimbaji kutoka nje? Tunaambiwa kwa maandishi kila leo kuwa wazalendo ndio watakuwa wanachimba haya madini ya vito lakini hadi leo wageni ndio wametawala hii biashara ya madini ya vito, aibu! Tuangalie nchi zingine zinafanyaje mfano, Thailand.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini ina umuhimu mkubwa kwa maendeleo ya nchi yetu kwani umeme ndio unaotumika viwandani, ofisini na hata majumbani. Nchi zote zilizoendelea zimeendelea kutokana na umeme. Wote tumeshuhudia jinsi gani uchumi ulivyodidimia pale umeme wa gridi ya Taifa ulipokuwa wa mgao baada ya kushuka kwa kiwango cha maji katika bwawa la Mtera.

Pamoja na umuhimu wa umeme ni jambo la kusikitisha kuona kuwa baada ya miaka 46 ya Uhuru bado ni 10% tu ya Watanzania wana umeme, hii ni aibu. Pamoja na ongezeko la pato la umeme bado haina maana kama baadhi ya wilaya hazina umeme. Kama nilivyosema umeme ni chachu ya maendeleo na ushahidi ni kuwa pale pote penye umeme nyumba zimeboreka kutoka kwenye nyasi na kujenga za batili ili kuweza kupata umeme.

Gesi ni muhimu sana na Mungu ametujaalia kuwa na gesi ambayo itatuwezesha kushindana na tishio la bei ya mafuta. Nchi zote duniani zinahangaika kupata mafuta na chakula, hivyo uwepo wa gesi hii utatusaidia sana kuongeza Pato la Taifa na hivyo ni wakati muafaka wa Serikali kutafuta soko la gesi yetu.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi yenyewe madini mengi kama dhahabu, *Tanzanite*, almasi na kadhalika, cha kusikitisha ni kwamba Serikali imeachia wawekezaji migodi hivyo Pato la Taifa kupotea mfano ni *Williamson Diamond* ambapo nchi haina hisa. Nchi imekuwa ikitumia fedha nyingi kwa ajili ya kuwavutia wawekezaji. Inawezekanaje Tanzania itoe ruzuku kwa makampuni ya wawekezaji? Hii ni sawa na kutoa maji mferejini na kupeleka baharini.

Mheshimiwa Spika, siku za nyuma wachimbaji wadogo wadogo wakisaidia sana maendeleo ya nchi hii mfano kule Mererani walijenga sana mji wa Arusha ambao kwa

kweli unavutia sana. Lakini baada ya wawekezaji kuingia hakuna maendeleo yoyote yanayoonekana pale Arusha.

Mheshimiwa Spika, ukikaa karibu na waridi nawe utanukia waridi. Cha ajabu ukienda sehemu nyingi zenyi madini wala huwezi kujua mfano kule Geita, wananchi wanaishi maisha ya taabu japo wapo juu ya dhahabu, hii ni kwa sababu ya wawekezaji ambao faida yote hupelekwa kwao. Ionekanavyo nchi imeshindwa kuwadhibiti wawekezaji na hii ni hatari kubwa kwani wananchi wanawenza kuvamia migodi kama ilivyotokea Musoma/Tarime.

Mheshimiwa Spika, umeme vijiji ni muhimu sana kwani huku ndio msingi lakini bado tatizo kubwa sasa hivi kuna mpango wa maendeleo ya afya ya msingi na ule wa elimu unaohusu ujengwaji wa zahanati na shule za sekondari kwenye Kata. Kumekuwa na kilio kikubwa cha masomo ya sayansi kwamba hatuna wanafunzi wa kuchukua masomo haya kwani hawana msingi mzuri. Msingi wenye ni kuwa na maabara lakini kama hakuna umeme maabara hizi zitatumikaje lakini pia zahanati zetu pia pia zinahitaji umeme kwa ajili ya kuchunguza magonjwa mbalimbali mfano malaria na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, gharama za kuunganisha umeme majumbani ni kubwa mno kwani inafikia shilingi 600,000/=. Nchi yetu bado ni maskini na wananchi wengi hata mlo mmoja ni tatizo. Lakini pamoja na ughali huu, bado hata wenye kidogo wanashindwa kwa ukiritimba uliopo. Ni vyema basi vifaa vya kuunganisha kuanzia nyaya, mita na kadhalika mtu unalipa na unashiri hata zaidi ya mwaka.

Mheshimiwa Spika, *capacity charges IPTL* ni dola 200.850 Kiwira ni dola 3.65 kwa mwezi wakati ambapo hatuhitaji umeme wa dharura. Hizi ni fedha nyingi sana kwa nchi maskini kama yetu ni vyema mikataba hii iangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, suala la nishati mbadala ya kuni au mkaa ni lazima lishughulikiwe kwani zaidi ya 80% ya Watanzania wanatumia nishati hii. Wakati Serikali inazungumzia kutokata kuni/mkaa bado Serikali hii inapandisha gharama za umeme. Je, Serikali inategemea wananchi watumie nini kupikia? Kula ni lazima hivyo Serikali lazima ama ipunguze gharama za umeme au itafute nishati nyingine mbadala.

MHE. MARIAM R. KASEMBE: Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpungeza Waziri wa Nishati na Madini, Naibu Waziri na watendaji wote toka Wizara hii na wadau wote, kwa kuandaa hotuba ya Bajeti ya mwaka 2008/2009 ambayo imeanza kuonyesha dalili za kuandaa utatuzi wa kero mbalimbali zinazowakabili wananchi, na nchi kwa ujumla. Pia nashukuru maoni ya Kamati na maoni ya Kamati ya Rais, kwani wamechambua kwa undani na kutoa maoni mbalimbali nini kifanyike ili kutatua matatizo.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni Wizara ambayo inaonekana ni kero kubwa kwa wananchi na kwamba nchi ina rasilimali za kutosha ambazo zingeweza kuingiza pato kubwa kwa Taifa na kuwaondolea umaskini wananchi wetu, lakini Wizara inashindwa

kabisa kusimamia utekelezaji wa mipango mizuri. Inayopangwa kufuatana na Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005 inavyosema na kukidhi mahitaji ya wananchi hasa katika sekta ya madini kwa wachimbaji wadogo wadogo na sekta ya umeme pia.

Mheshimiwa Spika, nitaanza na sekta ya umeme. Umeme ni nishati muhimu kwa matumizi ya nyumbani, viwandani na kadhalika kwa uzalishaji mali, lakini hadi sasa inashangaza kuona upatikanaji umeme vijiji umekuwa ni ndoto katika nchi yetu na wananchi wameshakata tamaa, hawajui ni mwaka gani umeme utawafikia, hapo kuna uzembe mkubwa katika utekelezaji wa usambazaji wa umeme.

Kwa mfano, Wilaya ya Masasi inasambaza umeme katika Wilaya ya Newala, Tandahimba, Nachingwea, lakini baadhi ya vijiji vilivyopo katika barabara zinazopita umeme huo kwenda wilaya nyingine havina umeme ingawa wananchi wake wapo tayari kuchangia gharama zinazohitajika na maombi yapo kwa muda mrefu sana lakini utekelezaji wake hakuna. Kwa mfano, ukitoka Masasi kwenda Nachingwea unapita vijiji vifuatavyo – Lisekese kilometra mbili Temeke kilometra nne – Chikunja kilometra 8 toka sehemu umeme unapozalishwa lakini vijiji hivi havina umeme kabisa.

Kama vijiji cha Chikunja ni kijiji kikubwa sana, kina wakazi wengi na maombi ya kuwekewa umeme walishapeleka *TANESCO* zaidi ya miaka miwili iliyopita lakini hawajapata umeme hadi leo hii na ukihoji *TANESCO* wanadai Bajeti wanayopata toka mkoani ni ndogo hivyo haitoshelezi kununua nguzo kwa usambazaji, je, ni lini Mkoa wa Mtwara ni lini watapata fedha za kutosha ili kusambaza umeme vijiji? Je, kama vijiji ambavyo viro barabarani ambapo umeme umepita hawajapata umeme, je, vijiji ambavyo viro mbali kama Namututwe, Chiwale, Mpanyani, Nanyindwa, Lilala, Namajani, Nambawala na kadhalika, kweli watakuwa na ndoto ya kufikiwa umeme kwa mwaka gani? Lakini hata vile vijiji ambayo hivi sasa vina umeme kumekuwa na tatizo kubwa sana la mgao wa umeme kutokana na uchakavu wa mashine zilizopo Masasi.

Ombi kwa Wizara, tunaomba Serikali ichukue jitihada za haraka kuidhinisha pesa ili zinunuliwe nguzo za kuunganisha umeme wa gesi ya *Mnazibay* toka Nyangao – Ndanda ili maeneo ya Masasi, Nachingwea, Newala na Tandahimba kuwe na umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sekta ya madini, pia ina tatizo kubwa sana, lakini naomba nizungumzie kuhusu madini katika Mikoa ya Kusini. Katika Mkoa wa Mtwara hasa Masasi na Nanyumbu – Ruangwa Mkoa wa Lindi, Nachingwea, Tunduru. Viro vijiji vingi ambavyo kuna madini na wachimbaji wadogo wadogo wamekuwa wakichimba madini ya aina mbalimbali ingawa hawana utaalam wa kutosha.

Naiomba sasa Serikali ingefanya utafiti wa kutambua maeneo yenyе madini katika mikoa hii na kuandaa taratibu zinazotakiwa na kutenga maeneo ya wachimbaji wadogo waweze kupata maeneo rasmi ili wachimbaji wakubwa na wawekezaji watakapokuja kusiwe na migogoro na wenyeji kama maeneo mengine yanayotokea.

Mwisho, naishauri Serikali kufuata mikakati iliyowekwa hasa katika kutatua kero na migogoro mingi iliyopo katika sekta hii. Pili, kutafuta uwezekano wa kusambaza umeme vijijini. Tatu, kuangalia taratibu za kutambua na kutenga maeneo ya uchimbaji madini katika mikoa ya Kusini.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. EUSTACE O. KATAGIRA: Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri na timu yake yote kwa maandalizi ya Bajeti nzuri.

Mheshimiwa Spika, umeme wa Wilaya ya Karagwe kusambazwa Vijijini. Wananchi wa majimbo ya Kyerwa na Karagwe wameahidiwa tangu zamani kwamba kwa ufadhili wa *SIDA* umeme utasambazwa vijijini katika Wilaya yote. Kwa kuongezea mwezi Februari Mheshimiwa Rais ametembelea Karagwe na aliwaahidi kuwa umeme unafungwa. Bajeti hii haina chochote juu ya hili. Tunaomba sana umeme huu usambazwe.

Kuna nia na mpango wa kuendeleza kituo cha Murongo kwa njia ya uwekezaji binafsi kwa kushirikiana na mwekezaji toka upande wa Uganda. Serikali iwasaidie na kuwapa *support* ili Uganda wasiendeleze wenyewe peke yao na kutuuzia sisi upande wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE: ALHAJ DR. JUMA NGASONGWA: Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza Mheshimiwa William Ngeleja, Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Adam Kighoma Ali Malima, Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Katibu Mkuu, Makamishna na watumishi wote wa Wizara.

Pili, napenda kutangaza kuunga mkono hoja hii. Napenda kumshurukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuipanga Malinyi, Wilaya ya Ulanga (na siyo Wilaya ya Mahenge) ukurasa 75 wa hotuba ya Waziri, katika mpango wa utekelezaji wa msaada wa *MCC*. Kilio cha mji mdogo wa Malinyi na Jimbo la Ulanga Magharibi juu ya kupelekewa umeme ni cha siku nyingi. Habari nilizonazo juu ya mpango huu ni kwamba umeme huu utatoka *Kihansi Hydro-Power Station* kuititia Mlimba hadi Malinyi na Itete. Hivyo vijiji vitakavyonufaika ni Mpanga, Ngalimila, Biro, Ngoheranga, Tanga, Malinyi (mji mdogo na makao makuu ya Tarafa ya Malinyi), Lugala, Igawa, Misegese, Mwembeni, Sofi Majiji, Kiswago, Usangule, Mtimbira, Munga, Madibira, Kipenyo hadi Itete (Njiwa na Minazini).

Aidha, shule za sekondari za kata kumi na shule za sekondari za Tarafa mbili seminari moja na hospitali ya Kilutheri ya Lugala yenye hadhi ya hospitali ya wilaya. Aidha, eneo hili lina uchumi unaokua haraka hasa kilimo cha mpunga, mahindi na mbegu

za mafuta. Hivyo juhudi hizi za kupeleka umeme Malinyi zina msingi wa kiuchumi na kijamii. Tuutekeleze mradi huu kwa ari, nguvu na kasi mpya.

Tatu, napenda kuonyesha kutoridhika kwangu katika juhudi za Serikali hasa Wizara za kushughulikia uchimbaji mdogo na wachimbaji wadogo. Katika hotuba ukurasa wa 29 na 35 inadai kuwaendeleza wachimbaji wadogo na kuwasaidia kutatua migogoro inayowakumba wachimbaji wadogo dhidi ya wachimbaji wakubwa. Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 imetajwa mara kadhaa katika hotuba lakini ukweli ni kwamba siku zote wachimbaji wakubwa wamenufaika zaidi katika migogoro hiyo kuliko wachimbaji wadogo.

Mfano dhahiri ni Wilayani kwetu Ulanga kwa wachimbaji wadogo wa kijiji cha Epanko. Wachimbaji wadogo wa Epanko ndio waliogundua madini ya *Spinel* na baadhi yao kuomba na kupewa leseni za utafiti na wengine, ingawa waliomba walicheleweshewa kupata hizo leseni. Hali hii imesababisha mchimbaji mkubwa kuchimba *spinel* eneo lili lile walilokuwa wakichimba wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine ni ule wa mchimba mdogo Salim Saidi Madinga, mwenye kampuni ijulikanayo kama *Madinga Mining Enterprises Company Ltd.* katika eneo lake la Simbanguru Dodoma Vijijini. Ingawa Ndugu Madinga aliwahi kuligundua eneo hili na kupata *PL* lakini kiujanja ujanja akakatiwa eneo hilo hilo *Shanta Gold Company* inayomilikiwa na Wahindi maarufu wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, suala hili la Madinga na Simbanguru lililetwe hapa Bungeni mwezi Julai, 18, 2006 (*Hansard* Ukurasa wa 32 – 35). Tatizo hapa ni la *double allocation* na Shanta kinyemela wakaingiza eneo hili katika *London Stock Exchange* na kuvuna mamilioni ya dola za Marekani badala ya kumwezesha mswahili Madinga kunufaika na jasho lake.

Hoja hii ililetwa Bungeni na Mheshimiwa Kilontsi Mpologomyi, Mbunge wa Kasulu Magharibi na alitaka na nanukuu: “Mheshimiwa Spika, ni aibu kwa Taifa hili kama tunataka kuendelea naomba hoja hii ya Simbanguru ijibiwe kwa uhakika tunapata aibu.”

Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini alimjibu na nanukuu; “Mheshimiwa Spika, ndugu yangu Mheshimiwa Kilontsi Mpologomyi, amezungumza kwa uchungu sana juu ya miradi midogo midogona mimi namkulalia ni muhimu.”

Mheshimiwa Spika, ujumbe uliongozwa na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini pamoja na wadau ulitembelea Simbanguru na majadiliano ya kwenye *site* yalidhihirisha dhuluma aliyofanywa Ndugu Salim Saidi Madinga wa *Madinga Mining Enterprises Co. Ltd.* ambayo pia alipata *strategic investor* na kukubaliana kuanzisha *NMM Joint Venture Company* na ilipata kibali cha uwekezaji na *Tanzania Investment Centre (TIC)*. Yote haya yameshindikana hadi leo kutokana na urasimu na hujuma dhidi ya Ndugu Madinga.

Hoja yangu hapa ni ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi, sera ambayo imo katika Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005, na kwa kweli ni moja ya mambo makuu mawili ambayo ni ujenzi wa uchumi wa kisasa wa Taifa linalojitegemea na kuwawezesha wananchi kuiuchumi.

Suala la kuendeleza wachimba wadogo na kujenga mahusiano mazuri kati yao na wachimbaji wakubwa linaletwa katika Ilani kwa msingi wa kuwawezesha wachimbaji wadogo kiuchumi katika utekelezaji wa sera hii ya msingi ya uwezeshaji wananchi kiuchumi na sekta ya madini ni moja ya sekta kuu za uwezeshaji wananchi kiuchumi. Tukishughulikia suala la wachimbaji wadogo *mechanically* hatutekelezi sera hii ya msingi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Waziri wa Nishati na Madini na nategemea kupata maelezo ili wasilazimike kusimama tena wakati wa Kamati ya Matumizi.

MHE. KABUZI F. RWILOMBA, Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Naomba nielezwe *MCC* inaanza lini miradi yake. Naomba nielewe gharama yake kwa maeneo ya Buselesele/Katoro, Bukoli, Nyarugusu, Rwamgasa, Nungare na Bukondo.

Mheshimiwa Spika, Matabe itatolewa lini kwa wachimbaji wadogo. Naomba majibu. Pia naomba hati ya mgogoro wa *Rijet Geita* na *GGM* umefikia wapi kesi hiyo ipo ofisini kwa Mheshimiwa Waziri. Naomba maelezo. Naomba sana *Ndala T.T.C* na Ndala Hospitali, Nzega ipelekewe umeme nguzo zinapita maeneo yao, siyo vizuri.

Naomba Naibu Waziri aje jimboni kwangu akiwa na wataalam wafuatao, Kamishna wa Madini na msimamizi wa *MCC*. Ili atoe maelekezo kwa watu wangu.

MHE. JAMES D. LEMBELI: Mheshimiwa Spika, napenda kuanza mchango wangu mfupi kwa kusema naunga mkono hoja.

Naunga mkono hoja hii kwa sababu licha ya Bajeti kuwa ndogo ukilinganisha na majukumu ya Wizara hii kwa maendeleo ya nchi imepangwa vizuri walau kukidhi mahitaji na matarajio ya wananchi na Taifa kwa jumla kutoka sekta za nishati na madini. Ombi langu Wizara ihakikishe kwamba mipango yote iliyoko katika Bajeti hii inakamilishwa kikamilifu, vinginevyo uzuri wa Bajeti hii utaingia dosari.

Napenda pia katika mchango wangu huu kuipongeza Wizara kwa usikivu wake. Baada ya wananchi wa Buzwagi kupiga kelele dhidi ya mapungufu yaliyokuwa yemejitokeza katika mgodi wa Buzwagi, hatimaye Serikali ilisikia kilio chao. Naipongeza Serikali inayoendelea kulishughulikia tatizo hilo na ninaamini kwa jinsi ambayo Serikali inaendelea kushughulika, suluhu ya kudumu itapatikana.

Wakati huo huo naiomba Serikali kutumia uzoefu itakaoupata katika kutatua mgogoro wa Buzwagi, iutumie katika kuhakikisha migogoro kama hiyo haitokei katika maeneo mengine ya nchi yetu. Ni muhimu Wizara kuwa na ufuatiliaji wa karibu katika

masuala ya fidia ili kuepuka udanyanyifu unaoweza kutokea kwa baadhi ya viongozi wa Wilaya na mikoa kuhusu masuala ya fidia.

Mheshimiwa Spika, nishati ni moja ya nyenzo muhimu katika maendeleo ya nchi yoyote. Katika jimbo la Kahama wananchi wanahamu sana ya kujipatia umeme ili kuboresha uchumi wao, tatizo sugu ni ukiritimba unaoashiria rushwa ambapo licha ya kulipia gharama zote za kuunganishiwa umeme wananchi wanasubiri kuunganishiwa hadi miaka mitano. Jambo hili si zuri, tunaomba (wananchi) tatizo hili lishughulikiwe.

MHE. MARIA I. HEWA: Mheshimiwa Spika, natoa pongezi nyingi kwa Waziri na ofisi yake yote kwa hotuba yenye ufanuzi mzuri hasa katika utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005.

Kuhusu kusitisha mkataba kati ya *TANESCO* na *Dowans*, katika hili nchi nzima inalipongeza tendo hili maana liliibuka Bungeni kama kero kubwa na baadae kuungwa mkono na wananchi nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja ya kufutiwa deni *TANESCO*. *TANESCO* ni Shirika letu ambalo linafanya kazi chini ya masharti ambayo karibu yote huwa chini ya udhibiti wa Serikali. Deni analolipa *TANESCO* limesababishwa na mpango mbovu ndani ya mikataba ambayo Serikali imeshiriki. Ushauri wangu ni kwamba deni hilo lipelekwe Serikalini na Hazina ihusike kikamilifu kulirejesha vinginevyo hawataweza kutumikia mabwana wawili kwa mfano, ushindani na wawekezaji watakaojitokeza na kuendelea kulipa deni.

Kuhusu hoja ya gharama za ufungaji umeme, wananchi nchini walio wengi wanapenda kuvuta umeme katika makazi, ofisini na maeneo mengine mengi kwa nia ya kujiletea maendeleo na kukidhi mpango wa MKUKUTA. Tatizo kubwa ni gharama za tangu mwanzo wa ununuzi wa nguzo, nyaya, *bulbs* na zote zimejaa VAT. Je, huyu mwananchi wa kawaida ataweza? Niliomba Taifa/Serikali kuona kwa kila atakayejitokeza apewe punguzo aidha, kufuta VAT au kuwe na ruzuku ndani ya taratibu zote hizi za uvutaji wa umeme katika maeneo ya watu wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. IDDI M. AZZAN: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Makampuni makubwa ya madini yameweka mitambo (*x-ray*) kwa ajili ya kuwachunguza wafanyakazi hasa Watanzania kama wametoka na madini au kwa kuyameza na kadhalika, na kwa sababu mitambo hiyo ina athari kubwa sana kiafya, naomba sana Serikali itueleze ni hatua gani imechukuwa ili kulinda afya ya wananchi wetu kabla hayajatokea madhara makubwa? Mitambo hiyo ya *x-ray* iko pia *Tanzanite One*.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Kwanza napenda kuweka wazi kwamba nina maslahi na mradi wa gesi wa Rasi ya Mnazi kwani imo ndani ya Jimbo langu. Kwanza napenda kupinga mawazo ya Mheshimiwa Raynald Mrope, Mbunge wa Masasi, anafanya hivyo kwa sababu ye ye ni mjumbe wa

Bodi ya *ARTUMAS* kwa hiyo hawakilishi mawazo ya wananchi wa Mtwara, ye ye anatetea maslahi yake yaliyoko kwenye *ARTUMAS*.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mtwara wanahitaji gesi hiyo itumike kwa umeme, Kiwanda cha Saruji na Kiwanda cha Mbolea. Haitakuwa busara hata kidogo kusafirisha gesi nje ikatengenezwe mbolea halafu tuje tuinunue kwa bei mbaya. Tuwe na huruma na nchi yetu tuache maslahi binafsi. Tumalize majadiliano.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa William Ngeleja, kwa kuteuliwa kwake kuwa *full Minister*, inaonyesha uwezo mkubwa alionao na jinsi anavyokubalika katika jamii, lakini pili katika uwasilishaji wa hotuba yake, hakika amedhihirisha umakini wake.

Mheshimiwa Spika nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Adam Malima, kwa kuteuliwa kwake kuwa Naibu Waziri ingawa tuna m-miss sana kama mpiganaji mwenzetu, ambaye sasa kanyang'anywa silaha zote.

Pia niipongeza Wizara yote kwa maana ya Katibu Mkuu na Wakurugenzi, Makamishna na watendaji wote kwa kazi nzuri wanayoifanya, ingawa wapo wachache wanaoichafulia Wizara, lakini wakati wao ukifika na uthibitisho wa dhahiri ukiwepo wataondolewa tu. Hakuna jinsi kwani nyakati zimebadilika.

Awali nipongeze sana mapokezi tunayopewa tufikapo Wizarani. Binafsi na wengine wengi tunasifu huduma tunayopewa, na hasa ukizingatia kauli za watendaji, hata kama jambo limekuwa gumu, linakuwa jepese, bila kusahau ukarimu wa wahudumu, kwa ujumla wao pamoja na masekretari wanastahili kupongezwa.

Pamoja na kwamba Waziri amesema na Mheshimiwa Waziri Mkuu pia kasema, kuna kila sababu ya marekebisho ya sheria ya madini. Kama nchi tunaathirika na pia sisi tunaotoka maeneo ya madini. Athari ni kubwa sana kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na shukrani za eneo kutengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo ndani ya Wilaya ya Kilindi, zoezi limechukua muda mrefu sana tangu mwaka 2004 hadi leo. Naomba maeneo yanayotengwa kwa jinsi hii, kuwa na masharti nafuu ili kuwezesha zoezi kukamilika kwa wakati na kwa utaratibu ambao hauathiri utaratibu mzima.

Kuhusu malipo, yote yawe ya leseni ndogo au ya utafiti hupelekwa Serikali kuu, je, Wilaya yenye rasilimali hiyo inatakiwa kufaidika lini hasa kiuchumi, mazingira yanayoathirika ni yetu, tunahitaji hizo fedha angalu *some percentage*.

Suala la elimu kwa wachimbaji wadogo na viongozi na wataalamu ni muhimu hasa Kilindi.

MHE. SALUM KHAMIS SALUM: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa malalamiko ya wafanyakazi wa Mgodi wa *Tanzanite One* uliopo Mererani kuhusiana na mambo yafuatayo, kwanza, wafanyakazi kupita kwenye *x-ray* kila wanapotoka kwenye mgodi huo, wafanyakazi kuvuliwa nguo zote wakati wa upekuzi kila wanapotoka mgodini, wafanyakazi hufanya kazi wakiwa kifua wazi na bila vifaa vyote vyaa kufanya kazi na walinzi wa mgodi kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri atoe maelezo yaliyo sahihi kuhusiana na mambo hayo ukianzia *x-ray* hiyo ni hatari kwa sababu *x-ray* hiyo ina *label* ambayo ni ya hatari kwa afya ya binadamu.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi kuvuliwa nguo ni vitendo vyaa kuwanyanya na si utaratibu unaofaa. Wafanyakazi kufanya kazi wakiwa bila nguo pia ni unyanyasaji mkubwa usiofaa. Walinzi wa mgodi kutoka nje ni kupoteza ajira kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri atoe ufanuzi wa wafanyakazi hawa.

MHE. ENG. LAUS O. MHINA: Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme vijijini hili ni suala la ukombozi kwa wakazi wengi wa maeneo ya vijijini. Jimbo la Korogwe Vijijini linategemea sana mradi wa umeme vijijini chini ya wakala wa umeme vijijini na mfuko wa umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, vijiji vingi katika jimbo la Korogwe Vijijini, vilikwisha ahidiwa huduma hii muda mrefu uliopita lakini hadi sasa hakuna utekelezaji uliofanyika. Wananchi wengi walikwishaandaa majengo yao (kufanya *wiring*) tayari kupokea huduma hii. Baadhi ya vijiji hivyo ni Dindira, Kerenge (Kibaoni, Lusanga) na Kwemazandu.

Mheshimiwa Spika, katika kata yote ya Kizara huduma hii haijafika kabisa katika kijiji chochote na umeme unapita katika kata ya jirani ya Mashewa.

Vile vile katika kata ya Mkalamo kipo kituo cha afya cha kisasa kilichojengwa na wahisani wa asasi ya kidini ya Italia. Katika kituo hicho kuna vifaa/mashine mbalimbali ambazo hazitumiki kutokana na kutokuwepo kwa umeme.

Mheshimiwa Spika, maombi yalikwishapelekwa siku nyingi *TANESCO* lakini hadi sasa hakuna umeme katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, masuala haya wananchi wa Korogwe Vijijini wanaomba watizamwe kwa undani.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Korogwe Vijijini linao utajiri mkubwa wa madini ya vito hivi karibuni kamati ya Rais ya Kushauri Serikali kuhusu usimamizi wa sekta ya madini ilitembelea migodi mbalimbali hapa nchini. Bahati mbaya Kamati hii haikufika Wilaya ya Korogwe. Hili halikuwafurahisha wananchi wengi wa Korogwe.

Mheshimiwa Spika, katika mgodi wa Kalalani/Kigwasa Wilayani Korogwe kuna wachimbaji wakubwa na wadogo.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi hutokea mgongano kati ya wachimbaji wakubwa (wawekezaji) na wachimbaji wadogo, kila upande ukidai unayo haki kwa njia moja au nyingine. Serikali ya Wilaya na Mkoa zimejitahidi mara nyingi kusuluhisha migogoro hii lakini hakuna suluhisho la kudumu.

Mheshimiwa Spika, tunaiomba Wizara husika iende Kalalani/Kigwasi na kujiona yenye ili ufumbuzi wa kudumu upatikane kati ya wachimbaji wakubwa (wawekezaji) na wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO: Mheshimiwa Spika, napenda kumpogezza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake Mheshimiwa Adam Malima, Katibu Mkuu wa Wizara Ndugu Arthur Mwakapugi, wasaidizi wake wote Wizarani na viongozi wa taasisi zilizo katika sekta ya nishati na madini kwa kazi nzuri mnayofanya hasa kwa utayarishaji wa hotuba hii ya mwaka 2008/2009. Nampongeza yeze binafsi kwa jinsi alivyoiwasilisha hotuba yake kwa ufasaha mkubwa ndani ya muda uliowekwa na kanuni za Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utalenga katika maeneo yafuatayo, muundo wa Bajeti, sekta ya nishati na mahitaji ya nishati katika Wilaya ya Kisarawe.

Mheshimiwa Spika, tumezoea sana kuona Bajeti za ulaji, yaani matumizi makubwa katika Bajeti ya kawaida na fedha kidogo tu kwa ajili ya Bajeti ya maendeleo. Mimi ni muumini wa kuweka fedha zaidi katika Bajeti za maendeleo ili kujenga uwezo wa kuzalisha zaidi kwa siku za mbele. Bajeti yenu hii ya shilingi 362,922,265,600/= imeweka uzito katika sehemu inayostahili kwa kutenga shilingi 320,067,385,600/= kwa miradi ya maendeleo na shilingi 42,854,880,000/= au asilimia 11.8 tu kwa matumizi ya kawaida . Hongereni kwa kuweka mbele maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mbali ya kuweka mbele maendeleo, kati ya shilingi 320,067,385,600/= za maendeleo, Wizara imepanga kutumia shilingi 223,468,694,600/= au asilimia 73 fedha za nje kutoka kwa wahisani na asilimia 12 tu fedha zetu wenye. Huu ni uamuzi mzuri wa kutumia fedha zetu wenye. Huu ni uamuzi mzuri wa kutumia fedha kidogo sana za kwetu lakini nyingi za mikopo ambayo itahitaji kurejeshwa miaka ijayo katika eneo ambalo litazalisha hivyo kuwa na uwezo wa kurejesha mikopo. Hongereni sana.

Kuhusu sekta ya nishati, miradi ya umeme imezingatia agizo la Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (mwaka 2005), iliyoazimia upatikanaji wa nishhati kwa wingi. Kwa hiyo, kuhakikisha katika Bajeti hii kuwa umeme unafikishwa katika Makao Makuu ya Wilaya zote, maeneo yenye upungufu wa umeme kama vile Kigoma, Singida, Shinyanga, Lindi, Mtwara, Songea na kadhalika, ni kuitekeleza Ilani hiyo kwa vitendo na kuijenye CCM uhalali wa kuendelea kushika madaraka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nishati jadidifu na mbadala, uamuzi wa kutilia mkazo uzalishaji wa nishati jadidifu na mbadala ni wa busara sana. Kwanza wataalam wa nishati wanatabiri kuwa nishati ya mafuta ya ardhini inayotegemewa sana duniani, inazidi kupungua. Kwenye miaka ya hamsini ijayo huenda uzalishaji usitosheleze mahitaji.

Pili, bei za mafuta hayo zinazidi kupanda kiasi tutafika pahala hatutawezza kuyanunua. Tatu, nishati inayotokana na nguvu za maji haiaminiki kwa sababu maji yanategemea hali ya hewa ambayo haitabiriki. Vile vile katika kipindi kirefu hali ya joto imekuwa ikiongezeka, hivyo kupunguza wingi wa maji duniani kote.

Kwa upande mwengine, Tanzania imebahatika kuwa na vyanzo vya nishati mbadala kama vile juu kwa wingi, upopo mwangi nchini, jotoardhi na mimea kama vile *jetrophta* ambayo inaweza kutengeneza nishati za mafuta (*biofuels*). Kwa hiyo, kwa Bajeti hii kuanza kufikiria vyanzo kama hivi, ndiyo inalenga katika nyanja za ukombozi wa matatizo yajayo ya nishati.

Mheshimiwa Spika, ingawa zipo tahadhari za kukaribisha njaa kama tutaendeleza uzalishaji wa *biofuels*, hili ni suala la kupanga wapi vizalishwe vyakula na sehemu zipi ziendelezwe kwa kilimo cha mimea ya kuzalisha nishati. Nahofia kuwa kama tutabweteka, tukaacha kuangalia uzalishaji wa nishati mbadala, endapo kweli mafuta ya ardhini yatakwisha, hatutakuwa na pahala pa kukimbilia.

Kuhusu hali ya nishati Kisarawe, kama nilivyoeleza katika barua yangu ya tarehe 11 Februari, 2006 kwa Mheshimiwa Waziri, ukiondoa pale Makao Makuu ya Wilaya na sehemu ndogo kando kando ya barabara ya Dar es Salaam – Morogoro, Wilaya nzima iko gizani, lakini mahitaji ni makubwa. Tunahitaji umeme wa kutusaidia katika viwanda vidogo vidogo vya kusagishia na kukobolea vyakula na matunda, umeme kwenye vituo vyetu vya afya na zahanati, umeme kwenye shule za sekondari zaidi ya 15 na za msingi zaidi ya 70, umeme wa kusukumia maji kutoka Mto Ruvu, mabwawa na visima na kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Kwa bahati mbaya Wilaya haijamuona wakala wa nishati vijijini anayeongolewa katika ibara za 16 hadi 18 katika hotuba hii. Tulitegemea Kisarawe kuwemo katika orodha ya Jedwali Na. 7. Wapi hatumo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri katika jibu lake la msingi kwenye swalilangu Namba 147 ameellezea kutenga shilingi 750,000/= kwa upimaji wa kina na uagizaji wa baadhi ya vifaa kwa kuititia mifuko ya *REA* na *REF (Rural Energy Amount and Rural Energy Fund)*. Sikuridhika na kiwango cha fedha kutoka mfuko wenye fedha zaidi ya shilingi 10,000,000,000=/. Naomba mgao uongezwe ili upimaji uende haraka na sisi Kisarawe tuwasogelee Watanzania wengine.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja yake kwa asilimia mia moja. Asante sana.

MHE. MAGALLE JOHN SHIBUDA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kutumia fursa hii kumpongeza Waziri wa Nishati na Madini na Mbunge wa

Jimbo la Sengerema, Mheshimiwa William Ngeleja, kwa usimamizi makini wa Wizara hii. Vile vile napenda kuwapongeza viongozi wote ambao ni fungamano na wajibu wa Wizara hii kwa maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali inahimiza maendeleo kwa ustawi wa jamii na kuwa na msimamo wa kujenga uchumi endelevu wa hatma ya nchi kujitegemea kwa hiyo, sasa naiomba Serikali katika mipango yake ya kufaulisha dhamira ya ustawi wa jamii na kujitegemea wananchi wa jimbo la Maswa itupatie gawio la uwezeshaji kuibua nishati endelevu. Hivyo namwomba Mheshimiwa Waziri arejee kwenye mchango wangu wa kuchangia Muswada wa Sheria ya Umeme ya mwaka 2007.

Vile vile naomwomba arejee kwenye mchango wangu kuhusu Mapato na Matumizi kwa ajili ya Bajeti ya Serikali ya mwaka 2008/2009. Vile vile namwomba Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini arejee barua yangu ya tarehe 16 Juni, 2008

Mheshimiwa Spika, kumbukumbu hizi ni vielelezo vya kuiomba Serikali itupatie kauli ya wajibu wake kwa utatuzi wa shida za nishati kwa wananchi wa jimbo la Wilaya ya Maswa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tangu mwaka 2005 hadi leo nimekuwa naomba gawio la pesa za kuibua nishati endelevu kwa ustawi wa maendeleo ya wananchi wa Maswa, na kwa kuwa nishati endelevu kwa Maswa ndio ufunguo wa maisha bora, afya bora na kivutio cha miundomibinu ya msako wa uchumi endelevu kwa vita dhidi ya umaskini, na kwa hiyo, sasa namwomba Mheshimiwa Waziri awaabie wananchi wa Maswa ametugawia nini kwa kujenga nishati bora kama nilivyoomba kwa mujibu wa kumbukumbu zote ambazo amezipokea tangu nitoe maelezo ya mdomo ambayo yamo katika *Hansard* na katika barua yangu ya tarehe 16 Juni, 2007.

Mheshimiwa Spika, natambua uwezo wa Mheshimiwa wa kukumbuka ahadi zake na kwamba kauli zake ni vitendo. Sasa namwomba vitendo kwa kauli zake ili nipeleke matokeo ya kauli za Serikali wananchi jimbo la Maswa.

Mheshimiwa Spika, kurahisisha marejeo ya majadiliano na marejeo ya barua yangu sasa nayaambatanisha kwa maelezo haya ili aweze kunipa majibu sawia. Naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja ya Wizara yake ya mwala 2008/2009.

MHE. ELIETTA N. SWITI: Mheshimiwa Spika, juhudhi za Serikali za kusambaza umeme nchini kote zinaonekana wazi tena mimi nitasema kwa kasi mpya na dhana ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Katika juhudhi ya Serikali naomba basi nifafanuliwe ni kwa nini *TANESCO* haizungumzii tena kuvuta umeme wa gridi toka Mbeya kwenda Sumbawanga hadi Mpanda kama ilivyoainishwa na utafiti wa *SWECO/DECON* kwa kuvuta umeme huo kwa mzungo wa KV 220 toka Mbeya. Lakini pia ikiwa sasa tunaongelea umeme wa gesi toka *Mnazi Bay* na Songsongo ambapo tunategemea kuwa

upo uwezekano wa gesi hiyo kuwezesha baadhi ya umeme huo kuunganishwa na gridi ya Taifa hivyo huongeza nguvu.

Mheshimiwa Spika, Rukwa tunashukuru kwa Serikali kuendeleza nishati jadidifu na mbadala mkoani kwetu. Hata hivyo natoa ushauri kwa Serikali kuendeleza kwa kasi kilimo cha mmea wa mbono katika mkoa huo kwani tayari kiwanda kinajengwa Mpanda. Tukizingatia kuwa hata nchi kama Marekani yenze akiba kubwa ya mafuta bado inatengeneza *biofuel* kwa kutumia mahindi (hata kama huku tunakufa kwa njaa); iko haja ya sisi kujizatiti katika hili. Naipongeza Serikali kwa umakini katika kuwezesha uwepo wa *biofuel* hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie pia uwezekano wa umeme kutokana na upopo; kwa mkoa wa Rukwa hili likiwezekana hata vijijini.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali, Waziri wa Nishati na Madini na watendaji wa Wizara ya Nishati na Madini kwa kuvunja mkataba wa *Dowans*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu wa maandishi katika hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini.

Kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuunda Kamati ya kuishauri Serikali kuhusu usimamizi wa sekta ya madini. Hii ni hatua moja kubwa na nzuri sana kwa maendeleo ya sekta ya madini na hata uchumi wa Taifa. Pia napenda kuipongeza Kamati hii ya Rais kwa kufanya kazi nzuri ya kuichunguza sekta ya madini na hatimaye kutoa taarifa inayojitosheleza na kimsingi ni nzuri mno. Vile vile naipongeza Serikali kwa sheria mpya ya umeme ambayo italeta mapinduzi makubwa katika sekta ya umeme.

Kwa kuwa mambo mengi yanazungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wenzangu na mengine kudhihirishwa na Kamati ya Rais, ningependa kusisitiza mambo machache kama ifuatavyo, kwanza madini ni *non-renewable resource*, hivyo yanavyoendelea kuchimbwa ina maana yanapungua na hatimaye yatakwisha kabisa.

Naiomba Serikali iyafanyie kazi kwa haraka bila kupoteza muda mapungulfu yote pamoja na mapendekezo yaliyoelezwa na Kamati Teule ya Rais ya kuishauri Serikali kuhusu usimamizi wa sekta ya madini. Vinginevyo tukichelewa tutakuta madini yote yamekwisha. Pili, Serikali ikamilishe mazungumzo yake na kampuni ya *ARTUMAS* ili gridi ya Taifa iweze kupata *megawatts* 300 za umeme na kuzisambaza katika maeneo mengi ya nchi yetu.

Pamoja na kwamba Manispaa ya Mtwara inapata umeme wa gesi, nasikitika kusema kwamba umeme huu bado si wa uhakika sana kutokana na uchakavu wa miundombinu. Pia Wilaya zote zilizobaki za Mtwara ni kama hazina umeme, kumbe basi

Serikali iwe mstari wa mbele kuhakikisha kuwa *line* za Mtwara - Tandahimba na Nyangao – Ndanda haraka ili wananchi wetu wapate umeme.

Mheshimiwa Spika, Wizara ikumbuke kuwa ukosefu wa umeme una athari katika sekta nyingine hususan afya na maji. Kwa mfano, ukosefu wa maji umekuwa ni kero kubwa katika Wilaya za Newala na Tandahimba na sababu mojawapo ni *pump* kutofanyakazi kutokana na ukosefu wa umeme. Pia hospitali zimesitisha baadhi ya huduma kama za upasuaji kutokana na uhaba wa maji na umeme. Vile vile si rahisi kuendesha viwanda vidogo vidogo pasipo umeme hivyo uchumi kuathirika.

Tatu, kuhusu wawekezaji wa umeme na madini wasaidie shughuli za kijamii vya kutosha na kwa uwazi bila ubabaishaji. Kipaumbele kiwekwe kwenye kutatua tatizo la uhaba wa maji na wasaidie kuweka umeme wa *solar* kwenye shule zetu za kata ili watoto waweze kupata elimu ya kompyuta na kuweza kujisomea usiku.

Mwisho, nichukue nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Nishati na Madini kwa kazi zao nzuri na zinazotia matumaini kwa Watanzania wengi. Naunga mkono hoja na ahsante.

MHE. USSI AMME PANDU: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kuchukua nafasi hii kuipongeza Wizara hii kuitia kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara hiyo kwa kuwasilisha Bajeti nzuri ambayo inakidhi haja ya Watanzania, lakini pia ni Bajeti ambayo inatekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 naipongeza sana sana.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sasa wananchi wa nchi hii wamekuwa wakisumbuka kulipia umeme kwa gharama kubwa kwa watumiaji kutokana na mikataba mibovu ambayo imeliingiza shirika hili la *TANESCO* kwenye gharama zisizokuwa za lazima na kusababisha bei ya umeme kupanda kwa wananchi wa kuongeza ukali wa maisha. Je, Mheshimiwa Waziri kwa kuwa mkataba huo Serikali imeshaamua kuuvunja (*Richmond*) haoni kuna haja ya kuwapunguzia wananchi gharama za umeme ambazo zilipanda kwa sababu ya mikataba mibovu?

Mheshimiwa Spika, mwisho nimalizie kwa kuunga mkono hoja kwa asilimia zote.

MHE. SAID AMOUR ARFI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu ameanza vizuri pia, pongezi za dhati anastahili. Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, Naibu Waziri, uongozi wa Wizara na *TANESCO* kwa kusitisha mkataba wa *Dowans/Richmond* kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, lakini isiishie kwa *Dowans* tu ni vema mikataba mingine ambayo ni mizigo kwa Taifa na *TANESCO* ya *IPTL, Aggreco* na kadhalika, hatua sahihi zichukuliwe mara moja.

Mheshimiwa Spika, tunapaswa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyetupa neema tele katika nchi yetu ardhi, maji, madini, wanyama, misitu na vingine vingi.

Tatizo kubwa la nchi yetu ni kuchukua maamuzi na kwa wakati sahihi. Kila siku nchi hii ni ya mikakati, programu, mipango, maandiko na maneno mengi lakini hakuna utekelezaji madhubuti na bora kwa ajili ya nchi yetu na maendeleo ya watu wake. Kila siku ni hadithi tu. Lazima sasa tubadilike kama tuna dhamira ya dhati na utashi wa kisiasa wa kuwaondoa Watanzania katika umaskini.

Mheshimiwa Spika, neema nilizozitaja je, zimepunguza umaskini wa Watanzania kwa kiasi gani? Kilimo matatizo, misitu matatizo, nishati na madini nayo matatizo kadhalika.

Mheshimiwa Spika, lazima tukubali nchi yetu ni maskini, tuna raslimali pesa kidogo tunazitawanya hapa na pale hazileti tija, hatuna kipaumbele na wala hatujui tuwekeze wapi hizi pesa kidogo ambazo mwisho wa siku zitaleta ufanisi na kuwa sababu ya kichocheo cha maendeleo badala ya kuomba misaada kila siku.

Mheshimiwa Spika, tuna gesi asilia, hivi mipango yetu ni kumleta mzungu anufaika na kuondoka na utajiri kama Watanzania tunashindwa wapi? Tunao wataalam wazalendo wanathaminiwa na ushauri wako unakubalika na kutekelezwa au mpaka waje wakubwa toka Washington, *WB* na *IMF* na dawa ya kuondoa umaskini wetu, haiwezekani umaskini wa Watanzania utaondolewa na Watanzania wenyewe wakipewa fursa na kusikilizwa.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengi wamechangia sana kwamba tunaweza tukaondoa umaskini wetu kama tutakuwa na dhamira njema ya kuitumia raslimali hii ya gesi asilia kwa kuiwezesha *TPDC* kusimamia na kuendeleza eneo hili si kwa maeneno kwa kutumiza yale tunayoamua.

Mfano mwaka 2004/2005 mahitaji ni shilingi milioni 4.751, wakatengewa shilingi milioni 1726 wakapewa shilingi milioni 200 sawa na 4%. Mwaka 2005/2006 mahitaji ni shilingi milioni 5,039, wakatengewa na walizopewa ni 0 sawa na 0%. Mwaka 2006/2007 mahitaji ni shilingi milioni 5,830 wakatengewa shilingi milioni 6,000 wakapewa shilingi milioni 600 sawa na 7%. Kwa style hiyo ni kweli tunataka kuondoka kwenye Umaskini?

Mheshimiwa Spika, lipo swalı lingine la kujiuliza, mitambo ya kuzalisha umeme na zaidi ya viwanda 20 hapa nchini kwa sasa wanatumia gesi kuendesha mitambo yao na kupunguza kwa kiasi kikubwa sana gharama za uzalishaji je, bidhaa zinazotoka viwandani zimepungua bei kwa kiasi gani? Wananchi wamepata nafuu kwa bidhaa wanazonunua au ndio mwendelezo ule ule wa mwenye kingi kuongezewa?

Mheshimiwa Spika, nani anajali hata kuangalia eneo hili la bei za bidhaa ili kumpunguzia makali ya maisha Mtanzania maskini? Inasikitisha sana kwa mfano sasa gesi wanapewa wazungu kusambaza Dar es Salaam ambao lengo lao ni faida, wamelenga

kupeleka katika *centre* na hoteli za wazungu na sio kwa waswahili wa Kariakoo na Magomeni.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza tukibadilisha mtazamo wa akili zetu na dhamira ya kisiasa (*political will*) Tanzania umaskini utakuwa ni hadithi. Tukitumia vizuri bahari na reli tukasimamia kwa sheria za haki na usawa raslimali ya madini, uvuvi na kadhalika, Watanzania hawatapaswa kuchangia elimu, afya, maji, hata ujenzi wa shule na hospitali.

Mheshimiwa Spika, sasa niangalie kidogo matatizo ya jimbo langu na Mkoa wa Rukwa kwa ujumla wake katika maeneo mawili, umeme na madini kama tunavyofahamu sote Rukwa hajaungwa katika gridi ya Taifa. Napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri na *TANESCO* kwa jitahada za kupunguza kero ya umeme Mpanda lakini ni ufumbuzi wa muda mfupi wa kuokota vipuri vichakavu na kufungwa Mpanda lakini tatizo linaendelea. Naiomba Wizara na *TANESCO* kuliangalia tatizo la Umeme Mpanda kadhalika na bili za umeme kuwa kero kubwa kwa watumiaji wa umeme.

Mwisho, ni viwanja vya madini ambayo vinagawanywa kiholela eneo hili litazamwe tena.

MHE. RUTH B. MSAFIRI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Pia naomba yafuatayo yazingatiwe.

Kwanza, nilianza kuulizia umeme wa Kagoma na kuomba wapatiwe umeme kwani wako barabarani na walio tayari kufunga umeme ni wengi zaidi ya watu 80 sasa ikiwa miundombinu muhimu kama Kagoma Sekondari, Zahanati (Kituo cha Afya kijacho) Kagoma ambayo ipo kata sasa Ofisi ya CCM Kata, Ofisi za Serikali, Kata na vijiji Kagoma na Nsisha. Shule ya msingi Kagoma, Misikiti miwili, Makanisa na vitu vingine vingi. Naomba Kagoma sasa ipate umeme wa *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, pili, naomba pia Serikali inagalie suala zima la kupeleka umeme kwenye shule zangu za Sekondari zinazopitiwa na nguzo za umeme karibu, zikiwemo Izigo Sekondari, Ruhenga, Ibuga ziwenze kuanza masomo ya kompyuta na muda wa ziada wa kujisomea.

Mheshimiwa Spika, tatu, naiomba Serikali ivizingatie vijiji vyote vinavyopitiwa na nguzo za umeme vikiwemo, Ruhanga, Bushumba, Bushangala na vingine vingi.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iangalie kwa karibu na kushauriana na wahusika ili tupate umeme wa jua (*solar*), hasa kwa maeneo ambayo bado hayajafikiwa na umeme wa *TANESCO*(gridi).

Mheshimiwa Spika, shule nyingi tulizojenga na zinazoendelea hata sasa na Zahanati nyingi vikiwemo vituo vya afya na kuwaimarisha wajasiriamali waishio vijijini ni vigezo tosha vya kuifanya Serikali iangalie kwa umakini wa kipekee upatikanaji wa umeme wa jua na ufungwe vijijini hali ambayo itabadi haraka maisha ya Watanzania.

MHE. LUCY T. MAYENGA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja. Naipongeza Wizara kwa hotuba nzuri.

Naomba kupata ufanuzi kuhusu masuala yafuatayo, kwanza *TANSOLT* itahamishwa lini kuja Tanzania? Kuna maandalizi gani ya kuhamisha *TANSOLT* kuja Tanzania? Nashauri kabla ya uamuvi wa kuirejesha hapa Tanzania *TANSOLT* ni vizuri kufanyika kwa upembusi yakinifu kuhusu namna wataalam wa kuchonga almasi utakavyotayarishwa sambamba na utaalam wa ku-grade aina mbalimbali za almasi. Swala hili halina budi kushughulikiwa kwa sababu hata ofisi ya *TANSOLT* iliyopo London wataalam Watanzania waliopo pale ni wachache sana. Je, Serikali itafanya nini kuongeza wataalam hao?

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni kuhusu wizi wa mafuta unaotokea katika vituo vya mafuta. Naomba Serikali iweke chombo maalum kitakachotumiwa kupima mashine za mafuta katika vituo vya mafuta. Hii ni kwa sababu baadhi ya vituo vinapunja mafuta pindi watu wanapokuwa wanarusua katika vituo hivyo.

Suala la mwisho ni kwamba kwa nini hivi sasa Serikali inawaachia watu wanatumia *prospective licence* kuchimba madini ya kuuza? Serikali ina mkakati gani kukabiliana na tatizo hilo?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ZUBERI ALI MAULID: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwamtipa naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mchango wangu ni mdogo tu na unahu suala la umeme kwa ujumla katika Visiwa vya Unguja na Pemba, Zanzibar. Bei ya *unit* ya umeme iko juu mno kwa wananchi wa visiwani, tunaiomba Serikali ikae na wenzao wa Visiwani ili kuangalia kwa undani suala la bei ya umeme.

Mheshimiwa Spika, suala la gesi asilia wengi wamelichangia na kwa kweli ni mapinduzi makubwa kwenye suala la nishati kwa ujumla. Liangaleni kwa karibu na linahitaji usimamizi makini.

Mheshimiwa Spika, sina la ziada, naunga mkono hoja.

MHE. WILSON M. MASILINGI: Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Muleba Kusini na kwa niaba yangu binafsi, kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini na Naibu Waziri wa Nishati na Madini, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais, kuiongoza Wizara hii. Nawahakikishia ushirikiano wangu. Aidha, nawapongeza watendaji wote katika Wizara na Mashirika yaliyoko chini ya Wizara hii kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri, atoe maelezo kuhusu Mradi wa Umeme Vijijini, hususan Vijiji vya Tarafa za Kimwani, Nshamba na Muleba, ambao tulielezwa katika Bunge hili kwamba, utapata fedha toka *SIDA* – Sweden. Katika Hotuba ya Waziri, Mradi huu haukutajwa kabisa na hivyo kuwaondolea matumaini wananchi wa Jimbo la Muleba Kusini walioko vijijini.

Mheshimiwa Spika, naomba pia Mheshimiwa Waziri, atoe maelezo kuhusu mkakati wa kupunguza gharama za kufunga umeme katika majumba na gharama za umeme wenyewe. Serikali ifikirie kuwafungia wananchi umeme na kuwakata fedha pole pole. Kwa hiyo, kwa sababu Serikali inakopesheka, ilidhamini Shirika la *TANESCO* ili lipate mkopo kutoka Benki kutekeleza Mpango huu ninaoupendekeza.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali izingatie kikamilifu ushauri wa Kamati ya Bunge kwamba, itenge fedha za kutosha ili *TPDC* wawekeze katika kuchimba na kuvuna gesi. Aidha, *TPDC* iwezeshwe fedha hata kwa mdhamina katika Benki ili tuwekeze hata katika kutafuta na kuvuna petroli. Tusiposhiriki katika kuwekeza kwenye kuvuna gesi na petroli, watoto wetu na wajikuu watatulaani.

Mheshimiwa Spika, naomba nipewe majibu ya kina kwa yote niliyoomba yapatiwe ufanuzi

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. IDD M. AZZAN: Mheshimiwa Spika, pamoja na ponezi kwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii, wakiongozwa na Katibu Mkuu, kwa uandaaji na uwasilishaji wa Bajeti kwa umakini na ufasaha wa hali ya juu.

Kuna jambo ambalo ninahitaji maelezo ya kina, kwa faida ya wapiga kura wangu na ikiwezekana kwa Watanzania wote, nalo ni kuhusu gharama za uwekaji umeme majumbani na kadhalika. Gharama ni kubwa sana, ukilinganisha na uwezo wa wananchi wetu. Ni vyema Serikali ikaangalia uwezekano wa kupunguza au kuondoa kabisa gharama hiyo ya uwekaji umeme au *TANESCO* wapeleke umeme huo na wananchi walipe gharama hizo kidogo kidogo, kuitia bili zao za umeme na ninashauri zitumike luku badala ya mita za kawaida.

Ni vyema *TANESCO* wawe na utaratibu wa kupata wateja wengi, kwa kuondoa kero zisizo na msingi. Ukiwa na wateja wengi utapata faida kubwa. Endesheni *TANESCO* kibiashara huku mkivutia wateja wenu. Jifunzeni kwa wenzeni wa Makampuni ya Simu za Mikononi, jinsi wanavyovutia wateja wao na hatimaye kuwa na wateja wengi kwa gharama nafuu.

Kuhusu vituo vya kuuzia Luku Dar es Salaam, hasa Kinondoni ni vichache hivyo kusababisha misururu mirefu ya wanunuvi. Ni vyema *TANESCO* wakaongeza vituo hivyo ili kuondoa kero hasa maeneo ya Magomeni, Kinondoni, Mwananyamala, Sinza na Tabata?

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni athari ya moto katika majumba ya watu na kuteketeza nyumba, mali na mara nyingine uhai wa watu wetu. Mara nyingi moto unapotokea, inaelezwa kuwa ni kutokana na hitilafu ya umeme; ni vyema *TANESCO* wakaliangalia hili kwa makini ili kuepusha maafa ya moto, lakini ni vyema pia *TANESCO*/Wizara waangalie uwezekano wa kulipa fidia au kutoa kifuta machozi kwa wale walio/watakaoathirika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ANTHONY M. DIALLO: Mheshimiwa Spika, nimeona nimsamehe Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, asije kuninyima nyama kesho, lakini mawili madogo niliyoyasahau:-

Kwanza, Mradi wa Maji toka Mwanza hadi Kahama/Shinyanga, *originally* ilikuwa upate umeme tokeo Misasi hadi Ihelele. Wizara ya Maji ililipa *cost* ya *project* hiyo na nguzo/nyaya zikaletwa. Baadaye *engineers* waliona umeme huo hautoshi toka Bulyanhulu kama *Project* mpya. Sasa swalii; kwa nini *line* hiyo haikuachwa na kuwa *energized*? Kwa nini vifaa hivyo viliondolewa na *TANESCO* wakati vilikuwa vimelipiwa na Mkandarasi kuanza kazi? *Can this be an institutional robbery?*

Pili, Wizara inafanya nini kuongeza matumizi ya gesi kwa mfano, kuondoa kodi ya ushuru kwa magari yanayotumia gesi au kuanzisha *project* ya kutumia *energy serving bulbs* na kupunguza matumizi ya umeme kama walivyofanya Kenya, Uganda, Mozambique na Ghana? *it will save about 30% of our energy consumption. It is time you initiate this project under TANESCO.* Naomba nipewe maelezo yakiwa ni majibu ya kina kwa nyongeza ya mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. BENSON M. MPESYA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba nianze kwa kutamka waziwazi, ninaiunga mkono hoja ya Waziri wa Nishati na Madini, kwa kuwa mara tu baada ya Wizara hii kukabidhiwa Mheshimiwa Ngeleja, yapo mabadiliko makubwa ya utendaji kazi akisaidiwa kwa karibu na Mheshimiwa Adam Malima, Naibu Waziri wake

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa Bodi ya *TANESCO* kuufuta Mkataba wake na Dowans ni *indicator* njema kuwa, kilio cha wananchi wengi kinazingatiwa na Waziri ni msikivu kwa matatizo ya nchi. Nashauri sasa Bodi ya *TANESCO* igeukie suala la *IPTL*, ili Taifa lisiendelee kulipa *capacity charge* ambayo ni kubwa kuliko hali halisi. Aidha, Serikali ifanye maandalizi ya kuinunua kabisa kampuni hii ya *IPTL* ili kupunguza gharama kubwa inayolipwa na Serikali.

Baada ya maelezo yangu ya utangulizi, naomba nitoe ushauri katika maeneo yafuatayo:-

(a) Tatizo kubwa la usambazaji wa umeme katika maeneo mengi ya nchi limekuwa ni uhaba wa nguzo. Naishauri Serikali iamue sasa kukirudisha kiwanda cha nguzo pale Mbeya ili kupunguza gharama za kuagiza nguzo toka Afrika Kusini. Awali bei ya miti ya nguzo Mbeya na Iringa ilikuwa ni ya chini sana na hatua ya kui-*treat* nguzo nayo haikuwa kubwa sana. Ni sababu zipi zinazopelekea kuagiza nguzo toka nje ya nchi? Je, Shamba la Nguzo la Utambalila kule Mbozi, ambalo lilikuwa linamiliikiwa na *TANESCO* lipo katika hali gani sasa; pia nataka kujua nguzo moja toka Afrika Kusini inauzwa kiasi gani mpaka leo hii?

(b) Uingizaji umeme ndani ya nyumba ni kilio cha jamii yote kuwa, gharama zimepanda mno si pungufu ya shilingi milioni moja, pesa ambayo mtu wa chini si rahisi kuimudu. Serikali lazima iwe na *deliberate efforts* za namna ya kupunguza gharama hizi?

(c) Awali bei ya mafuta ya taa, dizeli na petrol zote zilikuwa zinauzwa kwa bei ile ile kwa nchi nzima. Aidha, bei zote zilikuwa zinarekebishwa. Hivi sasa mtu wa Mbeya, ananunua petroli kwa Sh.2,200 kwa lita moja, wakati maeneo mengine ya nchi ni Sh.1,750 - 1,800.

Naishauri Serikali ihawilishe bei zote katika nchi nzima, pia nashauri uwe ni wakati wa kuchimba mafuta yetu wenyewe pale Msambati – Mtwara; tuamue sasa kuchimba mafuta yetu pale Msambati.

(d) Mheshimiwa Spika, naomba sasa nielekeze mchango wangu ndani ya Jiji la Mbeya, hasa maeneo ambayo mpaka sasa hayapati huduma ya umeme.

(i) Itende ni eneo ambalo karibu sana na Kambi yetu ya JKT, umeme uliopolekwa ni wa *Phase I* kwenda Zahanati ya Kata. Wananchi wanashindwa kuutumia umeme huu, shida ya hapa ni kupeleka umeme wa *Three Phase*. Haingii akilini kuwa tumeshindwa nyaya za kupeleka umeme huko Itende, pamoja na ahadi ya Wizara toka 2003, mpaka sasa bado.

(ii) *Iyela One* ni eneo lenye watu zaidi ya 30,000 ndani ya Jiji la Mbeya. Eneo lenye taasisi nyingi za Serikali na Sekta Binafsi. Hitaji lao kuu ni nguzo sita tu, umeme unakuwa tayari na tayari nilikuomba Mheshimiwa Waziri utusaidie katika eneo hili. Ofisi zetu za *TANESCO* Mkoa, hawana uwezo wa kulimaliza eneo hili, naomba *intervention* ya Mheshimiwa Waziri.

(iii) Isyesye – toka 2004 tuliahidiwa kuwa maeneo haya ni *prime area* na hitaji kubwa ni huduma ya umeme. Tumepima viwanja 1,500 vipyta kwenye maeneo haya, kama sehemu ya Mpango wa Mradi wa Kupima Viwanja. Naiomba Serikali, ili kuleta *cohesion* ya shughuli za Serikali, ninaomba sana eneo hili lipatiwe umeme, tayari ombi langu limewasilishwa kwako.

MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninamshukuru Waziri wa Nishati na Madini na Viongozi wote wa Wizara hiyo. Baada ya pongezi hizo, nitaendelea na hoja ifuatayo:-

Mji wa Kigoma ulikuwa giza mwaka 2007 (Novemba – Desemba). Aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Karamagi, alikuja Kigoma katika mkutano wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Mkoa na akaahidi kuwa, wameagiza jenereta kubwa la kuweza kuhimili Mji wa Kigoma. Akaahidi pia kuwa, baada ya miezi 18, jenereta hiyo itakuwa tayari.

Sasa Mheshimiwa Waziri katika taarifa yake amesema jenereta hiyo itakuwa tayari mwishoni mwa mwaka 2009, ina maana kutokana na ahadi tuliyopewa ilikuwa ni mwezi Septemba, 2009. Ina maana katika hotuba hii, pesa bado haijatumwa ili jenereta hizo zitengenezwe. Inaonekana kama haijulikani vizuri ni lini tutapatiwa jenereta hizo.

Mheshimiwa Spika, tunaiomba Serikali na sisi ituone kama binadamu wa mikoa mingine. Baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja.

MHE. KIUMBWA MAKAME MBARAKA: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia uhai na uzima na kunipa uwezo wa kuchangia Hotuba hii ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru tena wapiga kura wangu, Akina Mama wa Mkoa wa Kusini Unguja, kwa juhudhi kubwa wanazozifanya, kwa kunisaidia katika kazi zangu na mimi sina budi kuwasemea yale walijonitura.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna kilio kikubwa cha umeme, ambao umepanda bei. Ilikubalika kutumia bei inayozungumzwa, wananchi watashindwa kutumia nishati hiyo ambayo ni muhimu katika kukuza uchumi na kumwongezea kipato mwananchi.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ni kueneza umeme katika vijiji vyote vya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Serikali ya Zanzibar, imechukua juhudhi kubwa kuitekeleza Ilani hiyo na imefanikiwa. Juhudi hizi zitakuwa hazina maana, kwa sababu wananchi watashindwa kuutumia umeme kutokana na bei. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali irudishe bei hiyo na ibakie kama ilivyokuwa hapo awali. Kama kuna matatizo mengine, Serikali wayakabili wao na wasitupiwe wananchi.

Mheshimiwa Spika, kaulimbiu ya Chama chetu cha CCM ya Ari Mpya, Kasi Mpya na Nguvu Mpya, baada ya mfumko wa bei ya chakula, mafuta na hivi sasa umeme; Zanzibar inazungumzwa vibaya na watani wetu na hali imekuwa mbaya kwa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, suala hili liangaliwe kwa makini kuinusuru Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, natamka kwamba, naunga mkono hoja.

Hii ni Wizara moja ambayo ina sura ya Muungano, lakini bahati mbaya sio ya Muungano.

Zanzibar ambayo ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano, inategemea nishati ya umeme kwa asilimia mia moja. Ingekuwa ni jambo la busara na kuijali Zanzibar, kama Mheshimiwa Waziri angelitaja japo kidogo, maendeleo yaliyopo na kasoro zake kwa faida ya Wazanzibari.

Tuseme hilo kwa Mheshimiwa Waziri sio muhimu, lakini ninachoelewa ni kwamba, Zanzibar imetumia fedha zake nyingi, kuweka miundombinu ya umeme ulioanzia Bara kuititia baharini hadi Zanzibar yenewe. Kuna mitambo, majengo na nyaya za umeme, zote ununuzi na ujengaji wake ni wa fedha za Zanzibar.

Kinachoshangaza, kwa vile vifaa na majengo yaliyopo sehemu ya Tanzania Bara vyote ni mali ya Tanzania Bara na inapotakiwa ieleweke vimekuwa hivyo kwa namna gain, basi *TANESCO* haitoi jibu la kiungwana. Sio hivyo tu, vifaa hivyo kama nyaya ambazo zimekekwa kwa fedha za Zanzibar na kutumika kwa kusambaza umeme maeneo ya Tanzania Bara, hakuna lugha nzuri au hata fidia inayoelekezwa kwa mmiliki wa asili wa mradi ule.

Kama hayo hayatoshi, bado hakuna uwazi unaoeleweka kama Zanzibar Shirika lake lizungumze na *TANESCO* kama ilivyo tangu awali au izungumze na *EWURA* au panapotokea mambo mazito yazungumzwe na Serikali zetu mbili?

Mheshimiwa Spika, ingawa Mheshimiwa Waziri, hakutaka haya yaeleweke lakini ni vyema ajue kwamba, haya yapo na Wananchi wa Zanzibar wanataka waelewe wanaelekewa wapi, kwani wanategemea umeme kutoka Wizarani na Mradi mwingine unakuja kati ya Tanga na Pemba.

Mheshimiwa Spika, suala la utafutaji wa mafuta na gesi asilia ni la Muungano kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini kwa namna lilivyowekwa ndani ya Kitabu cha Mheshimiwa Waziri, Uk.50 ni kama suala jepesi, halina maelezo ya kina, wala uzito wowote. Hata hivyo, tumefarijika kidogo kusoma Kiambatisho I cha Taarifa ya Kamati ya Rais ya kuishauri Serikali kuhusu usimamizi wa Sekta ya Madini.

Nimegundua udhaifu uliokuwepo hapo nyuma; vyombo ambavyo si vya Muungano kupewa kazi nzito ya Muungano. Mfano, *TPDC* kutiliana saini na Kampuni ya Canada kutafuta mafuta Zanzibar au Shell kushinda zabuni ya Vitlo – huko Zanzibar mwaka 2002 ili itafute mafuta. Sijui aliyetao zabuni hizo ni nani; ni Wizara za Muungano au Shirika ambalo sio la Muungano?

Nadhani kasoro hizi na nyingine, zimeonekana na kujadiliwa vya kutosha na ndio maana Mheshimiwa Waziri, asiwe na mengi ya kueleza.

Namtakia kila la kheri Mheshimiwa Waziri na kwa hili la mafuta, tunasubiri kwa hamu kukamilika kwa kazi ya Kampuni ya AUPEC Novemba, 2008, kwani gesi asilia tayari tunayo Watanzania.

MHE. AZIZA SLEYUM ALLY: Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Watendaji, pamoja na Waziri na Naibu Waziri, kwa kazi kubwa wanayoifanya. Naipongeza Wizara kwa muundo mzuri wa ugawaji wa viwanja vya kuchimba madini bila ya kugonganisha Kampuni au watu binafsi, licha ya kuwa na malalamiko madogo madogo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia yafuatayo:-

Kwanza, suala la *solar*; naomba kuishauri Serikali iangalie namna ya kuondoa kodi kwenye *solar*. Napenda kuifahamisha Serikali, suala la umeme vijijini litachukua muda sana kufika, huo ndio ukweli. Kama kodi itatolewa, wananchi wataweka *solar* katika majumba yao, kwani mwananchi wa kawaida atatumia mobile *solar* ambayo ni ndogo, atawasha *bulbs* zake sita na hakuna mambo makubwa zaidi ya kuiweka juani. Kwa hivi sasa, unapata kwa shilingi laki mbili, tatu mpaka tano, kulingana na matumizi yako. Kwa kuzingatia hayo, naomba nifahamishwe kama Serikali itaitoa kodi hiyo?

Wakati tunapitisha Sheria ya Kupeleka Umeme Vijijini, nilichangia haya sikupata majibu nadhani kipindi hiki mtajibu kiutendaji na sio kisiasa, wananchi wanapata shida kubwa. Ninashauri tutoe kodi ili umeme wa *solar* uweze kuwafikia wananchi wa vijijini, ambapo kila mmoja kwao hakuna umeme huo kijijini alikotokea; ni baadhi tu wanaopata umeme, tukubali kubadilika ili wananchi wabadilike. Natarajia majibu.

Pili, Mheshimiwa Spika, kuna nini huko Madini; Sera na Sheria ya Madini imekuwa kitendawili. Muda ni mrefu, kila Bunge miaka inaenda, miezi inaisha hakuna Sera wala nini; huo upembuzi yakinifu haujaisha tu; mtapembua mpaka miaka mingapi ili mlete Sera hapa Bungeni?

Naomba kufahamu ni lini Sera hiyo italetwa hapa Bungeni na Kamati/Tume ilishaundwa pesa zilishatumika, majibu na utekelezaji wa Sera hiyo hauna kitu. Naomba kufahamu.

Serikali iwaeleze wananchi; umeme utafika Nzega lini ili wasikie kauli ya Serikali hapa Bungeni; wao wapate wana nini na Bukene wakose wana nini?

Serikali imefanya utafiti kujua mikoa ipi ina madini na ni madini gani?

Serikali inapotoa mrabaha huzingatia nini katika maeneo hayo na pesa hizo zinatolewa taarifa kwa wananchi kushirikiana na Halmashauri?

Kwa kuwa wananchi wengi hulalamikia wawekezaji wa madini maeneo husika na kuna sehemu wawekezaji hao wanatoa misaada hiyo; je, Serikali inaweza kuanza kutoa mchanganuo wa kila maeneo na wanavyochangia ili kupunguza migogoro isiyi ya lazima na kutoana mashaka?

Serikali imeandaa vipindi vingapi vya *TV – Radio* ili kuwaelimisha wananchi kuhusu upandaji wa umeme, kuvuta umeme, faida ya wawekezaji migodini na mafanikio ya wanaozunguka migodi hiyo?

Kwa kuwa *EWURA* ndiyo inayoidhinisha upandaji wa bei na kabla haijaidhinisha, *TANESCO* wanapandisha na kuanza kutoza pesa hizo. Unasema nini kwa hilo; nina ushahidi na Serikali imekaa kimya?

Kutoka ndani ya Hotuba ya Waziri Uk.23, kipengele cha 43, kuhusu Serikali kuilipa *IPTL*, *capacity charge* ni zaidi ya kiasi kilichostahili na kukiri kuwa huo ndio msingi wa mgogoro. Mazungumzo ya *TANESCO* na *IPTL* ni kuvunja mkataba si lingine; na kama utaendelea maana yake hakuna faida ya kujua kama kuna ulipaji hewa (na hasara ya kiasi gani mpaka sasa walicholipwa na pesa hizo zitarudishwa lini Serikalini na kwa muda gani)?

Mpaka sasa Serikali imeshawasaidia wachimbaji wadogo wangapi; wako wapi na kiasi gani; na wachimbaji wadogo wangapi wamepimiwa viwanja na wapi; na kwa thamani gani?

Mapato katika migodi yanatozwa na nani na yanalipwaje; kuitia *TRA* au Wizara yenye?

Kwa kuwa katika migodi hiyo kuna mwakilishi wa Serikali; kuna matatizo gani yaliyojitokeza na akaisaidia Serikali kuzuia ukiukaji wa kudhulumu nchi yetu; amesaidiaje Mwakilishi huyo?

Je, machimbo yote yanahakikiwa kabla hawajaondoka hapa nchini?

Taasisi ya Madini imeiingizia Tanzania kodi ya kiasi gani kwa miaka miwili iliyoisha; dhahabu, almasi, *Tanzanite* na kadhalika.

MHE. CASTOR R. LIGALLAMA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda niwapongeze Waziri, Mheshimiwa William Ngeleja, Naibu Waziri, Mheshimiwa Adam Malima, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wa Wizara hii, kwa hotuba yao nzuri.

Mimi nitajikita katika suala la nishati ya umeme, kwa sababu Wilaya yangu ina migodi miwili yenye kufua umeme, ingawa wenye bado tuko gizani. (Kidatu na Kihansi).

Nishati ya umeme ni muhimu katika ku-support mipango mizuri ya kilimo katika mchakato mzima wa kuanzisha *AgroProcessing Industries*. Naomba Waziri, katika majumuisho yake, anijibu maswali yangu yafuatayo:-

Kwa kuwa Mgodi wa Kihansi, kwenye *switchyard* kuna kila kinachohitajika kuwezesha umeme kusambazwa kwa kujenga *transmission lines* na kuweka *transformer* katika kila kijiji ambako umeme unapelekwa. Vifaa vilivyopo *switchyard* ni *Transformer* yenye ukubwa wa *MW 8.5; 33KV BAR; Sparefeeders* zenye njia tatu; na *Circuit Breakers*.

Je, ni sababu zipi ambazo Wizara inaweza kuwaeleza Wananchi wa Wilaya ya Kilombero (hasa vijiji vilivyo jirani na Mgodi huo wa Kihansi) za kuwanyima umeme?

Nimewahi kuandika *Feasibility Study Report*, yenye kueleza kwa nini *Electrification* ya vijiji katika Kata ya Mchombe, Chita, Mlimba, Utengule, Mofu na Idete ni muhimu kiuchumi, kijamii na kiufundi. Nilitegemea Wizara ingenisaidia hata kama ikishindwa, basi hata vijiji vilivyo pua na mdomo na Mgodi kwa kuzingatia ndivyo vilivyotoa nguvukazi wakati Mgodi unajengwa.

Consumption ya umeme katika Mji Mdogo wa Mlimba, pamoja na eneo la Mgodi wenyewe ni *0.8 MW* tu, kiasi cha kuacha *transformer* hiyo ya *MW 8.5* kuwa *underutilized*.

- Katika Jedwali Namba 9 ukurasa 79, umeonyesha maeneo ambayo Wilaya yangu itanufaika chini ya Mpango wa *MCC*.
- Hapa napenda kuwashukuru kwa nia nzuri ya kutaka kunisaidia. Lakini ukiondoa Mji wa Ifakara, maeneo mengine yalijotajwa siyo yangu.
- Illovo Sugar wanazalisha umeme kutumia *bagasse*, sasa sijui wanataka kufanyiwa nini ikiwa na wao wanaiuzia umeme *TANESCO*?
- Naomba sana Waziri katika majumuisho yake, anieleze ni vijiji gani hasa alitaka kunisaidia katika Wilaya yangu. Naamini hao walioandaa bajeti walikuwa na ramani. Ikiwa eneo au Jimbo langu halifahamiki, Waziri atakuwa tayari kunishirikisha ili idadi ile ile ya vijiji ambavyo si vya Wilaya yangu, niweze kusaidia kuvitaja na kuingizwa kwenye Mpango huu.
- Ni muhimu Waziri alifafanue hili kwenye majumuisho yake, la sivyo, itabidi niombe ufanuzi wakati Bunge litakapokaa kama Kamati ya Matumizi leo.
- Kwa kusaidia ikiwa itakuwa vigumu kupata ramani, vijiji vinavyokaribia Mgodi ni vifuatavyo: Udagaji, Chita, Chita JKT, Ikule, Kidete, Mkangawalo, Mchombe, Mngeta, Lukolongo, Njage, Mbingu, Mofu, Nanwawala, Idete, Ihanga mpaka Lumemo

Ifakara. Upande wa pili ni Chisano, Kalengakero, Mlimba na vitongoji vyake; Mpanga, Utengule na Ngalimira.

- Vijiji hivi viwo kwenye barabara moja ambayo ni barabara kuu kutoka Ifakara – Mlimba – Utengule – Ngalimira.
- Wilaya yangu ina mashamba makubwa matano; Gereza la Idete (Ha 10,000); Shamba la Ruipa (Ha 20,000); Shamba la Mngeta (*Kilombero Plantations Ltd.* 6,000 Ha); Shamba la JKT Chita (Ha 10,000+); na Shamba la Mpanga (Ha 15,000+).
- Kama Mkoa wa Morogoro umepangwa kuwa ghala la Taifa, hatuwezi kuhamasisha kilimo bila kuingiza umeme katika suala zima la *Agro Processing Industries*.
- Tunaomba Wizara kwa makusudi, iunge mkono wito wa Rais Jakaya Mrisho Kikwete wa kuufanya Mkoa wa Morogoro kuwa ghala la chakula (*National Granary*). Kwa kiasi kikubwa, ukiongelea kilimo Mkoa wa Morogoro, unaongelea Kilombero, Ulanga na Kilosa, ambako kuna mabonde makubwa yenye rutuba kwa ajili ya kilimo.

MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA: Mheshimiwa Spika, naungana na wenzangu kutoa pongezi za dhati kwa Waziri, Naibu Waziri, pamoja na Watendaji wa Wizara hii, kwa kuandaa taarifa hii nzuri na inayofahamika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizi, nathubutu kusema kuwa, bajeti hii kwa upande wa kazi za maendeleo ni bajeti tegemezi kwa asilimia kubwa, tangu bajeti ya mwaka 2007/08 na mwaka huu pia imeendelea kuwa tegemezi.

Mheshimiwa Spika, Waziri anaweza vipi kutuhakikishia kama fedha hizo za nje zitapatikana na zisipatikana, haoni kuwa kazi zilizopangwa kutekelezwa zitashindwa kama ilivyokuwa mwaka 2007/08? Serikali iondokane na utegemezi. Ni afadhali ikope kuliko kutegemea wafadhilli.

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* inatoza fedha nyingi sana (Sh. 600,000) kwa ajili ya kumuingizia mteja umeme bila kujali hali za wananchi. Serikali ipunguze gharama hizo. Umeme sio anasa, bali ni kitu muhimu kwa maendeleo.

Mapendekezo ya Kamati ya Rais ya Kuishauri Serikali kuhusu Usimamizi wa Sekta ya Madini, yafanyiwe kazi kwa kina na utekelezaji wake usicheleweshwe hasa kwa mapendekezo ambayo yanahitaji utatuzi wa haraka.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nampongeza Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Ngeleja na Naibu wake, Mheshimiwa Malima, Katibu Mkuu na Wataalam wote wa Wizara, kwa kuandaa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kigoma una Wilaya tatu; kati ya wilaya hizo ni Wilaya moja tu ndiyo yenye umeme wa *generator* nayo ni Kigoma Mjini.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kasulu na Wilaya ya Kibondo, hazina umeme kabisa. Hivyo, ninaiomba Serikali ituambie ni lini Wilaya hizo mbili zitapewa umeme wa *generator*?

MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN: Mheshimiwa Spika, nianze na utangulizi ya kwamba, nchi yetu ina bahati kubwa ya gesi nyingi, tulioigundua wakati huu muafaka, kwani hivi sasa dunia yetu ipo kwenye janga kubwa la upungufu wa mafuta. Bahati mbaya, hali hii inaendelea kwa kasi kubwa na sijui mwisho wake utatufikisha wapi?

Kwetu sisi naona ni wakati muafaka kabisa, tukaanza kujipanga vizuri ili tuweze kuitumia fursa hiyo na ni vyema tukaanza kuitumia gesi hiyo kwa masuala ya usafiri na mambo mengineyo, badala ya kuendelea kutegemea mafuta. Ili kufanikisha wazo hili, ingelikuwa vyema Wizara husika ikaandaa miundombinu haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, gharama za uzalishaji *TANESCO* ni tatizo na kero kubwa kwa wananchi wetu na moja ya sababu ya kupanda kwa bei hizo ni gharama kubwa ya nyaya na nguzo za umeme. Kusema ukweli, siyo haki kabisa kuwabebesha gharama hizo wananchi. Kuwatoza gharama wananchi ni ukiukaji wa haki za binadamu na utawala bora.

Ningeshauri ya kuwa, kama *TANESCO* haina uwezo wa kugharamia gharama hizo, ingelikuwa vyema ifanye mkataba na mwananchi mhusika ili gharama wakakatane kwenye *units* ambazo angetumia mwananchi huyo, itakayolingana na gharama zilizofanywa.

Mheshimiwa Spika, usafirishaji wa umeme kutoka Ras Kilomon hadi Ras Fumba; waya huu hivi sasa umechakaa na muda wake wa matumizi umeshapita. Hivi karibuni, tulishuhudia janga kubwa la kukosekana kwa umeme huko Zanzibar na hii ilituathiri sana kiuchumi na kijamii. Hili liwe somo kubwa kwetu Chama Tawala, kwani tulishuhudia jinsi Upinzani walivyolifungia njuga, kwa kuitumia hali hiyo kama fimbo na kejeli kwa Chama Tawala. Badala ya kusikitika, Wapinzani wetu walifurahishwa sana na hali hiyo na walithubutu kuyabeza mazuri yote yaliyofanywa na Chama Tawala.

Mheshimiwa Spika, kwa unyenyekevu kabisa, namwomba Mwenyezi Mungu, asitujaalie hali kama hiyo ikatokea wakati wa uchaguzi ujao. Naomba kuishauri Serikali yetu sikivu, itathmini hali ya *sub-marine cable* hiyo na ikiwezekana iwekwe *cable* mpya ili hali hiyo isitokee tena.

Mheshimiwa Spika, wazo la kuzalisha mkaa ni zuri sana, lakini masuala ya uharibifu wa mazingira yazingatiwe kwa kina, kwani hivi sasa kuna uchafuzi huo Kiwira, unaotokana na moshi mchafu unaotokana na kuchomwa kwa mkaa huo.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango wangu huo, naomba kuunga mkono hoja hiyo.

MHE. MARYAM S. MFAKI: Mheshimiwa Spika, kwanza, nachukua nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa jitihada wanazofanya katika Wizara za kusimamia kazi ambazo matokeo yake yanaonekana kwa wananchi, kwa mfano, kusitisha Mkataba wa Dowans. Vilevile inaonekana wanaendelea kusoma mikataba yote ya Wizara na hata kubaini kasoro ya Mkataba wa *IPTL*. Hii inaonyesha wazi, jinsi Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, wanavyokerwa na mikataba mibovu. Mimi nawatakia kila la kheri na Mwenyezi Mungu atawalinda.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa nachangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, inavyoonekana nchi yetu imejaliwa na Mwenyezi Mungu, Nishati na Madini mengi ndani ya ardhi yetu, kwa sababu siku hadi siku, kunagunduliwa maeneo mapya yenyeye madini kama vile Winza Wilayani Mpwapwa na kadhalika. Mimi ningependa kujuu, kama kuna madini mengine yameendelea kugunduliwa na naomba orodha ya machimbo ya madini yanayochimbwa na ambayo yamegunduliwa katika maeneo mbalimbali. Pamoja na hayo, naishauri Serikali iendelee kufanya utafiti wa nishati na madini na yanapopatikana, yatangazwe na yaweze kupata wawekezaji na hii itawezesha kuongeza Pato la Taifa.

Kuhusu kuongezeka kwa gharama za kuvuta umeme, ambao unasababishwa na kupanda kwa gharama ya nguzo, tungeomba Wizara ifanye utafiti wa aina ya miti kama miyombo iliyopo katika maeneo mengi, ambayo ikitiwa dawa inaweza kutumika kwa kazi hiyo.

Naipongeza Serikali kwa kuanzisha Mfuko wa Mzunguko wa Mikopo. Naomba Mfuko huo, usambazwe machimbo yote yakiwemo machimbo ya Winza Wilayani Mpwapwa. Mfuko huo usimamiwe vizuri ili uweze kufaidisha walengwa.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iongeze kasi ya kusambaza umeme katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Dodoma, ikiwepo Wilaya mpya ya Bahi. Kuna baadhi ya maeneo ambayo ni rahisi kuwfakishia umeme kama vile Wilaya ya Kondoa, ukianzia ule umeme uliopo Bolisa, ukaenda Kolo ukafika Mnenia, Pahi, Busi, Mondo na kufika Kondoa na kutoka tena Kolo kwenda Bereko na kuunganisha na Wilaya ya Babati. Kwa Mpwapwa, unaweza kusambazwa vyema. Nawatakia kila la kheri na muendelee kufanikisha kazi hii. Naishauri Serikali iweke utaratibu; wawekezaji wawe na ubia na Watanzania na hiyo iwe ni Sheria na kama Sheria haipo, basi itungwe ili Watanzania wawe ni walinzi wa mali yao na watadhibiti kitakachopatikana na kodi italipwa kihalali.

Matumizi ya gesi asilia ambayo sasa hivi imeongezeka, tunaomba Serikali ifanye utafiti hasa kwa njia nyepesi ya kupata majiko ya kutumia gesi yawe ya bei rahisi yatumike vijijini ili kupunguza matumizi ya mkaa na kuni ili kuokoa ukataji wa miti na mazingira yabaki salama. Tatizo ni bei ghali ya majiko.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iendelee kupitia mikataba na kipingele cha *Capacity Charge*, ambayo inalipwa fedha nyingi. Kwa nini wakati mitambo imewekwa katika ardhi yetu halafu tulipie tena? Vipengele kama hivyo vifutwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia.

MHE. CLEMENCE B. LYAMBA: Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, kwa mpangilio mzuri sana wa hotuba yake, ambayo imegusa Sera, Mipango na Utekelezaji wa utoaji huduma mbalimbali kwa wananchi kwa kupitia Watumishi wa Wizara yenyewe na Mashirika yaliyo chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, lililonikuna zaidi ni namna hotuba ilivyorejea mara kwa mara, maelekezo yaliyomo katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2005 katika kuonyesha hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa Miradi mbalimbali inayosimamiwa na Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nampongeza pia Naibu Waziri, Mheshimiwa Adam Malima na wataalamu wote wa Wizara na *TANESCO*, kwa kumsaidia Mheshimiwa Waziri, kufanikisha majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wengi wanatambua jitihada za Wizara kuongeza kasi ya kupeleka umeme vijijini, kwa sababu magari mengi zaidi hivi sasa yanaonekana barabarani yakiwa yanasarifisha nguzo za umeme kutoka eneo moja hadi jingine na hali kadhalika nyaya za umeme. Vitendo hivi vinaongeza imani na matumaini kwa wananchi kuwa, hatua kwa hatua, sasa umeme unasambazwa kwenda vijijini kwa *speed* kubwa zaidi kuliko ilivyokuwa miaka michache iliyopita.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Serikali kusimamia kazi hii na tunaomba jitihada hizi ziendelee ili kuwaletea Watanzania maisha bora.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa kuitikia maombi ya umeme ya Wananchi wa Vijiji vya Kivungu (Kata ya Kilangali), Masanze Sekondari (Kata ya Masanze), Kondoaa (Kata ya Mabwerebwere), Kisanga (Kata ya Kisanga) na Kitete (Kata ya Ruhembe), ambayo niliyawakilisha kwa nyakati tofauti mwaka 2006 na mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, kufuatia maombi haya, *TANESCO* wamekwishachukua hatua za kupata *transformer* inayohitajika kufungwa Kijiji cha Kivungu ili umeme uweze kuunganishwa baada ya kupeleka nguzo za umeme. Nguzo za umeme zimeanza kupelekwa Masanze Sekondari; ambapo katika bajeti ya 2008/09, upelekaji umeme katika Vijiji vya Kondoaa, Kitete, Kisanga na Msolwa Sekondari utaanza.

Mheshimiwa Spika, huu utakuwa ni ukombozi mkubwa sana kwa wananchi wa vijiji husika, kwa sababu nyingi, kama vile; wanafunzi wataweza kujisomea usiku,

mashine za kukoboa na kusaga zitanunuliwa na kupunguza adha za kupata unga wa nafaka kwa ufanisi zaidi na kadhalika. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa hatua hizi.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atoe ufanuzi; Miradi ya Umeme inayofadhiliwa na *MCC* katika Wilaya ya Kilosa (ukurasa 79) kwa sababu Vijiji vya Msolwa Sekondari, Kisanga na Kitete ni vijiji vilivyomo katika Wilaya ya Kilosa, lakini katika ukurasa 79, vijiji hivyo vimeonyeshwa kuwa vimo katika Wilaya ya Kilombero, ambapo sio sahihi.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa, naomba Mheshimiwa Waziri atamke masahihisho husika.

Mheshimiwa Spika, ili kuwawezesha wanavijiji wengi nchini kuvuta umeme katika nyumba na makazi yao, naiomba Serikali itoe Ruzuku kwa gharama za kuunganisha umeme na gharama za nguzo zinazotakiwa kulipwa na mteja. Hii inatokana na hali ngumu ya maisha inayowakabili wanavijiji, kwa sababu ya mfumko mkubwa katika uchumi duniani kote, ambapo nchi maskini zaidi kama Tanzania, wananchi wake wanaathirika kwa kiasi kinachotisha.

Mheshimiwa Spika, endapo Serikali itashindwa kutoa ruzuku, basi ifikirie kuweka utaratibu wa kuwakopesha wanavijiji gharama za nguzo na kuunganisha umeme kwa udhamini wa Serikali. Hili linawezekana kwa kuwashawishi wanavijiji kuunda vikundi katika mpango huu. Naiomba Serikali ilifikirie suala hili, ili fursa ya kuwepo kwa fedha za *MCC* itumike kuwaletaa wananchi wengi huduma hizi.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanapochelewa kulipa ankara zao *TANESCO*, hudaiwa riba. Kwa mfumo huo huo, naiomba Serikali iilekeze *TANESCO* kuwa na sera kwamba, endapo kuna wateja wanaotaka kulipa gharama za umeme *in advance*, wapewe *discount* inayostahili, ili kuwahamasisha wenye uwezo huu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kugundulika kuwa *IPTL* ilikuwa na *equity* ya Sh.50,000 tu, namwomba Mheshimiwa Waziri, wakati akijibu hoja, alieleze Bunge lako Tukufu ni kwa nini ugunduzi huu umechelewa kwa muda mrefu, kiasi cha zaidi ya miaka mitano? Je, mbini ipi ilitumika kuificha taarifa hii au kulikuwa na watumishi waliofahamu wakala njama kuificha taarifa hii? Hatua gani za kinidhamu zitachukuliwa dhidi ya wahusika, endapo itabainika kulikuwa na njama katika jambo hili, kwani, mahesabu ya *IPTL* hayakuweza kuonyesha hali hii?

Mheshimiwa Spika, napendekeza watumishi waliogundua kuwa *equity* ya *IPTL* ilikuwa Sh. 50,000 tu, wazawadiwe kwa kuibua ukweli huu, ambao utaliokolea nchi yetu na wananchi wake gharama kubwa.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali iingize katika bajeti ya 2008/09 na 2009/10, Mpango wa Kupeleka Umeme katika Kijiji cha Uleling'ombe (Kata ya Waling'ombe), kwa sababu mwekezaji *M/S Kastan Mining Company Ltd.* iko mbioni

kujenga kiwanda cha kuchimba *copper* na madini mengine. Kiwanda hiki kitatumia umeme mwangi sana.

Mheshimiwa Spika, Mpango huu ukiwezekana, njia itakayofaa kuutoa umeme huu inaelekea kuwa ni Mji wa Mikumi. Kwa maana hii, fursa hii itawezesha ku-*extend* umeme kwa viji vya njiani na jirani kama vile Madizini, Kikonga (Kata ya Kisanga), Kitunduweta, Mhenda, Ilakala hadi Ulayama na Nyameni (Kata ya Ulaya); Zambo, Nyali, Madudumizi na Ivuma (Kata ya Zombo).

Mheshimiwa Spika, Kata za Ulaya na Zombo ndio *Bread Basket* ya kuzalisha mahindi, ufuta na alizeti kwa wingi Mkoani Morogoro (Wilaya ya Kilosa). Uzalishaji utaongezeka sana na kusaga nafaka ambazo hulimwa mara mbili kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naiomba Serikali/TANESCO ipeleke umeme Kata ya Vidunda, ambayo Bwawa la Kidatu linapakana nayo na nguzo za umeme zinazokwenda Iringa, nyaya zinawapita juu, wao wakiwa walinzi wa maeneo hayo na rasilimali hizo.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huu, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. ELIZABETH N. BATENGA: Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Waziri na Naibu Waziri. Aidha, nawapongeza Wataalam wote kwa kuwasilisha hotubu nzuri, inayoelekeza wazi utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi katika Sekta ya Nishati na Madini. Tunasubiri utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, Wilaya za Ngara, Biharamulo na Chato, zilipatiwa umeme miaka minne iliyopita lakini haujaweza kusambazwa katika maeneo makubwa zaidi ya Makao Makuu ya Wilaya, kutokana na majenerata kuwa mabovu kwa uchakavu (yaling'olewa Babati na Kondoa) na hivyo kushindwa kufanya kazi.

Naushauri na kumwomba Mheshimiwa Waziri, afute wazo la kuleta majenereta yaliyokuwa Mtwara na Lindi, kwenye Wilaya za Ngara na Biharamulo bali atafute njia nyingine za kusaidia Wilaya hizi, kwa vile nina hakika hayo majenereta nayo ni chakavu kwa kuwa hata huko yalikokuwa, walikuwa wakilalamika

Mpango wa muda wa kati kulingana *PSMP* kuhusu kuzalisha umeme na MW 60 eneo la *Rusumo Falls* ndiyo suluhisho la tatizo la umeme katika Wilaya ya Ngara na kuwasaidia uendeshwaji wa Mgodi wa Kabanga Nickel. Mpango huu uharakishwe.

Mheshimiwa Spika, bado Serikali haijaonyesha kusikia kilio cha wananchi kuhusu gharama kubwa za kuvuta umeme. Nguzo zimepanda bei na wananchi wanalazimika kugharamia nguzo zote zinazowezesha umeme kufika kwake, hata kama zinapita maeneo ambayo kuna watu ambaeo baadaye watavuta umeme. Naomba suala hilo liangaliwe, utaratibu uwe kama zamani.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kutumia gesi kwa kuendesha magari uharakishwe.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuufuta Mkataba wa Uzalishaji Umeme wa *Dowans*. Serikali iendelee kuangalia Mikataba mingine *IPTL* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nawatakia utekelezaji mwema. Naunga mkono hoja.

MHE. ESTHERINA J. KILASI: Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa William Ngeleja, Waziri wa Nishati na Madini na Naibu Waziri, Mheshimiwa Adam Malima, kwa kazi nzuri na kwa kweli wameanza vizuri sana, tunategemea mabadiliko makubwa. Nampongeza Katibu Mkuu na Wataalamu wote, kwa jitihada za kutekeleza majukumu ya Wizara hii yenye changamoto nyingi. Naomba niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Hotuba ni nzuri sana, ila naomba ufanuzi kwa Mradi wa Umeme ulioanza mwaka 2002 na kuzinduliwa rasmi na Mheshimiwa Makamu wa Rais, Wilayani Mbarali, kama ndio umeishia hapo au kuna mpango gain, kwani nimepitia kwenye Hotuba ya Waziri na Kitabu cha Maendeleo sikuona mahali popote ambapo Mradi huu unatajwa au kupangiwa pesa yoyote?

Tulikwishafanya majadiliano na Waziri, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Mkurugenzi na Watendaji wa *TANESCO* na kuwapa mahitaji yanayohitajika ili kukamilisha Mradi huu wa kupeleka Umeme Mbarali. Nilitegemea bajeti hii ingejumlisha hata Wilaya ya Mbarali, ukizingatia kuwa, wananchi wanaendelea kulipia umeme hasa kwenye Kata ya Rujewa, Usuruku, Mapogoro na Mawindi.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mbarali kuna wachimbaji wadogo wa dhahabu katika Kijiji cha Mabadaga Kata ya Mapogoro. Wamekuwa wakifanya kazi hiyo kwa muda mrefu sana, sioni kama Serikali au Wizara iliwhi kulitilia kipaumbele cha kutembelea eneo hilo ili kutoa ushauri na kuona kiasi na aina ya madini yaliyopo eneo hilo. Naomba Wizara ilifanyie kazi eneo hilo.

MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara iwezeshe kuanza kwa utekelezaji wa Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini, unaofadhiliwa na *SIDA*, pamoja na Serikali yetu. Mradi ninaozungumzia ni ule wa kusambaza umeme Bukoba Vijijini, Missenyi (Nkenge), Karagwe na sehemu ya Wilaya ya Muleba. Mradi huo kwa muda mrefu, umeelezwa kwamba, utatekelezwa na Wananchi wa Ishozi na maeneo mengine ya Wilaya ya Missenyi katika Jimbo la Nkenge, wanasubiri utekelezaji wa Mradi huo. Ikiwezekana, itakuwa jambo zuri Mheshimiwa Waziri, akiwaeleza Wananchi wa Missenyi, Bukoba Vijijini na wengineo, *status* ya Mradi huo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. OMAR SHEHA MUSSA: Mheshimiwa Spika, sina budi kumpongeza Waziri, Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, pamoja na Watendaji wako wa Wizara ya Nishati na Madini, kwa kutayarisha bajeti nzuri, iliyo wazi kuhusu Wizara yako.

Pili, naunga mkono bajeti hiyo kwa asilimia mia moja na mchango wangu utalenga maeneo yafuatayo; nishati ya mafuta na umeme na Sekta ya Madini (Mikataba yake).

Mheshimiwa Spika, maelezo yangu ni kuwa, ipo haja kubwa kabisa kwa Wizara ya Nishati na Madini kuwa makini katika masuala haya mawili, yaani Nishati ya Mafuta na ile ya Umeme.

Kwenye mafuta, Serikali inapaswa kuzingatia mfumko wa bei za mafuto duniani na kutafuta njia ya kupunguza upandaji wa bei kiholela, kwa kuzitaka mamlaka zinazohusika na mafuta kama vile *TPDC* na *EWURA*, kusimamia utarabu mzuri wa biashara hiyo kwa niaba ya Serikali ili kuwapunguzia mzigo wananchi.

Mheshimiwa Spika, kinachotakiwa kufanya ni Serikali kuweka Mfuko wa kupunguza makali ya bei ya mafuta utakaoitwa *Fuel Stabilization Fund*, fedha ambazo zitatomana na sehemu ya kodi za mafuta (mfano Sh. 5 kwa kila lita) ili ziwekwe amana kufidia ongezeko la bei kipindi baada ya kipindi. Hili linawezekana endapo nchi yetu itagawiwa katika *zone*, ili bei zilingane na gharama za usafirishaji kwa kila sehemu ya nchi yetu Tanzania.

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* nayo imebebeshwa mzigo wa kulipa *Capacity Charges* kwenye Mikataba ya *IPTL*, *SONGAS* na kadhalika. Hili tatizo lilikwishapigwa kelele na Wabunge wengi kipindi cha nyuma na hivi sasa ili *TANESCO* iweze kupumua, suala zima la mikataba hii lingebebwa na Serikali na *TANESCO* ikafanyiwa *restructuring* ili iweze kupanga *Business Plan* yake itakayowezesha Shirika hilo kupata faida miaka ijayo na vilevile kuwezesha ubora wa huduma za nishati ya umeme. Pendeleko hili ni vyema lifanyiwe kazi haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, utafutaji wa mafuta nchini unaongozwa na sheria husika, inayosimamiwa na *TPDC* kwa niaba ya Serikali na kwamba tenda zilitolewa siku za nyuma kuyapa makampuni kadhaa fursa hiyo kuelekea Mikataba ya *Production Sharing Agreements (PSA)*. Ni vyema sasa Serikali ikaliarifu Bunge, idadi ya mikataba hiyo kwenye *Blocks* ambazo ziliteuliwa kufanyiwa utafiti wa uchimbaji mafuta na gesi.

Mheshimiwa Spika, wakati umefika hivi sasa Serikali kuliarifu Bunge, hatua ya utafiti ilipofikia juu ya uwezekano wa kuwepo mafuta kule *Block* ya Zanzibar/Pemba na je, mazungmzo ya SMT – SMZ nayo yakoje juu ya jambo hili, kabla ya kungojea Ripoti ya Mshauri aliyyeteuliwa na wananchi wa pande zote mbili za Muungano, wana hamu ya kujua mapema juu ya suala hili?

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Madini nayo inahitaji kutazamwa kwa makini, ili iweze kuchangia mapato, angalau asilimia kumi ya *GDP* (Pato la Taifa). Hivi sasa Serikali inapata mrabaha asilimia ndogo sana, kama ilivyotajwa kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini. Nashauri, baada ya kupata uzoefu wa miaka mingi, pamoja na kujifunza uzoefu wa nchi za Botswana, Ghana na South Africa.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwenye eneo hili lazima iwekeze kila mgodi, ili iwe na sauti kwenye uendeshaji wa biashara hiyo kwa lengo la kujua ukweli wa faida ya biashara hiyo.

Mheshimiwa Spika, mtindo uliojitokeza wa kampuni zenyenye kumiliki migodi, kuonyesha hasara kwenye hesabu zao za kibashara kila mwaka. Huu ni ujanja uliopangwa na lazima Serikali iwe macho, kwani kampuni hizi huwa na kampuni mama (*Parent Companies*), ambazo zipo nchi za nje na zipo *Registered* kwenye *Stock Exchange*, ambapo huonyesha faida wapatazo kwenye biashara ya madini kutoka Tanzania. Huu ni unyonyaji unaofanyiwa Tanzania kwa miaka mingi sasa.

Mheshimiwa Spika, huo ndio mchango wangu juu ya Hotuba ya Wizara ya Nishati na Madini. Naunga mkono hotuba hiyo.

MHE. MAULIDAH ANNA KOMU: Mheshimiwa Spika, kabla ya yote, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara, kwa kazi nzuri ambayo mpaka sasa wanaendelea nayo, japo kuwa muda mfupi tu Waziri na Naibu wake, wamekabitihwa kazi hiyo. Namwomba Mwenyezi Mungu, awe nao na awaongezee hekima na busara na awaondoe kabisa wala wasisogee kwenye kundi la Mafisadi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, nishati ni kitu muhimu sana, kwenye maendeleo ya nchi yoyote, hakuna hata jambo moja litakalowezekana kuleta maendeleo bila ya Nishati ya Umeme kuanzia wakati wa uja uzito, vipimo; wakati wa kujifungua, malezi ya mtoto na hata anapokuwa tayari anataka Elimu, yote haya lazima umeme uwepo.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli umeme umekuwa mateso kwa Watanzania; upatikanaji wa umeme vijijini ni kitendawili; bei ya kuunganisha umeme ni ghali sana; na umeme wenye malipo (*Bills*) ni habari kubwa, kwani hakika Watanzania walio wengi, hawamudu kulipia umeme (Bill za kulimbikiza na bado zinaendelea).

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iangalie upya gharama hiyo na ipungue ili Watanzania walio wengi waimudu.

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha Dharura, yaani (*Emergency*) ni muhimu sana kwa jamii, kwani inapotokea hatari yoyote, hawa inabidi wawahii sana kwenye eneo husika. Lakini ni bahati mbaya, kwani ni eneo ambalo wanazorota sana, mpaka ajali inatokea ndipo wanafika. Je, kuna tatizo gani linalofanya wachelewe? Nashauri wapatiwe vifaa vinavyohitajika (magari) na vifaa vyote muhimu. Wapatiwe pia mawasiliano ya haraka.

Mheshimiwa Spika, natoa mfano wa Kitengo hiki kwa kumwambia Mheshimiwa Waziri, akiangalie upya Kitengo hiki. Eneo la Kingamboni ni eneo linalokua kwa haraka sana, inabidi liangaliwe katika shughuli zake za hatari lazima Wizara iangalie yafuatayo: Ijengwe ofisi ya *Emergency* haraka; kama haiwezekani kwa sasa basi kuwe na gari la dharura na mafundi ambao watakuwa karibu wakati wowote wakihitajika; na waruhusiwe kupita tu pale kwenye Pantoni sio kupanga foleni na wasilipishwe chochote.

Mheshimiwa Spika, umeme ni mzuri unatupa mwanga lakini ni mbaya kwa maisha yetu, inapotokea hitilafu uharaka ni muhimu.

Mheshimiwa Spika, madini kwa kweli kama tutaacha ujisadi, yatatusaidia kuondokana na umaskini, tuna madini mengi sana nchi hii lakini i yamegubikwa na mikataba mibovu. Nashauri tuingalie sana na kusoma kwa makini Taarifa ya Kamati ya Rais ya Kuishauri Serikali Kuhusu Usimamizi wa Sekta ya Madini. Tuitekeleze taarifa hiyo, tuifanyie kazi. Isiwe kama taarifa zinazotolewa halafu zinatiwa kapuni.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie sana madini yetu na kuhakikisha tunaiwezesha *STAMICO* kuangalia siyo wachimbaji wadogo tu hata wakubwa. Tunabiwa sana madini yetu, wenzetu wa nchi nyiningine wanafaidika na madini yetu na sisi tunabaki maskini.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na kuiambia Serikali tena na tena, tusimamie nishati zetu kama gesi asilia na madini yetu tuliyonayo ili Watanzania wafaidike. Ahsante.

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Ngeleja na Naibu wake, Mheshimiwa Malima. Kazi inatia moyo sana, uwezo mkubwa na wanakabalika mbele ya jamii.

Tangu Adamu na Eva, Wananchi wa Mji wa Mbanga, wanaishi gizani. Sasa neema imewafikia. Tunashukuru majenereta mawili yatoayo *MW 3* yanafungwa na baada ya mwezi mmoja mji mzima utapata umeme. Tunalo jenereta dogo linaloendesha umeme Mji wa Mbanga, kwa sasa Wilaya inashauri jenereta hilo ambalo ni mali ya Halmashauri ya Wilaya, mara baada ya majenereta mawili makubwa kufungwa, basi lipelekwe Mji Mdogo wa Mbambabay, ambao ni *potential* kwa baadaye. Umeme wa Mbanga usiishie mjini pekee, bali upelekwe hadi vijiji vya jirani vya Kigonsera, Litembo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

SPIKA: Sasa tumefunga mjadala kutoka kwenye *floor*, tunaingia hatua ya Mheshimiwa Naibu Waziri na baadaye mtoa hoja. Wanazo dakika 75 na wamezigawa dakika 30 Mheshimiwa Naibu Waziri na dakika 45 Mheshimiwa Waziri Mtoa hoja. Kwa hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Malima, Naibu Waziri Nishati na Madini, anayo nusu saa ya kuanza kujibu hoja zilizotoka kwa Waheshimiwa Wabunge.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, naomba kwa heshima kubwa nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia kwenye bajeti hii ya Wizara yetu ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea, naomba nitumie nafasi hii nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano - Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kunituea mwezi Februari, 2008 kuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mazingira na mahitaji ya sekta za nishati na madini kwa wakati huu ninatambua kila siku ya utekelezaji wa majukumu haya kwamba nimekabidhiwa dhamana kubwa na Mheshimiwa Rais kwa niaba ya Watanzania wenzangu, dhamana hii ni heshima kubwa mno kwangu, familia yangu na wapiga kura wote wa Wilaya ya Mkuranga na ninamwomba Mwenyezi Mungu anijalie niifanye kazi hii kwa uadilifu mkubwa na imani kubwa kwa manufaa ya Watanzania wenzangu wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kufanya tathmini ya Wizara yetu kama mnavyofahamu tuna masuala makubwa mawili, yaani Nishati na Madini. Lakini hili la nishati limejigawa pande mbili, tunaliangalia upande wa gesi, matumizi ya gesi asilia na nishati ya umeme.

Mheshimiwa Spika, labda niseme tu awali kwamba kazi ya kujibu hoja ni ya Mheshimiwa Waziri wangu wa Nishati na Madini, lakini kwa ridhaa yake ameniruhusu nzungumzie masuala kwa ujumla na kwa niaba yake nitajibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kuwatambua kila mmoja kwa michango yao ni ya kwake mwenyewe. Wakati tunaanza kutekeleza majukumu haya kitu kimoja kilikuwa bayana kabisa, kwamba Watanzania wenzetu walikuwa na matarajio makubwa na Serikali hii chini ya uongozi wa kazi wa kila siku wa Mheshimiwa Waziri Mkuu Mizengo Kayanza Peter Pinda. Ni wazi Watanzania pia walikuwa na matarajio. Wanataraji uwajibikaji wa hali ya juu zaidi ya wasimamizi wa sekta hizi. Tunaelewa kinachotakiwa kwetu ni kitu gani, hata hivyo kwa ridhaa yako, naomba niseme yafuatayo kuhusu kazi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nzungumzie huduma ya umeme. Huduma ya umeme siyo anasa, ni hitaji la msingi katika kuelekea kwenye maendeleo kama ilivyo maji, elimu na afya. Mchango wa masuala ya miundombinu kama barabara na nishati, katika maendeleo ya maisha ya binadamu ya kila siku zina mchango wa moja kwa moja katika tathmini za maendeleo zinazofanywa na wanauchumi na wanajamii wote.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nakumbuka tu mwaka 1995 wakati namalizia *Masters dissertation* yangu kuna sentensi, kila ninapoikumbuka huongezeka ukweli wakati tunafanya *political economy of development*. Sikumbuki neno kwa neno ila nakumbuka kwamba tulikuwa tunazungumza tunasema *whether Poverty Eradication ama Alleviation*, vyovoyote utakavyotaka kuifanya, lakini *whatever the concept is, it is true*

that the development agenda over time is going to be more and more complicated because of its ever changing, diverse nature and it's multi-dimensional characteristics.

Mheshimiwa Spika, haya mambo ya kuchambua maendeleo na umaskini kila muda unavyokwenda, mambo yanaongezeka. Kwa hiyo, tukifkiria tunasema labda masuala ya maji ndiyo yanachangia umaskini, masuala ya elimu, lakini kadri muda unavyozidi mambo yanazidi kubadilika, mambo yanazidi kuingia ndani. Kwa hiyo, kusema kweli, kwa sasa hivi kwa kila wanajamii wote unaowasoma wanakubaliana kwamba upatikanaji wa nishati kimsingi inachangia sana katika maendeleo ya kila siku ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa ridhaa yako, naomba nizungumzie suala la umeme kwa lengo la kutoa utangulizi kabla Mheshimiwa Waziri na Nishati hajatoa ufanuzi kama nilivyotoa maelezo hapo awali. Miradi ya umeme ni sehemu ya ajenda hii ya maendeleo, kama umeme ulikuwa anasa miaka 30 iliyopita, ilikuwa anasa kwa sababu wengi waliokuwa nao walikuwa wanatumia kwenye *bulb* tu lakini sasa hivi ni sehemu kamili ya msingi wa maendeleo kwa mtu mmoja mmoja kwa kumtazama binafsi, lakini pia ni sehemu ya maendeleo kwa jamii nzima kwa mtazamo wa pamoja.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme vilevile kwamba ni mtazamo wa Wizara yangu kwamba hakuna mradi wa umeme ulio muhimu zaidi kuliko mwingine katika macho yetu. Hakuna Mtanzania anayestahili kupata mradi wa umeme kuliko Mtanzania mwingine. Lakini ukweli wa utekelezaji wa miradi ya umeme ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, miradi ya umeme ni miradi yenyе gharama kubwa sana na inachukua muda mrefu kuitekeleza. Kwetu sisi kama Watanzania kwa kipindi kirefu tumeshindwa kufanya uwekezaji wa makusudi ili umeme usubiri watu, siyo watu wasubiri umeme.

Mheshimiwa Spika, Watanzania sasa hivi tupo takribani milioni 40 na tunazalisha *Megawatt* kama 1,000, hizo ni pamoja na hizi *thermals* hizi zinazoingia *watsila* na kadhalika. Naomba nitoe mfano wa uchumi mkubwa kama Afrika Kusini. Afrika Kusini wako kama milioni 45 wanatumia *megawatt* elfu 40. Kwa hiyo, ukiangalia *population* zetu zinataka kufanana, lakini wao wanatumia *megawatt* elfu 40 na bado haziwatoshi, sisi tunakidhi mahitaji ya asilimia kumi ya watu wetu wao, na umeme umeme wao pamoja na wote huo wanakidhi mahitaji ya umeme wa kama watu asilimia 55 hadi 60.

Mheshimiwa Spika, Kenya, Uganda nao, hatupo nao mbali wako kwenye asilimia 18 ya watu wao, Nigeria na Angola na mafuta yote hayo waliyokuwa nayo bado wanashindwa kuwapatia wananchi wao, wapo kwenye asilimia 70 hivi.

Mheshimiwa Spika, kwanza, kwa sababu kuna tatizo la tathmini la vyanzo, katika kuliangalia hili na ndiyo maana tunasema tuzungumze na Waheshimiwa Wabunge ili waelewe ugumu wa maamuzi tuliyokabiliwa nayo, lakini tunatarajia kwamba tutafanya nao kazi kwa pamoja katika kuhakikisha kwamba tunavuka katika hatua hii, sisi tuna

vyanzo vya *hydro*, tuna makaa ya mawe, tuna gesi, sidhani kama kuna Taifa lolote Afrika ambalo lina uwezo wa vyanzo vya umeme kama tulivyokuwa nao sisi

Mheshimiwa Spika, katika misingi hiyo hiyo tunakabiliwa pia na tatizo la uhaba wa uwezo wa kiuchumi. Labda nizungumzie vyanzo vitatu tu. Tuna chanzo cha Ruhuji *Megawatt* 350 tuna *VLPP* za gesi tunaweza kuleta *Megawatts* 350, tuna makaa ya mawe tunaweza kuleta *Megawatt* 350. Kwa hiyo, vyanzo hivi vitatu tu ambavyo vinawenza kutekelezwa ndani ya miaka saba tukawa na *Megawatts* 1000 zaidi tutahitaji labda zaidi ya dola bilioni 1.3.

Mheshimiwa Spika, hizo ni fedha ambazo tukiziwekeza kwenye miradi hiyo hazifanyi kazi yoyote kwa muda wa miaka minne hadi sita mpaka miradi hii itengemae. Huo ndiyo ukweli wa uchumi wetu. Tunachofanya ni kwamba tunaongeza *capacity* ya kujenereti umeme kwa hizi *thermals* lakini pia limesemwa hapa wakati wa tathmini ya Wizara ya Fedha kwamba Serikali iangalie namna ya umuhimu wa miradi hii kwa maendeleo ya Taifa letu na kukopa kwa makusudi.

Mheshimiwa Spika, hapo tutakapoweza kukopa kwa makusudi tutaongeza *capacity* ya umeme na tunaweza tukaongeza *for that matter transmission* na *distribution* ya umeme huo. Naomba niseme kwamba tumesikia kilio cha Wabunge, kilio cha Mheshimiwa Mama Teddy Kasela-Bantu, Mheshimiwa Selelii na mimi mwenyewe nijililie mwenyewe, lakini ndiyo ukweli wa *reality* ya *generation*, halafu hata tukimaliza *transmission*, bado tuna *cost* za *distribution* ambazo Wabunge wote wamesimama na wamesema kwamba *overtime cost* za *distribution* *zime-spiral out of control*, sasa hivi unataka umeme unaambiwa ufunge laki saba ndiyo *cost* ambazo *TANESCO* wanaweza kufunga umeme na *ku-recover*

Mheshimiwa Spika, ni lazima tufike sehemu tuambizane ukweli kwamba hii ndiyo gharama ya umeme kuanzia *stage one* mpaka *three*, lakini hiyo haiondoi suala la kwamba lazima tufikie hatua tutafute ufumbuzi wa miradi hii ya umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa mazingira haya, naomba niseme kwamba labda katika kufanya maamuzi, tumeangalia miradi ambayo inakaribia kumalizika, miradi ambayo iko kati, miradi ambayo haijaanza kabisa na ile miradi ambayo imeanza kidogo, pamoja na tamaa ya kuleta miradi mingi zaidi ili tukidhi matakwa ya watu wengi zaidi, ni ukweli kwamba miradi ya umeme lengo lake ni kwamba inavyozalisha inaweza yenyewe ikagharamia kuingiza miradi mipyä katika mfumo, lakini kila siku tukiwa tunaanzisha miradi mipyä bila kukamilisha baadhi ya miradi tutajikuta tuna lundo la miradi ambayo haijakamilika.

Mheshimiwa Spika, *for that matter*, tukijikuta tuna lundo la miradi ambayo haijakamilika, tutajikuta hatuna uzalishaji wa aina yoyote ya umeme ambayo unarudisha fedha iliyogharamiwa kwenye uwekezaji uliofanywa kwa mradi mmoja mmoja. Mheshimiwa Waziri atakuja kujibu.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie mambo matatu kabla sijaingia kwenye maelezo ya sekta nyingine. Tuna mradi wa Somanga Fungu. Mradi huu umezungumzwa na Wabunge na pamoja na kwamba ni *Megawatt* sita, lakini ni ukombozi mkubwa wa wananchi wa Kilwa, Rufiji, Mkuranga na mpaka utakapoungana na umeme hapa Temeke, tuna miaka sasa karibu miwili ambapo mradi huu umechelewa.

Mheshimiwa Spika, tumesikia malalamiko ya Wabunge, naomba niwataarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini amezungumza na Mkandarasi na tumekubaliana kwamba tarehe 31 mwezi Agosti, atakabidhi mradi huu.

Mheshimiwa Spika, tumefika hatua ambayo ukiangalia, sisi tukichelewa, Wakandarasi na wengine wanachelewa, lakini wakichelewa wao, sisi hatuwachukulii hatua. Kwa hiyo, tumefikia hatua sasa ya kusema hapana, ni lazima tupime gharama za wao wanavyotucheleweshea miradi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie kwamba ni matarajio katika mipango ya Wizara kwamba tutakopokuwa kwa mfano, kama tumepeleka umeme tumesema tumeiombea Kigoma shilingi bilioni 13 ambazo Hazina wameridhia. Miradi hii kwa sasa ni miradi ya *thermals*, lakini matarajio ni kwamba umeme wa Malagarasi utakapokamilika kwenye *MCC* baada ya miaka mitatu au minne, *uta-concide* na kufunguka kwa *central corridor* kwa sababu ni matarajio kwamba unapofungua uchumi kwa ujumla mahitaji ya baadhi ya mambo kama haya yanakuwa moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, nimetoa mifano tu kwamba hiyo ndiyo misingi ambayo tunatarajia kufanya tathmini ya wapi tupeleke miradi ya umeme, lakini tunaomba ushirikiano wa Waheshimiwa Wabunge wote kwa sababu kusema kweli zoezi hili ni gumu sana.

Mheshimiwa Spika, limezungumzwa pia suala la mkakati kabambe *PSMP*. Labda niseme tu kwamba *PSMP* siyo msahafu, ni mwongozo tumepewaa na wataalamu, lakini utekelezaji wake utategemea tathmini ya kiuchumi na mahitaji ya kijamii ambayo tunafanya sisi wenyewe. Serikali kwa kusaidiana na Wabunge, tunatarajia kwamba ni ushauri wa kitaalamu, lakini bado mahitaji ya kitaifa yanaamuliwa humu ndani ya Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, pia nalazimika kwa ufupi nizungumzie suala zima la nishati ya gesi pia, kama ilivyozungumzwa na Wabunge wengi katika hali hii ya sasa ambayo bei ya mafuta inazidi kupanda, suala la gesi kama nishati mbadala linazidi kuchukua umuhimu mkubwa sana, ni vizuri tuseme ukweli kwamba kama ilivyo kawaida kwa mambo mbalimbali, tumechelewa kufanya uwekezaji wa makusudi ndani ya sekta ya gesi ambayo labda tungefanya miaka sita ama saba nyuma, leo tungkuwa tunafaidi matunda ya uwekezaji ule, tofauti na ilivyo.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji ndani ya gesi ni jambo la gharama kubwa sana. Tulikuwa tunafanya tathimini kuchoronga shimo moja na kuangalia kama wanapata au hupati linachukua kama dola milioni 12 mpaka 15 na kwa bahati nzuri utafiti

umeonyesha Tanzania tuna gesi nyingi sana, kuanzia Mnazi *bay* mpaka Songosongo mpaka Mkuranga na kuna maeneo mengine bado hayajagundulika, lakini bado *problem* ni ile ile ya uwekezaji. Unawekeza, unaacha kutumia kwenye nini ili ukatumie kwenye gesi.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna maamuzi ambayo ni magumu lazima yafanywe, kuna mambo mawili ambayo yamezungumzwa. Moja, limezungumzwa na Kaka yangu Mheshimiwa Siraju Juma, kuhusu suala la matumizi ya gesi, ni kweli kwa sasa hivi ni lazima tuseme kwamba *majority* ya gesi tuliyokuwanayo inakwenda kwenye umeme na nyingine kusema kweli bado iko chini. *Artumas* wamegundua wana gesi nyingi, lakini bado hawajaweka uwekezaji. Uwekezaji waliofanya ni *BCF* 242 tu ambazo gesi hiyo kimsingi sasa hivi inatumika kwenye umeme wa Lindi - Mtwara. Kwa sababu ya mazingira ya kiuchumi, imeonekana labda gesi hiyo pia itumike kwenye uzalishaji wa sementi mkubwa na uzalishaji wa mbolea.

Mheshimiwa Spika, kwa nini tunasema uzalishaji wa Mbolea? Kwa sababu gesi inatoa mbolea za aina mbalimbali, lakini mbolea mbili kuu ni *Amonia* na *Urea*. Hizi ni mbolea ambazo ni *standard*. Sisi Mwenyezi Mungu ametujalia, Tanzania tuna *phosphate*, matokeo yake ni kwamba ukiweza *kuzi-blend* hizi pamoja unapata mbolea ambayo Mzee Wasira atanisaidia, inaitwa *NPK* ambayo ni mbolea yenye *quality* kubwa zaidi. Ukifanya *analysis* na ukazingatia kwamba Tanzania asilimia 70 wanategemea kilimo, unaona ugumu tuliokuwa nao wa kuamua kuhusu matumizi ya gesi, lakini *it makes more and more sense* kwamba katika maamuzi ya awali tuelekee kwenye mbolea ambayo itatoa manufaa kwa Watanzania zaidi ya asilimia 80, itafanya uzalishaji wao wa kilimo uwe ni bora zaidi na kwa maana hiyo, uchumi utapanuka zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini gesi tuliyokuwa nayo inaturuhusu twende kwenye miradi mingine ya umeme kama kuleta *Megawatt* 350 kuziunganisha kwenye *grid* na pia kuleta *liquid natural gas* ambayo itatumika kwenye majumba na magari kama alivyoshauri Mheshimiwa Hasnain Dewji, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga na Waheshimiwa wengine.

Mheshimiwa Spika, lakini pia ni lazima tuelewane kwamba mradi huu wa kuleta *gas into liquid natural gas* ili tuingize gesi majumbani na tuondokane na hili tatizo la kuni kama nishati ambayo inaharibu mazingira na kadhalika, ina uwekezaji mkubwa na taaluma kubwa.

Baadhi ya watu wameshafanikiwa wengi kuifanya, wanatumia gesi kwenye magari, majumbani mpaka sasa hivi tulivyosema humu Bungeni tuna wataalamu kutoka China wanatusaidia, tumesema tunataka tuangalie ile *study* ambayo gharama zake ni kama shilngi milioni tatu na ile *pilot study* iki-take off na tunadhani ita-take off kwa sababu mpaka sasa hivi hata hiyo nishati inayotumika sasa hivi ya mkaa imekuwa ghali sana. Nishati ya mafuta ya taa imekuwa ghali mno, kwa hiyo, ni matarajio yetu pamoja na kwamba tunasukuma mradi huu ili Watanzania waupokee, lakini kama tukifanikiwa kuzalisha gesi kwa unafuu zaidi tunavyofanya ni matarajio yetu kwamba Watanzania

wataupokea mradi wa *liquid natural gas* na ndani ya miaka mitano hadi kumi itakuwa ni mfumo wa matumizi ya nishati majumbani mwetu.

Mheshimiwa Spika, ni lazima tuelewane kwamba katika mambo ambayo pia yanatukwaza kwenye uwekezaji wa gesi ni kwamba wenzetu wengi ambao wanatumia gesi katika mfumo huu, gesi yao inatokana na kuchimba *petrol*. Kwa hiyo, *petrol* ndiyo lengo kuu. Gesi ni *by product*. Kwa hiyo, *petrol* yenye we inakuwa imeshalipia gharama za gesi. Sisi gesi yenye we ndiyo lengo lenyewe. Kwa hiyo, gharama zetu za uzalishaji wa gesi umekuwa mkubwa, lakini katika tathmini ya kiuchumi inaonekana kwamba kama tukiipatia matumizi ambayo yana *broad benefit* kama hizi za kilimo kwa Watanzania waliokuwa wengi na kupunguza athari za mazingira na nini faida yake *over time* na kwa tathmini pana itakuwa ni kubwa.

Naomba Waheshimiwa Wabunge watunge mkono katika hili na tunaahidi kwamba tunafanya mikakati ya dharura kama tulivyoshauriwa na Waheshimiwa Wabunge kuleta sera na sheria pia ya matumizi ya gesi hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ni suala la madini. Nilikuwa naomba niseme mambo matatu. Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia suala la *STAMICO*, naomba tu niseme kwamba Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini na mimi kama msaidizi wake tuko mstari wa mbele kabisa na tumepokea ushauri wa Kamati ya Nishati na Madini ya kushauriana na wenzetu ili tufanye mkakati wa haraka wa ku-despecify *STAMICO* pia kuiongezea majukumu kutokana na mazingira haya mapya yaliyopo sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, katika uwekezaji wa madini, tunapoteza mambo mengi kwa sababu wanasema Wazungu hatuna mkono wa *honey jar*. Yaani lile bakuli la asali sisi hatuna mkono, matokeo yake wengine wenye mkono wakitia mkono mle wakitoa sisi tunabakia kulambalamba ile asali iliyobaki nje. Tunataka tufanye mikakati ya makusudi kabisa ili tuwe na uangalizi wa karibu zaidi ndani ya sekta ya madini na mmoja ambaye anaweza akatusaidia kufanya hivyo bila shaka yoyote ni *STAMICO*.

Mheshimiwa Spika, *STAMICO* wana historia ya madini ya nchi hii, wana ufanisi wa muda mrefu, wafanyakazi wao wengi wamehamahama, lakini bado wapo wataalamu wengi mle, lakini *STAMICO* wanawenza kufanya kazi hii kwa kushirikiana na kituo cha Jiolojia ambacho kipo hapa Dodoma. Wana utaalamu mkubwa, lakini wanachotakiwa wote wawili ni uwekezaji. Kwa hiyo, Serikali tunataka tufanye mikakati ya makusudi ili tuwawekeze wenye kuhitaji vifaa vya kuchoronga, vifaa vya maabara na kadhalika waweze kutusaidia moja kwa moja kwenye sekta ya madini kwa niaba yetu sisi wote lengo ni kuwawezesha *STAMICO* na *GST* kama tulivyoeleza kwenye hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la wachimbaji wadogo wadogo, kama inavyoelekeza kwenye ilani ya uchaguzi suala la wachimbaji wadogo wadogo tumefanya mkakati, tumefanya *pilot study* Katente, Bukombe kuna ushirika wa wachimbaji wadogo wadogo ulikuwa unatafuta *capitalization* ya milioni 150, Wizara yangu tumewatafutia mwekezaji ambaye amewapatia kama shilingi milioni 300 anafanya

nao kazi kwa karibu na sisi kama Serikali tutakuwa karibu pale ili kuhakikisha kwamba maslahi yao yanalindwa.

Mheshimiwa Spika, tutafika wakati ambapo wachimbaji wadogo wadogo na vikundi vyao kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge wengi ndiyo mwelekeo wa baadaye. Hivi vikundi ndiyo vita-*generate* baadaye kuwa na *capitalization* mpaka hapo katikati. Ni lazima tutafute ufumbuzi wa kuwawezesha tunachotaka kufanya na tumeanza majadiliano na taasisi mbalimbali za fedha kuangalia namna ambavyo watawezesha *mining activities*.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa kama wanavyosema kwenye kilimo na kwenye *mining* ni *too risk*, lakini tunaangalia pia uwezekano kama tunaweza kukawa na wenzetu wa Wizara ya fedha tunaweza tukawapatia *Government guarantees*. Kusema kweli, sekta ya madini kwa upande wa wachimbaji wadogo wadogo, tathmini inayofanywa ni kwamba ina mchango mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba nizungumzie suala la mikataba. Katika hili, naomba niliseme tu kwa haraka haraka, kuna kitu kinaitwa *cooperate social responsibility*. Mara nyingi katika mikataba hii mtu akishakuwa na kile kipengele cha *cooperate social responsibility* kwamba mimi nawapa kidogo vijihospitali na kadhalika wanajiona wamemaliza, huu labda ni udhaifu ambao tumeuuweka kwenye mikataba. Tumegundua kitu kimoja kwa kushauriana na wenzetu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kupitia upya mikataba si jambo ambalo linafanywa Tanzania tu, nchi nyingi zimepitia mikataba, Canada wamepitia mikataba, lakini utakuta tukitaka kufanya sisi Watanzania tunaambiwa, ooh, hili litaathiri uwekezaji, lini imetokea? Mwekezaji anakuja kufanya biashara anatarajia kwamba akifanya *investment* yake apate faida.

Mheshimiwa Spika, Mwekezaji ambaye anataka yeye apate faida sisi tutumie, huyo si Mwekezaji. Huyo ana lake lingine, siyo Mwekezaji! Sasa naomba niwaahidi Wabunge na nikuahidi wewe kwamba, katika kupitia mikataba hii na tunamshukuru sana Jaji Bomani na Kamati yake kwa kufanya kazi nzuri ambayo sisi tumeichukua, tumeipitia, tunataka tuingie kwenye mikataba na tujaribu kutengeneza mikataba upya tufikie hatua kwamba ina *a win win situation*, hatuvezi tukategemea wao waumie kwa sababu wao hawaji kazi za *charity* wanakuja kufanya kazi za biashara lakini na sisi tusumie.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme tu kwamba katika mikataba hii tunajiweka upya ili Wizara ya Nishati na Madini iangalie mambo haya na tuwe na jicho la karibu zaidi katika manufaa yanayotokana na mikataba hii kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba nitoe shukrani kwako na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, Wazee wangu humu Bungeni, naomba nimshukuru sana kwa dhati ya moyo wangu Mheshimiwa William Ngeleja - Mbunge wa Sengerema, bosi wangu, wakati mimi nimeingia Wizarani pale nilikuwa mgeni kabisa sijui A wala B, kwa hiyo,

mambo mengi ambayo najitanua tanua hapa kusema kweli, ahsante Mwalimu nashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru wazazi wangu wote wawili na familia yangu. Naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, alinipa miaka saba ya neema na mapenzi makubwa na Marehemu Mke wangu, mara ya mwisho niliposimama hapa nilimtaja nikamshukuru kwa mapenzi yake kwangu, sikujua kwamba Mwenyezi Mungu alikuwa amenipa muda mdogo uliobaki kukaa naye hapa duniani, nashukuru sana Mwenyezi Mungu kwa miaka saba ya mapenzi haya yote niliyokuwa nayo na ushirikiano wake ye ye na nawashukuru Wabunge wenzangu wote humu ndani kwa mapenzi makubwa waliyonionesha katika kipindi hiki kigumu sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa mwongozo wake na kwa kutushika bega na sikio kila mara tunapohitaji uongozi wake na ninaomba niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wengine kwa ushirikiano wao katika kufanya mikakati ya Serikali. *This is the collective responsibility.*

Mheshimiwa Spika, kwa unyenyekevu na heshima kubwa, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Adam Malima, kwa ufanuzi uliotoa. Sasa ni zamu ya mwenyewe mtoa hoja Waziri wa Nishati na Madini.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote na mimi niungane Waheshimiwa Wabunge, pamoja na wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika, kumshukuru Mwenyezi Mungu, kutuwezesha kufikia siku ya leo na hasa hatua hii ya kuweza sasa kutoa majumuisho kuhusu hoja yetu ya Wizara ya Nishati na Madini ambayo inahusu makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kutoa ufanuzi wa hoja mbalimbali, nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kazi kubwa aliyofanya sasa lakini pia kwa kazi kubwa ambayo amekuwa akifanya na tumekuwa tukifanya kazi kwa ushirikiano pamoja na watendaji wetu katika kusimamia na kutekeleza mipango mbalimbali kupitia sekta ya nishati na madini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunakushukuru wewe binafsi kwa mwongozo wako. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wenye viti wote wa Bunge na Wabunge wote kwa ujumla. Kwa Serikali, tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, sisi wote ni wagoni lakini mmetusaidia sana kwa kutuongoza kufikia hapa tulipofikia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo ada tuanze kwa kuwatambua waliochangia hoja yetu ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, tuna wachangiaji wengi, lakini nitapenda tu mnivumilie niwatambue kwa sababu ya kuweka kumbukumbu sawa. Nianze kwanza na waliochangia kwa maandishi.

Waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Profesa Mark Mwандосya, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Profesa Sarungi, Mheshimiwa John S. Malecela, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Mohamed R. Abdallah, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Savelina S. Mwijage, Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Mheshimiwa Dr. Emmanuel John Nchimbi, Mheshimiwa Capt. Chiligati, Mheshimiwa Brig. Gen. Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Stephen Wasira, Mheshimiwa Fatma Fereji, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mheshimiwa Zainab Vulu, Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Anthony Diallo, Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami, Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge na Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Nuru A. Bafadhili, Mheshimiwa Mathias Chikawe, Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, Mheshimiwa Riziki O. Juma, Mheshimiwa Dunstan Mkapa, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Mgeni J. Kadika, Mheshimiwa Ludovick Mwanzila, Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura, Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Joel N. Bendera, Mheshimiwa Omar S. Kwaangw' Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda, Mheshimiwa Benedict Ole- Nangoro, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Fred Mpendazoe, Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Eng. Christopher Chiza, Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa William Lukuvi, Mheshimiwa Mwanne Mcemba, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa Balozi Abdi H. Mshangama, Mheshimiwa Mbaruk K. Mwandoro, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Suzan Lyimo, Mheshimiwa Mariam Kasembe na Mheshimiwa Wilson Masilingi. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Idd Azzan, Mheshimiwa Benson Mpesa, Mheshimiwa Sijapata F. Nkayamba, Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbaraka, Mheshimiwa Mwakhamis Saidi, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Masolwa C. Masolwa, Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mheshimiwa Parmukh Sing Hoogan, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Clemence B. Lyamba, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Omar Sheha Mussa, Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, Mheshimiwa Capt. John Komba, Mheshimiwa Fatma Maghimbiri, Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, Mheshimiwa Dr. David Mathayo, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Hassan C. Kigwalilo, Mheshimiwa G. Kayombo, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis na Mheshimiwa Damas P. Nakei. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Profesa Idris Ali Mtulia, Mheshimiwa Dr. Luka J. Siyame, Mheshimiwa Ernest G. Mabina, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Abdul J. Marombwa, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Mheshimiwa Maria I. Hewa, Mheshimiwa James D. Lembeli, Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, Mheshimiwa Idd M. Azzan, Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mheshimiwa Dr. Charles O. Mlingwa, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Salum Khamis Salum, Mheshimiwa Eng. Laus Mhina, Mheshimiwa Athumani S. Janguo, Mheshimiwa Magalle John Shibuda, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Mheshimiwa Elietta Switi, Mheshimiwa Anastazia J. Wambura, Mheshimiwa Ussi Ame Pandu, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Ruth Msafiri na Mheshimiwa Lucy Mayenga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie majina ambayo yamebaki.

SPIKA: Hatimaye utatamka idadi Mheshimiwa Waziri, ili tujue tu *for a record*, wangapi hawa sasa? (*Makofi*)

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa kuongea ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Fred M. Tungu, Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mheshimiwa Anthony Diallo, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakar, Mheshimiwa Profesa Feethman Banyikwa, Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Ephraim Madeje, Mheshimiwa Hasnain Dewji, Mheshimiwa Alyoce B. Kimaro, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Teddy Kasella- Bantu, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Profesa R. Mwalyosi, Mheshimiwa Mohamed Said Sinani, Mheshimiwa Emmanuel J. Luhahula, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Christopher Ole- Sendeka, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Rwilomba F. Kabuzi, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Mohamed H. J. Mnyaa, Mheshimiwa Dorah Mushi, Mheshimiwa Ernest G. Mabina na Mheshimiwa Naibu Waziri Adam Malima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia tumekuwa na wachangiaji ambao wamemalizia kwenye *session* hii, Mheshimiwa Mpina. Natambua pia mchango wa Mheshimiwa Michael Lekule Laizer.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, waliochangia kwa kuongea ni wachangiaji 29 pamoa na Mheshimiwa Naibu Waziri lakini pia waliochangia kwa maandishi ni Waheshimiwa Wabunge 128. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja zilizotolewa ni nyingi, kwa ujumla tuna takriban wachangiaji zaidi ya 150 na kuna hoja nyingi kweli.

Mheshimiwa Spika, lakini nasema pamoja na yale ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameелееza, napenda nianze kwanza na maelezo ya jumla. La kwanza, ambalo nitapenda kuliongelea kwa faida ya Bunge hili Tukufu lakini pia kwa faida ya Watanzania kwa ujumla, ni kuhusu kasi ya usambazaji umeme.

Mheshimiwa Spika, tangu tuwasilishe bajeti lakini hata kabla ya kuwasilisha bajeti yetu, kulikuwa na maswali mengi yanaongelewa kuhusu kasi ya usambazaji umeme nchini na kwa kweli watu walikuwa wanatabiri na kubashiri mambo mbalimbali. Nikiri kwamba hata sisi wenyewe kama Wizara tumefuatwa sana na vyombo vya habari vikitaka kujua hivi bajeti hii itakuwa tofauti? Hata baada ya kutoka bajeti bado kumekuwa na mtazamo unaotofautiana jambo ambalo sisi tunalikubali kwa sababu ndiyo mchakato wenyewe wa kufikiria.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja zimejitokeza kwamba pengine bajeti hii haitofautiana sana na bajeti zingine. Napenda kutumia fursa hii kuliarifu Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla kwamba bajeti hii ni tofauti na bajeti zingine kwa sababu kuu mbili tu. Ya kwanza, tumeweka mazingira ambayo yanatuwezesha sasa kwenda kasi zaidi kuliko ilivyokuwa awali ikiwemo kupitisha Sheria ya Umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, ni kuhusu suala la kupata ufadhili wa miradi mbalimbali ambayo kimsingi inatuwezesha kupiga hatua kubwa na kasi zaidi kuliko miaka iliyopita.

Mheshimiwa Spika, napenda niliweke wazi hili kwa sababu pengine tusipoweka msisitizo, inaweza ikaonekana kama *business as usual*, hapana. Kwa mfano, tunesema katika miradi ambayo itafadhiliwa na huu ufadhili wa *MCC (Millennium Challenge Corporation)*, iko wazi kwamba sisi tuna Mikoa sita. Leo Tanzania ambayo imefadhiliwa kupitia huu mfuko wa *MCC (Millennium Challenge Corporation)*, imewezesha sasa kufikishiwa umeme katika maeneo mengi sana Tanzania.

Mheshimiwa Spika, waliosoma masuala ya Sheria wanafahamu kuna mambo ya kubishania na mambo ambayo huwa hayabishaniwi, huwa ni mambo ya ukweli. Kwamba William Ngeleja ni mwanaume kwa kuonekana kijinsia haiwezekani akaja mtu mwingine akasema mimi ni Joyce kwa jinsia, hapana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nalisema hili jambo kusisitiza kwamba tunapiga hatua kwa ufadhili wa *Millennium Challenge Corporation* katika Mikoa sita.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia lile jedwali ambalo limeonekana pale limetupeleka mbali zaidi. Nashukuru kwamba Waheshimiwa Wabunge wengi wamekiri hapa kwamba kwa kweli kupitia ufadhili huu tutafikia miradi mingi sana.

Mheshimiwa Spika, nataka niliweke vizuri na nafahamu kwa sababu nafahamu Watanzania wanatusikiliza wajue kwamba ni nini kinatoka katika kuongeza kasi ya kupeleka maendeleo hasa katika suala la nishati ya umeme maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia tuna ufadhili unaotokana na Benki ya Maendeleo ya Afrika, kwanza kwenye huu ufadhili wa *Millennium Challenge Corporation*, tumepata dola za Kimarekani milioni 206.5 na huu ni ufadhili endelevu na kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri hapa suala la huduma ya umeme likishafika mahali ndiyo mwanzo wa safari nyingine.

Kwa hiyo, tunaposema jambo hili litakapoanza kutekelezeka na utekelezaji wake unaanza kwa mfano kwa yale masuala ambayo tulikuwa tunaulizwa hivi huu mradi wa *MCC* unaanza kutekelezwa lini? Tumesema kwenye hotuba yetu narudia tena kusisitiza kwamba utekelezaji wake unaanza mwezi wa saba huu huu. Sisi tunasema kila ambako umeme utafika, utafika kupitia huu ufadhili maana yake ni kwamba umerahisisha kuwafikia Watanzania wengine katika maeneo hayo, ni tofauti kama tungekuwa kama ambavyo tunakwenda kwa *speed* yetu sisi ya uwezo wetu wa kifedha Watanzania kwa mfuko wetu wa ndani. Kwa hiyo, nasema hili ili tuliweke sawa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kupitia Benki ya Maendeleo ya Afrika, tumepata takribani dola za Kimarekani 50 pale, tuna Mikoa mitatu, tuna Mkoa wa Arusha, Mkoa wa Shinyanga na Mkoa wa Mwanza. Lakini niseme pia hapa katika hili na nimuombe Mzee wangu, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, ninafahamu kuna hoja ya msingi hapa ulishaahidiwa sana lakini narudia kusema kwamba safari hii katika ufadhili huu kwa mradi ambao utaanza hivi karibuni na niseme unaanza mwezi wa saba, Mheshimiwa Lekule Laizer kwanza huna sababu ya kwa nini usigombee Ubunge mwaka 2010 kama ambavyo ulishatueleza hapa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia naomba nimhakikishie Mheshimiwa Lekule Laizer, haya si maneno ya kukufariji. Uchungu ulionao au uchungu walionao wananchi wa Longido, tunaufahamu kama nchi na ndiyo maana Serikali imekuwa ikifanya juhudu pamoja na Waheshimiwa Wabunge hapa ambao wamechangia kuisaidia Serikali kuwezesha kupata wafadhili mbalimbali. Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, nakuomba baba yangu, ulinieleza nia yako ya kutoniunga mkono, nakuhakikishia na wananchi wa Longido wanasikia, hizi siyo hadithi za Alinacha na tunakuambieni kwamba tutatekeleza hii miradi na taratibu zimeshaanza. Kwa hiyo, nakuomba baba yangu, uniunge mkono na nakuomba kabisa kwamba kama una nia ya kuendelea kuwatumikia Watanzania mwaka 2010 isiwe hoja ya kwamba umeahidiwa tangu kipindi cha miaka kumi na kitu iliyopita leo tunawahakikishia kwamba jambo hili litawezekana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, bado tuko kwenye kasi ya kupeleka maendeleo katika maeneo ya vijijini, tunasema tuna ufadhili hapa wa kupitia ule *World Bank* wa Dunia, tuna ufadhili wa mradi wa kuendeleza kupanua uwigo *TEDAP*, tuna milioni 111.5 na hizi zinashiriki kuimarishe miundombinu yetu ya *transmission line* zetu, gridi ya taifa na hii inahusika katika Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha na Kilimanjaro, utekelezaji wake unaanza mwezi ujao mwezi wa nane na tumeainisha vijiji ambavyo vitafaidika katika huu mradi. Leo mtu anakuambia kwamba bajeti hii ni kama zilizopita, hapana. Hatusemi hili, hatu-*personalize*, si kwa sababu Naibu Waziri na Mheshimiwa Ngeleja tuko hapa, tunasema ni juhudu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli, narudia tena kusema huu ni kati ya ukweli ambao hauwezi kupingika. Kama kuna watu wanadhani ni utani hebu wasubiri, watupe mwaka mmoja wakati utekelezaji unaendelea tuone kama tunaanzia mahali ambapo tunganeanzia jana, si tutaanzia mbele zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumepata dola milioni 10 kutoka kwa Shirika la Maendeleo ya Japan kuimarisha mfumo wetu pale Dar es Salaam. Tunafahamu Dar es Salaam inahitaji mtazamo wa aina yake kwa sababu Dar es Salaam hata mchango wake katika kiuchumi, tumelisema hili jambo lakini si hivyo tu.

Mheshimiwa Spika, tuna mradi wa kutoka Makambako kwenda Songea tunakwenda mpaka Mbinga tunapitia Ludewa kwa Mheshimiwa Profesa Mwalyosi na tunaelekea mpaka Namtumbo kwa Mheshimiwa Vita Kawawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini nakuhakikishia Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wangu nakufahamu vizuri. (*Kicheko*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, husikiki sasa. (*Kicheko*)

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, silisemi kiutani. Nalisema hili, tunesema huu mradi una dola milioni 70.4 ambazo zinawezesha sasa hiyo *transmission line* ijengwe kwa msongo mkubwa. Tunakwenda mpaka Mbinga kwa Mheshimiwa Kayombo pamoja na Mheshimiwa Komba.

Mheshimiwa Spika, lakini tunesema na mimi nafahamu *concern* ya Mwenyekiti, jana umesema kwa uchungu sana, *seriously* kidogo nitoe machozi, tunaambiwa wanaume ni wagumu kidogo kutoa machozi lakini ilikuwa ni Al-manusura kwa sababu ya uchungu aliokuwa anausema Mheshimiwa Mwenyekiti wangu, Jenista Mhagama.

Mheshimiwa Spika, lakini tunesema, ukisoma ile hotuba yetu, utekelezaji wa mradi huu unaanza mwezi wa tisa, tukichelewa sana ni mwezi wa 10 mwaka huu. Lakini ninachosema wenzetu wa Sweden wamethibitisha na tunesema asilimia 90 ya fedha ni msaada, asilimia 10 ndiyo tunachangia na ni mkopo wa masharti nafuu. Tunesema tukishafika Songea tutakwenda mpaka Mbinga, Namtumbo lakini pia tunesema kila tunakopita mahali ambako kuna *potential customers*, kama kuna mahali ambako huo mradi utapita patahudumiwa.

Mheshimiwa Profesa Mwalyosi ananifahamu vizuri sana ninavyosema hili, maeneo yote ambayo yatakuwa yamefanyiwa *feasibility study* na inafahamika kwamba jamii iliyoko pale inakidhi mahitaji yale ya kuweza kutumia huduma ya umeme, hautapitiliza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasisitiza hili la Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa sababu kwa kweli ametishia mshahara wangu, lakini mimi kwa wema alionifanyia mwaka jana, Mheshimiwa Mwenyekiti ni mtu mwema sana. Amenikaribisha, kwanza alitoa ahadi hapa Bungeni na sina sababu ya kuficha wema alionitendea. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa wema alionitendea sina sababu ya kuficha na tuelewe kwamba pia sisi wenye dhamana hizi ni binadamu na wema ni sehemu yetu ya ubinadamu. Ukitendewa wema siwezi kusema shurti urudishe lakini ninachosema kwa hili Mheshimiwa Jenista Mhagama, nakuhakikishia na wananchi wa Peramiho wasikie, nafahamu una madai yako pale ya shilingi milioni 306 kwa ajili ya kuunganisha kwenda pale Peramiho lakini tulishakuahidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nafahamu alitaka tuseme kauli ambayo itawafanya wananchi wa Peramiho wasikie lakini Bunge hili liliishaarifiwa mradi huo unaokwenda kule mpaka Mbanga na mpaka Namtumbo tukishafika pale Wilayani kwenda pale Peramiho ni karibu sana na amekwishatuletea hesabu zake tunazifahamu ni milioni mitatu na kitu.

Mheshimiwa Jenista Mhagama, hana sababu ya kushika shilingi yangu kama wote tunapigania maendeleo ya Tanzania. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, baba yangu Lekule Laizer, amesema jambo la msingi, ukisoma ule ukurasa wa 81, kwenye kitabu chetu cha hotuba ya Bajeti hii, tumeainisha miradi. Nafahamu *concern* ya Mheshimiwa Lekule Laizer lakini nataka niseme kwa sababu jambo hili linahusu Waheshimiwa Wabunge wengi kwa maeneo mengi ambayo yameonyeshwa katika miradi hii ya ufadhili mbalimbali, tulisema wakati wa uanzishaji wa miradi, mara nyingi hii miradi haizingatii mipaka hii ya kijiografia ya Kiwilaya na ndiyo maana utakuta ukiangalia chini yako tu Mheshimiwa Lekule Laizer pale kuna mradi wa Bukombe unashirikisha Wilaya ya Kahama, haijitokezi lakini vijiji vyote vimejumuisha pale.

Mheshimiwa Spika, nadhani nitumie nafasi hii kufafanua kwamba hiyo pia Mheshimiwa Lekule Laizer isiwe sababu ya kushika shilingi kwa sababu siyo mradi wa Longido tu ambaو umechanganywa ukaonekana ndani ya Wilaya ya Arumeru, haiwezi kuwa sababu kwa sababu kuna miradi mingi zaidi ya hiyo.

Cha msingi ni kwamba tunawafikia wananchi wangapi katika maeneo ya Tanzania kupitia ufadhili huo. Namwomba baba yangu, Mheshimiwa Lekule Laizer, tupo pamoja, tunamhakikishia kwamba tutaendelea kulisimamia hili jambo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, wametushauri, wamechangia lakini nafahamu kuna Waheshimiwa Wabunge wamelalamika kwa uchungu sana, uchungu ule nawambieni unatugusa kama unavyowagusa nyinyi, lakini kikwazo chetu hapa ni uwezo wa rasilimali fedha.

Mheshimiwa Spika, wote tunafahamu tungependa Tanzania hii yote tui-*electrify* lakini tunafahamu na ndiyo maana tulikuwa na miongozo tukasema tupange basi kwa kufuata vipaumbele. Nafahamu mama yangu pale Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, jana aliongea kwa uchungu sana na kwa kweli ametukumbushia ya miaka ya nyuma na ninafahamu.

Mheshimiwa Spika, lakini nataka nitoe siri moja. Mimi mwaka jana, kwa uchungu alionao Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu na kwa sababu wote tunawatumikia Watanzania bila kujali wanatoka Jimbo gani, mimi nilipangwa kwenda kufanya ziara Mkoani Singida wakati tunatoa taarifa kuhusu matumizi ya fedha ambazo zimekwenda kwa Halmashauri zetu, tulikuwa tunakwenda tunafafanua mambo mbalimbali wote tunafahamu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kumaliza kazi ya Mkoa wa Singida nikasema kwa sababu Bukene ninaifahamu na mimi nimesoma Mpwapwa *Secondary*, wakati nasoma *O-Level*, nikitoka Mwanza nilikuwa napita Bukene sijui kama Bukene hakuna umeme lakini nayafahamu mazingira yale.

Nilikwenda katika Jimbo la Mheshimiwa Mbunge na ye ye alikubali kwamba hilo halikuwa kosa, ingawaje alitamani kuwepo na mimi, lakini kwa sababu mimi nilianzia njiani hiyo safari, nilikwenda kufika Bukene kuiona jinsi ilivyo *potential* na jinsi inavyohitaji umeme na nikamweleza Mheshimiwa Mbunge, mama yangu hapa kwamba sisi tutahakikisha kwamba Bukene unakwenda umeme kwa sababu tunafahamu. Lakini katika ziara hiyo pia niliambatana na kaka yangu pale Mheshimiwa Lucas Selelii anafahamu.

Mheshimiwa Spika, tulikwenda Ndala, Ndala tulifika usiku, mimi na Mheshimiwa Selelii tulikuwa tunazunguka, lengo ni kutaka kuyajua mazingira kwa sababu pia tunafundishwa, kujifunza kwa kuona inaongeza uelewa wa jambo. Tulikuwa na Mheshimiwa Lucas Selelii, tulifanya kazi mpaka usiku. Narudia tena kusema kwamba tunafahamu uchungu walionao na sisi hatutaki kusema kwamba tutaendeleza ahadi ambazo haziwezekani.

Mheshimiwa Spika, nirudi kwenye hoja ya msingi kwamba kwa nini tunashindwa kutekeleza mipango yetu ya maendeleo kwa wakati kwa jinsi ambavyo tungependa iwe. Ndiyo maana tukasema tuenze kwanza na Makao ya Wilaya, hivyo ndivyo wote tunavyo elekezwa na Ilani ya Uchaguzi, hivyo ndivyo tunavyo elekezwa na miongozo mbalimbali likiwemo suala la MKUKUTA. Tunasema tuenze na Makao Makuu ya Wilaya kwa sababu ndiyo utaratibu wa kawaida kwamba tukishafika katika maeneo hayo umeme utakwenda mbali zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninawaomba ndugu zangu, lakini niwahakikishie, Mheshimiwa Lucas Selelii anafahamu kwamba tulishakubaliana, mchango wake wa maandishi Mheshimiwa Lucas Selelii umenitisha kwa sababu haonyeshi dalili zozote za kuniunga mkono. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Lucas Selelii mimi na ye ye ni ndugu, Watanzania wote ni ndugu, lakini tukubali kwamba kuna undugu wa damu pia. Mheshimiwa Lucas Selelii hana sababu ya kutoniunga mkono kwa sababu nilikwishakumhakikishia ndiyo maana tukajitolea tukafanya kazi usiku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, anafahamu nimekwisha kumhakikishia kwamba mwaka huu wa fedha miradi yote tutaishughulikia, Bukene na Ndala, sasa tatizo linatoka wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikwambie tulikuwa pia na mpango wa kufika kwenye Jimbo la Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lucas Selelii ni shahidi, lakini ratiba iligoma. Lakini niwahakikishie wananchi wa Jimbo la Mheshimiwa Spika, kwamba tunaendelea kushughulikia ndani ya mwaka huu wa fedha, *Inshallah*, Mwenyezi Mungu atasaidia.

Waheshimiwa Wabunge, tunaamini tutakapokuwa tunamalizia kuongea hapa, namwomba sana Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, tuharakishe maendeleo haya, mpitishie hii bajeti, mkishapitisha hii bajeti, sisi tumeomba shilingi bilioni 20 kwa ajili ya REA... (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kumbukeni Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuna hizo *project ambazo zinafadhiliwa* na ufadhili wa kutoka nje. Lakini sisi pia tumeomba ombi la Serikali hapa kutoka kwenye mfuko wa ndani shilingi bilioni 20. Kumbukeni hii miradi inayokwenda kwa kupitia hiyo miradi ya nje, itaunganishwa na hii miradi inayopitiwa na shilingi bilioni 20, nina uhakika umbali ambao utakuwepo sasa utakuwa umepungua kutoka kwenye miradi ambako kuna umeme na hayo ma-gap yatakuwa yamepungua.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi ndugu zangu ninawaombeni turuhusuni twende sasa, twende tukaanze kushughulikia hizi bilioni 20, sasa hivi tuna- *up date* zile taarifa kwa sababu tunahitaji *kuzi-up date* kwa sababu makadirio mengine Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu kwa mfano, anasema tumrudishie shilingi milioni 50 yake, halafu tumuungeze shilingi milioni 50 nyingine, haitasadidua kwa sababu miradi yake inahitaji milioni 700. Mimi nimemhakikishia na wananchi wa Bukene wanaskia ni mojawapo ya mpango ambao tunakwenda kuutekeleza ndani ya mwaka huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, twende pamoja katika hili, tusaidieni, tuna maombi chungu nzima ambayo yamesimama.

Mheshimiwa Spika, kaka yangu Mheshimiwa Mbunge wa Solwa pale, nafahamu tangu mwaka jana lakini namwambia ombi lake tunalijua na tunalitambua. Kwa misingi hiyo ya *priorities*, tutakwenda.

Mheshimiwa Luhaga Mpina, usichukie, wewe ni kijana mwenzangu, tupo pamoja, hatuna sababu, kwa sababu tunasema fedha sasa hivi zinatafutwa. Nafahamu sana mambo haya.

Mheshimiwa Spika, Mwalimu wangu, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, nafahamu wananchi wa Kyela wanamsumbuu kuhusu ile hospitali, lakini tunasema tutayafanya tu hayo mambo. Kwa sababu, hapa kwa mfano sisi tumetoa taarifa kwamba sisi tumekubaliana katika Serikali tunaweka lile tozo la 3% kwa matumizi ya umeme na hili ninaomba sana ndugu zangu na hasa Waandishi wa Habari wasilifikishe kwa nia

mbaya kwamba pengine tumeongeza gharama za utumiaji wa umeme, hapana.
(*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, leo Watanzania hatufiki hata milioni moja ambao tunatumia umeme lakini ukitaka kusema bila hofu ya kusemwa, unasema kwamba hao ambao wanatumia umeme kwa kweli kwa ulinganifu tuna uwezo zaidi kuliko wananchi wenzetu ambao hawatumii umeme.

Mheshimiwa Spika, sasa sisi tunasema hatutaki kusaliti nafsi zetu, tunaomba mtukubalie, tunaweka hilo tozo la 3%, tutakapokwenda, itatuongezea, kuna bilioni kadhaa pale. Hii faida yake ni nini? Leo tuseme kwa mfano *TANESCO* wapo wateja 800,000 kadri wanavyoongezeka na fedha itaongezeka.

Mheshimiwa Spika, Sisi makadirio yetu ya awali pengine ni shilingi bilioni 10 kupata nyongeza pale lakini kadri wateja wanavyoongezeka na fedha zitaongezeka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sisi tutakapokuja kutoa taarifa hapa pengine tuseme nusu ya mwaka wa fedha huu, tutakuja na taarifa nyingine tofauti kabisa katika kueneza umeme vijijini.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, sisi tunawaomba, tuna nia ya dhati, hakuna ambaye anapiga danadana. Tena Mheshimiwa Luhaga Mpina, ametumia maneno makali mno yalikuwa yanatuchoma sana. Serikali hii inatupiga danadana, Serikali haiwezi kupiga danadana, angalia miradi hii ndiyo tunaisema hii. Kwa hiyo, tunawaomba sana ndugu zangu, mtuelewe.

Mheshimiwa Spika, kule Singida kwa Mheshimiwa Mohamed Missanga, tunafahamu kuna Ihanja, Isepuka kule, kuna miradi chungu nzima inatusubiri, ipo sitaki hata kuitaja.

Mheshimiwa Spika, lakini cha msingi tu niseme kwamba Mheshimiwa Godfrey Zambi, kaka yangu sina hakika kama yupo, amekwishatushika mashati muda mrefu, tunafahamu kule Mbozi Mashariki kulivyokuwa na matatizo.

Mheshimiwa Spika, lakini tunasema yote hayo tunayazingatia na *Inshallah*, tuseme kwamba kama Bajeti hii itapita na mimi kwa kweli sitaki kuficha dhamira yangu, nawaomba muipitishe twende mbele tukaanze haya mambo haraka sana.
(*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nimeulizwa swal la jumla na wenzangu hapa, hivi yule Mshauri Mwelekezi, anayeshauri kuhusu mgawanyo wa mapato na matumizi kuhusu masuala ya mafuta na gesi ilionekana kama kulikuwa na neno ambalo lilikosekana kama gesi asilia, hapana.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimkumbushe kaka yangu pale Mheshimiwa Mbunge akisoma kule kwenye maelezo ya kitabu changu, tumesema katika hali ya

kawaida labda niseme kwa neno la Kiingereza ambalo linasema na kuna maneno ambayo yanatumika kama *common mistake* kwamba kusema mafuta na gesi asilia wakati mwingine wanasesma tu mafuta, lakini haya mambo yanakwenda pamoja. Kwa hiyo, Mheshimiwa Ababukar Bakary isije ikawa ni suala tena la kuniambia kwamba hapana.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia maudhui kwa jumla ya ile *paragraph* inayosema masuala ya mafuta na gesi asilia, Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, kaka yangu, anafahamu Waziri mwenzangu tumekuwa naye tangu kwenye Kamati anafahamu maana yake ni nini na hili jambo linakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, lingine la jumla ni gharama za *TANESCO*, nalo tumelizingatia. Tunafahamu kwa kweli gharama ni kubwa, sasa hivi tunavyoongea nguzo moja inakaribia shilingi 600,000 lakini ukweli ni kwamba hebu angalia vipato vya Watanzania wenzetu ndiyo hivyo, ni wangapi wenye kipato hicho kwa mwaka, tunafahamu.

Mheshimiwa Spika, tumekubaliana kwa maana ya Wizara, pamoja na wenzangu; wenzetu wa *EWURA* na *TANESCO*, tutakaa tuangalie namna nyingine, kwa sababu hili linakwenda pia pamoja na juhudi nyingine ambazo Serikali inazifanya, kupunguza mzigo kwa *TANESCO* na kuboresha utendaji. Hivi tukikaa pamoja kwa yote haya, haiwezekani tukafika mahali tukapunguza hizi gharama? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nataka niliambie Bunge lako Tukufu na Wananchi, tunachosema sasa tunakwenda kulifanyia kazi. Katika *stage* hii, *we are non-committal*, hatusemi kwamba, tunakwenda kupunguza gharama na naomba ninukuliwe vizuri na Waandishi wa Habari. Tunasema ni hoja ya msingi, tunakwenda kuifanyia kazi. Katika mchakato mzima huu, hatuwezi kufikia mahali tukapunguza hizi gharama. Tunadhani kwamba, ipo namna. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kuliahidi Bunge lako Tukufu na Wananchi kwa ujumla, hili jambo tunakwenda kulifanyia kazi. Kuna hoja nyingine ya msingi sana, *retention* kuhusu *TPDC*. Tumesema sisi tunafanya kazi kwa mchakato, Serikali hatimaye mwezi wa tatu mwaka huu, imepitisha maamuzi haya sasa kwamba, *TPDC* itakuwa *in-retain* kiasi fulani. Tunafahamu, tungependa jambo hili litokee jana, lakini tunaomba Bunge lako Tukufu lituamini, sisi tunalifuutilia kwa karibu, tunawasiliana na wenzetu wa Wizara ya Fedha na Uchumi tuone ni jinsi gani tunaweza kufanya. Ni kweli katika Bajeti hii tulionayo leo, halijitokezi lakini si kwamba hatutaki jambo hili lifanikiwe, kwa sababu sisi tumekuwa tukilisukuma jambo hili. Naomba pia mtupe nafasi ya kutuamini, tukalifanyie kazi. Tunakwenda kulifanyia kazi suala hili, tuone ni jinsi gani ambavyo *TPDC* inaweza kupata *retention*.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo ambalo lilikuwa na matarajio makubwa, lilisemwa ndani ya kikao cha jana na leo na kwa kweli niseme, wananchi walikuwa na hamasa kubwa na bado wana hamasa kulisikia, kwa jinsi ambavyo limejitokeza, ni suala la KIWIRA.

Mheshimiwa Spika, naomba kusema kwa mara nyingine, naliarifu Bunge lako Tukufu na wananchi kwa ujumla kwamba, kama ambavyo tumekuwa tukisema kwenye vyombo vyta habari, Serikali kupitia maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wizara ya Nishati na Madini, imepewa jukumu hili la kutoa ufanuzi kuhusu masuala yote ambayo yanazungumzwa kuhusu suala la *Kiwira Coal and Power Company Limited*. Siwezi kusema kwamba, jambo hili kwa kuzingatia mambo yalivyokuwa mengi, tulidhani busara zetu zilituongoza kwamba, haitakuwa sawa kulichanganya na mambo mengine ambayo tunayaongelea hapa kwenye bajeti kwa ujumla ya Wizara. Tunaahidi kulisema, kwa kulitolea kauli ndani ya Mkutano huu huu wa Bunge unaoendelea. Tutawasiliana na wewe, tulilet hapa kwa muda muafaka. Kama tunavyosema, tupo tayari kulitolea maelezo lakini tulidhani kwamba, kwa busara zetu pengine haikuwa sahihi kulileta hapa kwa jinsi lilivyojipambanua wakati wa mijadala iliyokuwa imetangulia kabla ya bajeti yetu. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge watuamini, tunaahidi tutalisema hapa Bungeni ndani ya Mkutano huu unaoendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni hili suala la MEREMETA. Nafahamu Mheshimiwa Waziri Mkuu alishaliongelea, akalisema maudhui yake, sina sababu ya kuliongelea. Ninachowenza kusema Waheshimiwa Wabunge, ndugu zangu, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Kiongozi wetu, Mheshimiwa Dr. Slaa, tumekusikieni. Mheshimiwa Waziri Mkuu, yupo hapa; mimi nitakachofanya naliwasilisha kwake rasmi. Aminini kwamba, tumekusikieni na nina hakika wakubwa wote mpo hapa, hili jambo nadhani sina maelezo ya kusema zaidi ya hapa ambapo tumefikia. Kwa hiyo nakuombeni sana lisije likawa ni suala la kuweza kukwamisha mambo yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa nifafanue na niombe radhi awali kabisa kwamba, haitawezekana kuzijibu hoja zote kwa sababu ya michango ambayo imezidi. Wachangiaji mia moja na hamsini na kitu, kwa vyovyote vile hoja zilizoko pale siyo chini ya mia tatu na kitu. Niseme tu kwamba, yapo ambayo tutayapitia kwa haraka haraka.

Nianze na la kwanza, ambalo Msemaji wa Kambi ya Upinzani amelizungumzia, lile ambalo lilionekana kama kulikuwa na mambo ya kutokekusa ukweli kuhusu takwimu ambazo zinahusu bajeti yetu, tulipokuwa tumekutana kwenye Kamati ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, hoja ilikuwa kwamba, kwenye Bajeti ya 2007/2008, tuliongeza matumizi ya kawaida na tukapunguza matumizi ya maendeleo. Mheshimiwa Mnyaa, alitaka kujua kiasi kilichokasimiwa kwa robo ya tatu ya mwaka 2007/2008; ilikuwa ni bilioni 5.6. Akahoji je, hiyo robo ya mwisho zilizopatikana zilikuwa ni shilingi bilioni 306.7 au hazikupatikana tena? Vipi hali hii? Kumbukumbu za Wabunge ni kuwa, tumepitisha Bajeti ya Maendeleo ya shilingi bilioni 312.4, sawa na asilimia 86.5. Aliyosema bajeti ya maendeleo imetekelezwa, siyo sahihi na ni ya kulidanganya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, hii ilikuwa ni *serious allegation*, lakini nafahamu tulishaongea na Mheshimiwa Mnyaa, tukabdalishana vi-note kidogo tukakubaliana kwamba, nadhani ilikuwa ni suala la kuelewana tu ambacho tulikuwa tunakisema. Niseme tu, ufanuzi wetu ni kwamba, katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Bunge lilipitisha jumla ya shilingi 465,202,173,000; ambapo shilingi bilioni 32,657,178,000 ziliwu fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 432,544,965,000 ziliwu ni kwa ajili ya maendeleo. Katika kipindi cha mwaka 2007/2008, Bunge lilipitisha jumla ya shilingi 353,959,143,900, ambapo shilingi 41,549,559,000 ziliwu fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 312,409,584,900 ziliwu ni fedha kwa ajili ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa matumizi ya kawaida katika mwaka wa 2007/2008, kulitokana na kutengwa kwa shilingi bilioni 10 za Mfuko wa Nishati Vijijini. Nia ya Serikali ilikuwa ni kufadhili utekelezaji wa Miradi ya Nishati Vijijini. Aidha, bajeti ya fedha za nje za maendeleo ya mwaka 2007/2008, ilipungua takriban maradufu ya fedha za nje zilizotengwa kwa mwaka wa fedha 2006/2007. Serikali haina uwezo wa kupanga matumizi ya fedha za maendeleo za wahisani wetu. Fedha wanazoahidi kutoa ndiyo zinazopitishwa na Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu kwa pamoja hoja kama ambavyo zilitolewa, ambapo kwa mpangilio ziliwu hoja Na. 3.4 na hoja Na. 3.6 kwa pamoja kama nilivyoeleza. Niseme tu kwamba, wakati nawasilisha nilisema utekelezaji kuhusu mapato na matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2007/2008, katika kikao cha Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini kilichofanyika mwezi Juni, Mjini Dar es Salaam kwa bajeti iliyopitishwa ilikuwa shilingi 353. Hii ndiyo ilikuwa bajeti kwa kile ambacho tulijadili pale. Ilikuwa ni 353,959,143,900. Kati ya hizo, narudia tena shilingi 41,549,559,000 ziliwu ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 312,409,584,900 ni fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo za Miradi ya Maendeleo, na ndiyo hoja ya msingi inapokuja kwa Mheshimiwa Mnyaa, kati ya Sh. 115,716,584,900 ziliwu ni fedha za nje na shilingi 196,993 bilioni ziliwu ni fedha za ndani.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nifafanue kwamba, kati ya shilingi hizo nilizosema Sh. 196,693 bilioni ambazo ni fedha za ndani, shilingi bilioni 191 ziliwu ni fedha chini ya *Multilateral Debt Relief Initiative (MDRI)* na shilingi bilioni 5,693 ni fedha kutoka Mfuko wa Serikali Kuu. Kati ya hizo, shilingi 124,678 milioni za *MDRI* zilitolewa. Kati ya hizo ambazo ziliwu shilingi 191 bilioni, zilizotoka ziliwu ni 124 bilioni tu. Niseme pia tena kwamba, shilingi 4,950,321,000 kati ya shilingi bilioni 5.6 za Mfuko wa Serikali Kuu zilitolewa, ambayo ni asilimia 86.95 ndiyo ile ambayo Mheshimiwa Mnyaa alikuwa anaiomba.

Mheshimiwa Spika, tunampa nakala ya ufanuzi huu ili twende pamoja na kama kuna nafasi anaweza pia kwa baadaye tukampa maelezo kati ya Wizara na ye. Kwa hiyo, ninachosema ni kwamba, maelezo niliyoyatao katika muhtasari kwa ajili ya Kikao cha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kilichofanyika Siku ya Jumatatu

na Jumanne, ambapo ilikuwa ni tarehe 16 na 17 Juni, 2008, Sura ya 4 ukurasa wa 11, aya ya 4.3 ni ya kweli. Kwa kweli hayakuwa ya kuliongopea Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, narudia kusema tena kwamba, kiasi kilichobaki cha shilingi bilioni 66,322 za *MDRI* zitatolewa katika mwaka huu wa fedha 2008/2009, kama ilivyoelezwa katika ukurasa wa 105 wa Mpango na Bajeti ya Wizara niliyoiwasilisha katika Kikao kilichotajwa hapo juu.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Juni, 2008, Wizara ilipokea fedha za Miradi ya Maendeleo jumla ya shilingi 153,323,147,776, ambazo ni sawa na asilimia 43.32. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa; shilingi 130,028,321,000 sawa na asilimia 66.12 ni fedha za ndani na shilingi 23.23 bilioni 294,826,786 sawa na asilimia 20.13 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, huu ndiyo ulikuwa ni ufanuzi kwenye hoja ambao ulijitokeza. Ninafahamu kama nilivyosema kwamba hoja ziliwu ni nyingi sana na kwa kweli kama tunavyofanya utaratibu wa kawaida tu kwamba sisi tunaahidi kuhusu hizi hoja zote zilizobaki kwa maandishi. Kwa sababu kwa kweli sasa hivi sitaweza. Niseme natambua sana, tunashukuru sana maoni na ushauri wa Kamati ya Nishati na Madini ya Bunge chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa William Hezekia Shellukindo, lakini pia na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Harrison George Mwakyembe. Ushauri na maoni mliyoyatoa tutayafanya kazi, lakini mengi Mheshimiwa Naibu Waziri ameyasema.

Mheshimiwa Spika, mwisho, lakini si kwa umuhimu, nzungumzie kuhusu Sekta ya Madini. Naungana na wenzangu kama nilivyosema jana, tunaipongeza na kuishukuru sana Kamati ya Mheshimiwa Rais, iliyokuwa inaongozwa na Mheshimiwa Jaji Mark Bomani, kwa kazi nzuri iliyofanya. Nafahamu michango mliyotoa Waheshimiwa Wabunge, inatuongoza vizuri, lakini mchango ambao umetolewa mchana wa leo na Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba na Wabunge wengine, tungependa utekelezaji wa mapendekezo hayo uanze jana. Kama tunavyofahamu, mambo makubwa na mazito yanahitaji umakini, yanahitaji muda, yanahitaji fursa ya kujipanga, mkafikiria mara mbili kabla ya kuyatekeleza.

Mheshimiwa Spika, tunawaahidi kama tulivyosema, tumesema utekelezaji wake utakuwa unaanza ifikapo robo ya kwanza mwaka kesho, kwa sababu moja; tunaongelea masuala matatu hapa. La kwanza, lazima sasa tukamilishe kuipitia Sera yetu, iweze kujumuisha haya ambayo yamejitekeza. Sisi tulishakamilisha kuandaa Sera siku za nyuma.

Kwa mazingira ya sasa na haya mapendekezo ambayo yamekuja ya Kamati ya Rais iliyooongozwa na Mheshimiwa Mark Bomani, imekuja na mawazo mengine ambayo hayakuwepo kwenye zile Kamati ambazo zilishaundwa kabla ya hizi.

Kwa hiyo, sisi tukadhani kwamba ni busara tukamilishe kwanza upitiaji wa Sera. Kwa utaratibu wa kawaida wa Vikao vya Bunge lako Sukufu, sasa hatuamini kama tunaweza kukamilisha ndani ya Mkutano huu, kwa sababu itabidi tutayarische Muswada; kwa mfano, tukishamaliza hatua ya Sera, tutayarische Muswada wa Sheria mpya, ambayo kwa vyovoyote vile itahitaji kujadiliwa na Waheshimiwa Wabunge na kwa sababu tunasema tunataka kufanya *total overhaul*; ni jambo kubwa hili.

Mheshimiwa Spika, naomba mtuvumilie sana, mwezi wa nne ni ratiba nzuri ya utekelezaji katika mikakati hii. Baada ya kusema hayo, nawashukuru sana. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge. Nawashukuru wote ambao wamechangia nje na ndani ya Bunge letu Tukufu. Nawaahidi kwamba, tutaendelea kuisimamia Sekta ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini. Umejieleza vizuri sana na nina hakika katika hatua inayofuata hutapata matatizo makubwa. Waheshimiwa Wabunge, hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kuhusu Makadirio ya Matumizi ya 2008/2009, imewasilishwa na imeungwa mkono. Tutaingia kwenye utaratibu wa Kanuni ya 100(1) ili tuweze kuhitimisha. Kwa hiyo, namwita Katibu ili atutangazie hatua hiyo.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Mwongozo wa Spika.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, nilitaka tu mwongozo wako, wakati Waziri anataja michango ilivyotiririka, nadhani utaratibu ni kwamba, anaanza mchango wa Kamati, mchango wa Msemaji wa Kambi ya Upinzani, halafu wachangiaji wengine. Sina hakika kama utaratibu umebadilika?

SPIKA: Ikiwa alipitiwa kufanya hivyo, siyo tatizo kubwa sana. Nina hakika, ninavyomfahamu Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, sidhani kama alifanya kwa makusudi kuacha kutamka Kamati yako na pia Kambi ya Upinzani, wote mmemoa hoja nzito sana. Uzuri wake zote zipo kwenye *Hansard*. Kwa hiyo, mambo yamekaa vizuri tu. Nadhani tuendelee. (*Makofi*)

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 58 – Wizara ya Nishati na Madini

Kif. 1001 – *Administration and General* Sh.1,915,860,000

MWENYEKITI: Katibu hebu chukua majina sasa, naona kuanzia huku; Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Felista Bura, Mheshimiwa Dr. Siyame, Mheshimiwa Dr. Mlingwa, Mheshimiwa Ali Salum, Mheshimiwa Mpina, Mheshimiwa Mtutura, Mheshimiwa Killimbah, Mheshimiwa Nyalandu, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Manyinyi, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Mpendazoe, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Ruhahula, Mheshimiwa Batenga, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Dorah Mushi, Mheshimiwa Fatma Maghimbii, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Dr. Slaa, Mheshimiwa Mnyaa, Mheshimiwa Salim Hemed, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Ole-Sendeka, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo na mumewe Mheshimiwa William Shellukindo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Bishop Mpesya, Mheshimiwa Hasnain Dewji, Mheshimiwa Mrope, Mheshimiwa Ameir Ali, Mheshimiwa Shibuda, Mheshimiwa Idd Azzan, Mheshimiwa Mwinchoum, Mheshimiwa Ligalama, Mheshimiwa Lyamba, Mheshimiwa Lwanji, Mheshimiwa Diallo na Mheshimiwa Dr. Limbu. Mmewaandika wote hawa? Wako wangapi? Haya tunaanza na Mheshimiwa Jenista Mhagama.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi katika kipindi cha jioni. Naomba nitumie *vote* hiyo ya 58, programu ya 10, kifungu kile kidogo cha 1001; ninaamini kwamba, kwa kuwa tupo wengi haina haja ya kuendelea kuvitaja hivyo vifungu vyote, tusipoteze muda.

MWENYEKITI: Sawa sawa.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, baada ya ufanuzi wa Mheshimiwa Waziri, kabla sijaomba ufanuzi mdogo sana, ninaomba kusema kwamba, sasa naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, nina uhakika zile Kata za Wino, Mahanje na Gumbilo, zitaingizwa kwenye mpango huo wa umeme utakapokuwa unaelekeea Songea. Ufanuzi wangu kidogo ni kwamba, *feasibility study* iliyofanyika kutoka Songea kwenda Peramiho haikuunganishwa na ule upembizi yakinifu wa kutoka Makambako, Njombe, Songea, Mbanga na hata Mheshimiwa Waziri Mradi huo anautarajia kwa utaratibu huo.

Naomba anifafanulie; je, atafanya nini ili Peramiho sasa ianze kutajwa kwenye Mradi huo ili fedha itakapoletwa na Peramiho iingizwe kama eneo la kutekeleza mradi huo. Hapo tu, lakini kwa kweli naunga mkono hoja kwa maelezo yake. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Imekuwa sawa sasa. Uthibitisho Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Ni kweli tumesikia hoja ya Mheshimiwa Mbunge, kuhusu vijiji vya Wino na mimi

navifahamu. Niseme tu kwamba, hoja ya kwamba Mradi uanze kuitambua Peramiho, Mheshimiwa Mbunge alishaisema siku ile. Niseme kwa sababu ni Mradi ambao unahusisha wafadhili wa upande wa pili na *conception* ndiyo ilikuwa hiyo, pengine haikuwezekana kubadilisha. Sisi tunazingatia na zipo njia mbili, tunakwenda kulifanya kazi tuone kama kunaweza kutokea marekebisho tukaingiza hivi Vijiji vya Owino na kile kingine. Endapo itashindikana iliyobaki, basi tunasema fursa ipo kupitia Mfuko wetu wa REA, kama tunavyosema mwaka huu tunatarajia kuuboresha, kwa sababu tuna tozo ambayo itakuja kutuongezea nguvu; ni mambo ambayo tunayafanya kazi.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Kifungu ni hicho hicho. Mheshimiwa Waziri amesema kwa maneno ya uchungu sana. Ninachotaka kwa sasa, nipate ufanuzi wa Mradi huu wa Umeme nilioutaja wa laini hii, ambao Mheshimiwa Waziri anaujua sana na amekuwa akinianidikia barua kwamba, utekelezaji wake utafanyika katika bajeti hii ya mwaka 2008/2009. Umeme unaotokea pale *junction Hoboko* unakwenda Isengwa, Mbalagane, Lubiga na Mwandoya.

Mheheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufanuzi.

MWENYEKIDI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri kwa ufanuzi.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Namshukuru sana Mheshimiwa Mpina, kwa sababu tunaelekea sasa kuongea kwa *frequency* zinazofanana. Ni kweli sasa nimkaribishe Mheshimiwa Mbunge, tuone wenzetu wa TANESCO ambao ndiyo wataalamu pekee sasa hivi wanapitia hii miradi tunayo. Anafahamu tumekuwa tukiyasema, lakini nilitaka ambacho hatutaki tuahidi kwa mfano, mtu unamuahidi Mradi wako kwa hesabu za mwaka 2006 unaghari mu milioni 200, kumbe sasa hivi ni milioni 400. Ndiyo maana nikasema, naweza nikatumia maneno ya utani, tunaogopa kusutwa kwamba, kwa nini tusijiridhishe kwanza gharama halisi halafu tuje tuseme na ndiyo maana wenzetu wanafanya jambo hilo.

Namuahidi Mheshimiwa Mpina kwamba, tuwasiliane tuone gharama zake, kwa sababu TANESCO wanaendelea kua-up *date* gharama halisi kwa ajili ya miradi vijijini. (*Makofifi*)

MHE. FELISTA A. BURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nina jambo dogo tu ambalo linahitaji ufanuzi wa Waziri. Katika mchango wangu wa maandishi, nilimwomba Mheshimiwa Waziri, alieleze Bunge lako Tukufu ni lini atasitisha malipo kwa IPTL, baada ya kugundulika kwamba *capacity charge* inayolipwa kwa IPTL na TANESCO ni zaidi ya kiasi kinachostahili? (*Makofifi*)

MWENYEKIDI: Mheshimiwa Waziri, ufanuzi.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu suala la IPTL linagusa hisia kwa wananchi wote, si Waheshimiwa Wabunge tu. Niseme tu kwamba, kama tulivyoeleza na mgogoro ambao sasa hivi baada ya wenzetu kuwashinda kesi Marekani, tukaambiwa twende kwenye utaratibu wa kawaida wa

usuluhishi. Walipokwenda kule Mahakamani New York Marekani, walikuwa wameruka huu utaratibu kwa sababu mkataba ulisema kama kuna kutokuelewana, kuna suala ambalo mnabishania kama tunavyobishana sasa, Serikali na *IPTL* basi kwanza upitie usuluhishi. Wenzetu wanataka kuruka.

Tumerudishwa kwenye usuluhishi lakini pia tuliporudi huku ikajitokeza kwamba na ilikuwa ni pande zote mbili. Sote tuna-*assess situation* ni lazima twende kwenye usuluhishi, hatuwezi kumalizana sisi wenyewe nje hata kabla ya kufika kwenye usuluhishi. Hoja ya msingi ni kwamba, tunabishana kwa kile ambacho sisi tunaamini ni sahihi; lakini na wao wana mtazamo wao.

Sasa ilibidi tufikie muafaka, tumekubaliana kwamba, tutafanya kikao cha pamoja na wenzetu tuna ratiba ambayo tumeipanga; ndani ya mwezi huu tutakutana pamoja, tukishindana pale tunakwenda Baraza la Usuluhishi. Kwa utaratibu wa kisheria, si sahihi sasa kusitisha kwa sababu tukisitisha itakuwa tumekiuka halijaamliwa. Kwanza, tushindane tusipoelewana tutakwenda kwenye usuluhishi; lakini faida yake ni nini, kwa sababu hili jambo si kusema ukichelewa utapoteza, hapana?

Sisi kama tutashinda mwisho wa safari, kama nilivyosema, kwa sababu mahesabu yanaonyesha timesha-over pay zaidi ya bilioni 150, maana yake hizi zote zitarudishwa. Sitaki kusema kwamba, linaweza kutokea jambo zuri kiasi gain; kwa sasa labda inatosha kusema kwamba, tuache utaratibu uchukue mkondo wake, lakini tutakuwa tunawaarifu wananchi kupitia Bunge hili Tukufu, kwa kadiri muda unavyokwenda. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Naona kama chombo hakifanyi kazi au kimekaa vibaya; basi jaribu nyingine tafadhali Mheshimiwa.

MHE. DR. FESTUS B. LIMBU: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru sana kwa busara zako, umeanzia mwisho ambako tulidhani tusingewenza kufikiwa. Wachimbaji wadogo wadogo hawa wa madini, wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu, kwa kutumia zana duni na nyenzo zilizopitwa na wakati.

Naipongeza Serikali kwa busara zake, kwa kuleta mradi wa kuboresha zana na nyenzo wanazofanyia kazi. Cha ajabu, mwaka huu fedha hizo hazikutolewa, zilitolewa shilingi bilioni moja bajeti iliyopita kwa mara ya kwanza. Je, ina maana kwamba, fedha zilizokuwa zimetengwa mwaka jana kwa mara ya kwanza, zimetosheleza mahitaji ya wachimbaji wadogo wadogo? Nilikuwa naomba ufanuzi huo Mheshimiwa Waziri. Ahsante sana Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Ufanuzi Waziri wa Nishati na Madini.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Namshukuru kaka yangu, Mheshimiwa Dr. Limbu kwa swali lake. Ni kweli pesa hazijatosha, lakini tumesema mwaka huu Mfuko kwa ajili ya wachimbaji wadogo ambao

una takriban kama bajeti tatu, zile zilizotangulia; mwaka huu ni kweli tunajaribu kuangalia ni jinsi gani ambavyo tunaweza kupata pesa za ndani, lakini pia tumeshaanza kuongea na wenzetu wa Benki ya Dunia. Tulipokuwa Arusha mwanzoni mwa mwezi wa sita kwenye Mkutano wa *Leon Sullivan* ...

Mimi nilibahatika kukaa na Rais na Makamu wa Rais wa Benki ya Dunia kwa Kanda ya Afrika, tukampeleka pia mpaka katika machimbo ya Mererani, akaona hali halisi ya mfano wa wachimbaji wadogo, mazingira wanayofanyia kazi. Tunakwenda vizuri, ndio maana tunaongea kwa kujimini kwamba, Mfuko huu ukianzishwa matokeo yake yataonekana, utakuwa wa kweli, sio kusema kwamba ni jambo ambalo tunaendelea kulitolea ahadi. Kwa hiyo, namwomba kaka yangu, Mheshimiwa Dr. Limbu, aamin fedha haikutosha lakini mwaka huu tunaendelea kujianga vizuri na tunaamini ndani ya mwaka huu wa fedha, tutatekeleza uanzishaji wa Mfuko huo, *revolving fund*. Ahsante.

MWENYEKITI: Naona bado, Mheshimiwa Dr. Limbu.

MHE. DR. FESTUS B. LIMBU: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Waziri kwa majibu mazuri. Ningependa kuelewa katika mchakato huo alioueleza; je na wachimbaji wadogo wadogo wa Ngasamo huko Magu, atawakumbuka?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu ni ndio. (*Makofii*)

MHE. ANTHONY M. DIALLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunikumbuka mapema. Mimi nipo kwenye mchango wangu wa maandishi. Nililetta *issues* mbili, kwanza, kwa kuchangia kwa mdomo nilitaka nipaye ufanuzi wa Miradi ya Wilaya ya Ilemela au Mkoa wa Mwanza, ambayo ipo chini ya *Millenium Challenge Compact*. Atupe ufanuzi, kwa sababu nimetafuta vitabu vyote vya *development* na sehemu nyingine sioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kwenye maandishi niliuliza, wakati wa Mradi huu wa kupeleka Maji Shinyanga na Kahama, *originally* ilikuwa umeme utoke karibu na *Manawa Genery*, ili uende mpaka Ihelele. Wizara ya Maji wakati ule wakalipa fedha, nguzo zikawekwa na nyaya zikawekwa. Baadaye ikaja kuonekana kwamba, waya ulikuwa hautoshi kwa sababu nguzo za umeme kuitia *line* hiyo zilikuwa ni ndogo, kwa hiyo ikaamuliwa wachukue umeme kutoka Bulyanhulu. Sasa baada ya hapo kilichotokea hizo nguzo na nyaya zote zilikuwa zimelipiwa, tulitegemea kwamba, hizo nyaya zingekuwa *energized*, yaani ile *line* ingekuwa *energized* ili wananchi wa maeneo yale wapate umeme. Badala yake, *TANESCO* wakaja kung'oa zile nguzo zote, *line* nzima, wakati zimeshalipiwa na badala yake ina maana wananchi hawana umeme. Sasa nilitaka kupata maelezo kwamba, *TANESCO* wametuibia au vipi?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tunakiri kupokea mchango. Kwanza, Mheshimiwa Diallo, alichangia kwa kuzungumza lakini baadaye akachangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, kuhusu Miradi ya Umeme; nafahamu alitaka kujuu hasa Mradi wa Kisesa – Kayenze mpaka Igombe, nakumbuka vizuri. Ukisoma kitabu cha hotuba ya bajeti ukurasa wa 77, umeelezea miradi ambayo imo ndani ya Mkoa wa Mwanza, hasa Wilaya ya Mwanza, ambapo kwa sababu wakati majadiliano yanaanza kuhusu huu Mradi wa *MCC*, Ilemela ilikuwa haijawa Wilaya. Kwa hiyo, kinachojitokeza hapa ni Wilaya ya Mwanza. Niseme tu kuwa haikuwa rahisi sana kumaliza maeneo yote, lakini faraja iliyopo ni kwamba, kama nilivyosema, ukishafika umeme kwa mfano, maeneo ambayo yatakuwa yameguswa, yapo mengi sana katika ukurasa wa 77. Itakuwa ni rahisi kuyafikia haya maeneo unayoyafahamu ya Kisesa, kutoka Kisesa kwenda Kayenze, nakufahamu kule, kwenda Igombe, kama hili halijitokezi vizuri, tutaangalia pia kupitia fursa nyingine ambazo tunazisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni Mradi wa Maji, nafahamu Mheshimiwa Shibiliti, alikuwa anafuatilia sana kwa sababu lipo Wilayani Misungwi. Kilichojitokeza ni kwamba, ule Mradi ulikuwa chini ya Wizara ya Maji, *TANESCO* walikuwa *contracted* lakini baada ya kubadilisha *scope* yake, matarajio waliyokuwa nayo wananchi kwamba, kwa sababu wangefaidika na kupitishwa kwa ile *line* kwenda kwenye kianzio cha maji. Nilishaongea na Mheshimiwa Shibiliti kuwa, tunalifanya kazi tuone, kwa sababu cha msingi hapa ni kuwafikishia wananchi huduma ya umeme, sio kurudisha tena zile nguzo ambazo maji tayari yalishakuwa *taped* kuanzia Ihelele. Kwa hiyo, sisi tunachosema, tunaendelea kulifanya kazi kupitia hivi vyanzo vyetu vya kawaida, tuone jinsi gani wananchi wa maeneo yale, ambao walikuwa na matarajio makubwa kama *line* ya mwanzo ingeendelea. Tunazidi kuwasiliana na Waheshimiwa Wabunge.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika machache niliyochangia, ningeomba ufanuzi kuhusu suala la kupeleka umeme Mgandu. Mheshimiwa Waziri, ametueleza juu ya ukarimu aliopewa Peramiho na akawaahidi, sasa ukarimu alioupata Mgandu, anawaambiaje hawa watu? Maana nakumbuka tulifuatana pamoa, akapewa ukarimu mkubwa sana, hajagusia kabisa hilo eneo. Je, ukarimu wetu ulikuwa mbaya kuliko ule wa Peramiho? (*Makof/Kicheko*)

Mhewshimiwa Mwenyekiti, la pili, ningeomba kujuu juu ya mgodi huu unaochimbwa huu wa *Litman* katika eneo hilo hilo la *Mgandu Complex*. Je, Serikali ina habari kwamba kuna machimbo yanayochimbwa kimya kimya hapo? Ahsante sana.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo huwa hayafanani, lakini pia hata Mgandu nilipata ukarimu wa hali ya juu, ingawa siwezi kulinganisha na wa Peramiho. Niseme tu kwamba, *seriously* mwaka jana nilikwenda na kaka yangu, Mheshimiwa Lwanji, tulitokea hapa Bungeni, tulifika Mgandu. Nafahamu anaongelea *line* ya kutoka Itigi kwenda Mgandu, kilometra 60. Nafahamu pia kwamba, Wananchi wa Mgandu, wapo tayari kuchangia kwa gharama zao wenyewe, kutekeleza ule Mradi, lakini kaka yangu anafahamu pia tumekuwa na mawasiliano ya hivi karibuni ofisini kwetu, mpaka nikamwomba atusaidie pia kusukuma kidogo wenzetu wa *TANESCO* wa *update* haraka zile gharama.

Tunamshukuru Mheshimiwa Mbunge, ametusaidia, tunamuweka kwenye mstari ule ule kama nilivyosema, pamoja na Waheshimiwa wengine, ambao maombi yao tunayo. Ningeweza kutaja orodha kwa sababu ninao wote, lakini pia pengine muda hautoshi. Niseme tu kwamba, tunatoa matumaini kwa Watanzania wengi kwamba, ndani ya mwaka huu wa fedha, tutatekeleza Miradi mingi kupitia huu Mfuko wa REA. Kwa sababu hizi bilioni 20, ukijumlisha na ile tozo, tuna hakika kwamba, tutakuwa na bilioni nyngi kiasi na juhudi nyininge zinaendelea.

Kwa hiyo, namuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba, Mradi wako tunaufikiria, tutakupa taarifa kamili baada ya kutuletea zile taarifa ulizotuletea, tutakupa taarifa. Tunamaanisha Wananchi wa Mgandu, tunawakumbuka na pengine tutakupa taarifa iliyo nzuri zaidi baada ya kujiridhisha kwa mambo ya kitaalamu. Ahsante sana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu la pili, tunafahamu haya machimbo tunayafanya kazi. Afisa wetu wa Madini Mkoa wa Singida, yupo analifanya kazi. Nadhani baada ya wiki mbili, tutakupa taarifa ambayo ni nzuri zaidi kuhusu nini kinaendelea katika maeneo ambayo umetuambia kwamba, unafanyika uchimbaji. Kwa sababu pia sio mara yako ya kwanza kuniambia mimi, ulipokuja juzi uliniambia pia. Ahsante sana.

MHE. CLEMENCE B. LYAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, pamoja na mambo mengine, nilikuwa naomba ufanuzi kuhusu kwa masuala mawili. La kwanza, kwenye ukurasa wa 79 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, chini ya Miradi ambayo inafadhiliwa na *MCC* kuna viji vitatu. Vijiji vya Msolwa Sekondari, Kijiji cha Kitete na kijiji cha tatu niwie radhi nimekisahau. Vijiji hivyo viro katika Wilaya ya Kilosa lakini kwenye kitabu imeandikwa viro katika Wilaya ya Kilombero. Niliomba Mheshimiwa Waziri, atoe ufanuzi. Kile kijiji cha tatu ni Kisanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kwamba, *niki-assume* kwamba, Kijiji cha Kisanga ni sahihi kipo katika Wilaya ya Kilosa, kwa maana ya kufungiwa umeme chini ya ufadhili huo. Kulikuwa na mpango wa kusogezwa umeme kupeleka kwenye Kata ya Ureling'ombe, ambako kuna muwekezaji ambaye yupo *busy kule prospecting for a copper*, dhahabu na vitu vingine ambavyo nafikiri Wizara inafahamu. Kwenye Hotuba ya Waziri, sikuona chochote kilichogusiwa kuhusu Mradi huo na kupelekewa umeme kwenye Kata ya Ureling'ombe. Nashukuru.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, itakuwa kama utani lakini pia Mheshimiwa Lyamba, mwaka jana tulikuwa naye kwenye eneo lake la kazi, tukafika tukayaona maeneo haya, nako tulikirimiwa, lakini niseme kwa hili. (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, muwe mnachukua na Spika, kwenye mambo. (*Makofi/Kicheko*)

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, tutakukumbuka. Ni kweli, hili linajirudia lile ambalo nililitoa maelezo ya jumla, nilitumia hoja ya Mheshimiwa Laizer, kufafanua mambo ambayo yanajitokeza kama ambavyo limejitokeza hili kwamba, wakati Miradi inaanza, suala la mipaka ya kijiografia si kubwa, suala kubwa ni kufikisha huduma kwa wananchi. Maeneo haya kama tunavyosoma jiografia, kama zilivyo nchi zetu tu, watu ni walewale lakini tumegawanywa Tanzania, Kenya, hata wao wakati wa *concept appraisal* haya mambo ya mipaka hayakuzingatiwa, ndio maana unakuta mambo yana-overlap. Cha msingi ni hicho kwamba, Mheshimiwa Lyamba, tunafahamu Miradi yako hii imo na kama unavyoona hapa, imejitokeza kwenye kitabu. Kwa hiyo, hii ya kwamba unaonyeshwa kama upo Kilombero, nakuomba tu utuwie radhi, lakini haikuwa nia mbaya. Wengine wote ambao miradi yao inaonekana haipo katika Wilaya zao, kama ambavyo wangependa isomeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu la pili, nafahamu ulikuja na muwekezaji ofisini kwetu, tunaendelea. Kama unavyosema, kwa Mradi huu sasa ipo fursa ya Miradi mingine, nikukaribishe tuendelee kuona kulingana na fursa zetu za uwezo wa kifedha, jinsi gani tunaweza ku-accomodate kwenda kwenye machimbo ambayo muwekezaji mlifanya nae ziara ofisini kwetu na gharama zinaweza kuwa kiasi gani. Nadhani halitakuwa jambo kubwa, tutaona tu jinsi ya kulitekeleza. Ahsante.

MHE. CASTOR R. LIGALLAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nami lilikuwa linahusiana na hilo hilo kwamba, hapa uwakilishi wetu tunafanya wa kijiografia. Sasa inapoonekana Wilaya yangu ya Kilombero imeandikwa vijiji sita lakini vitano viro Wilaya ya Kilosa, mimi napata faida gani kuandikiwa tu majina ya mtu mwingine? Je, Waziri, anaweza kunifafanulia hilo kwa kuniwekea vijiji sita vingine vyta wilaya yangu vinavyotoka kwenda kwa ndugu yangu hapa sasa? (*Kicheko*)

MWENYEKIDI: Aah, si lazima iwe sawa, pengine ungevitaja ungemsaidia. Huwezi kusema tu vijiji vyovyyote, sasa itakuwaje?

MHE. CASTOR R. LIGALLAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nitaje vijiji ambavyo viro karibu na Mgodi wa Kihansi; Chita, Udagaji, Ikule, Nchombe, Ndingu, Mofu, Namawala na Idete,

MWENYEKIDI: Nadhani vinatosha, basi. Mheshimiwa Waziri, kwa hivyo vitano.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mheshimiwa Mbunge, nafahamu alishauliza pia swali hapa Bungeni, kuhusu Miradi hii na kweli ipo ndani. Ni kati ya Miradi ambayo tuna-update gharama zake halisi, lakini niseme kwamba, kwenye ile ya MCC ilivyo, tulivyofikia hapa si rahisi kubadilisha sana.

Kama nilivyosema, umeme ukishafika, kwa mfano kama ulikuwa umbali wa kilometra tano, sasa ukaja mpaka labda nusu kilometra au robo kilometra, inakuwa rahisi

zaidi kuufikisha hapo ulipo na kwa kutumia hasa vyanzo vyetu vya ndani. Kwa hiyo, nimpe matumaini Mheshimiwa Mbunge kwamba, hili lisikusikitishé.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine linalojitokeza, pengine sisi kama Wizara, tutachukua *initiative* ya ku-reconcile hasa hii Miradi ipo kwenye wilaya gani ili baadaye tuwape Waheshimiwa Wabunge, taarifa sahihi kwamba katika Wilaya yako, katika Wilaya au Jimbo lako, miradi inayohusika ni hii na hii, pengine itatusaidia sana kuondoa utata huu. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Aah, sasa nije Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Fatma Maghimbí.

MHE. FATMA MUSSA MAGHIMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri, wakati ana-*wind up* alisema kwamba, nguzo na nyaya za umeme zitapita kwenye kila *potential users*. Kwa nini Mheshimiwa Waziri, asiseme kwamba, nyaya zitapita kila pahala kwa sababu pia nilikuwa na wasiwasi kama labda kuna sehemu nyingine watu hawataweza kulipa? Mimi naona Watanzania wengi, wanao uwezo wa kulipia umeme hata kule vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kuna sehemu labda atasema hakuna watu; kwa nini nguzo zipite? Nataka kumkumbusha Mheshimiwa Waziri kwamba, Watanzania tunazaana sana. Kwa hiyo, leo sehemu hii unaikuta haina watu, nyaya hazipiti, lakini kesho ukija watu wengi wapo. Halafu isitoshe, wenzetu wakipima viwanja huwa wanatayarisha *infrastructure*; *infrastructure* ni pamoja na umeme. Kwa nini nguzo zisipite Tanzania nzima na hata hizo sehemu kabla hazijapimwa kuwekewa *infrastructure* kama hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaambiwa kwamba, umeme unaotumia maji ni umeme rahisi sana, kwa hivyo sikuona sababu kwa nini Waziri, anashuku kuwa sehemu nyingine?

MWENYEKITI: Mheshimiwa, unaruhusiwa chini ya kanuni ya 101, fasili ya 3, hoja mbili tu wakati wa Kamati ya Matumizi. Naona unaendelea, Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kumjibu Mama yangu Mheshimiwa Maghimbí ni kwamba, tunasema *potential users* kwa sababu ni kati ya yale mambo niliyoyasemea awali kwamba, yapo mambo ya ukweli kwamba, huduma ya umeme tunayoiongelea leo si huduma ya bure ni huduma ambayo ina gharama zake inalipiwa. Ili kukidhi eneo fulani kuweza kupata hiyo huduma, kuna vigezo vinatumika kuangalia watumiaji waliopo pale.

Nasema haya mambo, nguzo zinaweza kuwa zinapita lakini watu sasa hivi tuna teknolojia nyingi, unakuta labda eneo fulani limejaa *solar panels*, unafanyaje katika mazingira hayo Mheshimiwa Mbunge?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana tukasema kwamba, lazima ujue hiyo ni moja lakini pia sisi kama nchi, kwa jinsi tulivyo uwezo wetu wa kiuchumi si jambo la

ajabu kufika maeneo mengine ambayo *feasibility study* ikifanywa, inakuwa bado vigezo havijakamilika. Kwa hiyo, hatutaki kuliondoa hili tukasema tu pale ambapo kuna mkusanyiko au kuna makazi ya wananchi. Hili ni jambo amabalo tulikuwa tunaliongelea katika *context* hiyo, sio zaidi ya hapo. Cha msingi ni kwamba, maeneo yote ambayo yatapitiwa na yanakidhi vile vigezo, yatapata hii huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kuhusu ...

MWENYEKITI: Kupitisha maeneo ambayo hakuna hata watu.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba kwa nini tusiweke miundombinu kabla. Hili suala la kwamba, Watanzania tunazaana sana, sitaki kulisema kwa sababu sina ulinganifu. Niseme tu kwamba, kikwazo chetu ni gharama, tungependa tufikie hatua hiyo kwamba, weka miundombinu kwanza, huduma kwanza na mahitaji baadaye.

Nadhani kwa sasa si rahisi, lakini tutafika mbele ya safari. Namwomba tu Mheshimiwa Mbunge, aamini kwamba, juhudzi zinafanyika za kuwezesha kuona Watanzania wengi wanapata hii huduma ya umeme. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Fatma, hujaridhika?

MHE. FATMA MUSSA MAGHIMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka kumkumbusha Mheshimiwa Waziri kwamba, zipo pesa zitapatikana hivi karibuni ambazo *TANESCO* na Serikali, walikuwa wanalipa *DOWANS*. Sasa zile zikipatikana; kwa nini zisianze hiyo kazi haraka?

MWENYEKITI: Basi kama zipo wamesikia, nadhani watazitumia tu. Mheshimiwa John Cheyo.

MHE. JOHM M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wakati nachangia juu ya Ripoti ya Kamati, yaani niki-refer Ripoti ya Kamati, nilipata hisia kwamba, Mheshimiwa Waziri, alikuwa amemshauri Mheshimiwa Rais kwamba, baadhi ya mapendekezo ambayo yamo humu yatafanyiwa kazi haraka iwezekanavyo.

Katika kujibu hoja, Mheshimiwa Waziri, ameniacha mdomo wazi kwa kusema labda Aprili, 2009! Hili ni jambo la kusikitisha sana, kama ni kweli kuna mambo hapa ambayo tayari Serikali imeshazungumza na wawekezaji waliopo. Kwa mfano, 15% *additional allowance* na amebakia mmoja tu kukubali ni kitu gani kinachozuwia Serikali kuondoa kipengele hiki katika sheria? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo hapa ya mrabaha, kuna mambo ya unaifuu wa *fuel levy*; ni kitu gani kinauzuia Serikali kuleta hapa marekebisho na kusema watakaoweka mikataba mipyä watafuata utaratibu huu? Wale wengine walio na mikataba, tutaendelea kuzungumza ili waingie katika utaratibu mpyä. Ni kweli Waziri

ananiambia kwamba, hapatakuwa na mkataba tena kati ya sasa na Aprili, 2009? Ningependa ufanuzi.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, asubuhi Naibu Spika, alikubali kwa niaba ya Kiti kwamba, Taarifa ya Kamati ya Bomani, Spika aipangie wakati mzuri ijadiliwe. Nadhani mapendekezo ya Mheshimiwa John Cheyo, yanakiuka kanuni, yanaanza kuwahisha shughuli ambayo tutajadili baadaye.

Kwa hiyo, ningependa tuwe na subira. Kwanza, Spika wala hajaisoma, alikuwa *busy* hapa hapa. Kwa hiyo ni vizuri mpewe nafasi Waheshimiwa Wabunge, ili tuishauri Serikali yetu vizuri, hayapo hayo tu, yapo mengi mengine. Kwa hiyo, naona hakuna uhalali wowote wa Waziri kulijibu hilo kwa hivi sasa, tutasubiri wakati tunashughulikia kuijadili Taarifa ya Kamati, itapangiwa siku. (*Makofi*)

Narudi sasa mkono wa kulia, Mheshimiwa Dr. Siyame.

MHE. DR. LUKA J. SIYAME: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nianze kwa kusema kuwa, pamoja na kwamba, Wizara ya Nishati na Madini, ina Mawaziri, Katibu Mkuu na Watendaji wa Wizara hiyo, pamoja na taasisi zake, ambao ni marafiki zangu sana katika shida na raha, lakini leo hii naomba nitofautiane na hoja yao. Nasema napinga hoja yao, kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka huu wa fedha ...

MWENYEKITI: Kwa mujibu wa Kanuni, unatakiwa uombe ufanuzi sio kupinga hoja.

MHE. DR. LUKA J. SIYAME: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufanuzi katika hoja zifuatazo: Kwa bajeti yao ya mwaka huu wa fedha, Wilaya ya Mbozi, hususan Jimbo la Mbozi Magharibi, hakuna hata Mradi mmoja; uwe ule wa utekelezaji ama utafiti wa siku zijazo, ambao unaonekana. Halafu pia nilitegemea kwamba, wakati wa ufanuzi wa hoja hizi, kutokana na mchango wangu wa maandishi, Mheshimiwa Waziri, angeweza kulieleza Bunge hili kwa nini ile *transformer* ambayo ilikuwepo Tunduma ikielekea kupeleka umeme kwenye kituo cha afya ambacho kina *mortuary* inayotumika na wananchi wa pale Tunduma, imeondolewa ndani ya wiki moja iliyopita na kuwekwa sehemu nyingine ya majengo ya watu wa kawaida?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *Concern* ya Mheshimiwa Dr. Siyame, tunayo. Tumeona mchango wake wa maandishi, tumeongea na wenzetu wataalamu wa *TANESCO* tukiwa hapa, lakini tumekubaliana kwamba, tulifanyie kazi kwa kina; kwanza, tujue sababu zake kama ambavyo limejitokeza hapa. Bahati mbaya kwamba, sasa hatutakidhi matarajio ya jibu ambalo ungelipenda. Ninakuarifu rafiki yangu Dr. Siyame, kaka yangu, kwamba tumeshaanza kulifanya kazi. Bahati nzuri, wataalamu wetu wote wa Wizara wapo hapa na niseme tu kwamba, nikupe miadi ya Siku ya Ijamua, tukutane tukupe taarifa kuhusu tutakuwa tumefikia wapi. Ahsante sana.

MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba ufanuzi mdogo tu lakini muhimu sana. Kwanza, niliomba nielezwe maombi yangu ya muda mrefu ambayo Mheshimiwa Waziri, anayafahamu, ya umeme sehemu ya Neregani, ambako Mbunge wa sasa anaishi, lakini hakuna umeme, Bugaya Mbelele na Kiwanja cha Ndege cha Shinyanga ambacho wengi kama sio wote, mnafahamu hakina umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba ufanuzi kuhusu kupeleka umeme kwenye kiwanda kinachotajwa cha simenti cha *TANSEM* kitakachojengwa Kizumbi, ambako tayari wenyewe kiwanda wamekwishalipia gharama za kufanyiwa tathmini ya gharama za umeme. Naomba ufanuzi ni lini umeme utafika ninakoishi na maeneo niliyoyataja, pamoja na kwenye kiwanda hicho ambacho kinatarajiwa kuwa kitazalisha tani 1,000 za simenti kwa siku na kuajiri Watanzania 500 wa kudumu.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na hili la pili la eneo la kiwanda. Mahitaji ya kiwanda tarajiwa cha simenti pale Kizumbi, wenzetu wa *TANESCO* wataendelea kufanya mawasiliano na wenyewe kiwanda tarajiwa, kwa sababu pale kuna mambo ya ufundi. Hivi sasa *TANESCO* wana teknolojia ya kisasa zaidi, wanazidi kuboresha huduma zao. Yapo mambo ambayo hatuwezi kuyatolea ufanuzi, lakini halina utata hata kidogo, kwa sababu kiwanda ni kati ya watumiaji wakubwa na *TANESCO*, wangependa kunufaika na watumiaji wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la maeneo ya Nelegani na Bugaya Mbelele, nafahamu Mheshimiwa Mbunge, tumekuwa naye kwa muda mrefu tunalishughulikia. Inanisikitisha sana, kwa sababu nafahamu ni kati ya Watanzania ambao wanaathirika na ukosefu wa huduma ya umeme, lakini bado nakupa matumaini. Nimezingatia na tutaendelea kuzingatia, tupe muda kidogo tutalifanyia kazi. Nafahamu tumeshauriana sana mimi na wewe kwa muda mrefu, lakini endelea kuniamini kaka yangu, uone ndani ya mwaka huu wa fedha kitatokea nini. Ahsante sana. (*Makofî*)

MHE. AHMED ALLY SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa jinsi alivyopunguza ile *pressure* tuliyokuwanayo. Mimi nina mawili tu, la kwanza, katika maombi yangu niliyochangia kuna sekondari tatu ambazo gharama zake tayari nilishamuwasilishia na hazifiki hata shilingi 100,000,000 ili wanafunzi wasome vizuri na tuondoe giza ambalo linaleta matatizo pale. Ningependa anitafutie fedha katika bajeti hii ili Sekondari ya Kituli, Sekondari ya Tinde na Sekondari ya Samwea, zipate umeme. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kwa kuwa nilikwisha ahidiwa kwamba, Jimbo la Solwa, litapata umeme katika bajeti ya mwaka 2009/2010; kwa kuwa mwaka huu hatukupata fedha, ningependa Mheshimiwa Waziri, anihakikishie kama 2009/2010 Jimbo la Solwa, tutapata umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la Sekondari tumeshaongea na wenzetu wa *REA*, linafanyiwa kazi si kwa sababu Mheshimiwa jana alichangia kwa uchungu sana, hapana! Ndiyo utekelezaji tu wa miradi inayokuja na tuliyonayo katika ofisi zetu. Kwa hiyo, hili tumelizingatia na tunalifanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la Jimbo la Solwa kupata umeme, kama tulivyoongea ni kwamba, vipaumbele vyetu ni hivyo. Ahadi yake na ninashukuru kwamba, kaka yangu leo amerekebisha, maana jana lilivyokuwa linajitokeza ni kama vile ahadi ilikuwa kwenye bajeti hii. Tulikuwa na yale makabrasha, tulipojiridhisha tukaona kwamba, ahadi ile ni kwa ajili ya bajeti ya mwaka kesho. Nakushukuru kaka yangu ume-reconcile hizi takwimu na sisi tunakuahidi kwamba ni kweli mwaka kesho tutaanza kuutekeleza huu mradi.

SPIKA: Mheshimiwa Ahmed naona hujaridhika?

MHE. AHMED ALLY SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana, katika mchango wangu nilipokuwa nachangia nilisema siungi mkono hoja lakini kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, sasa hivi nasema naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Katika mchango wangu wa maandishi, nilizungumzia sana suala la umeme wa gesi kutoka Mnazi Bay wa *ARTUMAS*. Nilitegemea kwamba, aidha Mheshimiwa Naibu Waziri au Mheshimiwa Waziri mwenyewe, angweza kugusia kidogo lakini kwa bahati mbaya hakukuwa na maelezo yoyote.

Sasa naomba ufanuzi kutoka kwake, matarajio haya ya kuzalisha umeme zaidi ya megawatt 300 na kuunganishwa na Gridi ya Taifa; *grid* hiyo itaunganishwa kuitia wapi; itaunganishwa kuitia Namtumbo ambapo Wilaya ya Nanyumbu, pamoja na Tunduru tutanufaika au itapitia Kaskazini mwa Mtwara, ambapo Wilaya hii ya Nanyumbu pamoja na Tunduru haitanufaika? Hilo la kwanza.

La pili, naomba Mheshimiwa Waziri awafafanulie Wananchi wa Tunduru ni hatua ipi imefikiwa kati ya Wizara, pamoja na Kampuni ya Kanyan Capital, ambayo imeonyesha kupenda kuwekeza katika Wilaya ya Tunduru kwenye *mini-hydro*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Tunduru inufaike na Mradi kutoka wapi, tuenze na Mradi kutoka Makambako, utakapofikia Songea uende Namtumbo tu-tape kwenda hapo, tupasue lile pori tuelekee Tunduru ama tuendelee na Mradi wa *ARTUMAS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri mimi nimepita maeneo hayo mwaka jana, naifahamu jiografia ya Tunduru vizuri na naifahamu *potentiality* ya pale. Nirejee kuwapa

matumaini Wananchi wa Tunduru kwamba, tunaendelea kulifanya kazi, kwani ni jambo la kulifanya kazi. Tunaangalia ni urahisi upi utawezesha kufikisha umeme kwenye Dridi ya Taifa katika Wilaya ya Tunduru. Kote ni kilomita nyingi, lakini unaweza kusema pengine Mradi wa ARTUMAS kwa sababu utaanza mapema zaidi, unaweza kuwahi kufika. Bado nasema si ahadi, ndiyo itakavyokuwa kwamba, Mradi utakaowahi. Tunaamini kwamba, Mradi wa ARTUMAS utawahi kwa sababu wenyewe kimsingi ni mwendelezo, shughuli zilishaanza pengine unaweza kuwa ni mzuri zaidi.

Lakini kuna mambo ya kiutaalamu, nafahamu Mheshimiwa Mtutura, amefanya kazi kwenye Sekta ya Umeme; kuna mambo ya kwenda kuyafanya kazi kuona lipi litakalokuwa rahisi zaidi.

Nimuahidi tu kwamba, tutaendelea kuwasiliana mimi na yeye, Ofisi yetu ipo tayari ili tuone baada ya kufanya *study* ni wapi itawezesha kufikisha umeme wa gridi kwa urahisi zaidi katika Wilaya ya Tunduru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kuhusu *Kanyan Capital Company*, kwanza, namshukuru sana Mheshimiwa Mtutura na amekuwa ni mfuatiliaji wa karibu, amechukua hatua za kufuatilia hawa wawekezaji wanaoonyesha nia ya kuwekeza umeme unaotokana na maporomoko ya maji. Amekuwa ofisini kwetu tumeongea naye, tumeshauriana na wataalamu wetu hasa kile Kitengo cha Umeme wa Maji, wanaendelea kuwasiliana na kampuni kwa yale mambo ya kitaalamu. Tutampa taarifa, kwa sababu Mheshimiwa Mtutura tumekuwa naye kwa karibu sana na vilevile tunampongeza kwa kweli yuko nasi bega kwa bega.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MHE. JUMA H. KILLIMBAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi pia nataka ufanuzi katika mambo mawili.

Nilipotoa mchango wangu wa maandishi, nilikuwa nimezungumzia suala la uchimbaji wa madini aina ya *silicon* yaliyopo katika Kijiji cha Mwanduijembe, eneo la Kipuma Kata ya Kaselya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili wananchi wanachimba madini hayo ya *silicon* kwa muda sasa, lakini kwa mara kadhaa tumejaribu kuwaomba Wizara ili waje wawape uhalali wale wananchi, kwa sababu wanaweza kuvamiwa.

Kwa hiyo, nataka nipate ufanuzi katika hili; je, wanafahamu kwamba pale panachimbwa madini aina ya *silicon* na wanasesmaje kuhusu kuwapa uhalali wa kuendelea kuchimba madini katika eneo hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, mara kadhaa nimekuwa nikichangia hapa na tulichangia wakati ule na Mheshimiwa Waziri anajua, kuhusiana na masuala ya umeme. Nilizungumzia kipindi fulani kuhusiana na vijiji ambavyo vimepitiva na umeme uliopozwa, vijiji hivi havihitaji gharama yoyote; vijiji kama Simbalungwala, Sinziligi,

Kibaya na Songambele ili ufile Nbago Sekondari na Kijiji kama cha Kibigiri na Kijiji cha Mkulu, havihitaji gharama yoyote kwa sababu umeme umepita palepale na wananchi walishiriki kuchimba mashimo kuweka zile nguzo wakati umeme huo unapita.

Sasa nimeomba mara kadhaa na kwa kutumia Kampuni ya Chico, iliwahi kuacha *transformer* ambayo ilikuwa inafanya kazi kwa kujenga barabara ya kazi na sasa hizo *transformer* hazina kazi. Naomba ufanuzi, hawa wananchi mnawaambiaje ili na wao wapate umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 104(1), naomba kuongeza kipindi kisichozidi dakika 30 kuanzia saa mbili kasorobo ili tuweze kuwasikiliza wengine wanaohitaji ufanuzi.

Mheshimiwa Waziri, ufanuzi wa maswali ya Mheshimiwa Killimbah.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali ya Mheshimiwa Killimbah yanafahamika Wizarani kwetu. Suala la uchimbaji wa madini ya *silicon* tumekuwa tukilifuatilia, tujiridhishe kwa takwimu kwanza. Tusingependa kuwapa wachimbaji leseni, kwa sababu malengo ya Wizara siyo kuwapa tu wananchi leseni mahali ambapo unajua kwamba, hakuna mashapo ya kutosha. Wizara yetu imekuwa iki-reconcile information lakini Maafisa wetu wa Kanda ya Kati na hasa Afisa wetu waliopo pale Singida, tumeshawapa maelekezo walikamilishe. Hili Mheshimiwa Mbunge anafahamu kwamba, tumekuwa na mawasiliano ya karibu kuhusu suala la umeme kwa sababu suala la madini tunalifanya kazi tutampa taarifa.

Niseme tu kwamba, Wananchi wa Iramba Magharibi, nina hakika wamesikia lakini Mheshimiwa Mbunge unafahamu mimi na Wabunge hapa tupo karibu, lakini wewe ni kati ya watu tulio karibu zaidi na sababu zake zinajulikana kwa sababu tunacheza mpira pamoa. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge kulisema hili, nafahamu madhumuni yake, lakini ahadi yangu kwako inabaki kuwa ileile, tuseme tu kwamba, Wananchi wa Iramba Magharibi, miradi hii ni yenye gharama ndogo sana ni ile ambayo tunaweza kama alivyosema haina gharama, gharama zipo lakini ndogo sana. Kwa hiyo, niseme hii ni kati ya ile Miradi ambayo tunaitekeleza ndani ya mwaka huu wa fedha. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza kuwasikia 15 bado 23; kwa hiyo, sasa nahamia hapo katikati. Mheshimiwa William Shellukindo karibu.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kueleza kwamba, wakati nilipozungumza nikaomba mwongozo wako, haja yangu ilikuwa ni kumkumbusha Mheshimiwa Waziri kwamba, mtaji wake mkubwa ni

ule wa Kamati, kama Kamati imekubali, hao wengine ni mmoja mmoja mtaji mkubwa ni ule. Kwa hiyo, Kamati yangu iliunga mkono.

Sasa kuna ufanuzi kidogo napenda niupate, wakati Waheshimiwa Wabunge wanazungumza, baadhi ya Wabunge walidokeza kwamba, kuna suala la *gender* pale lingetazamwa, halafu nadhani Mheshimiwa Esther Nyawazwa alimtaja Dr. Joyce Singano kwamba ni mtaalamu. Nadhani tungepata maelezo, mbona ametajwa huyu amefanya nini, ili Bunge lielewe?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza, niseme kwa dhati kwa niaba ya Wizara ya Nishati na Madini, tunafarijika sana na michango na uongozi wa Mheshimiwa William Shellukindo, kwenye Kamati yetu ya Bunge ya Nishati na Madini.

Nadhani sisi Wabunge lakini pia na Watanzania kwa ujumla, wanafahamu hilo kwamba, Kamati ya Nishati na Madini, chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa William Shellukindo, ipo imara na maslahi ya Taifa yapo mbele zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba radhi kwamba, ilijitokeza kwamba badala ya kuanza kulia nikaanza kushoto, lakini haikuwa kwa nia mbaya kama ambavyo Mheshimiwa Mwenyekiti alisema. Tunaomba radhi sana, ilitakiwa kwa mtiririko wa kawaida, tuanze na Kamati halafu twende kwenye upande wa pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya *gender* imejitokeza jana na Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella aliongelea, akataka kujua kulikoni. Cha msingi tunachokisema ni kwamba, nikianza na wa jumla ni kwamba, Wizara ya Nishati na Madini na Taasisi zake zikoje kuhusu *gender*.

Sisi tunasema hata kama hatujafikia *level* ya *fifty – fifty*, lakini kwa madhumuni ya kuwa *gender balanced*, tuko *balanced*. Tuliowatambulisha jana kwa sababu ndiyo lilikuwa chimbuko la hoja, ilitokea tu kwamba baadhi ya Viongozi wa ngazi za juu katika Wizara na Taasisi zilizoko chini ya Wizara ya Nishati na Madini.

Tuna Maafisa Waandamizi wengi ambao ni akina mama, kwa hiyo, nataka kuwathibitishia na kulithibitishia Taifa kwamba, *gender* imizingatiwa. Kwa mfano, nikiangalia pale Wizarani kwetu, tunakaribia kuwa *fifty – fifty*, nitakuwa nina-*exaggerate* sana, lakini *trend* ni nzuri kwa wale ambao wanatembelea pale kwetu wanafahamu kuna akina mama wengi na pia Wabunge wengine niwakaribishe mnapokuwa mnafuatilia Miradi, mnaweza kujionea hilo jambo.

Kuhusu Dr. Joyce; ni kati ya Maofisa Waandamizi wetu aliyepo pale *TPDC* ni Ofisa Mwandamizi na ndiyo hasa ilikuwa chimbuko, kwa sababu nafahamu Mheshimiwa Nyawazwa amekuwa akisema na Waheshimiwa wengine mmeona kwenye Maonyesho ya Sabasaba yalioisha jana, amekuwa akifafanua mambo hasa matumizi ya gesi kwa kiwango ambacho nadhani kilivuta hisia za Mheshimiwa Nyawazwa na Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, kuweza kulileta hapa mbele ya Bunge. Huyu ni kati ya

Watanzania, akina mama ambao wanachapa kazi kwa ufasaha na kwa umakini. Si ye tu, wapo wengi sana, nigeweza kuwataja lakini kwa sababu limejitokeza kwa Dada Joyce Singano, nilisemee kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa William Shellukindo.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa maelezo yake na ufanuzi alioutoa. Sisi kama Wabunge, tulitaka tumtambue huyu Dr. Joyce Singano na bahati nzuri, tuliweka katika *addendum* yetu. Inawezekana Waheshimiwa Wabunge wengi hawakuisoma, kwa sababu ilikuja baada ya sisi kutembelea. Sasa labda ningesoma hiki kidogo tu ni kitu cha msingi kabisa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Shellukindo, unataka kumtambua huyo Dr. Joyce, maana sijakuelewa?

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mgunduzi kuna kitu amegundua.

MWENYEKITI: Ahaa! Uvumbuzi wake? Endelea.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo. Dr. Joyce Singano, kwa uwezo wake mkubwa wa kitaalamu, umemuwezesha yeye kugundua kitu kinachoitwa kisukuku; kiumbe kipyä ambacho kimepewa jina kinaitwa Hank Kenena Singanowaa. Huu ni ugunduzi na ningeomba utambulike hapa, kwa sababu Waheshimiwa Wabunge tumeuona kule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, sidhani kama lina ubishi hilo, nakushukuru sana Mheshimiwa Shellukindo kwa kutukumbusha hilo.

Tunaendelea na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, naona mzee amekwishesema wewe bado una lingine? (*Kicheko*)

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante wazee wapo majumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka tu fafanuzi ndogo mbili, moja ni kama *comment*. Ukurasa wa 77 wa kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri, katika Miradi inayofadhiliwa na MCC imeonyeshwa Miradi katika Wilaya ya Handeni. Baadhi ya vijiji vilivyotajwa mle ndani, tuseme karibu vingi vyote viro Wilaya ya Kilindi, vijiji hivyo ni Kwediboma, Mkuyu, Mswaki na Mafuleta. Sasa nitilaka hizo *records* ziwekwe sawa ili hapo kazi itakapoanza, tuweze kuwa pia na takwimu sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niseme kwenye hili, niliwahi kuuliza hapa Bungeni na nikajibwa na Wizara kwamba, tatizo lilikuwa ni *transformers*. Umeme umepita lakini *transformer* maeneo mengi hakuna, nikaambwa kwamba, zipo Tanga na kwamba, kumi zingepelekwa lakini hadi leo hakuna kitu, sijui kama Waziri anaweza akalijibu hilo lakini kama hawezi basi kwa wakati muafaka.

La pili, nililotaka kulisema katika hotuba yake amezungumzia utaratibu ambao ...

MWENYEKITI: Hilo la tatu!

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni la pili hili; la kwanza lilikuwa ni usahihisho halafu na hoja ni hiyo ya *transformer*.

La pili, sasa ...

MWENYEKITI: Haya kwa kifupi sasa.

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Kwa kifupi ni kwamba, katika hoja yake, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba, katika ofisi 22 za madini, wameweka nadhani mitambo hii, wenyewe wanaelewa kuiunganisha (*cadastral system* ya *information*). Utagundua kwamba, mitambo hiyo ni muhimu sana kwenye maeneo ambayo yanatoka madini, hususan kwa pande za Wilaya zetu. Mashine hizo katika maeneo mengi sana, hazifanyi kazi ni mbovu kwa muda mrefu sasa.

Katika vifungu nikiangalia, sioni kifungu ambacho kina fedha za kutosheleza kuweza kufanya matengenezo au kushughulikia hii *system* ambayo sisi tunaihitaji, kwa ajili ya utoaji wa leseni na usimamizi wa leseni. Sijui Mheshimiwa Waziri, anasemaje kuhusu hilo?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kuweka kumbukumbu sahihi, kuhusu miradi hii inavyojitokeza kama nilivyosema, tumeona kuna haja tutafanya hivyo. Tutapambanua vizuri ili tulete taarifa kwa kina kwa Waheshimiwa Wabunge, pengine kupitia *pigeon holes* zetu ili tujue jinsi ilivyokuwa *conceived* hapa, tuipambanue. Hatuondoi *scope* wala hatubadilishi lakini tuseme kwamba, katika hii Miradi kwa Wilaya gani itakuwa rahisi zaidi.

Masuala ya *transformer* kama alivyosema Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, hilo tunalifanyia kazi na nakuahidi kwamba, utapata. Linakwenda pia kwa kaka yangu, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah pale, tulishamuahidi *transformer* na ilikuwa ni ya milioni saba tu. Tunafahamu Mheshimiwa Dr. Nibuka, pale kwake Morogoro na wengine ni kwamba masuala haya ya *transformer* tunaahidi moja kwa moja kwamba, tutatekeleza tu ndani ya mwaka huu wa fedha.

Kuhusu suala la *cadastral System* ya kwetu, tunakubali kuna kipindi ilifeli lakini hizi ni *technical problems* ambazo zilijitokeza. Tunaendelea kuhakikisha kwamba, sisi tunafanya kazi vizuri, tunazingatia na tunakiri udhaifu wa *system* yetu wakati fulani, kwa

sababu ni mambo ya *technical*, ambayo kidogo inakuwa si rahisi sana na yanapojitokeza wakati mwengine hujui yatajitokeza lini. Kimsingi ni nia yetu kuona kwamba, *system* yetu inafanya kazi kwa kiwango ambacho kinatarajwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MHE. BENSON M. MPESYA: Mheshimiwa mwenyekiti, naomba nikushukuru kwanza, kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza na nipaye ufanuzi katika mambo yangu mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, katika mchango wangu wa maandishi nilionyesha jinsi ninavyokerwa na hali ya kuagiza nguzo za umeme kutoka Afrika ya Kusini, wakati pale Mbeya tulikuwa na kiwanda cha nguzo na *TANESCO* ilikuwa na shamba la miti kwa ajili ya nguzo Utambalalila kule Mbozi. Wakati huo huo, watu wa Mbeya na Iringa, wameotesha miti mizuri sana na ni bei rahisi kwa ajili ya nguzo.

Swali, ni nini hicho ambacho kinatupelekea kila kitu tuagize kutoka Afrika Kusini, kwa upande wa nguzo? Hilo la kwanza.

La pili, katika mchango wangu wa maandishi nilionyesha jinsi ukubwa wa tatizo la umeme kwenye maeneo ya *Airport* Iyela One, pale kwenye Jiji la Mbeya, Itende pamoja na Isyesye. Waziri katika hotuba yake, katika ukurasa wa 79 na 80 kwa umahiri mkubwa sana, Miradi yote hii ameipa nafasi kwa kupitia *MCC*. Ninaomba nimshukuru sana kwa hili, lakini naomba kujuu *time frame* kwa sababu ni fedha za wafadhili, ni lini miradi hii itaanza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa kumrudishia shukrani Mheshimiwa Benson Mpesa, Baba Askofu, kwa jinsi alivyo-appreciate ahadi tuliyompa siku nyingi kidogo, tunatambua.

Hili la pili, nimesema kwamba, utekelezaji wa Miradi iliyo chini ya *MCC* inaanza mwezi huu wa Saba (Julai, 2008), kwa hiyo, tunaanza na shughuli zitaendelea tu.

Kuhusu la pili, kwa ni nini hizi nguzo zinaagizwa kutoka nje. Hili lipo kwenye sura mbili; kwanza ni la kisera, tunafahamu nchi yetu imekuwa ikipitia hatua mbalimbali, ilifikia mahali tukasema na ndiyo *trend* tu ya hata nchi nyingine kwamba, Serikali ijipunguzie majukumu ya kufanya biashara. Serikali kwa maana ya *central*, lakini na Taasisi zake na Mashirika ya Umma.

Sasa tulipofikia mahali hapo, tukasema hayo Mashirika ya Umma ambayo yalikuwa yanajishughulisha na shughuli za kibiashara yaziachie. Tunafahamu sote historia ya ubinafsishaji. Kwa hiyo, hili lina sura hiyo ya kisera kwanza, kwamba ni suala la kisera, tumesema Serikali ijiondoe kwenye shughuli za kibiashara na soko huria

litawale, lakini kunakuja suala la ushindani. Sababu ya kwamba, kwa nini nguzo zinaagizwa kutoka Afrika Kusini tu kila wakati, tuliliongelea sana wakati tunajadili Muswada wa Umeme hapa na ilikuwa ni hoja ya msingi tu.

Nafahamu Waheshimiwa Wabunge, wangependa kuona kwamba kwa nini *TANESCO* yenye we isiwe na nguzo zake, lakini ninachosema ni kwamba, biashara ya kuwa na kiwanda cha nguzo siyo *core-business* ya *TANESCO* na kwa sababu *TANESCO* tumekubali kwamba ni taasisi ambayo tunairuhusu ijiendeshe kibiashara, kwa sababu ile ni *corporate entity, objectives* zake zinajulikana na pengine haitakuwa maamuzi ya Serikali kuiamulia *TANESCO*, Bodi ipo na jambo hili inalifahamu.

Linaleta sura upande wa pili kwamba, Tanzania tuna wafanyabiashara wengi, ikitokea wakaanzisha au wakashiriki katika biashara hii, wanaweza kuwijengea mazingira mazuri zaidi ya kununua nguzo hapa Tanzania, kupitia wafanyabishara wetu wa ndani amba wanaweza kujenga viwanda vya nguzo hapa. Kwa sababu soko lipo *TANESCO*; ni shirika ambalo hatutaki wala hakuna mtu anayefikiria kwamba, siku moja halitaonekana katika shughuli hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ufanuzi wangu wa sasa hivi ni kwamba, nguzo zinazochukuliwa Afrika Kusini na pengine hata katika nchi nyingine kwa sababu ya kibiashara tu. Nimesema kwenye hotuba yangu kwamba, hili linatokana na unafuu wanaouputa, vinginevyo wasingeweza kununua kitu cha aghali halafu wakaacha cha bei rahisi.

MHE. BENSON M. MPESYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, dogo tu nisingependa kumchosha Mheshimiwa Waziri, ambaye ameonyesha mfano mzuri wa kushughulikia matatizo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimuulize Mheshimiwa Waziri kwamba, kwa kuwa fedha hizi za *MCC* zina masharti; je, Serikali imetimiza masharti hayo mpaka tuamini kwamba, mwezi wa saba kila kitu kitakwenda sawa?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumbukumbu zetu kama Wizara, mpaka sasa hivi hatuna kikwazo chochote. Kwa upande wetu kama Serikali, hatujatimiza ambacho kinakwamisha kuanza utekelezaji wa suala la Miradi ya *MCC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hasnain G. Dewji ama kwa jina jipya *Panadol*. (*Kicheko*)

MHE. HASNAIN G. DEWJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwa kunipa hilo jina la *Panadol*, nitakuwa mkombozi kwa wanaoumwa kichwa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi langu moja dogo tu, kuhusu mrabaha kutokana na gesi asilia. Nilichangia hapa Bungeni, lakini Waziri hakutaja mrabaha huu kutokana na gesi asilia lini utapatikana ili Wilaya ya Kilwa ipate maendeleo zaidi?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni mojawapo ya maeneo ambayo yanavuta hisia kali kutoka kwa wananchi, naelewa Mheshimiwa Hasnain Dewji anaongea kwa niaba ya wananchi. Ni *feelings* za maeneo mengi tu na kwa kweli si suala la inavyopatikana gesi tu, tunafahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kama tunavyofahamu, tunaongozwa na Miongozo ya Sera na Sheria, hili kwa sasa labda niseme ni mapema sana kulisema, kwa sababu Sera yetu wala Sheria, haielekezi kutoa mrabaha kwa maeneo ambayo upatikanaji wa gesi umeanza.

Haya ni maamuzi ya nchi na maamuzi ya nchi yanafanya kutokana na *system* nzima ya uongozi ilivyo. Pengine mbele ya safari tunaweza kufikia hapo, lakini kwa sasa hivi kwa kweli hatujafikia hapo. Ninaomba Mheshimiwa Hasnain Dewji aamin kwamba, tunazingatia *concern* na pia tunaelekezwa na utaratibu wa jinsi ambavyo nchi inaendeshwa; kwa sasa hatuna hicho kipengele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Nakuja hapa katikati, Mheshimiwa Vita Kawawa.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuomba ufanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifungu hivyo hivyo lakini kwenye *sub-vote* 250100, kama Kanuni zinaruhusu naomba niushike mshahara wa Naibu Waziri. (*Makof/Kicheko*)

MWENYEKITI: Huruhusiwi! Kwanza, omba ufanuzi tu kabla ya kufikiria mambo ya kushika mishahara ya watu hapa.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufanuzi kuhusu Madini ya *Uranium*. Katika mchango wangu wa maandishi, nilizungumzia matatizo tunayopata na wachimbaji wa *Uranium* katika Jimbo la Namtumbo. Nilizungumzia mwaka jana kuhusiana na hili pia.

Ninaomba kupata ufanuzi kwamba, sasa hivi Serikalini kuna mfumo gani unaosimamia utafutaji na uchimbaji wa Madini hayo? Kwa sababu Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake amesema, itatungwa Sera na Sheria kwa maana hiyo, sasa hivi hakuna Sera wala Sheria ya usimamizi wa uchimbaji Madini hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kule kwetu sasa hivi makampuni yanayochoronga hayo Madini na mchanga ule, wananchi wanachukua wanakwenda kuweka nyumbani wakidhani kwamba Madini yale yanawenza yakauzwa kama dhahabu

au vito. Kwa hiyo, tuna wasiwasi na *radiation*. Kampuni ya *Western Metal*, imeanza kutoa elimu kwa Viongozi wa Mkoa na jana wametoa elimu kwa Wananchi wa Wilaya ya Namtumbo. Makampuni peke yake hatuwezi kuyaamini, ninaomba ufanuzi kama Serikali imejihuisha vipi kusimamia hili kwa sasa hivi? Je, imehusisha pia Tume ya *Radiation*, yaani Tume ya Mionzi ?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufanuzi.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Vita Kawawa. Tumekuwa na mawasiliano ya karibu sana mwaka jana mwezi wa kumi, nilifika pale maeneo ya *Western Metals* wanayofanyia uchorongaji huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niarifu Kamati yako kwamba, Serikali inashiriki kila hatua inayofanywa na makampuni yote yanayoshiriki kwenye shughuli za madini ni kwamba, kila mahali Serikali inatambua.

Kwa mfano, sisi kwa Mkoa wa Ruvuma na hasa Wilaya ya Namtumbo, tuna Ofisi pale Songea. Nafahamu na Mheshimiwa Mbunge anafahamu kwamba, ipo Ofisi yetu inayoratibu hiyo kanda yote kuhakikisha kwamba, shughuli za Madini zinakwenda vizuri.

Lingine sasa hivi Sheria yetu ya Madini ya mwaka 1998, inatambua shughuli za utafutaji wa Madini ya *Uranium* hapa Tanzania, lakini tumetoa taarifa kwenye hotuba yetu na tumesema tutatunga Sera na Sheria mahususi kwa Madini haya. Hii ni kwa sababu kwanza, sasa tuna hakika tuna makampuni mengi kama ilivyojitokeza kwenye hotuba yetu, yanayofanya shughuli za utafutaji wa Madini ya *Uranium*. Madini ya *Uranium* ni katni ya Madini *strategic* popote duniani, ndiyo maana tukasema ni vyema tukatunga Sera na Sheria yake mahususi, kusimamia shughuli za *Uranium* hapa Tanzania na tunafahamu kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mchimbaji atakayeweza kuchimba Madini ya *Uranium* ndani ya miaka miwili ijayo. Tunazo takwimu za watu wote wanaoshiriki kule, kwa sababu pia inahitaji ujenzi wa viwanda, hasa kujenga ile migodi. Kwa hiyo, tunafahamu ratiba tuliyonayo ya kiutendaji, tuna hakika haitakuwa nyuma ya utekelezaji au uanzaji wa ujenzi au uchimbaji wa Madini ya *Uranium*. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, pamoja na Watanzania kwa ujumla kwamba, hatutaachwa nyuma katika hili, tutawahi kutengeneza Sera na Sheria ambayo tutailleta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wasiwasi wa *radiation*, tunafahamu, Taasisi ya Mionzi Tanzania tumekuwa tunafanya nayo kazi kwa karibu sana na kila kinachoendelea wenzenetu tunashirikiana nao na tunahakikisha kwamba, hakuna matatizo mpaka hivi sasa.

MHE. RUTH B. MSAFIRI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kutaka kupata ufanuzi kama ifuatavyo: Katika mchango wangu wa maandishi, nilimwomba Mheshimiwa Waziri akumbuke ombi langu la tangu mwaka 2001 linalohusu umeme wa Kagoma, ambalo hata mahesabu yake nilimpelekea mapema

kabla hata hajaandaa bajeti, lakini hakusema jambo lolote kuhusu Kagoma wakati anawataja Wabunge wengine ambao amefikiria ama amezingatia maombi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, kuna maeneo ambayo, kwa bahati nzuri katika Jimbo la Muleba Kaskazini, katika maeneo mengi tayari tuna umeme, lakini tumekuwa tunaomba tupatiwe transfoma. Kwanza, tuna Sekondari za Izigo na Luhanga, tuna Vijiji vya Kafunjo, Bushagara, Bushumba na Katoki yenyewe, lakini tumekuwa tunaomba transfoma na hata nguzo katika maeneo mengine ambayo transfoma zipo, lakini nguzo tatu au nne hazipo. Jambo hili limeshindikana kwa kipindi kirefu. Je, Mheshimiwa Waziri atatusaidia vipi katika suala hili? Ahsante sana.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni kweli nimepata taarifa ya dada yangu, Mheshimiwa Ruth Msafiri, alitufuata ofisini akatupa hoja zake, tukamshauri. Tunashukuru kwamba, alitekeleza akatupa takwimu za sasa zaidi, lakini tunamuahidi kama nilivyosema kwamba, kuhusu transfoma Waheshimiwa Wabunge, ambao ndiyo wawakilishi wa nchi nzima hapa, matatizo yote ya transfoma tunaahidi kuyashughulikia. Kama yapo hata wale wengine ambao hawajatuletea watuletee, hatuamini kama transfoma inaweza kukwamisha shughuli za upatikanaji wa umeme kwa mwaka mzima. Kwa hiyo, ndani ya mwaka huu wa fedha, tutahakikisha kwamba, masuala yote ya transfoma tutayashughulikia

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitumie fursa hii kuuelezea Mkoa wa Kagera, ambao mwanzoni nafahamu kaka yangu Mheshimiwa Masilingi, mwakilishi wa Muleba Kusini; ana Kata zake tatu, alishaleta maelekezo, Mheshimiwa Blandes, Mheshimiwa Profesa Banyikwa, kaka yangu, Mheshimiwa Dr. Kamala, Mheshimiwa Karamagi na wengine; Mkoa wa Kagera kwa ujumla mwanzoni ulikuwa umewekwa kwenye Mradi wa SIDA, lakini bahati mbaya kwa mwaka huu wa fedha haujitokezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwape taarifa, tumekaa nao mwezi wa Tano, wametuahidi katika hili sitaki kusema wametuthibitishia, baada ya kufadhili huu Mradi wa Makambako kwenda Songea, wametuambia au wametushauri ile *approach* ya mwanzo kwa sababu mradi wa mwanzo ulikuwa ni Bukombe – Kagera, lakini Bukombe sasa hivi ipo *ADB*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokaa nao wametuambia kwamba, wanasubiri tupidishe hii bajeti na naomba hapa Mheshimiwa Masilingi, tusaidiane sana kwa sababu tunataka bajeti ii she. Wametuambia tukishapitisha hii bajeti, wataangalia tumetenga kiasi gani katika Mfuko wetu wa Nishati Vijijini ili na wao waanzie hapo, kuufadhili Mradi wa Kagera, kwa sababu kwa kipindi kile ulikuwa unahitaji Dola za Kimarekani milioni kumi kama tutakumbuka, watachangia lakini kupitia Mfuko wa Wakala wa Nishati Vijijini. Nilitaka niseme hili la ujumla, kwa sababu linahusu Mkoa wote wa Kagera na pengine hili jibu litawasaidia wote wa Mkoa wa Kagera. Ahsante.

MHE. EMMANUEL J. LUAHULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naomba ufanuzi kwa sababu bajeti ya safari hii kwangu ni nzuri sana na nimeisifu. Wakati nachangia bajeti ya mwaka 2006/2007 na ya hivi sasa, nimekuwa

nikiongelea watafiti walioko eneo la Nyakafuru, ambao sasa hivi wanaitwa Kampuni ya *Resolute*, lakini utafiti pale kwa taarifa nilizonazo umeanza mwaka 1993, leo ni miaka kumi na tano utafiti unaendelea na hakuna kinachoendelea. Nimeomba wakati nachangia kwamba, Waziri au Serikali; leseni zao zitakapokwisha wasitishe kutoa leseni tena ili tuwape wachimbaji wadogo wadogo ambao tayari katika Wilaya yangu tumeanza kufanya kama *pilot area*. Naomba ufanuzi.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie tena fursa hii kwa mara nyingine, kuliarifu Bunge lako Tukufu na wananchi kwamba, sisi Serikali na hasa kwa jambo hili tunaloliongelea kuhusu masuala ya nishati na madini, ndiyo wenye takwimu na taarifa sahihi zinazoendelea kuhusu masuala yote yaliyo ndani ya nchi yetu katika sekta zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimkumbushe kaka yangu, suala hili analolisema sasa limeshajitokeza hapa, tukalijibu hapa Bungeni, nafahamu *concern* pengine haya makampuni watu wamekuwa ni wale wale, lakini makampuni yanabadilika kila muda unavyokwisha. Hiyo *loophole* tunaiona, tunaifahamu na hiyo fursa ipo na ndiyo maana tukasema tunataka kufanya *total overhaul* kwenye sheria yetu. Haiwezekani kama utakuwa unaonekana ni yule yule, lakini unabdalisha majina, tunataka tutafute dirisha ambalo sisi kama Serikali tunaweza kulishughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimpe matumaini Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwanza, hiyo kasoro tumeshaibaini. Kwa sasa kumbukumbu zilivyo, hakuna anayefanya kazi kinyume cha taratibu na sheria tulizonazo nchini. Tunafahamu kumekuwa na mipenyo ambayo inatokana na misingi yetu ya sheria pengine na sera, lakini yote haya yatarekebishwa tukifikia hatua ya kurekebisha sera na sheria.

MWENYEKITU: Sasa Waheshimiwa Wabunge, bado dakika kumi tu, bahati mbaya Kanuni ya 104 safari hii imeruka suala la *guillotine*; kwa hiyo, naruhusiwa kutafsiri ninavyotaka. Kwa maana hiyo basi, nitaendelea kuwapa ruhusa mpaka dakika mbili kabla au chache hivi labda tano halafu ndiyo tuitishe kwa pamoja. Kwa hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Batenga.

MHE. ELIZABETH N. BATENGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba ufanuzi wa mambo mawili tu mafupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme uliowekwa Ngara na Biharamulo ni kwa kutumia majenereta yaliyokuwa yameng'olewa kutoka Babati na Kondoa, ambayo sasa hivi hayafanyi kazi kwa uwezo wake. Kwa hiyo, umeme haujaweza kusambaa katika sehemu nyingi kuliko tulivyotarajia. Jana wakati likijibiwa swali na 172 la Mheshimiwa Vita Kawawa, ilielezwa kwamba, majenereta yatakayotoka Lindi na Mtwara, yatapelekwa Ngara na Biharamulo, lakini pia nilikuwa nasikia malalamiko ya watu wa maeneo hayo kwamba, umeme wao ulikuwa hauna uhakika. Sasa nauliza; je, hayo majenereta ambayo tayari yamekwishatumika na bila shaka ni machakavu, yataweza kufanya kazi yoyote ile au ni kwenda kuongeza tatizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, katika ukurasa wa 18 ameeleza kwamba, kuna Mradi wa Kuzalisha Umeme katika Maporomoko ya Rusumo na tulifikiri kwamba, huu ndio ukombozi kwa Wilaya hizo nilizozisema. Je, huo umeme utaanza kushughulikiwa lini ili watu angalau wawe na matumaini? Ahsante. (*Makofî*)

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kuhusu yale majenereta namhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wa Ngara kwamba, hatuna nia ya kuwadhihaki wananchi kwa kuwapeleke vitu ambavyo haviwezi kukidhi kutoa huduma inayotarajiwa. Kwa hiyo, tunamhakikishia kwamba ni katika juhudzi za kuhakikisha kwamba, wakati tunaendelea na Mradi wa Rusumo ambao utachukua muda kidogo kama inavyojitokeza, kwa sababu unahusisha nchi tatu lakini pia na mambo mengine ya kiutaalamu ambayo kwa asili yake, yanachukua muda mrefu kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumeona kwamba ni bora basi Wananchi wa Ngara waendelee kufaidika na hii huduma kuitia majenereta haya. Kwa hiyo, haya majenereta yanafaa, yatafanya kazi lakini kama yatajitokeza matatizo ya kiufundi, yataendelea kushughulikiwa kama ambavyo sehemu nyingine ambazo zinapata huduma za majenereta zinavyoendelea kushughulikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Rusumo tunaendelea kuushughulikia. Kwa kimsingi, bado unaendelea kufanyiwa kazi.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote* hiyo hiyo ya 58. Katika mchango wangu wa maandishi, nilikuwa nimesema pamoja na Serikali kusitisha Mkataba wa *Dowans*, lakini kabla *Dowans* hawajamaliza ule Mkataba waliokuwa wamepewa, walikuwa kwa kila siku wanatakiwa walipe faini dola elfu kumi kwa kutomaliza ule mkataba.

Ningependa kujua Serikali ilikusanya kiasi gani kutokana na ile faini ili tuweze kuwashauri wataweza kuzitumia namna gani fedha hizo? Naomba maelezo.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii hili linahitaji takwimu, tunamkaribisha Mheshimiwa Mbunge, tutawasiliana na wataalamu wetu, tutalifikia tu. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Sasa ni wakati wa *guillotine* ili tuweze kumaliza shughuli ndani ya hizi dakika tano.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif.1002 – <i>Finance and Accounts</i>	Sh. 860,851,000
Kif.1003 – <i>Policy Planning</i>	Sh. 24,195,000
Kif.1004 – <i>Internal Audit Unit</i>	Sh. 191,411,000
Kif.2001 – <i>Minerals</i>	Sh. 3,768,419,000
Kif.2002 – <i>Madini Institute</i>	Sh. 954,409,000

Kif.2003 – *Research and Laboratory*

Services Sh.1,259,800,000

Kif.2004 – *TANSORT London*... Sh. 1,428,189,000

Kif.3001 – *Energy and Petroleum*... Sh. 32,228,746,000

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 58 – Wizara ya Nishati na Madini

Kif.1001 – *Administration and General*... Sh. 624,500,000

Kif.1003 – *Policy Planning*... Sh. 250,000,000

Kif.2001 – *Minerals*... Sh. 4,863,491,200

Kif.2002 – *Madini Institute*... Sh. 600,000,000

Kif.2003 – *Research and Laboratory Services*... Sh. 413,000,000

Kif.3001 – *Energy and Petroleum*... Sh. 313,316,394,400

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

(*Bunge lilirudia*)

T A A R I F A

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa taarifa, nilikuwa naomba niwatambue Waheshimiwa Wabunge, ambao walileta michango yao wakati nimeshapanda kwenye *podium* kama ifuatavyo: Mheshimiwa Lucy Mayenga, nadhani nilishamtaja, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Ussi Ame Pandu, Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mheshimiwa Elieta Switi na Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kuwa, Bunge limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2008/2009, kifungu hadi kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo basi, naliomba Bunge lako Tukufu, liyakubali makadirio haya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa
Mwaka 2008/2009 yalipitishwa na Bunge)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nimepata taarifa kutoka Serikalini, ambayo ni kauli ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo; kwa hiyo, ingawa *Order Paper* ilikuwa tayari, kwa kuwa taarifa hii ni muhimu, basi tutawaletea *Supplementary Order Paper* ili kauli iweze kutolewa baada ya matangazo kesho asubuhi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, sasa naahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 02.17 usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi,
Tarehe 10 Julai, 2008, Saa Tatu Asubuhi)*

(Kiambatanisho A)

**PROGRAMU YA MAENDELEO YA SEKTA YA MAJI
PROGRAMU NDOGO YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI
HALMASHAURI ZITAKAZOITA KAMPUNI ZILIZOCHAGULIWA
ILI ZIANDAE MAPENDEKEZO YA USANIFU WA MIRADI YA MAJI**

NA. MKOANA.JINA LA HALMASHAURINGAZI YA HALMASHAURI

1	Arusha	1	Arusha	HMS
		2	Arusha	HW
		3	Karatu	HW
		4	Longido	HW
		5	Meru	HW
		6	Monduli	HW
		7	Ngorongoro	HW
2	Dar es Salaam	8	Ilala	HMS
		9	Kinondoni	HMS
		10	Temeke	HMS
3	Dodoma	11	Bahi	HW
		12	Chamwino	HW
		13	Dodoma	HMS
		14	Kondoa	HW
		15	Kongwa	HW
		16	Mpwapwa	HW
4	Iringa	17	Iringa	HMS
		18	Kilolo	HW
		19	Ludewa	HW
		20	Makete	HW
		21	Mufindi	HW
		22	Njombe	HM

5	Kagera	23	Biharamulo	HW
		24	Bukoba	HMS
		25	Bukoba	HW
		26	Karagwe	HW
		27	Misenyi	HW
		28	Muleba	HW
		29	Ngara	HW
NA. MKOANA.JINA LA HALMASHAURINGAZI YA HALMASHAURI				
6	Kigoma	30	Kasulu	HW
		31	Kibondo	HW
		32	Kigoma/Ujiji	HMS
		33	Kigoma	HW
7	Kilimanjaro	34	Hai	HW
		35	Moshi	HMS
		36	Moshi	HW
		37	Mwanga	HW
		38	Rombo	HW
		39	Siha	HW
8	Lindi	40	Kilwa	HW
		41	Lindi	HM
		42	Lindi	HW
		43	Liwale	HW
		44	Nachingwea	HW
		45	Ruangwa	HW
9	Manyara	46	Hanang	HW
		47	Mbulu	HW
10	Mara	48	Bunda	HW
		49	Musoma	HMS
		50	Musoma	HW
		51	Serengeti	HW
		52	Tarime	HW
11	Mbeya	53	Mbeya	HW
12	Mtwara	54	Masasi	HW
		55	Mtwara	HMS
		56	Mtwara	HW
		57	Nanyumbu	HW
		58	Newala	HW
		59	Tandahimba	HW
13	Mwanza	60	Geita	HW
		61	Magu	HW
		62	Mwanza	HJ
		63	Sengerema	HW

NA.MKOANA.JINA LA HALMASHAURINGAZI YA HALMASHAURI

14	Pwani	64	Kibaha	HM
		65	Kibaha	HW
		66	Rufiji	HW
15	Rukwa	67	Mpanda	HM
		68	Mpanda	HW
		69	Nkasi	HW
		70	Sumbawanga	HMS
		71	Sumbawanga	HW
16	Ruvuma	72	Mbinga	HW
		73	Namtumbo	HW
		74	Songea	HW
17	Shinyanga	75	Bariadi	HW
18	Singida	76	Iramba	HW
		77	Manyoni	HW
		78	Singida	HMS
		79	Singida	HW
19	Tanga	80	Korogwe	HM
		81	Lushoto	HW
		82	Tanga	HJ

HW: Halmashauri ya Wilaya

HM: Halmashauri ya Mji

HMS: Halmashauri ya Manispaa

HJ: Halmashauri ya Jiji